BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

# RIPOTI YA KAMATI YA KUCHUNGUZA NA KUDHIBITI HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA NA MASHIRIKA (LAAC) KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

FEBRUARI, 2023

YALIYOMO UKURASA


1. SEHEMU YA KWANZA 2
2. UTANGULIZI 2
3. SEHEMU YA PILI 4
4. MAUDHUI YA RIPOTI 4

RIPOTI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KWA HESABU ZA MAMLAKA YA SERIKALI YA MITAA KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

5. BARAZA LA MANISPAA MJINI 6
6. BARAZA LA MANISPAA MAGHARIBI “A” 8
7. BARAZA LA MANISPAA MAGHARIBI “B” 12
8. HALMASHAURI YA WILAYA YA KASKAZINI “A” 44
9. HALMASHAURI YA WILAYA YA KASKAZINI “B” 52
10. BARAZA LA MJI KATI 60
11. HALMASHAURI YA WILAYA YA MICHEWENI 65
12. BARAZA LA MJI CHAKE CHAKE 73
13. BARAZA LA MJI MKOANI 81
14. BARAZA LA MJI WETE 89

RIPOTI YA UKAGUZI MAALUM UNAOHUSU UTEKELEZAJI WA MAAGIZO YA RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI MHE. DK. HUSSEIN ALI MWINYI WAKATI WA KUWAAPISHA VIONGOZI WAKUU

15. RIPOTI YA UKAGUZI MAALUM WA MALIPO YA FIDIA KWA WANANCHI WALIOATHIRIKA KWA KUPISHA MRADI WA UWEKEZAJI WA UJENZI WA BANDARI, BOHARI NA MIUNDOMBINU YA MAFUTA NA GESI MANGAPWANI/BUMBWINI 94

16. RIPOTI YA UKAGUZI MAALUM KUHUSU MALIPO YA NAULI YA WALIMU “BUS FARE” KWA SERIKALI ZA MITAA - PEMBA KWA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2020

17. BARAZA LA MJI MKOANI 109
18. BARAZA LA MJI CHAKE CHAKE 119

19. BARAZA LA MJI WETE 131
20. HALMASHAURI YA WILAYA YA MICHEWENI 141

RIPOTI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KUHUSU UKAGUZI WA MASHIRIKA NA TAASISI ZINAZOJITEGEMEA ZA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

21. SHIRIKA LA NYUMBA 152
22. SHIRIKA LA MAGAZETI 160
23. MAMLAKA YA UNUNUZI NA UONDOSHAJI WA MALI ZA UMMA ZANZIBAR (ZPPD) 170
24. MAMLAKA YA USAFIRI BAHARINI 177
25. SHIRIKA LA BIMA ZANZIBAR (ZIC) 188
26. SHIRIKA LA BANDARI ZANZIBAR (ZPC) 206
27. SHIRIKA LA BIASHARA LA TAIFA (ZSTC) 235
28. MAMLAKA YA VIWANJA VYA NDEGE (ZAA) 253
29. HITIMISHO 274

## SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali za Mitaa na Mashirika (LAAC) ni miongoni mwa Kamati za Kuduma za Baraza ambazo zimeundwa kwa mujibu wa kifungu cha 85(1) cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 sambamba na kanuni ya 107(1) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la mwaka 2020.

Kamati ya ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali za Mitaa na Mashirika (LAAC) ni moja kati ya Kamati za Baraza inayosimamia masuala ya fedha.

Hivyo, Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali za Mitaa na Mashirika (LAAC) pamoja na masharti mengine ya yaliyopo Kikanuni hufuatilia Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kwa kipindi hiki imefanikiwa kufanya ukaguzi wa Ripoti tatu zilizowasilishwa katika vipindi tofauti katika Baraza, Ripoti zenyewe ni:

i. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

ii. Ripoti ya Ukaguzi Maalum Unaohusu Utekelezaji wa Maagizo ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mh. Dk. Hussein Ali Mwinyi Wakati wa Kuwaapisha Viongozi Wakuu.

iii. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mashirika na Taasisi zinazojitegemea za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka wa fedha 2020/2021.

Hata hivyo, Kamati ya LAAC haikuweza kuikamilisha kuifanyiwa kazi, Ripoti hii kutokana na ufinyu wa muda, hivyo, Kamati inaahidi kuendelea kuikamilisha Ripoti hiyo katika mizunguko ijayo ya Kamati.

### 1.1 MAJINA YA WAJUMBE NA SEKRETARIETI YA KAMATI

Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali ya Mitaa na Mashirika, kwa mwaka huu wa uwasilishaji wa ripoti ya mwaka 2019/2020 na 2020/2021, inaundwa na Wajumbe 6 na Sekretarieti kama ifuatavyo:

#### 1.1.1 Wajumbe wa Kamati

1. Mhe. Habib Ali Mohamed - Mwenyekiti
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma - Makamo Mwenyekiti
3. Mhe. Bakar Hamad Bakar - Mjumbe
4. Mhe. Haji Shaaban Wazir - Mjumbe
5. Mhe. Shadya Mohammed Suleiman - Mjumbe

6. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Mjumbe

### 1.1.2 Sekretarieti ya Kamati

Sekretarieti ya Kamati hii iliongozwa na Makatibu wa Kamati kutoka Afisi ya Baraza la Wawakilishi na Maafisa wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Sekritarieti yenyewe ni:

1. Ndg. Nasra Awadh Salmin - Katibu
2. Ndg. Yussuf Mkamba Mwinyi - Katibu
3. Ndg. Shekhe Abdallah Ali - Afisa wa Ofisi ya Mdhibiti
4. Ndg. Maryam Alhaj Juma - Afisa wa Ofisi ya Mdhibiti
5. Ndg. Abdallah Khamis Omar - Afisa wa Ofisi ya Mdhibiti

## 1.2 UTARATIBU WA KAZI ZA KAMATI

Kamati imefanya kazi kwa mujibu wa masharti yaliyoelezwa katika Jadweli la Kwanza la Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2020.

Vile vile, Kamati hii ilizingatia matakwa ya Kanuni ya Kudumu inayoitaka Kamati kujipangia kazi zake baada ya kushauriana na Spika pamoja na kujipangia utaratibu mzuri wa kutekeleza majukumu yake.

Katika kutekeleza majukumu yake mbalimbali Kamati ilijipangia kukutana na Watendaji wa Serikali za Mitaa, Mamlaka za Serikali na Mashirika yanayojitegemea yaliyopo Unguja, Pemba na kufanya ziara huko Dar - es – Salaam katika Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA).

Vile vile, Kamati ya LAAC ilifanya ziara katika maeneo mbali mbali kwa lengo la kufanya ukaguzi ili kushuhudia uhalisia na usahihi wa maelezo yaliyowasilishwa na watendaji hao. Ukaguzi huo ulifanyika kwa mizunguko minne tofauti kama ifuatavyo:

**Mzunguko wa Kwanza:** Tarehe 28 Machi, 2022 hadi tarehe 14 Aprili, 2022.

**Mzunguko wa Pili:** Tarehe 01 Agosti, 2022 hadi tarehe 19 Agosti, 2022.

**Mzunguko wa Tatu:** Tarehe 31 Oktoba, 2022 hadi tarehe 18 Novemba, 2022.

**Mzunguko wa Nne:** Tarehe 16, Januari, 2023 hadi tarehe 03 Februari, 2022.

## SEHEMU YA PILI

## MAUDHUI YA RIPOTI

RIPOTI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KWA HESABU

ZA MAMLAKA YA SERIKALI YA MITAA KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

## 4.1 BARAZA LA MANISPAA YA MJINI ZANZIBAR

### Taarifa ya Mapato

Baraza la Manispaa Mjini kwa mwaka wa fedha 2019/2020 lilikadiriwa kukusanya jumla ya Tsh. 17,205,557,546. Kati ya hizo jumla ya Tsh. 4,775,400,000 ni kutoka katika vyanzo vya mapato ya Baraza na Tsh. 12,430,157,546 ni ruzuku ya mishahara na kazi za kawaida kutoka Serikalini.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2020 Baraza la Manispaa Mjini lilikusanya Tsh. 16,362,034,020.12 sawa na asilimia 95 ya makadirio. Kati ya hizo Tsh. 3,953,050,542 ni kutoka katika vianzio vya mapato vya Baraza na Tsh. 12,408,983,478.12 ni ruzuku ya mishahara na kazi za kawaida kutoka Serikalini.

### Majibu

Baraza la Manispaa Mjini halikuandaa maelezo ya moja kwa moja juu ya taarifa ya mapato na badala yake lilijibu hoja za Kamati kama zilivyoulizwa.

### Uchunguzi wa Kamati

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC ilibaini yafuatayo:-

1. Baraza la Madiwani lilipitisha bajeti ya Tsh. 17,400,318.618 ambayo ilitofautiana na bajeti iliyopitishwa baadae na Serikali ambayo ni Tsh. 17,205,557,546. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na utaratibu.
2. Fedha za DCU huwa hawapatiwi kila mwaka ingawa Manispaa huchangia katika Kitendo hicho na hutakiwa kuwasilisha miradi ya kutekelezwa. Kamati ya LAAC haikuridhika na hali hiyo.
3. Mapato ya Baraza la Manispaa Mjini yalishuka baada ya Baraza kukasimu kazi ya kukusanya mapato kwenye kianzio chake cha mapato cha maegesho ya vyombo kwa Kampuni.

### Mapendekezo ya Kamati

Ili kasoro kama hizo zisijitokeze tena katika siku zijazo, Kamati ya LAAC ilipendekeza yafuatayo:

1. Bajeti inayoidhinishwa na Baraza la Madiwani iheshimiwe na Serikali hasa ikizingatiwa kuwa Baraza la Madiwani ndio lenye dhamana na Baraza husika.
2. Baraza la Manispaa Mjini likahakikishe kuwa linafanya utafiti wa kutosha juu ya jambo lolote kabla ya kuchukua hatua ili kuepusha hasara isiyo na lazima.
3. Ni vyema kila mwanachama wa DCU kupata fedha ya mradi kwa kuwa mwanachama huyo anatoa mchango wake katika Kitengo hicho

### Taarifa ya Matumizi

Baraza la Manispaa Mjini kwa mwaka wa fedha 2019/2020 lilikadiriwa kutumia jumla ya Tsh. 17,205,557,546. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2020 jumla ya Tsh.

16,432,939,291 zilitumika sawa na asilimia 96 ya makadirio.

**Majibu**
Baraza la Manispaa Mjini halikuandaa maelezo ya moja kwa moja juu ya taarifa ya mapato na badala yake lilijibu hoja za Kamati kama zilivyoulizwa.

**Uchunguzi wa Kamati**

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC ilibaini yafuatayo:-

1. Mashine za EDF zimenunuliwa kwa kutumia mfumo wa LPO badala ya "Frame Work Contract".

2. Baraza la Manispaa Mjini limefanya matumizi yake kwa tukio moja kujumuisha matumizi ya zaidi ya kifungu kimoja jambo ambalo ni kinyume na taratibu za kifedha.

3. Kwenye Taarifa ya Fedha ya Mwisho wa Mwaka "Note" 9 imejumuisha mambo mbali mbali kinyume na taratibu za kifedha.

4. "Stationaries" zimetumia fedha nyingi, ambapo kwa robo mwaka zimetumia Tsh. 130,741,594 jambo ambalo linaleta utata.

Kutokana na kasoro hizo Kamati ya LAAC imelitaka Baraza la Manispaa Mjini kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa taratibu zilizopo Kisheria na Kikanuni ili kuepuka hoja zisizo za lazima.

**MATOKEO YA UKAGUZI**

Kamati ya LAAC haikupata majibu ya kutosheleza katika hoja zote zilizobainika na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kutokupatikana kwa vielelezo vilivyohitajika pamoja na kutokuwepo kwa baadhi ya Watendaji ambao walihusika moja kwa moja na hoja hizo, ingawa barua ya Kamati ilimtaka Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa Mjini kuhakikisha kuwa watendaji wote wanaohusika na hoja hizo wanakuwepo siku ya kikao husika.

Kwa mnasaba huo, Kamati ya LAAC haikuridhika na hali hiyo, hivyo, hoja hizo zimebaki kama zilivyo.

## 4.2 BARAZA LA MANISPAA MAGHARIBI "A"

**Taarifa ya Mapato**
Baraza la Manispaa Magharibi "A" kwa mwaka wa fedha 2019/2020 lilikadiriwa kukusanya jumla ya Tsh. 1,000,000,000 kutoka katika vyanzo vya mapato ya Baraza.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2020 Baraza la Manispaa Magharibi "A" lilikusanya Tsh. 1,227,991,234 zilikusanywa kutoka katika vyanzo vya mapato ya Baraza sawa na asilimia 100.9 ya makadirio.

**Majibu**
Baraza la Manispaa Magharibi "A" halikuandaa maelezo ya moja kwa moja kuhusiana na taarifa ya mapato, hata hivyo, Baraza lilijibu hoja za Kamati kama zilivyoibuliwa.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**
Katika kujadili taarifa ya mapato, Kamati ya LAAC ilibaini yafuatayo:

1. Mapato mengineyo (Other Receipt) yameongezeka maradufu kutokana na sababu zifuatazo:
    a. Kutokutengewa bajeti kianzio cha Minara katika mwaka wa fedha husika.
    b. Kuongezeka kwa faini za Vibali vya ujenzi
    c. Wananchi walishajihishika sana kuvua madagaa baada ya kubaini kuwa faida kubwa inapatikana kutokana na shughuli hiyo.
    d. Baraza limeanza kukodisha wenyewe maduka yake ya mbao baada ya Waliokodishwa kumaliza kujilipa gharama za ujenzi walizotumia.
2. Taarifa ya Fedha ya Mwisho wa Mwaka ina mapungufu kadhaa ikiwemo:
    a. "Note" moja kuwa na viwango tofauti vya fedha jambo ambalo ni kinyume na taratibu za ufungaji wa hesabu.
    b. Kasma moja kutumika kwa kifungu zaidi ya kimoja.

Kutokana na kasoro hizo Kamati ya LAAC imelitaka Baraza la Manispaa Magharibi "A" kuhakikisha kuwa inavitengea bajeti vianzio vyake vyote vya mapato ili kuwa na bajeti sahihi.

Aidha, Kamati inaishauri Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuhakikisha kuwa inatoa Kasma tofauti kwa kila kifungu ili kuondosha utata juu ya jambo husika.

**Taarifa ya Matumizi**
Baraza la Manispaa Magharibi "A" kwa mwaka wa fedha 2019/2020 lilikadiriwa kutumia jumla ya Tsh. 9,617,154,470. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2020 jumla ya Tsh. 9,974,736,974 zilitumika sawa na asilimia 105 ya makadirio.

**Majibu**
Baraza la Manispaa Magharibi "A" halikuandaa maelezo ya moja kwa moja kuhusiana na taarifa ya matumizi, hata hivyo, Baraza lilijibu hoja za Kamati kama zilivyoibuliwa.

**Uchunguzi wa Kamati**
Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC, ilibaini yafuatayo:

1. Matumizi ya Baraza yameongezeka kutokana na kuongezeka kwa watendaji.
2. Taarifa ya Fedha ya Mwisho wa Mwaka ina mapungufu mengi jambo ambalo limeishangaza sana Kamati hii kwa kuwa Taarifa hiyo huwasilishwa kwa

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kama ilivyoelezwa na kifungu cha 119 cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha ya mwaka 2016 na Afisi ya Mdhibiti huipitia Taarifa hiyo na inaweza kuitaka Taasisi kuifanyia marekebisho Taarifa hiyo.

Baadhi ya kasoro hizo ikiwemo; Maelezo ya "Note" kukinzana kwani "Note" 7 inaelezea "Personal Emoluments" na "Exchequer Issue" lakini pia, "Note" 9 inaelezea "Personal Emoluments" na kadhalika.

Kutokana na kasoro hizo nyingi zilizobainika katika Taarifa ya Fedha ya Mwisho wa Mwaka ni sahihi kwa Baraza hili kupata Hati yenye Shaka

3. Baadhi ya matumizi hayakupata maelezo, kwa mfano:
    a. Matumizi ya Tsh. 269,165,905 wakati Mpango wa Ununuzi (Procurement Plan) unatambua Tsh. 148,000,000 tu.
    b. Matumizi yaliyofanywa kwa kuwekwa bustani (garden).

**Mapendekezo ya Kamati**

Ili kasoro kama hizo zisijitokeze tena, Kamati ya LAAC ilipendekeza yafuatayo:

1. Afisi ya Mdhibiti kuhakikisha kuwa kasoro zote zinazobainika ndani ya Taarifa ya Fedha ya Mwisho wa Mwaka zinafanyiwa kazi ili kuepusha usumbufu kwa Watumiaji wa Taarifa hiyo. Kwani kwa mujibu wa kifungu cha 119(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha ya mwaka 2016 nakala ya Taarifa hiyo huwasilishwa pia kwa Mkuu wa Hazina (Tresury), hivyo, sio busara kwa Mtendaji huyu kupatiwa Taarifa yenye mapungufu.
2. Baraza la Manispaa Magharibi "A" lihakikishe kuwa linatekeleza shughuli zake kwa mujibu wa Sheria na Kanuni zilizopo ili kuepusha hoja zisizo na msingi.

## MATOKEO YA UKAGUZI

### 4.2.1 Kukosekana kwa vitabu vya stakabadhi za kukusanyia mapato

Ukaguzi umebaini baraza la Manispaa ya Magharibi "A" limekusanya mapato mbali mbali kwenye vitengo mbali mbali vya kukusanyia mapato ya Baraza, dosari iliobainika na ukaguzi ni kukosekana kwa vitabu vya risiti vilivyotumika kukusanyia mapato hayo. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma Namba 12 ya mwaka 2016.

**Majibu**

Vitabu vitano tu ndio vimekosekana wakati wa ukazi kati ya vitabu 43.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya LAAC haikuthibitisha kauli hiyo kwa kuwa Mtendaji wa Afisi ya Mkaguzi Mkuu ambaye alifuatana na Kamati hakuwa na uhakika na kile kilichoelezwa.

#### 4.2.2 Tofauti ya Tsh. 1,526,123,819 iliyojitokeza katika taarifa ya hesabu ya mwisho wa mwaka

Ukaguzi ulipitia taarifa ya hesabu ya mwisho wa mwaka wa fedha 2019/2020 pamoja na daftari la kutunzia fedha ili kuangalia uwiano kati ya taarifa ya hesabu za mwisho wa mwaka na daftari la kutunzia kumbu kumbu za mapato na matumizi ya Baraza la Manispaa ya Magharibi Ä".

Ukaguzi umebaini jumla shilingi 11,310,574,959 ni matumizi yaliyoonekana kutumika kwenye daftari la kutunzia fedha kupitia hesabu ya Baraza la Manispaa Magharibi "A". Aidha, jumla ya shilingi 9,784,451,140 ni matumizi yaliyoonyeshwa kwenye taarifa ya hesabu ya mwisho wa mwaka, hivyo kupelekea uwepo wa tofauti ya shilingi 1,526,123,819.

Kutoripotiwa hesabu sahihi katika taarifa ya hesabu ya mwisho wa mwaka kunapelekea taarifa hiyo kutokuonyesha uhalisia kwa mujibu wa viwango vya utayarishaji wa taarifa za fedha. Aidha kunaweza kupelekea taarifa za hesabu za Baraza la Manispaa ya Magharibi "A" kutoonesha sura halisi na sahihi. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC ililipitia "cash book" la Baraza na ilibaini uwepo wa tofauti ya Tsh. 110,266,346.61 na sio kama ilivyoelezwa kwenye Ripoti ya Mkaguzi Mkuu.

#### 4.2.3 Malipo Yasiokuwa na Vielelezo Husika Shilingi 47,266,200

Ukaguzi umebaini Baraza la Manispaa Magharibi "A" limefanya malipo ya shilingi 47,266,200 kwa ajili ya kugharamia shughuli mbalimbali za Baraza, dosari iliyobainika na ukaguzi ni kukosekana kwa vielelezo vya matumizi hayo, kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma Namba 12 ya mwaka 2016.

**Majibu**

Vielelezo vilivyokosekana wakati vya ukaguzi vipo tayari kwa kujiridhisha.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Hoja imebaki kama ilivyo, kwa kuwa vielelezo hivyo vimepatikana baada ya kutoka kwa Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

#### 4.2.4 Hati za Malipo Zilizokosekana kwa Ukaguzi Shilingi 42,879, 500

Ukaguzi umebaini Baraza la Manispaa Magharibi "A" limefanya malipo ya Shilingi 42,879, 500 kwa ajili ya matumizi mbali mbali, dosari iliyobainika ni kukosekana kwa hati za malipo husika, kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Usimamizi wa

Fedha za Umma Namba 12 ya mwaka 2016.

**Majibu**
Hati za malipo kwa matumizi mbali mbali tayari vipo kwa ukaguzi ili kujiridhisha

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**
Hoja imebaki kama ilivyo, kwa kuwa hati hizo zimepatikana baada ya kutoka kwa Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

### 4.2.5 Kukosekana kwa mikataba ya watoa huduma Tsh. 19,000,000
Ukaguzi umebaini Baraza la Manispaa Magharibi "A" limefanya malipo mbali mbali kwa ajili ya kulipia huduma kutoka kwa wasambazaji mbali mbali, dosari iliyobainika na ukaguzi ni kukosekana kwa mikataba kati ya wasambazaji hao na Baraza la Manispaa ya Magharibi "A" kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Namba 11 mwaka 2016.

**Majibu**
Mikataba ya vikundi vya usafi pamoja na Ankara ya matumizi ya "internet"
tayari vipo kwa ukaguzi ili kujiridhisha.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**
Hoja imebaki kama ilivyo, kwa kuwa hati hizo zimepatikana baada ya kutoka kwa Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

## 4.3 BARAZA LA MANISPAA MAGHARIBI "B"

**Taarifa ya Mapato**
Baraza la Manispaa Magharibi "B" kwa mwaka wa fedha 2019/2020 lilikadiriwa kukusanya jumla ya Tsh. 2, 100,000,000 kutoka katika vyanzo vya mapato ya Baraza.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2020 Baraza la Manispaa Magharibi "B" lilikusanya Tsh. 1,940,169,299.45 zilikusanywa kutoka katika vyanzo vya mapato ya Baraza sawa na asilimia 92.4 ya makadirio.

**Majibu**
Baraza la Manispaa Magharibi "B" halikuwa na maelezo ya moja kwa moja kuhusiana na taarifa za mapato, hivyo, Baraza lilijibu hoja za Kamati kama zilivyotolewa.

**Uchunguzi wa Kamati**
Katika kufuatilia hoja hii yafuatayo yalijitokeza:

1. Kamati ya LAAC haikuridhika na namna Baraza hili linavyopanga makadirio yake ya mapato. Hii ni kutokana na kuwa baadhi ya vyanzo vya mapato

mwaka wa fedha 2018/2019 vilikusanya zaidi isipokuwa kwamba katika mwaka wa fedha 2019/2020 vilikadiriwa kukusanya chini ya kiwango hicho. Kwa mfano eneo la maegesho ya gari "Parking" na Maombi ya fomu "Application Form".

2. Baadhi ya vianzio vya mapato hawakusanyi tena mapato baada ya Serikali Kuu kuagiza hivyo, kwa mfano mnada wa soko la Mazizini kwa kuwa soko hilo limejengwa na TASAF.

Kamati ya LAAC iliomba barua ya agizo hilo, hata hivyo, Watendaji wa Baraza la Manispaa walishindwa kuipatia Kamati barua hiyo kwa madai kwamba waliambiwa tu kwa mdomo na aliyekuwa Makamo wa Pili wa Rais, Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi.

Kutokana na kasoro hiyo, Kamati ya LAAC iliandaa kikao cha pamoja tarehe 25 Januari, 2023 kilichojumuisha Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Uratibu, Sera na Baraza la Wawakilishi, Wizara ya Nchi, (OR), Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, Baraza la Manispaa Magharibi "B", Kamati ya Soko la Mazizini. Katika kikao hicho, iliamulika kuwa Baraza la Manispaa Magharibi "B" iorodheshe maeneo yote yanayopaswa kukusanywa mapato ili Baraza liweze kupata mapato hayo kama Sheria na Kanuni inavyoelekeza.

3. Chanzo cha mapato cha maliasili hawakupata gawio kama ilivyotarajiwa.

4. Kwenye Hesabu ya Mwisho wa Mwaka (Financial Statement) "Note" 6 imeandikwa mara mbili kwa matumizi tofauti kitendo ambacho ni kinyume na taratibu za kihasibu.

### Mapendekezo ya Kamati

Ili kasoro kama hizo zisijitokeza katika siku zijazo Kamati ya LAAC ilipendekeza yafuatayo:

1. Baraza la Manispaa Maghribi "B" lipange makadirio ya bajeti yake kwa mwaka unaofuata kwa kuanzia na kiwango cha mapato yaliyokusanya katika mwaka uliopita.
2. Vyanzo vya mapato ambavyo Serikali vimeamua kukusanywa na Serikali Kuu na baadae mapato ya vianzio hivyo yagawiwe baina ya Taasisi mbili hizo, Taasisi husika zihakikishe kuwa zinazipatia kwa wakati na kwa kiwango halisi Serikali za Mitaa mgao wa fedha zinazotokana na vianzio hivyo, ili Serikali za Mitaa ziweze kutekeleza shughuli zake ipasavyo.
3. Viongozi na Watendaji wa Serikali wahakikishe kuwa wanatoa maagizo yao kwa maandishi kama Sheria zinavyoelekeza ili kupatikana kielelezo halisi kilichotoa agizo juu ya jambo husika.

**Taarifa ya Matumizi**

Baraza la Manispaa Magharibi "B" kwa mwaka wa fedha 2019/2020 lilikadiriwa kutumia jumla ya Tsh. 11,819,090,274. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2020 jumla ya Tsh. 11,354,907,446.25 zilitumika sawa na asilimia 96 ya makadirio.

**Majibu**

Baraza la Manispaa Magharibi "B" halikuwa na maelezo ya moja kwa moja kuhusiana na taarifa za matumizi, hivyo, Baraza lilijibu hoja za Kamati kama zilivyotolewa.

**Uchunguzi wa Kamati**

Kamati ya LAAC imeridhika na majibu mbali mbali yaliyotolewa na Watendaji wa Baraza hili.

### 4.3.1 Kukosekana kwa Ukaguzi wa Vitabu vya Stakabadhi za Mapato

Ukaguzi umebaini kukosekanwa kwa vitabu vya risiti vilivyotumika kukusanya mapato hayo, kufanya hivyo ni kwenda na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma Namba 12 ya mwaka 2016.

**Majibu**

Vitabu vyote viko na tayari kwa ukaguzi.

| TAREHE | NAMBA YA KITABU | KIASI | MAELEZO | MAJIBU |
|---|---|---|---|---|
| 19/9/2021 | 72101-72200 | 100,000 | Stakabadhi za malipo hazikupatikana kwa ukaguzi | Vitabu vyote vipo na viko tayari kwa ukaguuzi |
| 18/9/2019 | 72601-72700 | 100,000 | Stakabadhi za malipo hazikupatikana kwa ukaguzi | Vitabu vyote vipo na viko tayari kwa ukaguuzi |
| 18/9/2019 | 72701-72800 | 100,000 | Stakabadhi za malipo hazikupatikana kwa ukaguzi | Vitabu vyote vipo na viko tayari kwa ukaguuzi |
| 20/9/2019 | 72601-73000 | 100,000 | Stakabadhi za malipo hazikupatikana kwa ukaguzi | Vitabu vyote vipo na viko tayari kwa ukaguuzi |
| 25/9/2019 | 7401-74300 | 100,000 | Stakabadhi za malipo | Vitabu vyote vipo na viko tayari kwa |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | hazikupatikana kwa ukaguzi | ukaguzi |
| 26/9/2019 | 74501-74600 | 100,000 | Stakabadhi za malipo hazikupatikana kwa ukaguzi | Vitabu vyote vipo na viko tayari kwa ukaguuzi |
| 27/9/2019 | 74801-74900 | 100,000 | Stakabadhi za malipo hazikupatikana kwa ukaguzi | Vitabu vyote vipo na viko tayari kwa ukaguuzi |
| 2/10/2019 | 76101-76200 | 100,000 | Stakabadhi za malipo hazikupatikana kwa ukaguzi | Vitabu vyote vipo na viko tayari kwa ukaguuzi |
| 17/7/2019 | 52001-52100 | 100,000 | Stakabadhi za malipo hazikupatikana kwa ukaguzi | Vitabu vyote vipo na viko tayari kwa ukaguuzi |
| 17/7/2019 | 52101-52200 | 100,000 | Stakabadhi za malipo hazikupatikana kwa ukaguzi | Vitabu vyote vipo na viko tayari kwa ukaguuzi |
| 18/7/2019 | 52501-52600 | 100,000 | Stakabadhi za malipo hazikupatikana kwa ukaguzi | Vitabu vyote vipo na viko tayari kwa ukaguuzi |
| 9/7/2019 | 43901-44000 | 100,000 | Stakabadhi za malipo hazikupatikana kwa ukaguzi | Vitabu vyote vipo na viko tayari kwa ukaguuzi |
| 11/7/2019 | 49201-49300 | 100,000 | Stakabadhi za malipo hazikupatikana kwa ukaguzi | Vitabu vyote vipo na viko tayari kwa ukaguuzi |
| 11/7/2019 | 49301-49400 | 100,000 | Stakabadhi za malipo hazikupatikana kwa ukaguzi | Vitabu vyote vipo na viko tayari kwa ukaguuzi |
| 30/7/2019 | 55201-55300 | 100,000 | Stakabadhi za malipo hazikupatikana kwa ukaguzi | Vitabu vyote vipo na viko tayari kwa ukaguuzi |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 9/8/2019 | 59801-59900 | 100,000 | Stakabadhi za malipo hazikupatikana kwa ukaguzi | Vitabu vyote vipo na viko tayari kwa ukaguuzi |
| 19/8/2019 | 63001-63100 | 100,000 | Stakabadhi za malipo hazikupatikana kwa ukaguzi | Vitabu vyote vipo na viko tayari kwa ukaguuzi |
| 22/8/2019 | 63401-63500 | 100,000 | Stakabadhi za malipo hazikupatikana kwa ukaguzi | Vitabu vyote vipo na viko tayari kwa ukaguuzi |
| 22/8/2019 | 63501-63600 | 100,000 | Stakabadhi za malipo hazikupatikana kwa ukaguzi | Vitabu vyote vipo na viko tayari kwa ukaguuzi |
| 2/9/2019 | 68201-68300 | 100,000 | Stakabadhi za malipo hazikupatikana kwa ukaguzi | Vitabu vyote vipo na viko tayari kwa ukaguuzi |
| 3/9/2019 | 68701-68800 | 100,000 | Stakabadhi za malipo hazikupatikana kwa ukaguzi | Vitabu vyote vipo na viko tayari kwa ukaguuzi |
| 10/9/2019 | 70201-70300 | 100,000 | Stakabadhi za malipo hazikupatikana kwa ukaguzi | Vitabu vyote vipo na viko tayari kwa ukaguuzi |
| 10/9/2019 | 70301-70400 | 100,000 | Stakabadhi za malipo hazikupatikana kwa ukaguzi | Vitabu vyote vipo na viko tayari kwa ukaguuzi |
| 10/9/2019 | 70601-70700 | 100,000 | Stakabadhi za malipo hazikupatikana kwa ukaguzi | Vitabu vyote vipo na viko tayari kwa ukaguuzi |
| 17/10/2019 | 79801-79900 | 100,000 | Stakabadhi za malipo hazikupatikana kwa ukaguzi | Vitabu vyote vipo na viko tayari kwa ukaguuzi |
| 18/10/2019 | 80101-80200 | 100,000 | Stakabadhi za malipo hazikupatikana | Vitabu vyote vipo na viko tayari kwa ukaguuzi |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | kwa ukaguzi | |
| 18/10/2019 | 80201-80300 | 100,000 | Stakabadhi za malipo hazikupatikana kwa ukaguzi | Vitabu vyote vipo na viko tayari kwa ukaguuzi |
| 11/11/2019 | 86501-86600 | 100,000 | Stakabadhi za malipo hazikupatikana kwa ukaguzi | Vitabu vyote vipo na viko tayari kwa ukaguuzi |
| 11/11/2019 | 86601-86700 | 100,000 | Stakabadhi za malipo hazikupatikana kwa ukaguzi | Vitabu vyote vipo na viko tayari kwa ukaguuzi |
| 12/11/2019 | 87601-87700 | 100,000 | Stakabadhi za malipo hazikupatikana kwa ukaguzi | Vitabu vyote vipo na viko tayari kwa ukaguuzi |
| 18/11/2019 | 88601-88700 | 100,000 | Stakabadhi za malipo hazikupatikana kwa ukaguzi | Vitabu vyote vipo na viko tayari kwa ukaguuzi |
| 18/11/2019 | 88801-88900 | 100,000 | Stakabadhi za malipo hazikupatikana kwa ukaguzi | Vitabu vyote vipo na viko tayari kwa ukaguuzi |
| 19/11/2019 | 88901-89000 | 100,000 | Stakabadhi za malipo hazikupatikana kwa ukaguzi | Vitabu vyote vipo na viko tayari kwa ukaguuzi |
| 21/11/2019 | 89701-89800 | 100,000 | Stakabadhi za malipo hazikupatikana kwa ukaguzi | Vitabu vyote vipo na viko tayari kwa ukaguuzi |
| 21/11/2019 | 89801-89900 | 100,000 | Stakabadhi za malipo hazikupatikana kwa ukaguzi | Vitabu vyote vipo na viko tayari kwa ukaguuzi |
| 20/1/2020 | 94501-94600 | 100,000 | Stakabadhi za malipo hazikupatikana kwa ukaguzi | Vitabu vyote vipo na viko tayari kwa ukaguuzi |
| 24/1/2020 | 95001- | 100,000 | Stakabadhi za | Vitabu vyote vipo |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | 95400 | | malipo hazikupatikana kwa ukaguzi | na viko tayari kwa ukaguuzi |
| 24/1/2020 | 95301-95400 | 100,000 | Stakabadhi za malipo hazikupatikana kwa ukaguzi | Vitabu vyote vipo na viko tayari kwa ukaguuzi |
| 3/3/2020 | 4701- 4800 | 100,000 | Stakabadhi za malipo hazikupatikana kwa ukaguzi | Vitabu vyote vipo na viko tayari kwa ukaguuzi |
| 9/4/2020 | 12401-12500 | 100,000 | Stakabadhi za malipo hazikupatikana kwa ukaguzi | Vitabu vyote vipo na viko tayari kwa ukaguuzi |
| 21/4/2020 | 14501-14600 | 100,000 | Stakabadhi za malipo hazikupatikana kwa ukaguzi | Vitabu vyote vipo na viko tayari kwa ukaguuzi |
| 24/4/2020 | 15501-15600 | 100,000 | Stakabadhi za malipo hazikupatikana kwa ukaguzi | Vitabu vyote vipo na viko tayari kwa ukaguuzi |
| 28/4/2020 | 16901-17000 | 100,000 | Stakabadhi za malipo hazikupatikana kwa ukaguzi | Vitabu vyote vipo na viko tayari kwa ukaguuzi |
| 8/5/2020 | 24801-24900 | 100,000 | Stakabadhi za malipo hazikupatikana kwa ukaguzi | Vitabu vyote vipo na viko tayari kwa ukaguuzi |
| 13/5/2020 | 26301-26400 | 100,000 | Stakabadhi za malipo hazikupatikana kwa ukaguzi | Vitabu vyote vipo na viko tayari kwa ukaguuzi |
| 13/5/2020 | 26401-26500 | 100,000 | Stakabadhi za malipo hazikupatikana kwa ukaguzi | Vitabu vyote vipo na viko tayari kwa ukaguuzi |
| 14/5/2020 | 27001-27100 | 100,000 | Stakabadhi za malipo hazikupatikana kwa ukaguzi | Vitabu vyote vipo na viko tayari kwa ukaguuzi |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 26/5/2020 | 32001-32100 | 100,000 | Stakabadhi za malipo hazikupatikana kwa ukaguzi | Vitabu vyote vipo na viko tayari kwa ukaguuzi |
| 8/6/2020 | 34901-35000 | 100,000 | Stakabadhi za malipo hazikupatikana kwa ukaguzi | Vitabu vyote vipo na viko tayari kwa ukaguuzi |
| 12/6/2020 | 35401-35500 | 100,000 | Stakabadhi za malipo hazikupatikana kwa ukaguzi | Vitabu vyote vipo na viko tayari kwa ukaguuzi |
| 15/6/2020 | 36601-36700 | 100,000 | Stakabadhi za malipo hazikupatikana kwa ukaguzi | Vitabu vyote vipo na viko tayari kwa ukaguuzi |
| 18/6/2020 | 37101-37200 | 100,000 | Stakabadhi za malipo hazikupatikana kwa ukaguzi | Vitabu vyote vipo na viko tayari kwa ukaguuzi |
| 19/6/2020 | 37400-37500 | 100,000 | Stakabadhi za malipo hazikupatikana kwa ukaguzi | Vitabu vyote vipo na viko tayari kwa ukaguuzi |
| 25/6/2020 | 38401-38500 | 100,000 | Stakabadhi za malipo hazikupatikana kwa ukaguzi | Vitabu vyote vipo na viko tayari kwa ukaguuzi |
| 30/6/2020 | 39701-39800 | 100,000 | Stakabadhi za malipo hazikupatikana kwa ukaguzi | Vitabu vyote vipo na viko tayari kwa ukaguuzi |
| 30/6/2020 | 39801-39900 | 100,000 | Stakabadhi za malipo hazikupatikana kwa ukaguzi | Vitabu vyote vipo na viko tayari kwa ukaguuzi |
| 30/6/2020 | 40101-40200 | 100,000 | Stakabadhi za malipo hazikupatikana kwa ukaguzi | Vitabu vyote vipo na viko tayari kwa ukaguuzi |
| **JUMLA** | | **5,700,000** | Stakabadhi za malipo hazikupatikana | Vitabu vyote vipo na viko tayari kwa ukaguuzi |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | kwa ukaguzi | |

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**
Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC ilibaini yafuatayo:

1. Mdhibiti na Mkagzui Mkuu wa Hesabu za Serikali anavyowasilisha barua ya kuomba kufanya ukaguzi (engagement letter), Taasisi huwa hazianzi kujiandaa kwa kuviweka tayari vielelezo vya mwaka husika na ndio sababu inayopelekea Mkaguzi kukosa baadhi ya nyaraka anazozihitaji.
2. Baadhi ya vitabu vilivyokaguliwa na Kamati vinaonesha kuwa ni vipya mfano, kitabu cha Abdul Majid Ali chenye karatasi kuanzia 39701 – 39800 cha tarehe 06/04/2020.

   Hata hivyo, kutokana na uhaba wa muda Kamati haikuweza kuvipitia vitabu vyote.

Pamoja na hayo, hoja hii imebaki kama ilivyo kwa kuwa havikuwasilishwa kwa wakati kwa Mkaguzi Mkuu.

### 4.3.2 Dosari katika Ukusanyaji wa Mapato ya Minara Tsh. 78,174,340.34

Ukaguzi umebaini dosari zifuatazo katika ukusanyaji wa mapato hayo: -

- Ukaguzi haukupatiwa Utaratibu wa ushindani uliotumika kumpata wakala huyo wa ukusanyaji wa mapato wa niaba ya Manispaa ya Magharib B, kufanya hivyo ni kwenda kinyume cha sheria ya manunuzi na uondoshaji wa mali za umma sheria namba 11 ya mwaka 2016.

- Ukaguzi haukupatiwa Mkataba kati ya Baraza la Manispaa ya Wilaya ya Magharibi B ambao unaonyesha makubaliano ya pande mbili katika kazi ya ukusanyaji wa mapato hayo, kufanya hivyo ni kwenda kinyume na sheria ya manunuzi na uondoshaji wa mali za Umma sheria namba 11 ya mwaka 2016

- Ukaguzi haukupatiwa taarifa ya kibenki ya kampuni ya Aljumra ili kujiridhisha asili ya makusanyo halisi ambayo yanakusanywa kwa mwezi husika ili kubaini usahihhi wa kiwango kilichoripotiwa.

**Majibu**
Utaratibu uliotumika kupitia Wizara ya Nchi, Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Malum za SMZ ambapo kilifanyika kikao cha Wakurugenzi wote wa Serikali za Mitaa na kukubaliana kumtumia Wakala huyo ili kukusanya deni lililokuwa la muda mrefu katika kampuni za Minara.
Mkataba upo na tayari kwa ukaguzi.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC imebaini yafuatayo:

1. Serikali za Mitaa zilipewa tu agizo na Wizara yao ya kuitumia Kampuni ya Al jumura katika kusimamia shughuli za minara jambo lililopelekea kukiukwa kwa matakwa ya Sheria ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Namba 11 ya mwaka 2016.
2. Mapato ya minara hivi sasa yanakusanywa na Wakala wa Miundombinu ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano Zanzibar.

Ili kasoro kama hizi zisijitokeze tena katika siku zijazo, Kamati ya LAAC inaishauri Serikali Kuu kutoa maagizo yake kwa kuzingatia Sheria za nchi.

Kwa msingi huo, hoja hii imebaki kama ilivyo kwa kuwa taratibu za kuipata Kampuni ya Al jumura zimekiuka matakwa ya Sheria.

**4.3.3**: **Vifaa ambavyo havijaingizwa kwenye Daftari la Ghalani Tsh. 72,928,798**

Ukaguzi umebaini Baraza la Manispaa Magharibi "B" limefanya manunuzi ya vifaa mbali mbali vyenye thamani ya Tsh. 72,928,798 kwa ajili ya matumizi ya Afisi. Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kuwa vifaa hivyo havijarikodiwa katika daftari la ghalani. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Namba 11 ya mwaka 2016.

**Majibu**

| TAREHE | NAMBARI YA HATI YA MALIPO | JUMLA YA FEDHA ILIYOLIPWA | ALIYELIPWA | INVOICE | MAELEZO | MAJIBU |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 12/3/2020 | 34/3 | 4,000,000 | SKOTCH GENERAL SUPPLIES CO.LTD | T/INVOICE 054 12/03/2020 Rpts 093 ya 13/3/2020 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya zoezi la usafi na uzoaji wa taka katika majaa yasiyorasmi na yaliyorasmi kupelekwa | Uzoaji wa taka katika majaa ni kazi ya huduma ambayo alipewa msambazaji na kuifanya yeye mwenyewe kazi |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | kibele | hiyo. |
| 8/4/2020 | 2/4 | 5,631,068 | JAWAJA AUTO PARTS | Invoice 3063 ya 2/4/2020 Rpts 0289 ya 8/4/2020 | Ikiwa ni malipo ya ununuzi wa 1pc Gear box mashine Assy ya gari SMZ 368B Fusso | Imeshaingizwa na tayari kwa ukaguzi. |
| 1/4/2020 | 4/3 | 3,160,194 | SULEIMAN ISMAIL | Invoice 00175 ya 11/06/2019 Rpts 00095 ya 2/4/2020 | Ikiwa ni malipo ya 350pcs Matofali 4 trip Mchanga mweupe | Imeshaingizwa na tayari kwa ukaguzi |
| 3/4/2020 | 14/4 | 8,525,000 | JUSTIDIA TRADERS | | Ikiwa ni malipo ya Ufukuzaji wa dawa vituo vya Afya hazijatajwa | Huduma ya Upigaji wa dawa kipindi cha corona alifanya msambazaji mwenyewe |
| 15/4/2020 | 31 /4 | 4,582,524 | SKOTCH GENERAL SUPPLIES CO.LTD | | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya Ufukizaji wa dawa katika majaa | Huduma ya Upigaji wa dawa kipindi cha corona alifanya msambazaji mwenyewe |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 27/4/2020 | 74/4 | 5,882,353 | ABDULRAHMAN ISMAIL VUAI | T/INVOICE 9776 24/10/2020 | Ikiwa na malipo kwa ununuzi wa 1pc gear box engine Assy ya Z 347 FC | Imeshaingizwa stoo na tayari kwa ukaguzi |
| 24/3/2020 | 72/3 | 4,854,369 | ABDULSALAM BUILDING TZ LIMITED | 0361 11/3/2020 Rpts 0261 | Malipo ya kifusi Trip 14 kupitia Mfuko wa Maendeleo Wadi ya Fuoni kitaanzia njia tatu kwa Mashea mpaka Birikini | Imeshaingizwa stoo na tayari kwa ukaguzi |
| 15/4/2020 | 32/2 | 12,671,990 | ABDULSALAM BUILDING TZ LIMITED | Invoice 0359 of 15/2/2020 Rpts 0263ya 15.4.2020 | Ikiwa ni malipo ya ununuzi na usambazaji wa kifusi katika soko la Mombasa | Huduma ya mategenezo ya njia alifanya msambazaji mwenyewe |
| | 30/5 | 4,500,000 | SKOTCH GENERAL SUPPLIES | Invoice namba 0320 tarehe 15.5.2020 risiti namba 085 tarehe haipo | Malipo ya marekebisho ya jengo la kituo cha Afya magirisi kwa utiaji wa rangi, kusafisha tarazo, na upigaji wa | Marekebisho ya jengo la kituo cja afya magirisi kwa utiaji wa rangi, kusafisha tarazo, na upigaji wa vanish |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | vannish | alifanya msambazaji mwenyewe |
| 9/8/2020 | 28/8 | 3,800,000 | JAWABA AUTO PARK | Risiti 456 Hundi 001833 Inv 398 | Ikiwa ni malipo ya deni la gari iliyofanyiwa over Hall SMZ 515Fuso | Imeshaingizwa stoo na tayari kwa ukaguzi |
| 29/1/2020 | 17/2 | 1,940,000 | SKOTCH GENERAL SUPPLIES | Ankara 089, risit 065 | Ikiwa ni ununuzi wa vifaa kwa ajili ya matumizi ya kuanzisha shamba darasa la malisho ya mifugo shehia ya maungani | Imeshaingizwa stoo na tayari kwa ukaguzi |
| 22/1/2020 | 59/1 | 4,161,300 | ABDULSALAM BUILDING TZ LTD | Risit namba 0227 | Ununuzi wa vifaa vya Ujenzi wa skuli ya chekechea fumba (Wadi ya maungani) | Imeshaingizwa stoo na tayari kwa ukaguzi |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 28.1.2020 | 101/1 | 4,850,000 | ADAM ZUBEIR CHANDE | Ankara 073 risit 069 | Ununuzi wa vifaa vya Ujenzi wa kituo cha daladala mbweni | Ujenzi wa kituo cha daladala Mbweni alifanya msambazaji mwenyewe |

Uchunguzi wa Kamati

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC ilibaini yafuatayo:

1. Baada ya kupitia barua ya maombi ya fedha ya tarehe 12 Machi, 2020, baadhi ya malipo yaliyofanywa yalihusika moja kwa moja na utoaji wa huduma, hivyo, hakuna vifaa vilivyonunuliwa vilivyohitaji kuingizwa kwenye daftari la ghalani kama ilivyoandikwa kwenye Ripoti ya Mkaguzi Mkuu. Malipo yenyewe ni kama ifuatavyo:

    a. Kipengele namba 1 kinachohusiana na malipo ya Tsh. 4,000,000 kwa Kampuni ya Skotch General Supplies Co.Ltd ilikuwa ni malipo ya zoezi la usafi na uzoaji wa taka katika majaa yasiyorasmi na yaliyorasmi kupelekwa Kibele;

    b. Kipengele namba 5 kinachohusiana na malipo ya Tsh. 4,582,524 kwa Kampuni ya Skotch General Supplies Co.Ltd ilikuwa ni malipo kwa ajili ya ufukizaji wa dawa katika majaa; na

    c. Kipengele namba 8 kinachohusiana na malipo ya Tsh. 12,671,990 kwa Abdulsalam Building Tanzania Limited ilikuwa ni malipo ya ununuzi na usambazaji wa kifusi katika soko la Mombasa.

2. Baadhi ya shughuli zilifanyika siku za mapumziko (week end), hivyo, Mtunza Ghala hakuweza kujua shughuli zilizofanyika katika siku hizo.

Mapendekezo ya Kamati

Ili kasoro kama hizo zisijitokeze tena katika siku zijazo Kamati ya LAAC ilipendekeza yafuatayo:

1. Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali iwe makini wakati wa kuandika ripoti yake ili kuondosha lawama zisizo na msingi kwa Wakaguliwa.

2. Mtunza Ghala wa Baraza la Manispaa Magharibi “B” afuatilie kwa karibu majukumu yake ili aweze kujua matukio yote yaliyofanyika kwa siku.

### 4.3.4 Malipo yasiyokuwa na vielelezo Tsh. 43,552,105

Baraza la Manispaa Magharibi "B" limefanya malipo ya Tsh. 43,552,105 kwa ajili ya kugharamia shughuli mbali mbali za Baraza. Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kukosekana kwa vielelezo vya matumizi hayo. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu cha 34(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma Namba 12 ya mwaka 2016.

**Majibu**

| TAREHE | NAMBARI YA HATI YA MALIPO | ALIYELIPWA | JUMLA YA FEDHA ILIYOLIPWA | MAELEZO | MAJIBU |
|---|---|---|---|---|---|
| 7/7/2019 | 4/7 | BARAZA LA MANISPAA MAGHARIB B | 3,472,500 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya safari ya kikazi nje ya nchi katika mafunzo ya muda mfupi | Pesa za kujikimu nje ya Nchi hazina marejesho |
| 15/7/2019 | 21/7 | BARAZA LA MANISPAA MAGHARIB B | 2,130,000 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya posho la safari | Vielelezo vipo na viko tayari kwa ukaguzi |
| 22/8/2019 | 58/7 | BARAZA LA MANISPAA MAGHARIB B | 2,000,000 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya Ujenzi wa choo cha kwale pamoja na uchukuzi wa matofali | Malipo hayo alilipwa fundi mwenyewe na mkataba upo wa malipo hayo |
| 29/7/2019 | 33/7 | BARAZA LA MANISPAA MAGHARIB B | 2,000,000 | Ikiwa ni malipo ya watu wa bustani barabara ya Uwanja wa Ndege | Malipo haya yamefanyw a kwa mkataba na uko tayari kwa ukaguzi |
| 21/08/201 9 | | BARAZA LA MANISPAA MAGHARIB B | 19,299,605 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya mategenezo ya mashimo | Vielelezo vipo na viko tayari kwa ukaguzi |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | ya karo na kisima katika kituo cha Afya Bwefum pamoja na mategenezo ya nyumba ya daktari kituo cha Afya Bwefum | |
| 28/08/2019 | 72/8 | BARAZA LA MANISPAA MAGHARIB B | 12,650,000 | Ikiwa ni malipo ya fedha kwa ajili ya safari ya kikazi kwa kamati mbili, kamati ya fedha na kamati ya Mipango Miji | Tiketi zipo na ziko tayari kwa ukaguzi |

**Uchunguzi wa Kamati**

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC ilibaini yafuatayo:

1. Katika Hati ya Malipo namba 72/8 inayohusiana na tiketi za safari, idadi ya tiketi hizo haikukamilika.

2. Hati ya Malipo namba 58/7 inayohusiana na malipo ya ujenzi wa choo cha Kwale pamoja na uchukuzi wa matofali, namba sahihi ya namba hiyo ni 57/7 sio 58/7 kama ilivyoandikwa kwenye Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Hii ni kutokana na kuwa malipo yanayohusiana na Hati ya Malipo namba 58/7 ni malipo ya mwezi mwengine.

   Kwa mnasaba huo, kiwango cha fedha kilichoandikwa kwenye Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kitabadilika kutokana na mabadiliko hayo.

**Mapendekezo ya Kamati**

Kutokana na uchunguzi huo Kamati ya LAAC ilipendekeza yafuatayo:

1. Katibu wa Kamati husika ahakikishe kuwa anazikusanya tiketi za safari za Wajumbe wake mara wanavyofika safari.
2. Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali iwe makini wakati wa kuandika ripoti yake ili kuondosha lawama zisizo na msingi kwa

Wakaguliwa.

### 4.3.5 Kukosekana kwa Mikataba Tsh. 22,476,000

Ukaguzi umebaini Baraza la Manispaa Magharibi "B" limefanya malipo ya Tsh. 22,476,000 kwa ajili ya kugharamia vikundi mbali mbali vya Usafi na Ulinzi.

Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kukosekana kwa mikataba ya vikundi hivyo, ili kuweza kujiridhisha kiasi halisi cha malipo, muda na taratibu za malipo ya mikataba hiyo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Ununuzi na Uondoshwaji wa Mali za Umma Namba 11 ya mwaka 2016.

**Majibu**

| TAREHE | NAMBA YA HATI | NAMBA YA HUNDI | JUMLA YA FEDHA | ALIYELIPWA | MAELEZO | MAJIBU |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 2/3/2020 | 11/3 | TRANSFER | 2,000,000 | JUMUIYA YA KIKUNDI CHA TUMEFIKA | Malipo kwa ajili ya kikundi cha Tumefika kwa mwezi wa Febuari 2020 | Mkataba upo na tayari kwa ukaguzi |
| 17/3/2020 | 59/3 | 2360 | 1,952,000 | SUBIRA MAKAME MUSSA | Malipo kwa ajili ya kikundi cha usafi Shehia ya Pangawe | Mkataba upo na tayari kwa ukaguzi |
| 1/4/2020 | 4/01 | TRANSFER | 1,100,000 | JUMUIYA YA MAZINGIRA MOMBASA | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya kuwalipa wafanyakazi wa kikundi cha Mazingira Mombasa | Mkataba upo na tayari kwa ukaguzi |
| 27/4/2020 | 07/05 | 2498 | 3,000,000 | WAKALA WA ULINZI JKU | Ikiwa ni malipo kwa huduma ya Ulinzi | Mkataba upo na tayari kwa ukaguzi |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 25/3 | 2332 | 1,500,000 | WAKALA WA ULINZI JKU | Ikiwa ni malipo kwa huduma ya Ulinzi | Mkataba upo na tayari kwa ukaguzi |
| | 4/3 | 2295 | 1,500,000 | WAKALA WA ULINZI JKU | Ikiwa ni malipo kwa huduma ya Ulinzi | Mkataba upo na tayari kwa ukaguzi |
| | 05/06 | 2545 | 1,500,000 | WAKALA WA ULINZI JKU | Ikiwa ni malipo kwa huduma ya Ulinzi | Mkataba upo na tayari kwa ukaguzi |
| | 12/5 | 2545 | 1,500,000 | WAKALA WA ULINZI JKU | Ikiwa ni malipo kwa huduma ya Ulinzi | Mkataba upo na tayari kwa ukaguzi |
| | 12/5 | 2505 | 1,440,000 | ZANZIBAR MODIFYING SECURITY SERVICE | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya huduma ya Ulinzi katika kampuni | Mkataba upo na tayari kwa ukaguzi |
| | 73/05 | TT | 1,100,000 | JUMUIYA YA MAZINGIRA KWA MCHINA ZANZIBAR | Malipo kwa ajili ya posho la vijana wa sokoni | Mkataba upo na tayari kwa ukaguzi |
| | 8/06 | TT | 1,100,000 | JUMUIYA YA MAZINGIRA MOMBASA ZNZ | Malipo kwa ajili ya posho la vijana wa sokoni | Mkataba upo na tayari kwa ukaguzi |
| | 04/11 | TT | 1,784,000 | JUMUIYA YA MAZINGIRA MOMBASA ZANZIBAR | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya huduma za usafi | Mkataba uko na tayari kwa ukaguzi |
| | 02/11 | 2004 | 1,500,00 | WAKALA | Ikiwa ni | Mkatab |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | 0 | WA ULINZI JKU | malipo kwa ajili ya Huduma za Ulinzi | a uko na tayari kwa ukaguzi |

**Uchunguzi wa Kamati**
Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC ilibaini yafuatayo:

1. Hati ya Malipo namba 7/5 inayohusiana na malipo kwa huduma ya Ulinzi Tsh. 3,000,000 imerudiwa mara mbili. Hivyo, kiwango cha fedha kilicholalamikiwa kitapungua na kufikia Tsh. 19,476,000.
2. Wakati wa ukaguzi mikataba husika ilikuwa ofisini kwa Mkurugenzi wa Baraza ambaye hakuwepo kipindi chote cha ukaguzi.

**Mapendekezo ya Kamati**
Kutokana na uchunguzi huo Kamati ya LAAC ilipendekeza yafuatayo:
1. Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali iwe makini wakati wa kuandika ripoti yake ili kuondosha lawama zisizo na msingi kwa Wakaguliwa.
2. Baraza la Manispaa Magharibi "B" lianzishe daftari la mikataba (Contract Register), ili Baraza liweze kujua katika mwaka husika linafuatilia mikataba mingapi?.

### 4.3.6 Malipo ya mishahara kwa watumishi ambao mikataba yao imeshamaliza muda Tsh. 8,371,000

Ukaguzi umebaini kuwepo kwa wafanyakazi wa Mkataba ambao Mikataba yao ishamaliza muda kisheria jambo ambalo linaweza kupelekea kuwakosesha haki zao za msingi pale ambapo linapojitokeza tatizo la kisheria ambalo litahusisha na namna ya uajiri wake. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Utumishi wa Umma Namba 2 ya mwaka 2011.

**Majibu**

| JINA LA MFANYAKAZI | AINA YA KAZI | KIWANGO CHA MSHAHARA | TAREHE YA KUANZA MKATABA | TAREHE YA KUMALIZA MKATABA | MAJIBU |
|---|---|---|---|---|---|
| Sabra Maulid Mtoro | Karani Mapato | 200,000 | 1/1/2019 | 30/6/2019 | Mikataba imeshapitiwa na |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | imeshafungwa upya kwa wafanyakazi wote wa mkataba na ipo tayari kwa ukaguzi |
| Maryam Bakari Mussa | M/sheria | 200,000 | 8/1/2018 | 8/1/2019 | Mikataba imeshapitiwa na imeshafungwa upya kwa wafanyakazi wote wa mkataba na ipo tayari kwa ukaguzi |
| Radhiya Nassir Alawi | Karani Mapato | 200,000 | 1/1/2019 | 30/6/2019 | Mikataba imeshapitiwa na imeshafungwa upya kwa wafanyakazi wote wa mkataba na ipo tayari kwa ukaguzi |
| Zainab Khamis Mbarouk | Karani Mapato | 110,000 | 1/1/2019 | 30/6/2010 | Mikataba imeshapitiwa na imeshafungwa upya kwa wafanyakazi wote wa mkataba na ipo tayari kwa ukaguzi |
| Rehama Othman Ali | Karani Mapato | 110,000 | 1/1/2019 | 30/6/2019 | Mikataba imeshapitiwa na imeshafungwa upya kwa wafanyakazi |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | wote wa mkataba na ipo tayari kwa ukaguzi |
| Fatma Muhidini Nanyup | Karani Mapato | 110,000 | 1/1/2019 | 30/6/2019 | Mikataba imeshapitiwa na imeshafungwa upya kwa wafanyakazi wote wa mkataba na ipo tayari kwa ukaguzi |
| Shani Khamis Uleid | Karani Mapato | 200,000 | 1/1/2019 | 30/6/2019 | Mikataba imeshapitiwa na imeshafungwa upya kwa wafanyakazi wote wa mkataba na ipo tayari kwa ukaguzi |
| Amina Ramadhan Iddi | Karani Mapato | 200,000 | 1/1/2019 | 30/6/2019 | Mikataba imeshapitiwa na imeshafungwa upya kwa wafanyakazi wote wa mkataba na ipo tayari kwa ukaguzi |
| Fatma Abdalla Hassan | Tehama | 350,000 | 1/1/2019 | 30/6/2019 | Mikataba imeshapitiwa na imeshafungwa upya kwa wafanyakazi wote wa mkataba na ipo tayari kwa |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | ukaguzi |
| Asha Salum Matunda | Msafishaji | 110,000 | 1/1/2019 | 30/6/2019 | Mikataba imeshapitiwa na imeshafungwa upya kwa wafanyakazi wote wa mkataba na ipo tayari kwa ukaguzi |
| Fatma Abdalla Ali | Msafishaji | 110,000 | 1/1/2019 | 30/6/2019 | Mikataba imeshapitiwa na imeshafungwa upya kwa wafanyakazi wote wa mkataba na ipo tayari kwa ukaguzi |
| Amina Nuhu Ali | Karani Mapato | 400,000 | 1/1/2019 | 30/6/2019 | Mikataba imeshapitiwa na imeshafungwa upya kwa wafanyakazi wote wa mkataba na ipo tayari kwa ukaguzi |
| Maryam Khamis Nassor | Karani Mapato | 200,000 | 1/1/2019 | 30/6/2019 | Mikataba imeshapitiwa na imeshafungwa upya kwa wafanyakazi wote wa mkataba na ipo tayari kwa ukaguzi |
| Asha salum Moh’d | Karani Mapato | 200,000 | 1/1/2019 | 30/6/2019 | Mikataba imeshapitiwa |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | na imeshafungwa upya kwa wafanyakazi wote wa mkataba na ipo tayari kwa ukaguzi |
| Chausiku Abdalla Sama | Karani Mapato | 200,000 | 1/1/2019 | 30/6/2019 | Mikataba imeshapitiwa na imeshafungwa upya kwa wafanyakazi wote wa mkataba na ipo tayari kwa ukaguzi |
| Maryam suleman Haji | Karani Mapato | 200,000 | 1/1/2019 | 30/6/2019 | Mikataba imeshapitiwa na imeshafungwa upya kwa wafanyakazi wote wa mkataba na ipo tayari kwa ukaguzi |
| Kiwaliki Vuai Hassan | Karani Mapato | 200,000 | 1/1/2019 | 30/6/2019 | Mikataba imeshapitiwa na imeshafungwa upya kwa wafanyakazi wote wa mkataba na ipo tayari kwa ukaguzi |
| Najma Issa Fatawi | Karani Mapato | 180,000 | 1/1/2019 | 30/6/2019 | Mikataba imeshapitiwa na imeshafungwa upya kwa |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | wafanyakazi wote wa mkataba na ipo tayari kwa ukaguzi |
| Aziza abdalla Hassan | Karani Mapato | 200,000 | 1/1/2019 | 30/6/2019 | Mikataba imeshapitiwa na imeshafungwa upya kwa wafanyakazi wote wa mkataba na ipo tayari kwa ukaguzi |
| Jina Hamdu Shaka | Karani Mapato | 110,000 | 1/1/2019 | 30/6/2019 | Mikataba imeshapitiwa na imeshafungwa upya kwa wafanyakazi wote wa mkataba na ipo tayari kwa ukaguzi |
| Ana Selevesta Andrea | Karani Mapato | 110,000 | 1/1/2019 | 30/6/2019 | Mikataba imeshapitiwa na imeshafungwa upya kwa wafanyakazi wote wa mkataba na ipo tayari kwa ukaguzi |
| Mwanakhamis Iddi Khamis | Karani Mapato | 200,000 | 1/1/2019 | 30/6/2019 | Mikataba imeshapitiwa na imeshafungwa upya kwa wafanyakazi wote wa mkataba na |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | ipo tayari kwa ukaguzi |
| Fatma Ali Jeicha | Karani Mapato | 180,000 | 1/1/2019 | 30/6/2019 | Mikataba imeshapitiwa na imeshafungwa upya kwa wafanyakazi wote wa mkataba na ipo tayari kwa ukaguzi |
| Somoe Rashid ali | Usafishaji | 110,000 | 1/1/2019 | 30/6/2019 | Mikataba imeshapitiwa na imeshafungwa upya kwa wafanyakazi wote wa mkataba na ipo tayari kwa ukaguzi |
| Fatma Tongoa Issa | Karani Mapato | 110,000 | 1/1/2019 | 30/6/2019 | Mikataba imeshapitiwa na imeshafungwa upya kwa wafanyakazi wote wa mkataba na ipo tayari kwa ukaguzi |
| Ali Othman Ali | Fundi Magari | 110,000 | 1/1/2019 | 30/6/2019 | Mikataba imeshapitiwa na imeshafungwa upya kwa wafanyakazi wote wa mkataba na ipo tayari kwa ukaguzi |
| Jaha Faki | Usafishaji | 110,000 | 1/1/2019 | 30/6/2019 | Mikataba |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| KHalfan | | | | | imeshapitiwa na imeshafungwa upya kwa wafanyakazi wote wa mkataba na ipo tayari kwa ukaguzi |
| Hafsa Mohammed Makame | Tehama | 300,000 | 1/1/2019 | 30/6/2019 | Mikataba imeshapitiwa na imeshafungwa upya kwa wafanyakazi wote wa mkataba na ipo tayari kwa ukaguzi |
| Ali Mwinyi Mwalim | Fundi Magari | 110,000 | 1/1/2019 | 30/6/2019 | Mikataba imeshapitiwa na imeshafungwa upya kwa wafanyakazi wote wa mkataba na ipo tayari kwa ukaguzi |
| Othman shaaban Mabala | Mkaguzii | 110,000 | 1/1/2019 | 30/6/2019 | Mikataba imeshapitiwa na imeshafungwa upya kwa wafanyakazi wote wa mkataba na ipo tayari kwa ukaguzi |
| Abdul-Majid Ali Salum | Karani Mapato | 110,000 | 1/1/2019 | 30/6/2019 | Mikataba imeshapitiwa na imeshafungw |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | a upya kwa wafanyakazi wote wa mkataba na ipo tayari kwa ukaguzi |
| Kassimu Suleiman Khamis | Usafisahji | 110,000 | 1/1/2019 | 30/6/2019 | Mikataba imeshapitiwa na imeshafungwa upya kwa wafanyakazi wote wa mkataba na ipo tayari kwa ukaguzi |
| Yussuf Faki Khamis | Fundi Magari | 110,000 | 1/1/2019 | 30/6/2019 | Mikataba imeshapitiwa na imeshafungwa upya kwa wafanyakazi wote wa mkataba na ipo tayari kwa ukaguzi |
| Ramadhan Haji Khamis | Konda | 110,000 | 1/1/2019 | 30/6/2019 | Mikataba imeshapitiwa na imeshafungwa upya kwa wafanyakazi wote wa mkataba na ipo tayari kwa ukaguzi |
| Abeid Juma Haji | Fundi Magari | 250,000 | 1/1/2019 | 30/6/2019 | Mikataba imeshapitiwa na imeshafungwa upya kwa wafanyakazi wote wa |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | mkataba na ipo tayari kwa ukaguzi |
| Mohamed Fadhil Machano | Majenzi | 300,000 | 1/1/2019 | 30/6/2019 | Mikataba imeshapitiwa na imeshafungwa upya kwa wafanyakazi wote wa mkataba na ipo tayari kwa ukaguzi |
| Mohammed Abdalla Juma | Karani Mapato | 200,000 | 1/1/2019 | 30/6/2019 | Mikataba imeshapitiwa na imeshafungwa upya kwa wafanyakazi wote wa mkataba na ipo tayari kwa ukaguzi |
| Maulid Amour Pandu | Mkaguzi Majenzi | 250,000 | 1/1/2019 | 30/6/2019 | Mikataba imeshapitiwa na imeshafungwa upya kwa wafanyakazi wote wa mkataba na ipo tayari kwa ukaguzi |
| Othman Moh'd Othman | Ulinzi | 200,000 | 1/1/2019 | 30/6/2019 | Mikataba imeshapitiwa na imeshafungwa upya kwa wafanyakazi wote wa mkataba na ipo tayari kwa ukaguzi |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Abdulrazak Mwinyi Mussa | Usafishaji | 110,000 | 1/1/2019 | 30/6/2019 | Mikataba imeshapitiwa na imeshafungwa upya kwa wafanyakazi wote wa mkataba na ipo tayari kwa ukaguzi |
| Kombo Said Kombo | Dereva | 190,000 | 1/1/2019 | 30/6/2019 | Mikataba imeshapitiwa na imeshafungwa upya kwa wafanyakazi wote wa mkataba na ipo tayari kwa ukaguzi |
| Zubaeir Makame Shamata | Dereva | 110,000 | 1/1/2019 | 30/6/2019 | Mikataba imeshapitiwa na imeshafungwa upya kwa wafanyakazi wote wa mkataba na ipo tayari kwa ukaguzi |
| Muslim A. Muslim | Msimamizi maegesho | 200,000 | 1/1/2019 | 30/6/2019 | Mikataba imeshapitiwa na imeshafungwa upya kwa wafanyakazi wote wa mkataba na ipo tayari kwa ukaguzi |
| Salum Rashid Salum | Msimamizi maegesho | 200,000 | 1/1/2019 | 30/6/2019 | Mikataba imeshapitiwa na |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | imeshafungwa upya kwa wafanyakazi wote wa mkataba na ipo tayari kwa ukaguzi |
| Talib Saleh Khamis | Msimamizi wa maegesho | 200,000 | 1/1/2019 | 30/6/2019 | Mikataba imeshapitiwa na imeshafungwa upya kwa wafanyakazi wote wa mkataba na ipo tayari kwa ukaguzi |
| Murid Ali Jecha | Msimamiz wa maegesho | 200,000 | 1/1/2019 | 30/6/2019 | Mikataba imeshapitiwa na imeshafungwa upya kwa wafanyakazi wote wa mkataba na ipo tayari kwa ukaguzi |
| Juma Adam Daud | Dereva | 110,000 | 1/1/2019 | 30/6/2019 | Mikataba imeshapitiwa na imeshafungwa upya kwa wafanyakazi wote wa mkataba na ipo tayari kwa ukaguzi |
| Mtwana Kheir Mtwana | Mkaguzi | 160,000 | 1/1/2019 | 30/6/2019 | Mikataba imeshapitiwa na imeshafungwa upya kwa wafanyakazi |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | wote wa mkataba na ipo tayari kwa ukaguzi |

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**
Kamati ya LAAC imeridhika na majibu ya Baraza la Manispaa Maghribi “B”.

## 4.4 HALMASHAURI YA WILAYA YA KASKAZINI “A”

**Taarifa ya Mapato**
Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini “A” kwa mwaka wa fedha 2019/2020 lilikadiriwa kukusanya jumla ya Tsh. 649,225,700 kutoka katika vyanzo vya mapato ya Halmashauri.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2020 Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini “A” lilikusanya Tsh. 711,501,226 zilikusanywa kutoka katika vyanzo vya mapato ya Baraza sawa na asilimia 109 ya makadirio.

**Majibu**
Baraza la Mji Kaskazini “A” halikuandaa majibu ya moja kwa moja juu ya Taarifa ya Mapato na badala yake ilijibu maswali ya Kamati yaliyoulizwa.

**Uchunguzi wa Kamati**
Kamati ya LAAC ilitaka kujua sababu zilizopelekea Baraza la Mji Kaskazini “A” kukusanya mapato zaidi ya asilimia 100, ambapo Watendaji wa Baraza walieleza sababu zifuatazo:

1. Kuongezeka kwa idadi ya wafanyakazi
2. Kuongezeka kwa mashine za kukusanyia mapato na kuimarisha mfumo
3. Kuongezeka kwa vyanzo vipya vya mapato
4. Kuvifikia vyanzo vilivyokuwepo

Vile vile, Kamati ya LAAC ilibaini kuwa katika mwaka wa fedha 2019/2020 Baraza la Mji Kaskazini “A” lilikadiria bajeti ya mapato chini ya kiwango cha mwaka wa fedha uliopita (2018/2019). Hii ni kutokana na kuwa katika mwaka 2018/2019 Baraza hili lilikadiria Tsh. 698,890,348 na mwaka 2019/2020 lilikadiria Tsh. 649,225,700 kitendo

ambacho ni kinyume na taratibu za kihesabu.

Pamoja na hayo, Kamati ilibaini kuwa kuna tofauti ya taarifa za mapato kwenye Taarifa ya Hesabu za Mwisho wa Mwaka kwenye ukurasa wa 7 na 22. Kutokana na hali hiyo Kamati ya LAAC iliomba ufafanuzi kwa Mtendaji wa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali aliyefuatana na Kamati kwa kuwa Taarifa ya Hesabu ya kila mwaka huwasilishwa kwa Mkaguzi Mkuu kwa mujibu wa kifungu cha 119(1) kwa hatua zake.

Mtendaji huyo alikiri kuwa Taarifa za mapato zinatofautiana katika nyaraka hiyo, kwa msingi huo, Kamati ya LAAC ilishindwa kuendelea kuyachambua mapato na matumizi ya Baraza la Mji Kaskazini "A" kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kutokana na kasoro hiyo. Hii ni kutokana na kuwa hakukuwa na Mtendaji yeyote wa Baraza aliyeweza kutoa maelezo juu ya kasoro hiyo zaidi ya kueleza tu kuwa watendaji anaohusika moja kwa moja ambao ni Mkurugenzi wa Bazara yupo masomoni Malaysia na Mhasibu yupo Pemba kwenye mafunzo maalum.

### Mapendekezo ya Kamati

Ili kasoro kama hizo zisijitokeze tena katika siku zijazo Kamati ya LAAC ilipendekeza yafuatayo:

1. Baraza la Mji Kaskazini "A" kuwa makini wakati wa kuandaa Taarifa za Hesabu za Mwisho wa Mwaka kwa kuwa Taarifa hizo zinatumika katika kupanga mipango mbali mbali ya Serikali hivyo, haipendezi Taarifa hiyo kuwa taarifa zenye utata.

2. Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuwa makini wakati wa kuzipitia Taarifa za Hesabu za Mwisho wa Mwaka kwa kuwa Taarifa hizo zinatumika katika kupanga mipango mbali mbali ya Serikali hivyo, haipendezi Taarifa hiyo kuwa taarifa zenye utata.

3. Baraza la Mji Kaskazini "A" likipanga bajeti yake ianzie na mwaka wa fedha uliopo na sio kupanga chini ya hapo.

### MATOKEO YA UCHAGUZI

### 4.4.1 Kamati ya ukaguzi wa ndani

Kwa mujibu wa kifungu nambari 118 cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma namba 12 ya mwaka 2016 inaitaka taasisi ya serikali kuanzisha kamati ya ukaguzi wa ndani ili kutathmini mfumo wa udhibiti wa ndani katika taasisi hiyo. Ukaguzi umebaini kuwa kamati ya ukaguzi ya Baraza la Mji Kaskazini "A" haijakaa kikao hata kimoja kwa lengo la kutathmini udhibiti wa ndani kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu namba 118 cha sheria ya usimamizi wa fedha za umma namba 12 ya mwaka 2016.

Kutofanya kazi kwa kamati ya ukaguzi ya Baraza la Mji Kaskazini “A” kunaweza kupelekea vihatarishi vya Halmashauri kutokubainika mapema na kunaweza kupelekea ukiukwaji wa sheria mbali mbali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Mji Kaskazini “A” kuhakikisha kamati ya ukaguzi inafanya kazi zake kwa mujibu wa matakwa ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016.

**Majibu**
Ni kweli kwamba Kamati haikukaa vikao vyake vya kawaida lakini ofisi imechukuwa hatua za haraka kuhakikisha vikao vya Kamati ya Ukaguzi wa Ndani vinafanyika ili kutathmini udhibiti wa ndani iweze kuendana na Sheria ya Usimamizi wa Mali za Umma.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**
Kamati ya LAAC haikuridhika na majibu ya Baraza la Mji Kaskazini “A”, hivyo, hoja hiyo imebaki kama ilivyo.

### 4.4.2 Dosari katika taratibu za manunuzi Tsh. 116,230,000

Ukaguzi umebaini Baraza la Mji Kaskazini “A” imefunga mkataba na Kampuni ya Trident Limited wenye gharama ya shilingi 116,230,000 kwa ajili ya kazi za ukarabati wa barabara ya Hamburu. Ukaguzi umebaini kutofuatwa kwa taratibu za kumtafuta mzabuni wa kazi hiyo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma nambari 11 ya mwaka 2016, pamoja na kupelekea kufanyika kwa manunuzi yasiokuwa na tija.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Mji Kaskazini “A” kufanya manunuzi kwa kuzingatia Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma nambari 11 ya mwaka 2016.

**Majibu**
Taratibu za kumpata Mzabuni zilifuatwa kwa kutumia njia ya QUOTATION na Wazabuni watatu waliweza kujaza na wawili walifanikiwa kurejesha ambapo Kampuni ya TRIDENT LIMITED ilishinda na kupewa kazi hiyo.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**
Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC ilibaini kuwa Kampuni ya TRIDENT LIMITED ilifunga mkataba wa Tsh. 116,230,000 na Baraza la Mji Kaskazini “A”, isipokuwa kwamba, fedha halisi iliyokubaliwa kulipwa ni Tsh. 71,946,370.

Kutokana na kasoro hiyo kubwa iliyobainika Kamati ya LAAC ililitaka Baraza kufunga mkataba mwengine na Kampuni hiyo ili mkataba uoneshe uhalisia wa malipo

yaliyolipwa.

### 4.4.3 Kutowasilishwa kwa fedha za makato katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF) Tsh. 174,000,000.00

Ukaguzi umebaini Baraza la Mji Kaskazini "A" halikuwasilisha Michango ya jumla ya shilingi 174,000,000 ya wafanyakazi kwenda Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa miezi miwili ya Disemba na Januari, fedha hizo zilizopaswa kulipwa zilizotumika kwa ajili ya kazi nyengine za Baraza la Mji Kaskazini "A" kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Sheria nambari 2 ya mwaka 2015.

Kutumia fedha zilizokatwa kwa ajili ya malimbikizo ya wafanyakazi katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii na kutumika kwa matumizi mengineyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Mfuko wa Hifadhi wa Jamii nambari 2 ya mwaka 2015.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza la Mji Kaskazini "A" kuwasilisha Michango ya Wafanyakazi hao kwa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii mara moja, ili kuweza kuendana na mfumo mzuri wa uwekaji wa kumbukumbu za mkato ya wafanyakazi hao.

#### Majibu:

Ni kweli wakati wa ukaguzi kwa miezi ya Disemba, 2019 na Januari, 2020, Baraza la Mji Kaskazini "A" lilipokea fedha kwa ajili ya mishahara ya wafanyakazi kutoka Wizara ya Fedha na Mipango, kwa bahati mbaya Baraza lilifanikiwa kulipa mishahara hiyo na kuchelewa kuzipeleka fedha za mchango wa ZSSF zenye thamani ya Tsh. 174,000,000.00 hali iliyopelekea fedha hizo kutumika kwa matumizi mengine.

Hadi mwezi wa Juni 2020, Baraza la Mji Kaskazini "A" lilifanikiwa kupunguza deni hilo kwa kufanya malipo ya Tsh. 100,000,000.00 kwenda ZSSF.

Hata hivyo, kiwango cha fedha chenye thamani ya Tsh. 74,000,000.00 kimeshawasilishwa katika Mfuko wa ZSSF kwa mwaka wa fedha 2020 -2021.

#### Uchunguzi wa Kamati

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC ilibaini yafuatayo:

1. Baraza la Mji Kaskazini "A" halifanyi upatanishi "reconcilliation" wa hesabu zake kama taratibu za fedha zinavyoelekeza.
2. Mapato (fedha) yalivyoingia katika hesabu ya benki ya Baraza hayakujulikana yalitokana na jambo gani. Kitendo hiki kimechangia kwa asilimia kubwa kutowasilishwa kwa fedha za makato katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii.
3. Baadhi ya shughuli zilizotekelezwa hazikuwemo kwenye mpango kazi wa Baraza.
4. Baadhi ya shughuli zilizotekelezwa hazikupata ridhaa au baraka ya Madiwani

#### Mapendekezo ya Kamati

Ili kasoro kama hizo zisijitokeze tena Kamati ya LAAC ilipendekeza yafuatayo:

1. Baraza la Mji Kaskazini "A" lihakikishe kuwa linafanya upatanishi "reconcilliation" wa hesabu zake ili kuwa na taarifa sahihi pamoja na kubaini mapema kasoro zilizojitokeza katika mwezi husika.
2. Baraza la Mji Kaskazini "A" lihakikishe kuwa linalipa fedha za mkato wa ZSSF kwa watendaji wake kama Sheria inavyoelekeza ili kuepusha kutozwa faini.

### 4.4.4 Dosari katika ukusanyaji wa mapato ya minara

Ukaguzi umebaini Baraza la Mji Kaskazini "A" linakusanya mapato ya Minara na mabango kupitia wakala kampuni ya Al-Jumra ambapo ukaguzi umeshindwa kuona kima halisi cha fedha kilichokusanywa na kampuni hiyo.
Aidha, ukaguzi umebaini uwepo wa makubaliano baina ya kampuni hiyo na Baraza la Mji Kaskazini "A" ambapo kampuni ya Aljumra inachukua asilimia 40 ya mapato yaliyokusanywa na asilimia 60 inawasilishwa Baraza la Mji Kaskazini "A". Katika makubaliano hayo dosari mbali mbali ziliweza kubainika kama ifuatavyo:-

- Kukosekana kwa utaratibu wa ushindani uliotumika kumpata wakala huyo wa ukusanyaji wa mapato kwa niaba ya Baraza la Mji Kaskazini "A", kufanya hivyo ni kwenda kinyume na sheria ya manunuzi na undoshaji wa mali za Umma sheria namba 11 ya mwaka 2016.

- Kukosekana kwa taarifa ya kibenki (Bank Statement) ya kampuni ya Aljumra ili kujiridhisha kima halisi cha makusanyo ambacho kinakusanywa kwa mwezi ili kuweza kujiridhisha usahihi wa kiwango kilichoripotiwa.

- Kukosekana kwa Mkataba kati ya Baraza la Mji Kaskazini "A" ambao unaonyesha makubaliano ya pande mbili katika kazi ya ukusanyaji wa mapato hayo. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na sheria ya manunuzi na uondoshaji wa mali za Umma Sheria namba 11 ya mwaka 2016.

Kukusanya mapato kupitia wakala wa ukusanyaji wa mapato ya minara kunapelekea Baraza la Mji Kaskazini "A" kukosa mapato kwa kuwa kazi hiyo inaweza kufanywa na Baraza la Mji Kaskazini "A" bila ya kumtumia wakala.

Ukaguzi unashauri Baraza la Mji Kaskazini "A" kufanya Upembuzi Yakinifu ili kuhakikisha Baraza linapata tija katika utekelezaji na usimamizi wa rasilimali za umma, pamoja na kuhakikisha utowaji wa zabuni unafuatwa kwa mujibu wa Sheria ili kuwepo kwa uwazi na uwajibikaji katika utoaji wa zabuni na kuhakikisha mapato yanakusanywa kwa mujibu wa sheria.

### Majibu

Ni kweli wakati wa ukaguzi, Baraza la Mji halikufanikiwa kuwasilisha Mkataba wa makubaliano baina ya Baraza la Mji Kaskazini "A" na AL-JUMURA, baada ya kufatilia mikataba hiyo imeonekana na ipo tayari kwa kuwasilishwa.

Utaratibu wa ushindani wa kumpata wakala huyo ulifanyika katika ngazi ya Ofisi ya Rais TAMISEMI na Halmashauri ilipokea barua ya utambulisho wa wakala huo ya tarehe 08/02/2019.

Taarifa za kibenki za taasisi hiyo (Al-jumra) hazikuweza kupatikana kwa sababu wakala alishindwa kuwasilisha taarifa hizo kwa mujibu wa mkataba wa makubaliano. Kwa mujibu wa mkataba wakala alipaswa kuwasilisha makadirio ya makusanyo na siyo taarifa za kibenki (Bank Statement).

**Uchunguzi wa Kamati**

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC ilibaini yafuatayo:

1. Kutokana na muonekano wa mkataba, ni kweli kuwa mkataba huo ulikuwepo, isipokuwa kwamba, Baraza la Mji Kaskazini "A" linakabiliwa na changamoto ya uwekaji mbaya wa nyaraka zake.
2. Mapato ya yanayotokana na minara hivi sasa yanakusanywa na Wakala wa Miundombinu ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano Zanzibar, hata hivyo, Baraza hili halijapokea fedha yoyote kutoka kwa Wakala huyo.

**Mapendekezo ya Kamati**

Ili kasoro kama hiyo isijitokeze tena Kamati ya LAAC ilipendekeza yafuatayo:

1. Baraza la Mji Kaskazini "A" lihakikishe kuwa linahifadhi vyema nyaraka zake ili kuepusha hoja zisizo za lazima.
2. Wakala wa Miundombinu ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano Zanzibar wawapatie Baraza mapato yanayotokanana minara ili Baraza liweze kutekeleza vyema majukumu yake.
3. Baraza la Mji Kaskazini "A" liandae daftari la mikataba ili kuweza kujua mkataba gani unaendelea (upo hai) na mkataba upi umemaliza muda.

### 4.4.5 Kukosekana kwa mikataba ya kazi za uzoaji wa taka Tsh. 17,460,000.00

Ukaguzi umebaini Baraza la Mji Kaskazini "A" imefanya malipo ya shilingi 17,460,000 kwa ajili ya kugharamia kazi za uzoaji wa taka za Baraza, dosari iliyobainika na ukaguzi ni kukosekana kwa mikataba ya uzoaji wa taka, ili kuweza kujiridhisha kiasi halisi cha makubaliano ya malipo, muda wa mkataba pamoja na taratibu za malipo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali Umma nambari 11 ya mwaka 2016, pamoja na kutokupatikana tija.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Mji Kaskazini "A" kufuata Sheria ya Manunuzi n Uondoshaji wa Mali za Umma kwa kufunga mikataba na watoaji huduma ili kuwepo kwa uwajibiaji katika utekelezaji wa kazi za Baraza.

**Majibu**

Ni kweli kuwa wakati wa ukaguzi mikataba haikuwepo lakini kiuhalisia Baraza la Mji Kaskazini "A" liliingia mkataba na ALI SALUM MCHENGA tarehe 14/05/2019 na

kumalizika 14/11/2019 wenye thamani ya malipo ya Tsh. 3,000,000/= kwa kila mwezi.

Aidha, Baraza liliingia mkataba na MHM ENTERPRISES, Mkataba wa kwanza ulianza tarehe 04/06/2019 na kumaliza tarehe 04/09/2019, ambapo mkataba wa pili ulifungwa tarehe 05/09/2019 na kumaliza tarehe 05/12/2019. Mikataba yote ilikuwa na thamani ya Tsh. 1,200,000/= kwa kila mwezi.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC imejiridhisha kuwa ni kweli mkataba huo ulikuwepo, isipokuwa kwamba, Baraza la Mji Kaskazini "A" linakabiliwa na tatizo la uwekaji mbaya wa nyaraka zake. Kamati iliukagua mkataba huo na kutokana na muonekano wake unaonesha kuwa ni wa zamani.

Kutokana na kasoro hiyo Kamati ya LAAC ililitaka Baraza la Mji Kaskazini "A" kuhakikisha kuwa linahifadhi vyema nyaraka zake ili kuepusha hoja zisizo za lazima.

### 4.4.6 Malipo yasiyokuwa na vielelezo yenye thamani ya Tsh. 184,190,478.00

Ukaguzi umebaini Baraza la Mji Kaskazini "A" imefanya malipo ya shilingi 184,190,478 kwa ajili ya kugharamia shughuli mbali mbali za Baraza, dosari iliyobainika na ukaguzi ni kukosekana kwa vielelezo vya matumizi hayo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na sheria ya usimamizi wa fedha za umma sheria namba 12 ya mwaka 2016.

**Majibu**

Ni kweli wakati wa ukaguzi malipo haya vielelezo vyake havikukamilika na vyengine kutowasilishwa kwa wakati kwa Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu, hata hivyo, kuna baadhi ya hoja hizo zilijirudia na kusababisha kuongezeka thamani na kufikia Tsh. 184,190,478.00. Kwa ujumla Hoja ambazo zimewasilishwa tayari taasisi imeshazifanyia kazi dosari hizo na kukamilisha vielelezo vyake na vipo tayari kwa ukaguzi.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC ilijiridhisha kuwa baadhi ya dosari zilizoelezwa kwenye Jadweli Nambari 19 la Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali zimejirudia, hivyo, kiwango halisi cha malipo yasiyokuwa na vielelezo ni Tsh. 107,162,699 badala ya Tsh. 184,190,478.00.

Hivyo, Kamati ya LAAC inaishauri Afisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuwa makini wakati inavyoandaa taarifa zake ili kuepusha usumbufu kwa watumiaji wa taarifa hizo.

Pamoja na kasoro hiyo, hoja hii imebaki kama ilivyo.

### 4.4.7 Malipo yaliyofanyika ambapo vifaa vyake havikurikodiwa kwenye daftari la ghalani Tsh. 54,732,540

Ukaguzi umebaini kuwa Baraza la Mji Kaskazini "A" imefanya matumizi ya jumla ya shilingi 54,732,540 kwa ajili ya manunuzi ya vifaa mbalimbali. Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kuwa vifaa hivyo havikuingizwa kwenye daftari la kutunza vifaa vya ghalani ili kuweza kuthibitisha uhalali wa mapokezi pamoja na matumizi ya vifaa hivyo.

Kutoingizwa vifaa hivyo katika daftari la kutunza vifaa vya ghalani ni kwenda kinyume na Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma nambari 11 ya mwaka 2016.

#### Majibu

Ni kweli wakati wa ukaguzi vifaa hivyo Wakaguzi hawakufanikiwa kuviona katika daftari la ghalani ingawa viliingizwa, hivyo, Baraza la Mji Kaskazini "A" limelitatua tatizo hilo na daftari la ghalani liko tayari kwa ukaguzi.

#### Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Kamati ya LAAC ilishtushwa na majibu ya Baraza la Mji Kaskazini "A", hata hivyo, Kamati ililikagua daftari hilo ingawa ilikuwa vigumu kuamini maelezo ya Baraza hilo.

Pamoja na hayo, Kamati ya LAAC ilibaini kuwa Baraza hilo lilikuwa halina Afisa wa Ghalani "Store keeper" ambaye alikuwa na utaalamu wa kazi hiyo baada ya Afisa wa Ghalani aliyekuwepo kuhamishiwa katika Afisi nyengine.

## 4.5 HALMASHAURI YA WILAYA YA KASKAZINI "B"

#### Taarifa ya Mapato

Baraza la Mji Kaskazini "B" kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ilikadiria kukusanya Tsh. 2,090,933,373.00 kutoka vyanzo vya ndani vya Halmashauri. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2020 jumla ya Tsh. 1,263,389,912.95 zimekusnywa sawa na asilimia 60.4 ya makadirio.

#### Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Katika kufuatilia taarifa ya mapato Kamati ya LAAC imebaini yafuatayo:

1. Mapato halisi kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ni Tsh. 1,186,654,686.95, isipokuwa kwamba, mapato hayo yameonekana tofauti kwenye Taarifa ya Hesabu ya Mwisho wa Mwaka kwa kuwa wamejumuishwa na ruzuku na msaada "grant and aid".
2. Taarifa ya Mkaguzi wa Ndani haipo sahihi.
3. Mapato ya mchanga yanawasilishwa Hazina, isipokuwa kwamba, Halmashauri hupatiwa mapato hayo chini ya kiwango kilichokusanya.

**Taarifa ya Matumizi**
Baraza la Mji Kaskazini "B" kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ilikadiria kutumia Tzs.6,869,733,373 kwa kazi za kawaida na maendeleo na hadi tarehe 30 Juni, 2020 Halmashauri imeweza kutumia 6,414,575,696.49 sawa na asilimia 93% ya makadirio.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**
Katika kufuatilia taarifa ya matumizi Kamati ya LAAC imebaini kuwa Halmashauri ilitekeleza miradi ya maendeleo katika mwaka husika, hata hivyo, hakuna "Note" kwenye Taarifa ya Hesabu za Mwisho wa Mwaka inayozungumzia miradi hiyo.

Kutokana na kasoro hiyo, Kamati ya LAAC inamshauri Mhasibu na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuwa makini wakati wa kuandaa Taarifa hiyo ili taarifa zote muhimu ziweze kuingizwa kwenye Taarifa hiyo.

## MATOKEO YA UKAGUZI

### 4.5.1 Kamati ya ukaguzi
Kwa mujibu wa kifungu namba 118 cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma namba 12 ya mwaka 2016 kinaitaka kila Taasisi ya Umma kuanzisha Kamati ya Ukaguzi wa Ndani kwa ajili ya kutathmini mfumo wa udhibiti wa ndani. Halmashauri ya Wilaya Kaskazini B imeanzisha Kamati ya Ukaguzi kwa mujibu wa sheria.

Ukaguzi umebaini kuwa katika mwaka wa fedha 2019/2020 Kamati hiyo imefanya kikao kimoja tu, jambo linaweza kupelekea dosari za kiutendaji kwa kutokurekebishwa kwa wakati kutokana na Kamati kushindwa kufanya kazi kwa mujibu wa taratibu.
Kufanya hivyo ni kwenda kinyume Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma namba 12 ya mwaka 2016.

**Majibu**
Ni kweli katika mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 June, 2020; Kamati ya Ukaguzi wa ndani katika Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini 'B' imekaa kikao kimoja tu cha utendaji. Hali hii inatokana na sababu zifuatazo:-

a. **Uzoefu wa uendeshaji wa Kamati za Ukaguzi wa Ndani**

Awali, Mkaguzi wa Ndani pamoja na Kamati ya Ukaguzi wa Ndani ilikuwa chini ya dhamana ya (AR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, kwa mujibu wa utaratibu huo Halmashauri inakaguliwa na Wakaguzi wa Ndani kutoka Wizara pamoja na kushiriki katika Vikao vya Kamati ya Ukaguzi ya Wizara.

Baada ya utekelezaji hasa wa Ugatuzi katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Halmashauri na Manispaa zilitakiwa kila moja kuanzisha Kitengo cha Ukaguzi wa

Ndani pamoja na Kamati ya Ukaguzi wa Ndani, hali hii imepelekea Halmashauri kuanzisha Kamati bila ya kuwa na uzoefu na uendeshaji wa kamati hizo.

**b. Kutokamilika kwa Wajumbe wa Kamati ya Ukaguzi hadi kufikia 2020**

Baada ya kuanzishwa kwa Kamati katika Halmashauri, Wajumbe wanne waliteuliwa kutoka katika ngazi ya Halmashauri. Wajumbe hao ni wafuatao:-

| | |
|---|---|
| a) Mwanasheria wa Halmashauri | Mwenyekiti |
| b) Afisa Mipango wa Halmashauri | Katibu |
| c)Muhandisi wa Halmashauri | Mjumbe |
| d) Afisa Afya Jamii Halmashauri | Mjumbe |

Mjumbe wa mwisho anategemewa kutoka katika Wizara ya Fedha na Mipango ili kutimiza idadi ya wajumbe kamili wa Kamati hiyo.

Lakini uhalisia kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 June, 2020 Wajumbe wa Kamati ya ukaguzi wa ndani hawakukamilika kwa sababu zifuatazo:-

a. Mjumbe aliyetegemewa kutoka Wizara ya Fedha na Mipango hakuthibitishwa mpaka sasa uteuzi wake mbali na kukumbushia.
b. Mjumbe mmoja (Afisa Mipango wa Halmashauri) muda mfupi tu baada ya kuanzishwa kwa Kamati alipatiwa uhamisho wa kikazi siku chache baada ya kikao cha mwanzo.
c. Hali kadhalika, Mwenyekiti wa Kamati (Mwanasheria wa Halmashauri) alikuwa katika likizo ya uzazi (maternity leave).

Ikiwemo na uzoefu wa uendeshaji wa Kamati, pia sababu hizo hapo juu zimepelekea Kamati ya Ukaguzi wa Ndani kushindwa kuwa na uhalali wa kuendesha vikao vya kamati kisheria.

Hata hivyo, juhudi zimechukuliwa na uongozi wa Baraza kwa kuhakikisha Kamati inafanyakazi zake, kwa kufanya uteuzi wa nafasi zilizokuwa wazi pamoja na kuwapatia mafunzo stahiki wajumbe wa Kamati hiyo. Kwa mwaka wa fedha Julai, 2020 hadi Juni, 2021 Kamati imeanza na inaendelea na utekelezaji wa majukumu yake na imeshakaa vikao viwili (2) kwa mwaka 2020/2021.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Katika kufuatilia hoja hii Baraza liliieleza Kamati ya LAAC kuwa liliiandikia Wizara ya Nchi, (OR), Fedha na Mipango barua ya tarehe 18 Juni, 2019 yenye kumbukumbu HW/KASK.B/K.2/VOL.I/1 kuomba mjumbe wa Kamati hiyo hata hivyo, Wizara hiyo haikujibu barua hiyo.

Kwa kuwa kasoro nyingi zilizojitokeza zilikuwa nje ya uwezo wa Baraza na kwa kuwa Baraza limechukua juhudi mbali mbali ya kutatua changamoto hiyo, hivyo, Kamati ya

LAAC imeifuta hoja hiyo.

### 4.5.2 Vitabu vya Stakabadhi za Mazao ambavyo havikuonekana kwa ajili ya Ukaguzi

Ukaguzi umebaini kuwepo kwa vitabu vya stakabadhi za malipo ya ukusanyaji mapato ya mazao ambavyo vimerikodiwa kwenye daftari la kutunzia kumbukumbu za stakabadhi (Counterfoil Register) ambavyo havikupatikana kwa ukaguzi, kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu namba 30 (2) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma namba 12 ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini 'B' kusawazisha dosari hiyo kwa kutafuta vitabu hivyo vya stakabadhi kwa ajili ya ukaguzi. Mchanganuo wa vitabu hivyo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:- Jadweli nambari 21: vitabu ambavyo havikupatikana kwa ukaguzi.

**Majibu**

Ni kweli katika kipindi cha ukaguzi, baadhi ya vitabu vya stakabadhi za mazao havikuwasilishwa kwenye ukaguzi. Sababu iliyopelekea kutokuwasilishwa vitabu hivyo kwenye kipindi cha ukaguzi ni kuwa idadi kubwa ya vitabu hivyo bado vilikuwa vinaendelea kutumika katika shehia kwa ajili ya kukusanyia mapato, ambapo vitabu hivyo wamekabidhiwa Masheha katika maeneo yao.

Juhudi zimechukuliwa na uongozi wa Baraza kwa kuwataka Masheha kuviwasilisha vitabu hivyo 18 kwa hatua za ukaguzi. Kwa msingi huo vitabu vyote vipo kwa uthibitisho baada ya kukusanywa kutoka kwa Masheha.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC ilielezwa kuwa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali hakufanya kikao cha kutokea "Exit meeting".

Aidha, Kamati ya LAAC ilibaini kuwa idadi ya vitabu hivyo haikukamilika kama ilivyoelezwa na Baraza, hivyo, hoja hii imebaki kama ilivyo.

### 4.5.3 Dosari katika ukusanyaji wa mapato ya minara

Ukaguzi umebaini Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini 'B' inakusanya mapato ya minara na mabango kupitia Wakala wa Kampuni ya Al-Jumura ambayo jumla ya Tzs. 131,936,140 zilikusanywa. Aidha ukaguzi umebaini uwepo wa makubaliano baina ya kampuni hiyo na Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini 'B' ambapo kampuni ya Al-Jumura inachukua asilimia 40% ya mapato yaliyokusanywa ambayo ni sawa na Tzs. 52,774,456 na asilimia 60 inawasilishwa Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini 'B' ambapo sawa na Tzs. 79,161,684. Katika makubaliano hayo dosari mbalimbali ziliweza kubainika kama ifuatavyo:-

- Kukosekana kwa utaratibu wa ushindani uliotumika kumpata Wakala huyo wa

ukusanyaji wa mapato kwa niaba ya Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini B, kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya manunuzi na uondoshwaji wa mali za umma Sheria namba 11 ya mwaka 2016.

- Kukosekana kwa taarifa ya kibenki (bank statement) ya Kampuni ya Al-Jumra ili kujiridhisha kiasi halisi cha makusanyo ambayo kinakusanywa kwa mwezi ili kuweza kujiridhisha usahihi wa kiwango kilichoripotiwa.
- Kukosekana kwa Mkataba kati ya Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini B ambao unaonyesha makubaliano ya pande mbili katika kazi ya ukusanyaji wa mapato hayo, kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya manunuzi na uondoshwaji wa mali za umma Sheria namba 11 ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini 'B' kufanya upembuzi yakinifu (feasibility study) ili kuhakikisha Halmashauri inapata tija katika utekelezaji na usimamizi wa rasilimali za umma, pamoja na kuhakikisha utoaji wa zabuni unafuatwa kwa mujibu wa sheria ili kuwepo kwa uwazi na uwajibikaji katika utoaji wa zabuni na kuhakikisha mapato yanakusanywa kwa mujibu wa sheria.

### Majibu

Ni kweli kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini B inakusanya mapato ya minara na mabango ya matangazo kupitia Wakala wa Kampuni ya Al-Jumra kwa makubaliano ya kumlipa asilimia 40% ya mapato yaliyokusanywa kwa mujibu wa mkataba. Hali hii imechangiwa na ukosefu wa wataalamu katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa ikiwemo Halmashauri Kaskazini B katika fani za taarifa za matumizi ya minara na mawasiliano pamoja na matangazo.

Taratibu za kumpata mtoa huduma wa ukusanyaji wa mapato yatokanayo na minara zilifanyika katika ngazi ya Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa kuchaguliwa mtoa huduma (Al-Jumura) katika Mamlaka za Serikali za Mitaa Zanzibar (Manispaa na Halmashauri) ikiwemo Halmashauri ya Wilaya Kaskazini B Unguja.

Katika ngazi ya Halmashauri, tumeingia mkataba na mtoa huduma (Al-Jumura) mwezi wa Novemba, 2019 kwa muda wa mwaka mmoja. Pia Halmashauri iliingia mkataba wa nyongeza (addendum) ya kuendelea na kazi za ukusanyaji wa mapato yatokanayo na minara na mabango hadi mwezi wa Februari, 2021 mkataba ulipomalizika.

Kiuhalisia, makampuni yanayostahiki kulipa yanaingiza fedha moja kwa moja katika hesabu ya Baraza, mtoa huduma (Al-Jumura) anadai fedha zake (asilimia 40) kutoka Halmashauri na siyo kwamba anajilipa kutokana na makusanyo anayoyasimamia.

Kuhusu fedha zilizopitia katika hesabu ya Al-Jumura, fedha hizo ni mwa mwezi wa April 2020, Mei 2020 na Juni, 2020 kutoka Kampuni ya Viettel (Halotel), kuna

makubaliano baina ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa zanzibar, Kampuni ya Viettel, Wizara na Mtoa Huduma kuhusu kuingizwa kwa fedha hizo katika hesabu ya mtoa huduma.

### Uchunguzi wa Kamati

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC ilibaini yafuatayo:

1. Baraza lilipewa agizo na Wizara inayosimamia Baraza hili kuitumia Kampuni ya Al jumura kufuatia barua ya tarehe 08 Februari, 2019 yenye kumbukumbu Namba OR/TMSMIM/M.20/1/VOL III/60, jambo ambalo ni kinyume na utaratibu.
2. Wakala wa Serikali Mtandao ndio wanaosimamia minara hivi sasa, hata hivyo, Baraza la Mji Kaskazini "B" halijapokea fedha yoyote inayotokana na pato la minara tokea mwezi wa Februari, 2021 hadi Kamati inachunguza hoja hii terehe 04 Agosti, 2022.
3. Mapato yanayotokana na vileo, mchanga na minara yanasimamiwa na Baraza, hata hivyo, mapato hayo yanapelekwa Serikali Kuu (Hazina), isipokuwa kwamba, fedha hizo hazipatikani zote kama zilivyo kusanywa.
4. Baraza linaidai Kampuni ya Al jumura mapato ya miezi mitatu yaani kuanzia mwezi wa Aprili hadi Juni, 2020.

### Mapendekezo ya Kamati

Kutokana na kasoro hizo, Kamati ya LAAC ilipendekeza yafuatayo:

1. Serikali Kuu ibaki kuwa ni msimamizi tu na iache utaratibu wa kuziamulia mambo yake Serikali za Mitaa.
2. Baraza la Mji Kaskazini "B" lihakikishe kuwa linafuatilia deni linaloidai Kampuni ya Aljumura kwa kuwa mapato hayo yalikusanywa kwa niaba ya Baraza na Kampuni hiyo.
3. Wakala wa Serikali Mtandao wawapatie Baraza mapato yanayotokana na minara ili Baraza iweze kutekeleza shughuli zake ipasavyo.
4. Serikali Kuu izipatie Serikali za Mitaa fedha inazokusanya ili Serikali za Mitaa ziweze kutekeleza shughuli zake vyema na kuleta tija iliyokusudiwa ya kuanzishwa Serikali hizo.

### 4.5.4 Malipo yasiyokuwa na vielelezo shilingi 64,388,579

Ukaguzi umebaini Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini 'B' imefanya malipo ya shilingi 64,388,579 kwa ajili ya kugharamia shughuli mbalimbali za Halmashauri.

Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kukosekana kwa vielelezo vya matumizi hayo, kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma namba 12 ya mwaka 2016.

### Majibu

Ni kweli kuna baadhi ya hati za malipo katika Baraza hazijakamilika vielelezo ili

kuthibitisha uhalali wa malipo yaliyofanyika. Hali hii inapelekela kutia shaka katika ukaguzi kuhusu uhalali wa hati za malipo. Uongozi wa Baraza umekamilisha vielelezo vichache zilivyokuwa havikuambatanishwa na hati za malipo ili kuthibitisha uhalali wa hati hizo kwa malipo yaliyofanyika.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**
Kutokana na majibu Baraza, hoja hii imebaki kama ilivyo.

Pamoja na hilo, Kamati ya LAAC katika kufuatilia hoja hii imebaini kuwa Hati ya Malipo Namba 59 ya tarehe 26 Juni, 2020 imeandikwa mara mbili, hivyo, kiwango cha malipo yasiyokuwa na vielelezo kimepungua na kufikia Tsh. 49,122,579.

Kwa mnasaba huo, Kamati ya LAAC inaishauri Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuwa makini wakati wa kuandaa taarifa zake ili kuepusha lawama zisizo na msingi.

**4.5.5 Dosari katika taratibu za manunuzi Tzs. 218,347,200**
Ukaguzi umebaini Baraza la Mji Kaskazini B limeingia Mkataba na Kampuni ya Trident wenye gharama ya Tzs. 218,347,200 kwa ajili ya ujenzi wa barabara kupitia miradi ya Wadi. Ukaguzi umebaini kutofuatwa kwa taratibu za kumtafuta Mzabuni wa kazi hiyo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Manunuzi na Uondoshwaji wa Mali za Umma Sheria namba 11 ya mwaka 2016, pamoja na kupelekea kufanyika kwa manunuzi yasiokuwa na tija.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza la Mji Kaskazini B kufanya manunuzi kwa kuzingatia Sheria ya Manunuzi na Uondoshwaji wa Mali za Umma Sheria namba 11 ya mwaka 2016.

**Majibu**
**a) Hati ya malipo nambari 49/6 na 1/6**
Ni kweli Baraza la Mji Kaskazini B limeingia Mkataba na Kampuni ya Trident kwa ajili ya ujenzi wa barabara kupitia matumizi ya miradi katika Wadi. Mradi wa ujenzi wa barabara ya Donge Mbiji (Majenzi) hadi Chechele kilomita 2 na kutoka Donge Mbiji (kwa Kitarabu) hadi Donge Fuasini kilomita 1 kwa kiwango cha kifusi pamoja na ujenzi wa misingi ya kutiririsha maji na madaraja mawili (2).

Kwa mujibu wa Ilani ya Uchaguzi ya C.C.M ya mwaka 2015 - 2020 Baraza la Mji Kaskazini B lilipangiwa jukumu la kukamilisha miradi 8 katika Wadi na katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi wa CCM, takribani miradi 6 ilikuwa imeshakamilika isipokuwa miradi 2 katika Wadi ya Mkataleni na Vijibweni yote ya Jimbo la Donge ilishindwa kukamilika ndani ya wakati uliopangwa, hii ilitokana na uhaba wa fedha

uliojitokeza kutokana na maradhi ya Corona yaliyojitokeza nchini mwanzoni mwa mwaka 2020.

Kutokana na mwaka wa 2020 kuwa ni mwaka wa Uchaguzi Mkuu nchini, Baraza limelazimika kukamilisha utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015-2020 kwa kuhakikisha miradi 2 iliyosalia inakamilika kwa wakati ili kuondoa dhana ya upendeleo kwa baadhi ya Wadi. Hivyo, Baraza liliamua kutumia njia ya ushindani kwa wakandarasi (short list) kwa ajili ya ujenzi wa barabara hizo mbili za ndani zenye urefu wa kilomita 3 kwa masharti ya kukubali kufanyakazi kwa mujibu wa uhalisia wa upatikanaji wa fedha katika Baraza na malipo yatafanyika katika awamu 5 kwa mujibu wa mkataba.

Katika mchakato huo, jumla ya wakandarasi 4 walionesha nia (expression of interest) kwa kuwasilisha maombi ya ujenzi wa barabara na wakandarasi 3 kati ya 4 walirejesha barua ya maombi ya kazi za ujenzi, maelezo ya utekelezaji wa kazi (commitment) na taarifa ya makisio ya kazi (BOQ). Wakandarasi waliorejesha maombi ni Double J Building Contractors ltd, Sakhari Building Contratction ltd na Trident. Kutokana na vigezo Trident ilitimiza masharti na viwango na kupewa jukuma la ujenzi huo.

### b) Hati nambari 16/3 na 34/3

Kuhusiana na malipo ya gharama za uchongaji wa barabara ya Mangapwani pamoja na malipo ya awamu ya kwanza na awamu ya pili ya usambazaji wa kifusi. Bodi ya Zabuni ya Baraza la Mji Kaskazini B iliamuru kufanyika malipo kwa njia ya ushindani wa kawaida kwa kutumia ankara (invoice). Watoa huduma watatu walitoa ankara na Trident Limited alikuwa na kiwango cha chini zaidi na ndipo alikubalika kutoa huduma.

### Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Kutokana na majibu ya Baraza, Kamati ya LAAC iliomba kupatiwa barua ya Mamlaka ya Manunuzi iliyoelekeza hivyo, hata hivyo, Kamati ilielezwa kuwa ushauri huo umetolewa kwa mdomo.

Kwa msingi huo, Kamati ya LAAC ilishindwa kuthibitisha hilo na hivyo hoja hiyo imebaki kama ilivyo.

Pamoja na hayo, Kamati ya LAAC imelishauri Baraza kutekeleza shughuli zake kwa kuwa na kumbukumbu ya barua kwa kuwa kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Utumishi mawasiliano ya Taasisi yanatakiwa yafanywe kwa njia ya maandishi.

### 4.5.6 Vifaa ambavyo havijarikodiwa kwenye daftari

Ukaguzi umebaini kwa Baraza la Mji Kaskazini B imefanya matumizi kwa ajili ya manunuzi ya vifaa mbalimbali, dosari iliyobainika na ukaguzi ni kuwa vifaa hivyo

havikuingizwa kwenye daftari la kutunzia vifaa vya ghalani ili kuweza kudhibiti uhalali wa mapokezi pamoja na matumizi ya vifaa hivyo.

Kutoingizwa vifaa hivyo katika daftari la kutunzia vifaa vya ghalani ni kwenda kinyume na Sheria ya manunuzi na uondoshwaji wa mali za umma Sheria namba 11 ya mwaka 2016.

**Majibu**
Ni kweli wakati wa Ukaguzi wa Hesabu za Serikali uliofanyika katika Baraza, kuna baadhi ya vifaa havikuonekana kwenye daftari la kutunzia kumbukumbu za vifaa ghalani. Hali hii inapelekea kutia shaka katika kuthibitisha uhalali wa mapokezi ya vifaa pamoja matumizi ya vifaa vilivyonunuliwa.

Kutokana na kasoro hiyo iliyojitokeza, uongozi wa Baraza umeizingatia hoja hii kwa umakini na kuchukua jitihada za haraka za kukamilisha taratibu zote za mapokezi ya vifaa, kuhakikisha vifaa vyote vimeingizwa katika daftari la kutunzia vifaa ghalani na pamoja na utoaji wa vifaa.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**
Kutokana na majibu hayo ya Baraza hoja hii imebaki kama ilivyo.

## 4.6 BARAZA LA MJI KATI

**Taarifa ya Mapato**
Baraza la Mji Kati lilikadiriwa kukusanya jumla ya Tsh. 1,000,000,000 kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Hadi kufikia 30 Juni, 2020 jumla ya Tsh. 1,246,130,521 kutoka katika vyanzo vya mapato vya Baraza sawa na asilimia 124 ya makadirio.

**Majibu**
Baraza la Mji Kati haikuandaa taarifa ya mapato kwa maandishi, isipokuwa kwamba, lilitoa maelezo yake kwa mujibu wa maswali yaliyoulizwa na Kamati.

**Uchunguzi wa Kamati**
Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC ilibaini yafuatayo:

1. Mapato ya Baraza yaliongezeka kwa asilimia 24 kutokana na elimu iliyotolewa kwa wananchi juu ya umuhimu wa kulipa kodi.
2. Kumbukumbu za Kikao cha Madiwani zilikuwa hazina saini ya Mwenyekiti wala Katibu wa Baraza hilo ambae ni Mkurugenzi wa Baraza, jambo ambalo ni kinyume na utaratibu.
3. Chanzo cha Mapato cha leseni ya biashara "business licence" katika mwaka husika mapato yake yameshuka kutoka Tsh. 221,498,000 hadi Tsh. 216,313,000, hata hivyo, Kamati hii haikupatana maelezo ya kutosha kutokana

na sababu iliyopelekea hivyo.

**Mapendekezo**
Katibu wa Baraza ambaye ni Mkurugenzi wa Baraza hili ahakikishe kuwa anasimamia vyema majukumu yake ili kuepusha kasoro zisizo za msingi.

**Taarifa ya Matumizi**
Baraza la Mji Kati katika mwaka wa fedha 2019/2020 likadiriwa kutumia jumla ya Tsh. 8,784,446,000 kwa kazi za kawaida. Hadi kufikia 30 Juni, 2020 jumla ya Tsh. 8,717,958,654 zilitumika kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 99 ya makadirio.

**Majibu**
Baraza la Mji Kati halikuandaa taarifa ya matumizi kwa maandishi, isipokuwa kwamba, lilitoa maelezo yake kwa mujibu wa maswali yaliyoulizwa na Kamati.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**
Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC ilibaini yafuatayo:-

1. Hakukuwa na mradi wa maendeleo wenye tija ingawa wamekusanya zaidi ya fedha zilizokusudiwa.
2. Taarifa ya Hesabu ya Mwisho wa Mwaka ina mapungufu kadhaa ikiwemo:
    i. Baadhi ya "Note" zimeandikwa lakini hazionekani kwenye Taarifa hiyo;
    ii. "Note" 8 imetumika mara mbili kinyume na utaratibu.
3. Baadhi ya vitu kama vile gari ya kubebea wagonjwa "ambulance" na vespa vimenunuliwa vya mtumba "second hand".
4. Baada ya Serikali kufutwa ugatuzi, gari ya kubebea wagonjwa ya Baraza hili imekabidhiwa kwa Wizara ya Afya kufuatia agizo la Mheshimiwa Waziri kupitia barua yake ya tarehe 15 Oktoba, 2021 yenye kumbukumbu Nam. WN-OR/TMSIM/MW.I/VOL.I/82 ingawa gari hiyo haihusiki na ugatuzi.
5. Wizara ya Afya imekataa kulipa deni lililosalia la ununuzi wa gari hiyo kwa madai kuwa ununuzi huo haukufuata utaratibu uliowekwa na Serikali, gari hiyo iligharimu Tsh. 71,000,000.00.

    Kutokana na hatua hiyo, Kamati ya LAAC iliandaa kikao cha pamoja tarehe 31 Januari, 2023 na Watendaji wa Wizara ya Afya na baada ya majadiliano ya kina Kikao kiliamua kuwa kwa kuwa baada ya Serikali kufuta mfumo wa ugatuzi watendaji, mali na madeni yote yanayohusiana na ugatuzi kurejeshwa katika Taasisi husika. Hivyo basi, Wizara ya Afya inapaswa kulirithi deni hilo kama utaratibu ulivyoelekeza.

    Pamoja na hayo, Baraza la Mji Kati lilitakiwa kuwasilisha nyaraka zote zinazohusiana na gari hiyo kwa Wizara ya Afya haraka iwezekanavyo ambapo tarehe 08 Februari, 2023 Baraza la Mji Kati lilikabidhi nyaraka hizo.

## MATOKEO YA UKAGUZI

### 4.6.1 Kamati ya ukaguzi

Kwa mujibu wa kifungu nambari 118 cha sheria ya usimamizi wa fedha za umma namba 12 ya mwaka 2016 kinaitaka kila taasisi ya Umma kuanzisha kamati ya ukaguzi wa ndani kwa ajili ya kutathmini mfumo wa udhibiti wa ndani.

Baraza la Mji Kati imeanzisha Kamati ya ukaguzi kwa mujibu wa kifungu namba 118 cha sheria ya usimamizi wa fedha za umma namba 12 ya mwaka 2016. Ukaguzi umebaini kuwa katika mwaka 2019/2020 kamati imeshindwa kufanya vikao vyake kwa mujibu wa sheria.

Kutofanya kazi kwa Kamati ya ukaguzi ni kwenda kinyume na sheria ya usimamizi wa fedha za Umma sheria namba 12 ya mwaka 2016, aidha inaweza kupelekea dosari za kiutendaji kushindwa kurekebishwa kwa wakati.

**Majibu**

Uongozi wa Baraza la Mji Kati umepokea ushauri uliotolewa na mdhibiti na mkaguzi mkuu wa hesabu za Serikali wa kuhakikisha kwamba kamati ya ukaguzi inafanya kazi zake kwa mujibu wa matakwa ya sheria ya usimamizi wa fedha na kwamba kasoro hiyo haitajitokeza tena katika ukaguzi ujao.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya LAAC haikuridhika na majibu ya Baraza la Mji Wilaya ya Kati na ilitaka kujua sababu zilizopelekea kutofanya kazi kwa Kamati hiyo hasa ikizingatiwa kuwa Kamati hiyo ilikuwepo.

Kutokana na hoja hiyo Watendaji wa Baraza waliieleza Kamati hii kuwa Kamati ya Ukaguzi wa Ndani haikufanya kazi zake kwa kuwa Mkaguzi wa Hesabu za Ndani kahamishiwa Taasisi nyengine, hivyo, hakukuwa na taarifa za kuwasilishwa mbele ya Kamati hiyo.

Pamoja na maelezo hayo, Kamati ya LAAC haikukubaliana nayo na hivyo, hoja hiyo imebaki kama ilivyo.

### 4.6.2 Dosari katika ukusanyaji wa mapato ya minara shilingi 108,398,680.68

Ukaguzi umebaini Baraza la Mji Kati inakusanya mapato ya minara na mabango kupitia wakala kampuni ya Al-Jumra ambapo jumla ya shilingi 108,398,680.68 zilikusanywa. Aidha, ukaguzi umebaini uwepo wa makubaliano baina ya kampuni hiyo na Baraza la Mji Kati ambapo Kampuni ya Aljumra inachukua asilimia 40 ya mapato yaliokusanywa ambayo sawa na shilingi 43,359,472 na asilimia 60 inawasilishwa Baraza la Mji Kati ambayo sawa na shilingi 65,039,208.68. Katika makubaliano hayo dosari mbali mbali ziliweza kubainika kama ifuatavyo:-

- Kukosekana kwa utaratibu wa ushindani uliotumika kumpata wakala huyo wa ukusanyaji wa mapato kwa niaba ya Baraza la Mji Kati. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma nambari 11 ya mwaka 2016.
- Kukosekana kwa taarifa ya kibenki (Bank Statement) ya Kampuni ya Aljumra ili kujiridhisha kiasi halisi cha makusanyo ambacho kinakusanywa kwa mwezi ili kuweza kujiridhisha usahihi wa kiwango kilichoripotiwa.
- Kukosekana kwa Mkataba kati ya Baraza la Mji Kati ambao unaonyesha makubaliano ya pande mbili katika kazi ya ukusanyaji wa mapato hayo, kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma nambari 11 ya mwaka 2016.

**Majibu**

Ukusanyaji wa Mapato ya Minara ulianza na changamoto ya ukosekanaji wa aina hiyo ya mapato kwa mamlaka zote za serikali za mitaa.kutokana na hali hiyo kulipelekea ARTMSM za SMZ kateuwa mtu maalum kufuatilia madeni/ madai hayo. Hivyo basi, taratibu na mchakato wa kumpata wakala huyo wa ukusanyaji wa Mapato ya Minara na mabango (AL-JUMURA) uliongozwa na Wizara ya Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ Kwa niaba ya mamlaka zote na hatimae kuweza kupunguza madal hayo.

Hata hivyo, Baraza la Mji Kati kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Iinatarajia kusimamia upatikanaji na ukusanyaji wa Mapato kwa kupitia tenda itakayotolewa.

Aidha, mkataba baina ya wakala huyo na Baraza la Mji Kati upo kwa ajili ya ukaguzi.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya LAAC iliukagua mkataba huo na baada ya majadiliano na Watendaji wa Baraza ilibaini kuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali hakupatiwa mkataba huo kwa kuwa walikuwa hawajui ulipo, hivyo, mkataba huo ulikuwepo na kwa msingi huo, hoja hii imefutwa.

Pamoja na hilo, Kamati ya LAAC imelishauri Baraza kuwa makini katika uwekaji wa nyaraka zake ili kuepusha hoja zisizo za lazima.

### 4.6.3 Dosari katika utayarishaji wa malipo Tsh. 17,874,800

Ukaguzi umebaini kuwa Baraza la Mji Kati imefanya malipo ya shilingi 17,874,800 kwa ajili ya matumizi mbali mbali ya Baraza, dosari iliyobainika na ukaguzi ni kufanyika kwa malipo ya fedha kwa njia ya fedha taslimu (Cash Payment) badala ya kufanya malipo kwa kutumia hundi za benki, kufanya hivyo kunaweza kupelekea vihatarishi (Risk) katika utunzaji wa fedha za Umma. Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Mji Kati kufanya malipo kwa kutumia hundi za benki au kufanya uhaulishaji kupitia hesabu za kibenki ili kuendana na matakwa ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha

za Umma nambari 12 ya mwaka 2016.

**Majibu**
Uongozi wa Baraza la Mji Kati linakiri kufanya malipo hayo kwa njia ya fedha taslim (cash payments) na kwamba tutajitahidi kurekebisha dosari hiyo isitokee tena katika miaka ijayo ya fedha.

### 4.6.4 Malipo yasiokuwa na vielelezo Tsh. 35,382,232
Ukaguzi umebaini kuwa Baraza la Mji Kati imefanya malipo ya shilingi 35,382,232 kwa ajili ya kugharamia shughuli mbali mbali za Baraza. Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kukosekana kwa vielelezo vya matumizi hayo, kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016.

**Majibu**
Uongozi wa Baraza la Mji Kati linakiri kujitokeza kwa dosari hio na kwamba vielelezo vyote vilivyokosekana vimeshafunganishwa na vocha husika kwa ukaguzi,pia tunaahidi kurekebisha dosari hiyo isitokee tena kipindi kijacho cha fedha.

## 4.7 HALMASHAURI YA WILAYA YA MICHEWENI

**Taarifa ya Mapato**
Halmashauriya Wilaya ya Micheweni ilikadiriwa kukusanya jumla ya Tsh. 240,000,000.00 kutoka katika vianzio mbali mbali vya mapato, hadi kufikia tarehe 30.06.2020 ilifanikiwa kukusanya jumla ya Tsh. 264,333,480.00 sawa na asilimia 110% ya makadirio.

**Majibu**
Halmashauriya Wilaya ya Micheweni ilikusanya mapato hayo kupitia vianzio vyake vifuatavyo:

| NAM. | KIFUNGU-MAELEZO | MAKISIO | MAPATO HALISI | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | 1200 - ADA YA MAUZO | 15,000,000.00 | 12,955,800.00 | 86.37 |
| 2 | 1400 - USHURU WA USAFIRISHAJI | 79,000,000.00 | 35,749,966.00 | 45.25 |
| 3 | 1500 - LESSENI ZA BIASHARA | 59,070,000.00 | 89,024,000.00 | 150.71 |
| 4 | 1800 - ADA YA HUDUMA | 83,630,000.00 | 125,124,611.34 | 149.62 |
| 5 | 2000 - FII, FAINI NA ADHABU | 3,300,000.00 | 1,478,800.00 | 44.81 |
| **JUMLA KUU** | | **240,000,000.00** | **264,333,477.34** | **110.00** |

**Uchunguzi wa Kamati**

Katika kufuatilia taarifa hii Kamati ya LAAC ilibaini yafuatayo:

1. Baadhi ya vifungu vya taarifa ya mapato vinagongana kwa mfano:
    a. Kifungu cha Faini na adhabu makisio ya bajet yaliyopitishwa na Madiwani ni Tsh. 5,710,000, isipokuwa kwamba, makisio yaliyowasilishwa kwenye Kamati kwa kifungu hicho ni Tsh. 3,300,000
    b. Kifungu cha Huduma kwa Madiwani ni Tsh. 81,040,000 na kwa Kamati ni Tsh. 83,630,000
2. Kwenye Taarifa ya Hesabu za Mwisho wa Mwaka utaratibu wa uandishi wa vifungu haupo sahihi, kwani baadhi ya vifungu vyenye asili moja vimeandikwa kwenye "Note" tofauti. Kwa mfano, vifungu vinavyohusiana na huduma.

Kutokana na kasoro hizo Kamati ya LAAC inapendekeza yafuatayo:

1. Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni kuhakikisha kuwa inakuwa makini wakati wa kuandaa Taarifa ya Hesabu za Mwisho wa Mwaka ili kuepusha usumbufu kwa watumiaji wa Taarifa hiyo.
2. Halmashauri ihakikishe kuwa inakuwa makini wakati wa kuandaa taarifa zake ili iwasilishe taarifa zinazolingana.

**Taarifa za Matumizi**

Halmashauriya Wilaya ya Micheweni ilikadiriwa kutumia jumla ya Shilingi 4,522,700,000.00 kwa kazi za kawaida na 327,000,000.00 kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia tarehe 30.06.2020 jumla ya shilingi 4,237,776,856.00 zimetumika kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 93.70% ya makadirio na shilingi 231,172,268.00 kwa kazi za maendeleo sawa na asilimia 77.80% ya makadirio.

**Majibu**

Matumizi ya fedha hizo yalitumika katika mpangilio ufuatao:

| NA. | KIFUNGU-MAELEZO | MAKISIO | MATUMIZI HALISI | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | MATUMIZI YA MSHAHARA | 2,940,600,000.00 | 3,347,865,965.00 | 113.85 |
| 2 | MATENGENEZO NA UKARABATI WA KAWAIDA | 109,736,000.00 | 85,071,937.00 | 77.52 |
| 3 | MALIPO MENGINE | 65,545,000.00 | 45,704,259.00 | 69.73 |
| 4 | MANUNUZI NA MATUMIZI | 848,445,000.00 | 623,797,140.00 | 73.52 |
| 5 | MISAADA NA RUZUKU | 62,000,000.00 | 52,224,000.00 | 84.23 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 6 | UNUNUZI WA VIFAA NA UJENZI | 257,100,000.00 | 304,560,608.00 | 118.46 |
| **JUMLA KUU** | | **4,283,426,000** | **4,459,223,909** | **110.00** |

**Uchunguzi wa Kamati**
Katika kufuatilia taarifa ya matumizi yafuatayo yamebainika:

1. Matumizi ya mishahara yameongezeka kutokana na ajira mpya iliyofanywa na marekebisho ya mshahara watendaji, barua ya tarehe 19 Septemba, 2019 yenye kumbukumbu Namba OR/TMSMIM/U.ZO/I/VOL.IV/76 inathibitisha.
2. Baadhi ya taarifa zinatofautiana, kwa mfano:
    a. Makisio ya matumizi yaliyowasilishwa na Halmashauri na taarifa ya Mkaguzi wa Ndani.
    b. Taarifa ya Hesabu ya Mwisho wa Mwaka inaonesha kuwa jumla ya fedha zote zilizopokelewa ni Tsh. 4,468,949,124.34 wakati kwenye taarifa ya Kamati wameeleza kuwa wamepokea jumla ya Tsh. 4,237,776,856.00
3. Baraza la Madiwani halipitishi fedha za matumizi mengineyo na mishahara na badala yake linapitisha mapato ya ndani tu.

**Mapendekezo ya Kamati**
Ili kasoro kama hiyo isijitokeze tena Kamati ya LAAC ilipendekeza yafuatayo:

1. Baraza la Madiwani lihakikishe kuwa wakati wa kuandaliwa bajeti ya Halmashauri linajadili na kupitisha fedha za matumizi mengineyo, mishahara na mapato ya ndani.
2. Halmashauri kuwa makini wakati wa kutekeleza majukumu yake ili kuepusha kasoro mbali mbali.

MATOKEO YA UKAGUZI

**4.7.1 Malipo yasiokuwa na vielelezo Shilingi 55,179,459.00**
Ukaguzi umebaini Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni imefanya malipo ya shiliingi 55,179,459.00 kwa ajili ya kugharamia shughuli mbali mbali za Halmashauri.

Dosari iliobainika na ukaguzi ni kukosekana kwa vielelezo vya matumizi hayo, kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34 cha sheria ya Usimamizi wa fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016.

**Majibu**
Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni inakiri kwamba ni kweli jumla ya Shilingi 55,179,459.00 zimelipwa bila ya kuwa na vielelezo vya matumizi, ila inaahidi haitoendelea tena na kufanya makosa hayo, na vielelezo vyote vilivokosekana tayari vimeshafungamanishwa na vocha husika.

**Uchunguzi wa Kamati**

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC ilibaini yafuatayo:

1. Wakati Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anatekeleza jukumu lake baadhi ya vielelezo vilikuwa Mamlaka ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa – ZAECA.
2. Halmashauri haiifanyii kazi Ripoti ya Mkaguzi wa Ndani, hii ni kutokana na kuwa baadhi ya hoja zilizoibuliwa na Mkaguzi wa Ndani zimeibuliwa pia na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.
3. Halmashauri ilichelewa kupeleka majibu ya "Management letter" ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali jambo lililopelekea hoja kuonekana kuwa nyingi.

Hivyo, hoja hii imebaki kama ilivyo.

**Mapendekezo ya Kamati**

Kutokana na dosari hiyo, Kamati ya LAAC ilipendekeza yafuatayo:

1. Halmashauri izifanyie kazi hoja mbali mbali zinazoibuliwa na Mkaguzi wa Ndani ili kuepuka hoja zisizo na lazima.
2. Halmashauri ichukue juhudi za makusudi kujibu hoja zilizoorodheshwa na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwenye "Management letter" ili kuepusha kuwa na hoja nyingi na zisizo na msingi.

**4.7.2 Malipo kwa watowa huduma wasiosajiliwa Shilingi 57,316,551.00**

Jumla ya shilingi 57,316,551 zimelipwa kwa ajili ya huduma mbali mbali za Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni, ukaguzi umebaini kwamba watoa huduma hao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa mali za Umma ambapo kunapelekea kuikosesha Serikali mapato.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 23(1) cha Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma nambari 11 ya mwaka 2016 pamoja na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya nambari 12 ya mwaka 2016.

**Majibu**

Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni inakiri kwamba ni kweli jumla ya Shilingi 57,316,551.00 zimelipwa kwa watowa huduma wasiosajiliwa, ila inaahidi haitoendelea tena na kuwatumia watoa huduma ambao hawajasajiliwa.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya LAAC ilibaini kuwa kasoro hii imetokea kwa kuwa Watendaji wa Halmashauri walikuwa hawana taaluma ya kutosha ya Sheria husika.

Hivyo, hoja hii imebaki kama ilivyo pamoja na hayo Kamati hii inaishauri Halmashauri

kuwa makini katika kutekeleza shughuli zao.

### 4.7.3 Malipo yaliyofanywa nje ya vifungu vya miradi shilingi 49,458,855

Jumla ya shilingi 49,458,855 zimelipwa na Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Ukaguzi umebaini kwamba malipo hayo hayakulipwa kwa mujibu vifungu vya miradi husika bila ya kufuata utaratibu wa uhaulishaji.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 75(7) na kifungu nambari 80 cha Sheria ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa Zanzibar nambari 7 ya mwaka 2014.

**Majibu**

Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni inakiri kwamba ni kweli jumla ya Tsh. 49,458,855 zimelipwa nje ya vifungu vya miradi, ila Halmashauri inaahidi haitoendelea tena kufanya matumizi nje ya vifungu.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kutokana na maelezo hayo, hoja hii imebaki kama ilivyo pamoja na hayo Kamati hii inaishauri Halmashauri kuwa makini katika kutekeleza shughuli zao.

### 4.7.4 Vifaa ambavyo havijarikodiwa kwenye daftari la ghalani Shilingi 21,124,230.00

Ukaguzi umebaini Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni imefanya manunuzi ya vifaa mbali mbali vyenye thamani ya shilingi 21,124,230 kwa ajili ya matumizi ya Ofisi ya Halmashauri. Dosari iliyobainika ni kuwa vifaa hivyo havijarikodiwa katika daftari la ghalani.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Ununuzi na Ukodishwaji wa Mali za Umma nambari 11 ya mwaka 2016.

**Majibu**

Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni inakiri kwamba ni kweli jumla ya Shilingi 21,124,230.00 zimelipwa kwa vifaa mbali mbali kwa matumizi ya ofisi, vifaa hivyo tayari vimeshaingizwa katika ghala na Halmashauri inaahidi haitoendelea tena kutokuvingiza vifaa vyote vilivonunuliwa katika ghala.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya LAAC ilibaini kuwa Mtunza Ghala “Storekeeper” ndie aliyekuwa akitekeleza pia na jukumu la ununuzi hivyo, kutokana na wingi wa kazi alishindwa kuzitekeleza kazi zote kama utaratibu unavyoelekeza.

Hivyo, hoja hii imebaki kama ilivyo kwa kuwa kitendo kilichokuwa kinafanyika ni kinyume na utaratibu pamoja na hayo Kamati hii inaishauri Halmashauri kuwa na watendaji wawili tofauti watakaoshughulikia mambo ya ghalani na ununuzi.

#### 4.7.5 Hati za malipo zilizokosekana kwa ukaguzi Shilingi 236,647,141.00

Ukaguzi umebaini Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni imefanya malipo ya shilingi 236,647,141 kwa ajili ya matumizi mbali mbali. Dosari iliyobainika ni kukosekana kwa hati za malipo husika. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016.

**Majibu**

Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni inakiri kwamba nikweli Jumla ya Shilingi 236,647,141.00 zimelipwa kwa matumizi mbali mbali ya ofisi, Hati zote ambazo zimekosekana kwa ukaguzi zipo katika mafaili na Halmashauri inaahidi haitoendelea tena na kosa la kutoziwasilisha hati za malipo kwa Mkaguzi anapokuja kwa ukaguzi.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya LAAC ilibaini kuwa wakati Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anatekeleza majukumu yake baadhi ya hati zilikuwa zinatumiwa na Mkaguzi mwengine kitendo hicho kimepelekea baadhi ya hati kukosekana ingawa zilikuwepo.

Kutokana na hali hiyo, Kamati ya LAAC imeifuta hoja hii na imeishauri Halmashauri endapo itatokezea tena hali kama hiyo isisite kutoa taarifa hizo kwa yule Mkaguzi atakayeomba kufanya ukaguzi mwisho ili kuepusha hoja zisizo na msingi.

#### 4.7.6 Dosari katika ukusanyaji wa mapato ya Minara

Ukaguzi umebaini Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni inakusanya mapato ya Mnara na mabango kupitia wakala kampuni ya Al-Jumra ambapo umeshishwa kuona kima halisi cha fedha kilichokusanywa na kampuni hiyo.

Aidha, ukaguzi umebaini uwepo wa makubaliano baina ya kampuni hivyo na Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni ambapo kampuni ya Aljumra inachukua asilimia 40 ya mapato yaliokusanywa na asilimia 60 inawasilishwa Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni.

Katika makubaliano hayo dosari mbali mbali ziliweza kubainika kama ifuatavyo:

1. Kukosekana kwa utaratibu wa ushindani uliotumika kumpata wakala huyo wa ukusanyaji wa mapato kwa niaba ya Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma nambari 11 ya mwaka 2016.
2. Kukosekana kwa taarifa ya kibenki (Bank Statement) ya kampuni ya Aljumra ili kujiridhisha kiasi halisi cha makusanyo ambacho kinakusanywa kwa mwezi ili kuweza kujiridhisha usahihi wa kiwango kilichoripotiwa.
3. Kukosekana kwa Mkataba kati ya Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni ambao unaonyesha makubaliano ya pande mbili katika kazi ya ukusanyaji wa

mapato hayo, kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma nambari 11 ya mwaka 2016.

Kukusanya mapato kupitia wakala wa ukusanyaji wa mapato ya Minara kunapelekea Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni kukosa mapato kwa kuwa kazi hiyo inaweza kufanywa na Halmashauri bila ya kumtumia Wakala.

Ukaguzi unashauri Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni kufanya Upembuzi Yakinifu ili kuhakikisha Halmashauri inapata tija katika utekelezaji na usimamizi wa rasilimali za Umma, pamoja na kuhakikisha utowaji wa zabuni unafuatwa kwa mujibu wa Sheria ili kuwepo kwa uwazi na uwajibikaji katika utoaji wa zabuni na kuhakikisha mapato yanakusanywa kwa mujibu wa sheria.

**Majibu**

Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni inakiri kwamba ni kweli inakusanya mapato kupitia Kampuni ya Al – Jumura na jumla ya Shilingi 38,302,000.00 zimekusanywa na Kampuni hiyo kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ila suala la ukusanyaji wa mapato ya vianzio hivyo kwa sasa yameshachukuliwa na Serikali kuu na kuratibiwa ili Kampuni ya Serikali iweze kukusanya mapato hayo.

**Uchunguzi wa Kamati**

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC ilibaini yafuatayo:

1. Halmashauri hii haijapokea fedha hata moja tangu mapato hayo yaanze kukusanywa na Wakala wa Serikali Mtandao.
2. Kampuni ya Al jumura inaidai Halmashauri, hata hivyo, Halmashauri haijailipa Kampuni hiyo kwa madai kuwa muda wa mkataba umemalizika.

**Mapendekezo ya Kamati**

Kutokana na kasoro hizo Kamati ya LAAC ilipendekeza yafuatayo:

1. Wakala wa Serikali Mtandao iwalipe Halmashauri fedha zote za mapato zinazotokana na minara ili Halmashauri iweze kutekeleza shughuli zake ipasavyo.
2. Halmashauri ilipe deni la Kampuni ya Al jumura kwa kuwa Kampuni hiyo ilitekeleza wajibu wake.

### 4.7.7 Tofauti katika taarifa za makusanyo ya mapato

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwepo kwa tofauti katika kumbukumbu za mapato ya Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni. Hali ambayo inapelekea ukaguzi kushindwa kujuwa usahihi wa mapato halisi yaliyokusanywa kwa kupitia taarifa za kumbukumbu za mfumo wa mapato, daftari la mapato na taarifa za benki.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016.

**Majibu**
Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni inakiri kwamba ni kweli kuna tofauti katika uandaaji wa taarifa za mapato ila tayari imeshafanya mlinganisho wa taarifa za Halmashauri za zile za kibenki ili kuondoa mkanganyiko ulipo kati ya Benki na za Halmashauri.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**
Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC ilibaini kuwa mtandao "network" ulikuwa na matatizo na ndio maana taarifa zikatofautiana.

Hivyo, kutokana na kasoro hiyo, Kamati ya LAAC ilishauri Halmashauri kwenda sambamba na mfumo, aidha, mfumo uunganishwe na Benki ili kuwa taarifa sahihi na zinazolingana.

## 4.8 BARAZA LA MJI CHAKE CHAKE

**Taarifa ya Mapato**
Kwa mwaka wa fedha 2019/2020 Ofisi ya Baraza la Mji Chake Chake ilikadiria kukusanya jumla ya Tzs 600,000,000/= kutoka katika vianzio vyake mbali mbali na hadi kufikia 30 June 2020 ilifanikiwa kukusanya jumla ya Tzs 523,137,240/= sawa na asilimia 87.2% ya makidirio.

**Majibu**
Ofisi ya Baraza la Mji Chake Chake kwa mwaka wa fedha 2019/2020 halikufanikiwa kufikia malengo ya makusanyo kwa sababu ifuatazo;-
Kupungua kwa kianzio chake cha mapato yatokanayo na usafirishaji wa mali asili zisizorejesheka (kware) ambayo chanzo hichi kwa sasa kinakusanywa na serikali kuu kupitia wizara ya kilimo na mali asili na Ofisi ya Baraza kupewa mgao lakini tunacheleweshewa mgao huu.

Mchanganuo wa vianzio hivyo ni kama unavoonekana katika jadweli hapo chini.

| **Chanzo** | **Makadirio** | **Halisia** | **Asilimia(%)** |
|---|---|---|---|
| Masoko | 84,000,000 | 72,123,000 | 85.9 |
| Maegesho | 53,630,000 | 44,283,000 | 82.6 |
| Leseni zabiashara | 153,700,000 | 122,852,000 | 79.9 |
| Ada yausafi | 40,170,000 | 34,608,000 | 86.2 |
| Adaya kware | 57,840,000 | 15,420,000 | 26.7 |
| Ada ya diko | 1,800,000 | 2,764,000 | 153.6 |
| Kodi ya milango | 52,100,000 | 49,810,000 | 95.6 |
| Kodi ya ukumbi | 23,300,000 | 12,820,000 | 55.0 |
| Fomu za maombi | 4,800,000 | 4,785,000 | 99.7 |
| Chinjio | 12,000,000 | 5,635,000 | 47.0 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Ada ya mabango | 50,000,000 | 45,986,840 | 92.0 |
| Kodi ya gari | - | 21,550,000 | |
| Ada mbali mbali | 66,660,000 | 90,500,400 | 135.8 |
| **JUMLA** | **600,000,000** | **523,137,240** | **87.2%** |

### Uchunguzi wa Kamati

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC ilibaini yafuatayo:

1. Kware ndio kianzio kikuu cha mapato ya Baraza la Mji Chake chake.
2. Mapato ya fedha zinazotokana na kware yamepungua baada ya mapato hayo kukusanywa na Wizara ya Maji, Nishati na Madini. Kwa mwaka wa fedha 2018/2019 kianzio cha mapato cha kware kilikusanya 75,200,000 wakati mwaka wa fedha 2029/2020 kilikusanya 15,420,000.
3. Mwaka wa fedha humalizika bila ya Baraza la Mji Chake chake kupatiwa fedha yoyote inayotokana na kware.
4. Baraza linatakiwa lipatiwe asilimia 15 ya makusanyo ya kware hata hivyo kwa mwaka wanaopewa basi hawapewi kwa wakati.
5. Kianzio cha mapato cha Ada mbali mbali hakina "Note" yake jambo ambalo ni kinyume na taratibu za kifedha.

### Mapendekezo ya Kamati

Ili kasoro kama hizo zisijitokeze tena katika siku zijazo, Kamati ya LAAC ilipendekeza yafuatayo:

1. Wizara ya Maji, Nishati na Madini ilipatie Baraza fedha zinazotokana na kware kila mwaka na kwa wakati ili Baraza liweze kutekeleza shughuli zake na kuleta tija iliyokusudiwa.
2. Serikali ifanye utafiti wa kutosha kabla haijaamua baadhi ya mambo ili kuepusha kupata hasara, kwani mapato ya kware yameshuka baada ya kukusanywa na Wizara husika.
3. Kianzio cha mapato cha Ada mbali mbali kiwe na "Note" yake ili kijulikane kimejumuisha mambo gani.
4. Kianzio cha mapato cha kodi ya gari kimetokea katika ya mwaka, hivyo, kilipaswa kwa mwaka huo kionekane kuwa ni mapato mengineyo na mwaka unaofuata ndio kiwekwe kama ni kodi ya gari.

### Taarifa ya Matumizi

Baraza la Mji Chake Chake ilikadiria kutumia jumla ya Tzs 5,853,203,709 kwa matumizi ya kazi za kawaida lakini, hadi kufikia 30 June, 2020 ilitumia jumla ya Tzs 6,714,538,954/= sawa na asilimia 114.7% ya makadirio.

### Majibu

Baraza la Mji Chake Chake kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ilitumia zaidi katika matumizi ya kazi za kawaida kwa sababu ya Mishahara ya wafanyakazi kwa waajiriwa wapya.

Makadirio na Halisia ya matumizi ya kazi za kawaida ya Ofisi ya Baraza la Mji Chake Chake kwa mwaka wa fedha 2019/2020 yalikuwa kama ifuatavyo:-

| | **Makadirio** | **Halisi** | **Asilimia** |
|---|---|---|---|
| Uendeshaji | 5,853,203,709 | 6,714,538,954 | 114.7% |

Vile vile, Baraza lilikadiria kutumia TZS 165,000,000/= kwa kazi za maendeleo lakini, hadi kufikia 30 June, 2020 lilitumia TZS 160,189,900/= sawa na asilimia 97.1% ya makadirio.

Makadirio na Halisia ya matumizi ya kazi za maendeleo ya Ofisi ya Baraza la Mji Chake Chake kwa mwaka wa fedha 2019/2020 yalikua kama ifuatavyo:-

| **Jina la Mradi** | **Makadirio** | **Matumizi Halisi** | **Asilimia** |
|---|---|---|---|
| Ukamilishaji wa Skuli ya Maandalizi Mtimbu | 40,000,000 | 39,851,000 | 99.6 |
| Ujenzi wa Skuli ya Msingi Kwale | 20,000,000 | 19,797,000 | 99.0 |
| Ujenzi wa vyoo Skuli ya Ndagoni | 20,000,000 | 20,947,500 | 104.7 |
| Ukarabati wa maduka Soko la Chake Chake | 70,000,000 | 64,994,400 | 92.8 |
| Ukarabati wa daraja la Gawani | 15,000,000 | 14,600,000 | 97.3 |
| **JUMLA** | **165,000,000** | **160,189,900** | 97.1% |

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Katika kufuatilia taarifa ya matumizi Kamati ilibaini kuwa Taarifa ya Hesabu za Mwisho wa Mwaka haina "Statement of Financial Position" kitu ambacho ni muhimu kuwekwa ili kujua madeni, mali na kadhalika.

Kutokana na kasoro hiyo, Kamati ya LAAC imependekeza kwa Baraza kuwekwa taarifa hiyo ili kupata taarifa sahihi.

**MATOKEO YA UKAGUZI**

**4.8.1 Malipo kwa wafanyabiashara wasiosajiliowa Tsh. 6,742,687**

Jumla ya shilingi 6,742,687 zimelipwa kwa ajili ya huduma mbalimbali za Baraza la Mji Chake Chake, ukaguzi umebaini kwamba watoa huduma hao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzina Uondoshaji wa mali za Umma ambapo kunapelekea kuikosesha Selikali mapato.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 23(1) cha Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma nambari 11 ya mwaka 2016 pamoja na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya nambari 12 ya mwaka 2016.

**Majibu**
Mkaguzi kweli anaweza kuona malipo haya yamelipwa kwa wafanyabiashara ambao hawakusajiliwa na Mamlaka kwa kutoviona vyeti kwa hatua ya awali. Hata hivyo, wafanyabiashara hawa ni halali ambao wamesajiliwa kiukamilifu na Mamlaka ya Manunuzi. Hakikisho ni vyeti vya mamlaka.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**
Kamati imeridhika na majibu ya Baraza hivyo, hoja hii imefutwa.

### 4.8.2 Hati za malipo zilizokosekana kwa ukaguzi TZS 22,061,970

Ukaguzi umebaini Baraza la Mji Chake Chake limefanya malipo ya shilingi 32,388,860 kwa ajili ya kugharamia shughuli mbalimbali za Baraza. Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kukosekana kwa vielelezo vya matumizi hayo. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34 cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016.

**Majibu**
Hati hizi zote zilikuepo wakati wa ukaguzi na ni hati za chanjo ya kitaifa ya Surua Rubella ambayo ilifadhiliwa na UNICEF pamoja na WHO. Zilikaguliwa na ukaguzi kutoka Wizara ya Afya na walizitaka tuziweke kwenye faili lake maalum hata hivyo kutokuletwa kwa hatua ya awali ya ukaguzi wa CAG ni changamoto ya mawasiliano na upya wa watendaji wa sehemu ya hesabu.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**
Kamati ya LAAC haikuridhika na majibu ya Baraza kwa kuwa baada ya vocha hizo kukaguliwa na Kamati ilibainika kuwa vocha hizo zilikaguliwa na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, isipokuwa kwamba vocha hizo hazikukamilika.

Aidha, Kamati ya LAAC ilibaini kuwa baadhi ya Hati za Malipo zimeandikwa kwenye Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, ingawa Hati hizo zina alama ya kuwa Mkaguzi Mkuu amezikubali. Kwa mfano, Hati ya Malipo No. 128/9 yenye thamani ya Tsh. 6,490,000 na Hati No. 70/10 yenye thamani ya Tsh. 2,000,000.

Kwa msingi huo, kiwango halisi cha Hati za Malipo zilizokosekana kwa ukaguzi ni Tsh. 13,571,970 badala ya 22,061,970 zilizoelezwa na Mkaguzi Mkuu.

### 4.8.3 Malipo yasiokuwa na vielelezo TZS 32,388,860

Baraza la Mji Chake Chake limeingia mkataba wa usafi wa Mji kwa kipindi cha miezimitatu na kampuni ya usafi ya Track Force for Environment.

Ukaguzi umebaini kwamba Baraza limeipatia Kampuni hiyo gari la kubebea taka, Dereva, vifaa vya usafishaji pamoja na mafuta ya petroli lita 6,568 kinyume na mkataba, ambapo jumla ya shilingi 1,571,876 zimelipwa kwa Kampuni kwa ajili ya

huduma ya usafi wa Mji katika kipindi cha mwaka 2019/2020.

Kufanya malipo nje ya Mkataba kunaweza kupelekea upotevu wa fedha na rasilimali za Umma pamoja na kwenda kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016.

**Majibu**

Wakati wa ukaguzi ulipofanyika kuna baadhi ya vielelezo viliparaganyika katika hati nyengine kutokana na kutakiwa kufanyiwa ukaguzi wa mara kwa mara, hata hivyo, vielelezo hivyo viliwekwa kwenye hati zake husika.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya LAAC iliyakubali majibu ya Baraza kwani ilijiridhisha hilo kupitia barua ya tarehe 17 Novemba, 2021 yenye kumbukumbu Namba OR/TMSMIM/U.16/1/VOL.III/15 inayoeleza kufanyika kwa Ukaguzi Maalum wa Mkaguzi wa Ndani wa Miradi ya Maendeleo.

Hata hivyo, Kamati ya LAAC ilishtushwa na kitendo cha Mkaguzi wa Hesabu za Ndani wa Wizara kufanya ukaguzi na Pemba kwa kisingizio cha ukaguzi maalum ingawa Kamati ilielezwa kuwa hilo ni jambo la kawaida kufanyika.

Kutokana na hilo, Kamati ya LAAC inapendekeza kwa Serikali kuachana na utaratibu kwani ni kuitia Serikali hasara zisizo za lazima.

### 4.8.4 Matumizi yaliyofanyika nje ya mkataba wa usafishaji shilingi 14,571,876

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 10,000,000 zimelipwa kwa msambazaji Omar Hamad Kombo kupitia hati ya malipo nambari 12/8 ya tarehe 1/8/2019 kwa hundi nambari 003731 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi ikiwemo Mawe Trips 12, Matufali Pcs 3500, Mchanga Trips 6, Kokoto Trips 4, Saruji Pkts 210, Nondo mm 12 Pcs12, Nondo mm 10 Pcs 55, Nondo mm6 Pcs 20, Mbao 2x2, Pcs 130, Mbao 1x8 Pcs 120, Binding Wire Roli 5.

Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kwamba thamani ya vifaa hivyo hailingani na ujenzi wa vyoo hivyo pia ni kwenda kinyume na Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma nambari 11 ya mwaka 2016.

**Majibu**

Baraza la Mji Chake lilingia mkataba wa usafi na Kampuni ya Usafi Task Force for Environment na gari la kubebea taka, dereva wa gari, kuitia mafuta gari hiyo na baadhi ya vifaa vya usafi bado lilibaki kuwa ni jukumu la ofisi kama mkataba unavyoeleza. Hakikisho ni mkataba husika.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC ilibaini yafuatayo:

1. Kampuni ya Usafi Task Force for Environment ilitekeleza shughuli ambazo hazikuainishwa kwenye mkataba.
2. Mkataba uliofungwa haukuwa na tija kwa Baraza.

Kutokana na kasoro hizo Kamati ya LAAC imelitaka Baraza la Mji Chake chake kuwa makini katika kutekeleza majukumu yake ili kuepuka kulitia hasara Baraza hilo.

### 4.8.5 Kukosekana kwa thamani ya ujenzi wa vyoo vya skuli ya maandalizi Mtimbu Pujini Shilingi 10,000,000

Ukaguzi umebaini kuwepo kwa makusanyo yenye jumla ya shilingi 48,085,000 ambayo yameoneka kukusanywa kupitia mfumo wa ukusanyaji wa mapato (Revenue Colletion System) wa Baraza la Mji la Chake Chake. Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kwamba mapato hayo hayawasilishwi benki kupitia hesabu ya mapatoya Baraza. Kufanya hivyo kunaweza kupelekea upotevu na matumizi mabaya ya fedha za mapato Pamoja na kwenda kinyume na Sheria ya Usimamizimwa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016.

#### Majibu

Ziada ya vifaa hivi vilitumika katika ujenzi wa mashimo mawili kwa ajili ya matundu ya vyoo hivyo, ujenzi wa kuta mbili za ziada vyooni zilizotakiwa kujengwa ili kufanya hifadhi nzuri zaidi ya wanafunzi ambapo kabla ya hapo ujenzi huo haukuwepo lakini pia ni pamoja na ujenzi wa mzunguko mzima wa baraza ya vyooni.

#### Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Kamati ya LAAC haikukubaliana na majibu ya Baraza, hivyo, hoja hii imebaki kama ilivyo.

### 4.8.6: Mapato ambayo hayakuingizwa benki shilingi 48,085,000

Ukaguzi umebaini kuwepo kwa makusanyo yenye jumla Tsh. 48,085,000 ambayo yameonekana kukusanywa kupitia mfumo wa ukusanyaji wa mapato wa Baraza. Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kwamba mapato hayo hayawasilishwi benki kupitia hesabu ya mapato ya Baraza. Kufanya hivyo, kunaweza kupelekea upotevu na matumizi mabaya ya fedha za mapato pamoja na kwenda kinyume na Sheria ya Usimamiz wa Fedha za Umma Namba 12 ya mwaka 2016.

#### Majibu

Kama mchanganuo wa vyanzo vya mapato ulivyo hapo chini utaona kuwa mapato yameingizwa zaidi benki kuliko kwenye mfumo kwa kiasi cha Tsh. 30,394,400 i.e (523,137,240/= -492,742,840/=). Lakini Mkaguzi wa CAG alichokifanya ni kuchukua baadhi ya vyanzo vilivyokuwa vikubwa kwenye mfumo na kulinganisha na benki ambavyo ni kidogo sasa akajua yeye kuwa pesa hizo hazikupelekwa benki lakini haikuwa hivyo bali Changamoto ni kama zifuatazo:-

1. Upya wa watendaji kwa mara ya kwanza kutumia mfumo wa kielektroniki wa ukusanyaji wa mapato hivyo makosa ya muingiliano wa vyanzo yakijitokeza. Hata hivyo kwa sasa tumefikia pazuri kwa kufanyiwa mafunzo ya mara kwa mara ili kuondokana na changamoto hii.
2. Upya wa watendaji kutumia mashine za POS ambayo risiti ikiweza kutoka mara mbili au zaidi kwenye mashine ya POS lakini risiti za mkono (bank) inakua moja tu. Hivyo, kusababisha kwenye mfumo kuwa kukubwa kuliko benki.
3. Kutokuoana kwa vyanzo vilivyomo kwenye mfumo na cashbook ya mapato, lakini kwa sasa umeshaandaliwa utaratibu wa vyanzo hivyo viowane kuondosha usumbufu huo.

Hivyo, tofauti hii ya Benki kuwa kubwa kuliko Mfumo ni kuhamasika kwa wafanyabiashara kulipia benki moja kwa moja lakini halafu baadhi yao wanachelewa kuja kuchukua risiti zao kwa wakati ili kuingizwa kwenye mfumo, na fedha hizo zimeingia kwenye mfumo kwa mwaka wa fedha 2020/2021 baada ya wao kuja ofisini na kudai risiti zao**.**

Mchanganuo wa vianzio vya mapato ni kama ufuatao:-

| CHANZO | BENKI | MFUMO |
|---|---|---|
| SERVICE CHARGE (Ada ya Usafi) | 34,608,000 | 36,162,000 |
| MAEGESHO | 44,283,000 | 44,550,500 |
| LESSENI | 122,852,000 | 151,697,00 |
| USHURU | | 15,909,000 |
| USHURU MASOKO | 72,123,000 | 61,132,000 |
| KWARE | 15,420,000 | 16,930,000 |
| MADIKO | 2,764,000 | 2,200,000 |
| KODI YA UKUMBI | 12,820,000 | 12,420,000 |
| KODI YA MILANGO | 49,810,000 | 49,400,000 |
| MATANGAZO YA BIASHARA | 45,986,840 | 31,419,340 |
| MENGINEYO | 90,500,400 | 70,923,000 |
| ADA YA GARI | 21,550,000 | |
| FOMU ZA MCHANGA | 4,785,000 | |
| UINGIZAJI WA WANYAMA | 5,635,000 | |
| JUMLA KUU | 523,137,240 | 492,742,840 |

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC ililishauri Baraza la Mji Chake chake kufanya utafiti mara kwa mara kwa yale mambo ambayo wanayasimamia ili kuepusha kuonekana changamoto nyingi. Hii inamaanisha kwamba baada ya kuona kuwa mlinganisho “reconciliation” haupo sawa ni vyema wakachukua hatua mapema.

Pamoja na hayo hoja hii imebaki kama ilivyo.

### 4.8.7 Kushindwa kwa Baraza kukusanya ada ya usafi shilingi 33,864,000

Baraza la Mji Chake Chake lina wajibu wa kusimamia na kukusanya mapato kupitia ada ya usafi katika maduka 634 kati ya maduka 1,252 yaliyopo katika Wilaya ya Chake Chake kwa mwaka wa fedha wa fedha 2019/2020 ambapo kila duka linapaswa kulipia shilingi 9,000 kwa mwezi.

Ukaguzi umebaini kwamba Baraza limeshindwa kukusanya jumla ya shilingi 33,864,000 zitokanazo na ada ya usafi ambapo ni kuikosesha serikali mapato kupelekea kushindwa kufikia malengo yaliyokusudiwa kutekelezwa.

**Majibu**

Ukichukua jumla ya maduka ambayo yanatozwa ada ya usafi idadi (634*9000*12) = 68,472,000 na makusanyo halisi ni 34,608,000 ni kweli kuna tofauti ambayo haikukusanywa kwa mwaka huu wa fedha 2019/2020.

Hii ni kutokana na sababu zifuatazo:

1. Ukaidi wa wafanyabiashara kulipa ada kwa hiari.
2. Baadhi ya Wafanyabiashara kufunga biashara zao na kupelekea idadi ya maduka kupungua.

Hata hivyo, hatua za ofisi zilichukuliwa kama kuwapeleka Mahakamani kwa Wafanyabiashara ambao hawakulipa ada hiyo na fedha hizo zimeingia katika mwaka mwengine wa fedha 2020/2021.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC ilibaini yafuatayo:

3. Mahakimu wa Mabaraza wanalipwa mara mbili yaani wanalipwa na Taasisi zao na Mabaraza jambo ambalo ni kinyume na utaratibu.
4. Hakuna kiwango maalum cha malipo jambo linalopelekea Mahakimu hao kutokufanya kazi yao ipasavyo.

Kutokana na dosari hizo, Kamati ya LAAC inayashauri Mabaraza ya Miji kutokuwalipa posho Mahakinu kwa kuwa kufanya kazi katika Mabaraza ni sehemu ya kazi zao.

### 4.8.8: Kutokuonyeshwa kwa mapato katika taarifa za hesabu shilingi 21,355,000

Jumla ya Tsh. 21,355,000 ni fedha za mapato zilizokusanywa na Baraza la Mji Chake chake kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Ukaguzi umebaini kuwa fedha za makusanyo hayo hazikuripotiwa na kuoneshwa katika Taarifa za Hesabu za Mwisho wa Mwaka kunapelekea taarifa ya mapato kutokuonesha sura halisi na sahihi. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya usimamizi wa Fedha za Umma Namba 12 ya mwaka 2016.

**Majibu**

Mapato haya ambayo yametokana na chanzo cha vibali vya ujenzi yameingizwa kiukamilifu katika taarifa za mapato pia yameingizwa kiukamilifu katika taarifa za kufunga mahesabu ya Baraza (Financial Statements) katika mwaka wa fedha 2019/2020. Lakini zimeingizwa ndani ya kianzio cha ada mbalimbali na ndio maana kianzio hiki kikaonekana kina fedha kubwa za makusanyo kiasi cha TZS 90,500,400/=. Hii ni kuwa pia mapato ya fedha yatokanayo na vibali vya ujenzi yamo ndani yake. Lakini ofisi ya Baraza tayari imeshaifanyia kazi kasoro hii, hivyo kwa mwaka wa fedha unaofuatia chanzo hiki kitaonekana kwenye sehemu yake sahihi.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya LAAC ilijiridhisha na kilichoelezwa na Baraza hivyo, hoja hii imefutwa, hata hivyo, Kamati imelitaka Baraza kufunga hesabu zake kama taratibu za fedha zinavyoelekeza

## 4.9 BARAZA LA MJI MKOANI

**Taarifa ya Mapato**

Kwa mwaka wa fedha 2019/2020 Baraza la Mji Mkoani lilikadiria kukusanya jumla ya Tzs 340,000,000/= kutoka katika vianzio vyake mbali mbali na hadi kufikia 30 June, 2020 ilifanikiwa kukusanya jumla ya Tsh. 341,944,368 sawa na asilimia 100.57 ya makidirio.

**Majibu**

Baraza la Mji Mkoani halikuandaa maelezo ya moja kwa moja kuhusiana na taarifa ya mapato hivyo, lilijibu hoja za Kamati kama zilivyoulizwa.

**Uchunguzi wa Kamati**

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC ilibaini yafuatayo:

1. Hakuna utaratibu mzuri wa kuandaa Taarifa ya Hesabu ya Mwisho wa Mwaka, kwa mfano:
    a. Baadhi ya Kasma hazikuwekwa “Code”.
    b. “Note” 6 isomeke “Non Tax Revenue” au “Receipt” na sio “Other Receipt”.
    c. Kifungu cha “Others” kilichojumuishwa kwenye “Note” 6 kilipaswa kiwe ni “Note” inayojitegemea ili ijulikane kifungu hicho kimejumuisha mambo gani.
2. Kianzio cha mapato cha kware mapato yake yamepungua baada ya mapato hayo kukusanywa na Serikali Kuu.
3. Kianzio cha kware ndio kianzio kikuu cha mapato kwa Baraza hili.
4. Baadhi ya mambo yanaamuliwa na Madiwani nje ya Baraza lao jambo ambalo ni kinyume na utaratibu.
5. Madiwani hupitisha bajeti yao baada ya kumalizika kikao cha Baraza la

Wawakilishi jambo ambalo ni kinyume na utaratibu.

**Mapendekezo ya Kamati**

Ili kasoro kana hizo zisijitokeze tena Kamati ya LAAC imependekeza yafuatayo:

1. Baraza la Mji Mkoani liwe makini wakati wa kuandaa Taarifa ya Hesabu ya Mwisho wa Mwaka.
2. Maamuzi yote ya Baraza la Mji Mkoani yaamuliwe ndani ya Baraza na sio vyenginevyo.
3. Serikali Kuu ifanye utafiti kabla ya kuamua jambo ili kuepuka kupata hasara, hivyo, ni busara mapato ya kware yakabakia kukusanywa na Baraza.
4. Baraza la Mji Mkoani lihakikishe kuwa linafuata utaratibu uliowekwa wakati wa kuidhinisha bajeti ya Baraza.

**Taarifa ya Matumizi**

Baraza la Mji Mkoani lilikadiriwa kutumia jumla ya Shilingi 1,542,841,000.00 kwa kazi za kawaida na Tsh. 386,137,890.00 kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia tarehe 30.06.2020 jumla ya Tsh. 1,333,084,945.00 zimetumika kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 86.4 ya makadirio na Tsh. 200,000,000 kwa kazi za maendeleo sawa na asilimia 52 ya makadirio.

**Majibu**

Baraza la Mji Mkoani halikuandaa maelezo ya moja kwa moja kuhusiana na taarifa ya matumizi, hivyo, lilijibu hoja za Kamati kama zilivyoulizwa.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Katika kufuatilia hili Kamati ya LAAC ilibaini kuwa "Note" 9 imejumuisha matumizi ambayo hayapaswi kuwepo hapo, hivyo, Kamati imelishauri Baraza kuandaa Taarifa ya Hesabu za Mwisho wa Mwaka kama taratibu za fedha zinavyoelekeza.

MATOKEO YA UCHUNGUZI

### 4.9.1 Malipo kwa WafanyaBiashara Wasiosajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi ya Tzs 11,608,453

Jumla ya shilingi 11,608,453 zimelipwa kwa ajili ya huduma mbalimbali za Baraza la Mji Mkoani. Ukaguzi umebaini kwamba watoa huduma hao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ambapo kunapelekea kuikosesha Serikali mapato.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 23(1) cha Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma nambari 11 ya mwaka 2016 pamoja na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016.

**Majibu**

Ni kweli kwamba baadhi ya wafanya biashara waliolipwa na Baraza la Mji Mkoani walikua hawajasajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi ya manunuzi kwa mwaka 2019/2020. Malipo hayo yalitokana na malimbikizo ya malipo nyuma ambapo Bazara lilikua halina budi kumalizi kuyalipa malipo hayo, hata hivyo kwa sasa Baraza limeshachukua juhudi za kuwaamuru wafanya biashara hao waende kwenye ofisi za Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa mali za serikali kwa ajili ya kujisajili rasmi ili waweze kufanya kazi na Serikali, kwa hiyo hali hiyo imeendelea kupungua kwa kiasi kikubwa ni matarajio ya Baraza kwa mwaka huu wafanya biashara wote wenye nia ya kutoa huduma kwa baraza la Mji Mkoani watakua wameshajiliwa.

Hata hivyo, ushauri na Mapendekezo wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali wa kuhakikisha kua kila anelipwa na Serikali amesajiliwa tumeuchukua na tunaufanyia kazi.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya LAAC haikuridhika na majibu ya Baraza hivyo, hoja hii imebaki kama ilivyo, isipokuwa kwamba, Kamati imelitaka Baraza kutekeleza shughuli zake kwa mujibu wa matakwa ya Sheria na Kanuni zilizopo.

### 4.9.2 Vifaa ambavyo havikuingizwa kwenye Daftari la Ghalani vyenye thamani ya TZS 23,634,109

Ukaguzi umebaini kuwa Baraza la Mji la Mkoani limefanya matumizi ya jumla ya shilingi 23,634,109 kwa ajili ya manunuzi ya mafuta na vifaa mbalimbali. Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kuwa vifaa hivyo havikurikodiwa kwenye daftari la kutunzia vifaa vya ghalani ili kuweza kutbibitisha uhalali wa mapokezi pamoja na matumizi ya vifaa hivyo.

Kutoingizwa vifaa hivyo katika daftari la kutunzia vifaa vya ghalani ni kwenda kinyume na Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma nambari 11 ya mwaka 2016.

**Majibu**

Ukweli juu ya hoja hii ni kwamba vifaa hivi vilikua vimeshaingizwa kwenye Daftari la Ghalani lakini wakati wa ukaguzi havikuweza kuonekana kwa sababu daftari lililotumika kuingiza vifaa hivi lilikua halikuonekana hii ilitokana na mpangilio wa uwekeji wa madaftari ya Ghalani uliotokana na kaguzi mbali mbali zilizofanyika za mwisho wa mwaka. Hata hivyo, ila kwa sasa limeshaonekana na tupo tayari kuangaliwa na kuthibitisha hoja hiyo.

Aidha, Baraza la Mji Mkoani linachukua mapendekezo na ushauri wa Ofisi ya Mdhibiti

na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali za kuweka kumbukumbu kwa umakini kwa mali zinazonunuliwa kabla ya kufanya matumizi ya Mali hizo.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC ilibaini kuwa hakukuwa na mashirikiano baina ya Watendaji wa Baraza kwa kuwa daftari hilo lilikuwa likifanyiwa kazi na Mkaguzi wa Hesabu za Ndani. Hata hivyo, hoja hii imebaki kama ilivyo kwa kuwa Kamati imelikagua daftari hilo na haikuridhika na namna lilivyojazwa.

### 4.9.3 Ulipaji wa masurufu kinyume na utaratibu Tsh. 24,410,000

Jumla ya shilingi 24,310,000 zimelipwa kwa njia ya masurufu kwa ajili ya uendeshaji wa chanjo ya rubela na surua katika Wilaya ya Mkoani. Ukaguzi umebaini kwamba malipo ya masurufu hayo yamelipwa kupitia Mkaguzi wa Ndani wa Baraza kinyume na taratibu za malipo, ambapo Mkaguzi wa Ndani hakupaswa kupewa fedha kwa ajili ya malipo. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na maadili ya ukaguzi, aidha ni kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Baraza la Mkoani kuimarisha mafumo wa udhibiti wa ndani katika matumizi ya masurufu.

**Majibu**

Ni kweli kwamba Mkaguzi alikabidhiwa masurufu yaliyotajwa hapo juu kwa ajili ya kuwalipa washiriki wa zoezi la kitaifa la Chanjo ya Surua na Rubella.
Fedha hivyo inatokana na ukweli kwamba kulifanyika mafunzo ya zoezi la Chanjo maalumu iliyoendeshwa na UNICEF na WHO kupitia Wizara ya Afya kwa mashirikiano na Ofisi ya Baraza la Mji Mkoani.

Katika zoezi lile kwa bahati Mkaguzi wa Ndani na Msaidizi Mkurugenzi wa Afya ndio walioshiriki katika mafunzo hayo kwa sababu Mhasibu na mshika fedha hawakuwepo kutokana na sababu mbali mbali za kikazi na kibinadamu, kwa hiyo kwa kuwa Mkaguzi wa ndani ndie mtu pekee ambaye alionekana angalau anayo sifa kwa mujibu wa matakwa ya mashirika hayo, Mkurugenzi akaamua kumpeleka kwa ajili ya mafunzo hayo.

Aidha, Wafadhili wa zoezi hilo walisistiza kuwa wale tu waliopatiwa mafunzo kikamilifu ndio watakaoshiriki kuendesha zoezi hilo, hata hivyo utaratibu wa kuzitoa fedha hizo ulifanyika kwa kuzingatia matakwa ya sheria ya Fedhs na mkaguzi wa ndani alifanya kazi ya malipo chini ya uangalizi wa msaidizi Mkurugenzi wa Afya.

Pamoja na maelezo hayo Baraza la Mji Mkoani linapokea na kufanyia kazi mapendekezo na ushauri wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali ya kutokumpa fedha za masurufu Mkaguzi wa andani ambaye mwenyewe anatakiwa kukagua fedha jambo ambalo linaweza kupelekea kushindwa kujikagua mwenyewe.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya LAAC haikukubaliana na majibu ya Baraz na hasa ikizingatiwa kuwa fedha hizo zilikuwa zimeshaingizwa kwenye hesabu ya benki ya Baraza, hivyo, ilipaswa fedha hizo moja kwa moja zisimamiwe na mtu wa Afya.

Kwa mnasaba huo, hoja hiyo imebaki kama ilivyo.

### 4.9.4 Dosari Katika Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwepo kwa miradi mbalimbali iliyotekelezwa na Baraza la Mji Mkoani kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Katika utekelezaji wa miradi hiyo imebainika kuwepo kwa dosari zilizosababishwa na kutokufuatwa kwa taratibu za kisheria za utekelezaji wa miradi husika.

Dosari hizo zimebainika wakati wa kuhakiki Mpango kazi wa Baraza, Mpango wa ununuzi, taratibu za ununuzi, mikakati ya miradi, na taratibu za malipo.

**Dosari zilizojitokeza katika utekelezaji wa Miradi hiyo ni kama zifuatazo:-**

i. Kutokuwasilisha kwa Mpango wa Manunuzi wa mwaka kama ilivyoelezwa katika kifungu nambari 42 cha Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma nambari 11 ya mwaka 2016.

ii. Wajumbe walioteuliwa katika Kamati ya Tathmini ya miradi iliyotekelezwa hawakukidhi vigenzo kutokana na kutokuwa na barua za uteuzi, hati za kiapo cha maadili na pia kukosa uzowefu unaohitajika katika utekelezaji wa miradi hiyo jambo ambalo ni kinyume na kifungu nambari 32 cha Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

iii. Mikataba yote haijaeka muda wa uangalizi wa utekelezaji wa miradi (defect liability period).

iv. Manunuzi katika miradi yamefanywa kupitia njia ya kugawanya manunuzi ili kukwepa ushindani jambo ambalo linakwenda kinyume na Kifungu nambari 42(2) (c) cha Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma nambari 11 ya mwaka 2016.

**Majibu**

Baraza limetekeleza miradi minne (4) tu kati ya miradi mitano iliyotajwa katika hoja hii kwa kipindi cha mwaka 2019/2020. Ambayo ni ujenzi wa vyoo Mwambe, ukarabati wa kituo cha Afya Makombeni, ukarabati wa Barabara ya Mbuyuni - Chokaani na kituo cha Afya Tironi.

Kwa upande wa Mradi wa Ukarabati wa Skuli ya Mtu Haliwa, ukarabati huo ulifanywa na wafadhili kwa kugharimia malipo yote wenyewe na hakuna fedha ambayo ililetwa Baraza kwa ajili ya mradi huo ndio maana Baraza halina nyaraka yoyote ya fedha kuhusu mradi huo, aidha Baraza lilialikwa siku ya ufunguzi kushuhudia shughuli hiyo.

Aidha, kutokana na mapungufu madogo madogo yaliyobainika katika miradi iliyotekelezwa na Baraza kutoka na sababu mbali mbali, Baraza linapokea mapendekezo na ushauri wa Ofisi ya Mdhibiti na mkaguzi wa hesabu za Serikali ikiwemo

1. Kufuata kikamilifu mpango wa manunuzi na sheria ya manunuzi kwa utekelezaji wa miradi.
2. Kuteuwa kama ya tathmini ya miradi yenye ozoefu kama ilivyoshauriwa.
3. Kutekeleza miradi pale tu ambapo Baraza litakua na fedha kamili ili kuepuka utekelezaji mradi kwa awamu.
4. Kuweka muda wa uangalizi wa mradi (default Liability).
5. Kupata cheti cha ZEMA kwa miradi inayohusiana na mazingira kabla ya utekelezaji wake.

#### Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC ilibaini kuwa jumla ya miradi iliyotekelezwa na Baraza la Mji Mkoani ni minne badala ya mitano iliyoandikwa kwenye Ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Vile vile, Kamati ya LAAC katika kupitia hati za malipo imebaini kuwepo kwa hati moja tu ya malipo inayohusiana na mradi wa Chokaani. Hati yenyewe ni ya tarehe 31 Julai, 2019 yenye thamani ya malipo ya Tsh. 18,800,000 ikiwa ni malipo ya kuchawanya fusi na kujaza udongo wakati Taarifa ya Hesabu za Mwisho wa Mwaka inaeleza kuwa mradi huo ulitumia Tsh. 27,000,000 na Ripoti ya Mkaguzi Mkuu imeandika Tsh. 35,000,000.

Kutokana na kasoro hiyo, hoja hiyo imebaki kama ilivyo na pamoja na hayo Kamati ya LAAC ilibaini kuwa hakuna uwekaji mzuri wa kumbu kumbu katika Baraza la Mji Mkoani. Hivyo, Kamati ilipendekeza kwa Baraza hili kuwa na utaratibu mzuri wa utunzaji wa kumbu kumbu ili kuepusha hoja zisizo na lazima.

### 4.9.5 Mapungufu Katika Ujenzi wa Ofisi Ndogo ya Baraza la Mji Mkoani Tsh. 199,718,400

Baraza la Mji Mkoani limeingia makataba wa ujenzi wa Ofisi ndogo na Kampuni za Zenji Building Construction Ltd kwa thamani ya shilingi 199,718,400 ili kuondoa tatizo la ufinyu wa eneo la kufanyia kazi.

Kupitia ujenzi huo ukaguzi umebaini dosari mbalimbali kama zifuatazo:

1. Utaratibu usioridhisha wa kumpata mkandarasi wa ujenzi ikiwemo

kutokuwepo kwa vikao vya tathmini ya ujenzi vikao vya kufanya maamuzi ya kuanza kwa ujenzi, vikao vya kuitisha tenda, vikao vya kuzipitia na kumpata mkandarasi aliyekidhi vigezo.

2. Kutokuwepo kwa mshauri elekezi kwa ajili ya kulishauri Baraza juu ya utaratibu wa ujenzi.
3. Kutokuwepo kwa tarehe za kuanza na kumalizika kwa ujenzi ndani ya mkataba.
4. Pamoja na kutumia jumla ya shilingi 125,052,000 kati ya shilingi 169,252,880 ikiwa sawa asilimia 74 ya fedha zote za mkataba, ukaguzi umebaini kutokukamilika kwa vipengele vifuatavyo:

| Nam. | Kazi ambazo hazijafanywa | Jumla ya fedha zilizokadiriwa (Tsh.) |
|---|---|---|
| 1. | Kazi za umalizaji (Finishing works) | 43,090,000 |
| 2. | Milango na Madirisha | 25,680,000 |
| 3. | Mifumo ya maji safi na maji taka | 4,382,000 |
| 4. | Vipengele vyenginevyo ikiwemo kuweka umeme, tanki na shimo | 12,000,000 |
| **JUMLA** | | **85,152,000** |

**Majibu**

Baraza la Mji Mkoani limeanzisha ujenzi wa Ofisi ndogo ili kukidhi mahitaji ya wafanyakazi na kuondoa tatizo la ufinyinyu unalikabili Baraza kwa sasa. Katika kutekeleza mradi huo Baraza huwa linatenga fedha kadri iwezekanavyo kulingana na upatikanaji wa fedha za matumizi mengineyo (O.C) kutoka serikalini, mkataba wa malipo ya ujenzi huo inategemea namna ambavyo Baraza linapata fedha. Kutokana na uhaba wa upatikanaji wa fedha kwa muda mrefu Baraza halijaweza kukamilisha ujenzi huo kwa wakati, hata hivyo Baraza limeandaa Mikakati ya kutenga fedha kutokana na vianzio vya ndani kwa mwaka wa fedha unaokuja ili kuweza kukamilisha sehemu ya ujenzi iliyobakia.
Taratibu zote za kumpata Mkandarasi zilitumika ikiwemo kumpata mtu ambaye atajenga na kufanyiwa malipo kutokana na upatikanaji wa fedha wa Baraza.

Aidha, Baraza linapokea na kufanyia kazi mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa ajili ya kuondosha mapungufu hayo.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC ilishindwa kuthibitisha matumizi hayo, kwani taarifa ya matumizi ya ujenzi huo hayakuonekana kwenye Taarifa ya Mwisho wa Mwaka ya Baraza na Watendaji wa Baraza hawakutoa maelezo ya kutosha juu ya hoja hii. Hivyo, hoja hii imebaki kama ilivyo.

Kwa ujumla Kamati ya LAAC haikuridhika na utendaji wa Baraza la Mji Mkoani.

## 4:10 BARAZA LA MJI WETE

### Taarifa ya Mapato

Kwa mwaka wa fedha 2019/2020 Baraza la Mji Wete ilikadiria kukusanya jumla ya Tzs 325,000,000/= kutoka katika vianzio vyake mbali mbali na hadi kufikia 30 June, 2020 ilifanikiwa kukusanya jumla ya Tsh. 359,468,990/= sawa na asilimia 110.6 ya makidirio.

### Majibu

Baraza la Mji Wete halikuandaa maelezo ya moja kwa moja juu ya taarifa ya mapato na badala yake lilijibu hoja za Kamati zilizoulizwa.

### Uchunguzi wa Kamati

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC ilibaini yafuatayo:

1. Baraza la Mji Wete halina uwelewa mpana juu ya shughuli ya ukusanyaji au ufuatiliaji wa mapato ingawa limekusanya mapato kwa asilimia 110 ya makadirio. Hali hii inapelekea baadhi ya vyanzo vya mapato kukusanya chini ya matarajio yao.

2. Vyanzo vya mapato ambavyo vimekusanya zaidi ya makadirio ni kama vifuatavyo:

    a. Mapato Mengineyo “Other Receipt”;

    b. Ujenzi (DCU); na

    c. Ada na Adhabu (Fee na Penalty).

3. Katika mwaka wa fedha 2019/2020 chanzo cha mapato cha upasishaji wa gari za abiria kilikusanya kwa miezi mitano tu na kilifanikiwa kukusanya jumla ya Tsh. 2,400,000 sawa na 20% badala ya Tsh. 12,000,000 zilizokadiriwa. Kuanzia mwaka wa fedha 2020/2021 chanzo hiki kimehamishiwa Serikali Kuu.

4. Katika mwaka wa fedha 2019/2020 chanzo cha matangazo kimeonekana kukusanya kiwango kikubwa cha mapato ukilinganisha na mwaka uliopita. Hii ni kutokana na kuwa chanzo hicho kimejumuisha na mapato ya minara ambapo Minara ilikusanya Tsh. 7,500,000 na Matangazo Tsh. 5,752,000.

5. Serikali kupitia Wizara inayohusika na Serikali za Mitaa ilifunga mkataba na Kampuni ya Al Jumura kukusanya mapato kwa chanzo cha minara baada ya kubainika kwamba chanzo hicho hakiingizi mapato yake kama ilivyotarajiwa.

6. Mkataba uliofungwa baina ya Wizara na Kampuni ya Al Jumura ulikuwa na mapungufu kadhaa ikiwemo kutokuwepo kwa kipengele kilichojitosheleza kinachozungumzia masuala ya malipo (consideration), kutokuwepo kwa viambatanisho vilivyonukuliwa ndani ya mkataba huo na kadhalika.

7. Baadhi ya “Note” kwenye Hesabu ya Mwisho wa Mwaka (Financial Statement) hazina ufafanuzi. Mfano, kifungu cha Mapato Mengineyo “Other Receipt”.

8. Vianzio viwili vya mapato havikuoneshwa kwenye Hesabu ya Mwisho wa Mwaka kwa madai kuwa havikukusanya fedha yoyote. Vianzio vyenyewe ni; usafirishaji wa maliasili na ada ya mizigo bandarini. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na taratibu za kihesabu.

9. Madiwani hawana mamlaka ya kuuza Fomu za utoaji wa vibali vya ujenzi kwa kuwa hawakuandikwa kwenye fomu hizo.

### Mapendekezo ya Kamati

Ili kasoro kama hizo zisijitokeze siku zijazo, Kamati ya LAAC ilipendekeza yafuatayo:

1. Vifungu vyote vya mapato na matumizi vilivyokadiriwa fedha vioneshwe kwenye Hesabu ya Mwisho wa Mwaka hata kama vimepata sufuri ili kuwa na taarifa kamili ya mapato na matumizi hayo.

2. Watendaji wa Baraza la Mji Wete wapatiwe mafunzo juu ya mbinu za kukusanya mapato ili watekeleze majukumu yao kwa weledi zaidi.

3. “Note” zote kwenye Hesabu ya Mwisho wa Mwaka (Financial Statement) ziwekwe ufafanuzi ili kurahisisha usomaji wa “Note” hizo.

4. Watendaji wawe makini wakati wa kuandaa mikataba mbali mbali ili kuepusha kuitia hasara Serikali.

5. Kwenye Fomu za utoaji wa vibali vya ujenzi waongezwe na Madiwani

### Taarifa ya Matumizi

Baraza la Mji Wete lilikadiriwa kutumia jumla ya Shilingi 6,348,959,000.00 kwa kazi za kawaida na Tsh. 125,000,000.00 kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia tarehe 30.06.2020 jumla ya Tsh. 6,798,347,585.00 zimetumika kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 107.08 ya makadirio na Tsh. 57,000,000 kwa kazi za maendeleo sawa na asilimia 45.6 ya makadirio.

### Majibu

Baraza la Mji Wete halikuandaa maelezo ya moja kwa moja juu ya taarifa ya matumizi na badala yake lilijibu hoja za Kamati zilizoulizwa.

### Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Katika kuifanyia kazi hoja hii Kamati ya LAAC ilikagua matumizi mbali mbali yaliyooneshwa kwenye Hesabu ya Mwisho wa Mwaka (Financial Statement) na kubaini mapungufu kadhaa kama ifuatavyo:

1. Kipengele cha Matumizi Mengineyo (OC) kimewekwa “dash” ingawa fedha za matumizi hayo zilipatikana.
2. “Note” namba 12 na 13 zinazungumzia suala moja jambo ambalo ni kinyume na utaratibu.
3. Salio (Balance) iliyofungia mwaka sio iliyofungua mwaka uliofuata.
4. Taarifa ya Hesabu ya Mwisho wa Mwaka ina mapungufu kama vile:
    1. Ukurasa wa 13 kwenye “Note” 9 ufafanuzi wake unatofautiana na ufafanuzi wa “Note” 9 kwenye ukurasa wa 18. Kasoro kama hiyo imejitokeza pia kwenye “Note” 10.
    2. Baadhi ya vifungu vimewekwa kwenye sehemu ambazo sio sahihi.

Kutokana na kasoro hizo, Kamati ya LAAC imewataka Wahasibu kuwa makini wakati wa kuandaa Hesabu ya Mwisho wa Mwaka

MATOKEO YA UKAGUZI

4.10.1 Hati za malipo zilizokosa vielelezo Tsh. 72,081,914

Ukaguzi umebaini Baraza la Mji Wete limefanya malipo ya shilingi 33,674,900 kwa ajili ya kugharamia shughuli mbali mbali za Baraza. Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kukosekana kwa vielelezo vya matumizi hayo. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34 cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016.

Majibu

Ni kweli kwamba wakati wa ukaguzi wa Mwaka wa Fedha 2019/2020 Vielelezo vyenye thamani tajwa hapo juu vilikuwa havijafungamanishwa na Hati za Malipo husika, punde tu baada ya ukaguzi wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Ofisi ya Baraza la Mji Wete ilifanya juhudi za kuviweka sawa vielelezo hivyo katika mafaili husika, kwa sasa tayari vielelezo hivyo vimeshawekwa katika vocha husika.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Kamati ya LAAC haikukubaliana na majibu ya Baraza la Mji Wete kutokana na kuwa hoja hiyo iliibuliwa na Mkaguzi wa Ndani, hata hivyo, Baraza hili halikuchukua juhudi yoyote ya kuvitafuta vielelezo hivyo hadi Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anafanya ukaguzi Barazani hapo.

Kutokana na hali hiyo, Kamati ya LAAC inazitaka Taasisi za Serikali kuzifanyia kazi hoja za Mkaguzi wa Ndani ili kuepusha dosari zisizo na msingi.

### 4.10.2 Malipo kwa Wafanyabiashara ambao hawakusajiliwa Tsh. 14,900,079

Jumla ya shilingi 14,900,079 zimelipwa kwa ajili ya huduma mbali mbali za Baraza la Mji Wete, ukaguzi umebaini kwamba watoa huduma hao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa mali za Umma ambapo kunapelekea kuikosesha Serikali mapato.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 23(1) cha Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma nambari 11 ya mwaka 2016 pamoja na Sheria ya Usimamizi wa fedha za Umma ya nambari 12 ya mwaka 2016.

**Majibu**

Ni kweli kwamba, wakati wa matumzi kiasi cha fedha kilichotajwa hapo juu kwa wafanyabiashara waliotajwa katika hoja hii hawakusajiliwa na Mamlaka husika. Hali hii ilisababishwa na wafanyabiashara hao kuwa na uelewa mdogo katika kufanya usajili wa biashara zao katika Mamlaka ya manunuzi. Kwa sasa wafanyabiashara hao kwa kiwango kikubwa wamekamilisha utaratibu wa Usajili na Ofisi ya Baraza la Mji Wete inafanya kazi na Wafanyabiashara waliosajiliwa kisheria.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya LAAC haikukubaliana na majibu hayo hasa ikizingatiwa kuwa suala la usajili lipo kisheria, hivyo, hoja hii imebaki kama ilivyo.

Kutokana na hali hiyo, Kamati ya LAAC inazishauri Taasisi za Serikali kuwa makini wakati zinatekeleza shughuli zake.

Vile vile, Kamati hii inazitaka Taasisi za Serikali kuwatumia au kuwashirikisha Wanasheria wa Taasisi zao kabla ya kutekeleza shughuli mbali mbali ili waweze kujua taratibu zinaelekeza vipi kuhusiana na jambo husika.

### 4.10.3 Kutokutekelezwa kwa miradi ya maendeleo iliyopangwa kutumia Tsh. 68,000,000

Baraza la Mji Wete lilipanga kutekeleza miradi mbali mbali ya maendeleo yenye jumla ya shilingi 68,000,000. Ukaguzi umebaini kutokutekelezwa kwa miradi ya maendeleo iliyopangwa ingawa Baraza lilikusanya jumla ya mapato ya shilingi 359,468,990 sawa na asilimia 110.6 ya makadirio kukiwa na ongezeko la shilingi 34,468,990 ambayo ni sawa na asilimia 10.6 ya makadirio.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa nambari 7 ya mwaka 2014 pamoja na sheria ya Usimamizi wa fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016 ya Zanzibar.

**Majibu**

Ni kweli kwamba jumla ya miradi yenye thamani ya kiasi kilichotajwa hapo juu haikuweza kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2019/2020. Hali hii ilisababishwa na kutokupatikana kwa pesa za uendeshaji (Other charges) kwa Ofisi Kuu na sekta zilizogatuliwa.

Kutokupatikana kwa fedha hizo kulipelekea kutumika kwa fedha za makusanyo ya ndani ili kuweza kuzipatia huduma za uendeshaji taasisi zilizogatuliwa pamoja na Ofisi Kuu na badala yake kushindwa kutekeleza miradi ya maendeleo iliyotajwa katika hoja hii.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**
Kamati ya LAAC haikukubaliana na majibu hayo hasa ikizingatiwa kuwa kila kifungu kinapaswa kutumika kwa mujibu wa bajeti iliyopangwa, hivyo, hoja hii imebaki kama ilivyo.

**4.10.4 Kutokuoneshwa kwa mapato katika taarifa za hesabu Tsh. 34,140,000**
Jumla ya shilingi 34,140,000 ikiwa ni fedha za mapato zilizokusanywa na Baraza la Mji la Wete kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020. Ukaguzi umebaini kwamba fedha hizo za makusanyo yatokanayo na utoaji wa vibali vya ujenzi hazikuripotiwa na kuonyeshwa katika taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka.

Kutokuingizwa na kuonyeshwa mapato hayo katika taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka kunapelekea taarifa ya mapato kutokuonesha sura halisi na sahihi. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016.

**Majibu**
Kuna baadhi ya mapato ya ada za ujenzi yalipokelewa kwenye hesabu ya Baraza la Mji Wete na mapato haya ni kwa zile nyumba ambazo hazikukidhi vigezo vya kukubalika na DCU (Ujenzi wake ni wa kijijini na haukufuata masharti na vigezo stahiki vinavyotakiwa na DCU).

Katika kuwasaidia watu hawa Ofisi ya Baraza la Mji Wete ilipokea Fedha ya Mapato haya na kuwaruhusu kujenga.

Hata hivyo, Ofisi ya Baraza la Mji Wete ikaendelea kutoa elimu juu yaMipango Miji ili wananchi wajenge kama ilivyokusudiwa na Serikali kuu.

Wakati wa utengenezaji wa Taarifa ya Hesabu Fungu hilo liliingizwa katika Fungu la Mapato mengineyo “Other Receipts”.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**
Kamati ya LAAC haikuthibitisha maelezo ya Baraza hivyo, hoja hii imebaki kama ilivyo

## RIPOTI YA UKAGUZI MAALUM UNAOHUSU UTEKELEZAJI WA MAAGIZO YA RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI MHE. DK. HUSSEIN ALI MWINYI WAKATI WA KUWAAPISHA VIONGOZI WAKUU

## I. RIPOTI YA UKAGUZI MAALUM WA MALIPO YA FIDIA KWA WANANCHI WALIOATHIRIKA KWA KUPISHA MRADI WA UWEKEZAJI WA UJENZI WA BANDARI, BOHARI NA MIUNDOMBINU YA MAFUTA NA GESI MANGAPWANI/BUMBWINI

Malipo ya fidia yamejitokeza baada ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuzingatia mahitaji na kuongezeka kwa matumizi ya bidhaa ya mafuta nchini, iliamua kutenga eneo lenye ukubwa wa hekta 412 ambalo litayumika kwa shughuli za ujenzi wa:

1. Bohari za kuhifadhia mafuta na gesi,
2. Bandari ya kuhudumia upakizi na ushushwaji wa mafuta na gesi,
3. Miundombinu ya mafuta na gesi,
4. Ujenzi wa barabara ndani ya eneo la mafuta na gesi yenye urefu wa kilomita 3.5 na upana wa mita 30.

### MAMBO YALIYOBAINIKA KATIKA UKAGUZI MAALUM WA MALIPO YA FIDIA

### 4.5.1 Dosari katika usimamizi wa malipo ya fidia

Ukaguzi umebaini kwamba mwenendo mzima wa ulipaji wa fidia ulikuwa na udhaifu mkubwa kutokana na kutokuwepo na usimamizi mzuri tangu zoezi la kufanya tathmini lilipoanza kwa upande wa ZURA, dosari hizo zinatokana na kukosekana kwa mpango maalum wa kuorodhesha idadi na majina halisi ya waathirika kwenye fidia za vipando/miti wakati zoezi lilipoanza hadi kumalizika, ili kuepuka kulipa watu wasiohusika na kusababisha hasara kubwa Serikali.

### Majibu ya Mamlaka

ZURA iliwasilisha barua katika Afisi ya Kamisheni ya Ardhi Zanzibar (kmb-ZURA/ARDHI/29/6 ya tarehe 31/08/2017) ya kuomba kufanya tathmini ya eneo la mafuta na gesi la Mangapwani ili kujua tathmini ya mali na vipando vya wananchi ndani ya eneo hilo na kuelewa gharama halisi ya malipo ya fidia. Mipango na taratibu ya kazi hiyo ilitarajiwa ifanywe na Kamisheni ya Ardhi kwa vile ni jukumu lao kiutaalamu. Orodha ya majina ya walioathirika ipo na walilipwa kama ilivyohitajika na kuthibitishwa na Mtathmini na Masheha wa maeneo husika.

### Uchunguzi wa Kamati

Katika kufuatilia hoja hii yafuatayo yamebainika:

1. Kwa kuwa hoja hii imegusia zoezi hili kwa ujumla wake, Kamati ya LAAC iliridhika kuwa Watendaji wa ZURA hawakushiriki ipasavyo katika baadhi ya maeneo ambayo walipaswa kuchukua hatua.
2. Kamisheni ya Ardhi ilifanya uthamini kama ilivyoombwa kupitia barua iliyonakiliwa katika majibu ya Mamlaka.
3. Zoezi hili limefanyika nusu kwa kuwa baadhi ya wananchi walikataa kuchukuliwa maeneo yao ingawa Mradi huo umelenga hadi katika maeneo hayo.
4. Wananchi 20 bado hawajachukua fidia zao kwa kuwa wanahisi kiwango kilichopangwa kulipwa ni kidogo.
5. Wananchi waliokataa kulipwa kiwango hicho cha fedha kwa madai ya kuwa ni kidogo ni wale wananchi waliokataa kuwapatia maeneo yao Wawekezaji ambapo walikataa kulipwa fedha chini ya kiwango kilichopangwa na Serikali.
6. Kabla ya Sheria kufanyiwa marekebisho endapo wananchi eneo lake litachukuliwa na Serikali kwa maslahi ya umma mwananchi huyo alikuwa akilipwa thamani ya ardhi pamoja na maendeleo aliyoyafanya. Isipokuwa kwamba, kufuatia marekebisho ya Sheria hiyo eneo lililochukuliwa kwa madhumuni kama hayo mhusika analipwa maendeleo aliyoyafanya tu kitu kinachopeleka muathirika husika kulipwa fidia ndogo kinyume na ilivyozoweleka.
7. Fidia haijalipwa kwa umeme, maji na barabara.

**Mapendekezo ya Kamati**

Ili kasoro kama hiyo isijitokeze tena siku zijazo Kamati ya LAAC inaishauri Serikali kuzishirikisha ipasavyo Taasisi zenye kulipia shughuli husika kwa kuwa Taasisi hiyo ndio itakayowajibika na kasoro yoyote itakayotokea.

### 4.5.2 Kukosekana kwa takwimu sahihi za awali kutoka kwa masheha

Ukaguzi umebaini kuwa hakukuwa na takwim sahihi za utambuzi wa awali kwa wananchi wanaomiliki mashamba/vipando zikiambatana na namba za vitambulisho ili kuthibitisha jina sahihi la mmiliki wa shamba/vipando husika katika maeneo yaliyotengwa ya Ujenzi wa Miundombinu ya Mafuta na Gesi huko Mangapwani kabla ya tathmini kuanza.

Kukosekana kwa takwimu za awali za Waathirika kutoka kwa Masheha kunapelekea:

- Kutopatikana ushahidi kamili wa wamiliki wa mashamba/vipando vya wananchi walioathirika ambayo ingepaswa kulipwa na ZURA.

- Kuongezeka kwa idadi ya waathirika hewa na hatimae kulipa malipo ya fidia zaidi ya walichotarajiwa kulipa.

**Majibu ya Mamlaka**

Majibu ya maelezo haya ni kama yalivyoelezwa kwenye Hoja Namba 4.5.1

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC ilibaini yafuatayo:

1. Serikali iliiagiza ZURA kuhakikisha kuwa zoezi hilo linafanyika ndani ya siku 3 ingawa eneo husika ni kubwa jambo lililochochea kutokea mapungufu kadhaa wakati wa utekelezaji wa zoezi hilo.

2. Masheha walipatiwa orodha ya majina ya waathirika inawezekana wamezipoteza (misplace). Katika kurahisisha utekelezaji wa shughuli mbali mbali zinazofanana na hii Masheha hufanya tathimini awali, lakini, katika kadhia hii hawakufanya hivyo.

   Kwa kuwa Sheria hailazimishi jambo hilo kufanyika ZURA haikuwa na mashaka na utekelezwaji wa zoezi hilo.

3. Waathirika wa eneo hilo wamelipwa fidia, hata hivyo, hadi Kamati inafanya ziara katika eneo hilo tarehe 08 Aprili, 2022 bado wananchi wanaendelea kulima na endapo mwekezaji anahitaji kutumia eneo husika basi hulazimika kulipa tena jambo ambalo ni kinyume na utaratibu.

Kutokana na kasoro hizo Kamati ya LAAC ilipendekeza yafuatayo:

1. Serikali iandae mipango yake mapema ili kuwe na muda wa kutosha wa kutekelezwa mambo kama taratibu zinavyoelekeza. Jambo hili litasaidia kuepusha kasoro ya kuwaharakishwa Watendaji kutekeleza mambo ndani ya kipindi kifupi na hatimae kupelekea taratibu kadhaa kukiukwa.

2. Serikali ya Mkoa na Wilaya kufuatilia kwa karibu eneo husika ili kuepusha Mwekezaji kulipa fidia zaidi ya mara moja katika eneo moja, kitendo cha Waathirika kulipwa fidia zaidi ya mara moja kinaweza kikamvunja moyo Mwekezaji huyo.

3. kutokana na ufinyu wa muda Kamati ya LAAC haikuweza kulifanyia kazi kwa kina suala hilo, hivyo, Baraza la Wawakilishi kuteua baadhi ya Wajumbe kutoka Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati na Kamati ya LAAC kufuatilia kwa kina suala hili ili haki itendeke.

### 4.5.3 Kukosekana kwa ripoti ya Mtathmini Mkuu wa Serikali

Ukaguzi umebaini kuwa ZURA ilimkabidhi Mtathmini Mkuu wa Serikali jukumu la kufanya tathmini ya miti/vipando vilivyomo katika eneo lililotengwa kwa ajili ya Ujenzi wa Miundombinu ya Mafuta na Gesi huko Mangapwani Bumbwini, lakini ripoti ya Mtathmini Mkuu wa Serikali haikuweza kupatikana kwa ukaguzi kutokana na sababu zisizoeleweka. Kitendo hiki ni kwenda kinyume na Sheria Namba 5 ya mwaka 2015.

Aidha, ukaguzi umebaini kwamba hakukuwa na fomu zilizotumika wakati wa kufanya tathmini kwa mtu mmoja mmoja ili kuthibitisha thamani sahihi ya miti/vipando vya mmiliki. Hivyo basi kwa mujibu wa orodha iliyowasilishwa ZURA kutoka kwa Mtathmini Mkuu ilikuwa na dosari nyingi kama zinavyobainishwa hapo chini:-

i. baadhi ya wananchi kuongezewa idadi ya miti/mazao.

ii. baadhi ya wananchi kupunguziwa na kupewa wananchi wengine maeneo yao.

iii. baadhi ya wananchi kuongezewa thamani ya fedha kwa idadi ndogo ya mali walizopaswa kufanyiwa fidia.

iv. baadhi ya wananchi hawamiliki maeneo lakini wameingizwa katika orodha ya kulipwa fidia kinyume na sheria za tathmini.

v. kukosekana kwa baadhi ya majina ya wahusika waliostahiki malipo ya fidia (kama vile bwana Hassan Hamid Hassan, bwana Ali Salum Ali) ambao ni wamiliki wa mashamba.

Kukosekana kwa ripoti ya Mtathmini Mkuu wa Serikali kwa ajili ya malipo ya fidia kwa wananchi walioathirika kunapelekea kufanya malipo yasiyokuwa na uthibitisho wa thamani halisi kwa kujibu wa idadi ya miti/vipando vilivyolipwa kwa kila mwananchi.

#### Majibu ya Mamlaka
ZURA ilimuandikia barua Katibu Mtendaji wa Kamisheni ya Ardhi (ZURA/ARDHI/29/48 ya tarehe 14/04/2021) ya kuomba vielelezo na ripoti ya tathmini ya fidia kwa Kijiji cha Dundua Mangapwani pamoja na fomu zilizohusika wakati wa zoezi la usajili wa wananchi walioathirika huko Mangapwani.

#### Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati
Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC ilibaini yafuatayo:

1. Sheria hailazimishi kupatiwa fomu mtu mmoja mmoja ili kuthibitisha thamani sahihi ya miti au vipando vya mmiliki.

2. Mkaguzi alipatiwa Ripoti ya Tathmini, hata hivyo, aliandika kwenye Ripoti yake kuwa Ripoti ya Tathmini ilikosekana, hii ni kutokana na kuwa Ripoti hiyo haikuwa na taarifa za kina (yaani haijitoshelezi) juu ya zoezi husika jambo hilo

pia limethibitishwa na Kamati hii. Barua ya tarehe 21 Mei, 2021 kutoka Kamisheni ya Ardhi ilikabidhi Ripoti ya Tathmini kwa ZURA.

Ili kuepusha kasoro kama hizo zisijitokeze tena katika kutekelezwa shughuli kama hizo, Kamati ya LAAC imeishauri Serikali kuandaa muongozo maalum juu ya uandaaji wa Ripoti ya Tathmini ili kuwa na Ripoti iliyokidhi vigezo.

Kutokana na maelezo hayo, Kamati ya LAAC haikubaliani na Ripoti ya Mdhibiti ya kuwepo kwa hoja hiyo, kwa kuwa Ripoti ya Mthamini ilikuwepo ingawa ilikuwa na baadhi ya mapungufu.

### 4.5.4 Ukiukwaji wa taratibu za malipo ya fidia kwa waathirika wa eneo la ujenzi wa Bandari ya Mafuta na Gesi Mangapwani shilingi 94,284,500

Ukaguzi ulipitia taarifa za malipo ya fidia kwa wananchi walioathirika katika eneo lililotengwa kwa ajili ya Ujenzi wa Miundombinu ya Mafuta na gesi hadi kufikia Juni 2020 na kubaini kufanyika malipo zaidi ya mara moja kwa mtu mmoja kwa waathirika hao. Ukaguzi haukuweza kupatiwa sababu za kueleweka za kufanywa malipo zaidi ya mara moja kwa mtu mmoja.

Jadweli lifuatalo linaonesha fedha za fidia zilizolipwa zaidi ya mara moja kwa mtu mmoja bila ya sababu za msingi:-

| Nam | Jina kamili | Fedha zilizolipwa | | Hesabu ya benki |
|---|---|---|---|---|
| | | Tarehe | Kiasi | |
| 1. | Ziabu Juma Khamis | 3/01/2018 | 11,593,500.00 | 0206810000 PBZ |
| | | 25/01/2019 | 11,593,500.00 | 0203486000 PBZ |
| | | 12/02/2019 | 11,593,500.00 | 0206810000 PBZ |
| 2. | Mwanaisha Ali Mbarouk | 25/01/2019<br>12/02/2009 | 21,565,000.00<br>21,565,000.00 | 032206028204 PBZ |
| 3. | Mzee Abdulla Mzee | 27/09/2019<br>21/10/2019 | 8,187,000.00<br>8,187,000.00 | 02120141981 NBC |

Kulipa fedha zaidi ya zilizotarajiwa kulipwa kunapelekea kutokuwepo kwa udhibiti mzuri wa kufanya malipo hatimae kufanya malipo yasiyoeleweka.

Aidha, kunapelekea kutokuwa na hadhari kwa kutopitia orodha iliyowasilishwa kutoka kwa Mtathmini Mkuu ili kuondoa makosa yaliyojitokeza kulipa fedha zaidi ya

ulizotarajiwa kwa lengo lililokusudiwa.

Pia, kunapelekea kuibebesha mzigo mzito Serikali kwa kuitia hasara ya kulipa fedha zaidi ambazo zingetumika kwa shughuli nyengine za kuleta maendeleo.

**Majibu ya Mamlaka**
Kasoro za malipo zilizoonekana wakati wa kuwasilisha hati za malipo huko benki, zililazimisha kurejeshwa kwa hati hizo za malipo kwa ZURA ili kufanyiwa marekebsho yanayotakiwa. Hali hiyo ndio inayotoa taswira ya baadhi ya watu kuandikwa (kuonekana) zaidi ya mara moja kwenye nyaraka mbalimbali za benki, vielelezo vya malipo hayo vipo kwa ajili ya uhakiki.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**
Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC imebaini kama ifuatavyo:

1. Katika Jadweli kipengele Namba 1 kinachomuelezea Ndugu Ziabu Juma Khamis tarehe 3/01/2018 isomeke kuwa ni tarehe 3/01/2019 kwa kuwa zoezi hilo limefanyika mwaka 2019 na sio mwaka 2018.

2. Ni kweli kuwa Ndugu Ziabu Juma Khamis ameorodheshwa mara mbili kwenye orodha ya malipo ya tarehe 3/01/2018, ambapo, ameonekana kuwa ni mtu wa 11 na amelipwa Tsh. 1,397,500, lakini pia, ameonekana tena kwenye Namba 75 na amelipwa Tsh. 11,593,500, ingawa, amelipwa mara moja tu.

3. Malipo ya tarehe 12/02/2019 yenye thamani ya Tsh. 11,593,500 hayakulipwa kwa Ndugu Ziabu Juma Khamis kama ilivyoelezwa kwenye Ripoti ya Mdhibiti kwa kuwa fedha hizo zilitakiwa kuingizwa kwenye akanti Namba 0203486000 PBZ ambayo mmiliki ni mtu mwengine, hivyo, fedha hizo zilirudi kwenye akaunti ya ZURA.

4. Kutokana na ufinyu wa muda Kamati ya LAAC ilimfanyia uhakiki wa kina Mwathirika mmoja tu kati ya Waathirika watatu walioelezwa kwenye Ripoti ya Mdhibiti. Hivyo, Kamati iliridhika kuwa baadhi ya fedha zilirudi katika akaunti ya hesabu ya ZURA, isipokuwa kwamba, ZURA ilishindwa kuibaini kasoro hiyo mapema kutokana na kutofanya usuluhishi (Reconcilliation) wa hesabu zake kwa wakati.

5. Kwa kuwa baadhi ya akaunti za hesabu zilikosewa taarifa zinaonesha kuwa fedha zilizolipwa na Benki ni Tsh. 380,482,820 badala ya Tsh. Milioni 410.

Ili kasoro kama hizo zisijitokeze tena, Kamati ya LAAC iliishauri ZURA kuwa na tabia ya kufanya usuluhishi wa hesabu zake kila mwezi kwa lengo la kubaini mapema changamoto mbali mbali zitakazojitokeza.

### 4.5.5 Malipo ya fidia kwa wananchi ambao hawamiliki miti au vipando shilingi 65,029,550

Ukaguzi ulipitia taarifa za malipo na kufanya mahojiano na waathirika waliopisha

ujenzi wa bandari ya mafuta Mangapwani na kubini kwamba kuna malipo yamefanyika kwa baadhi ya wananchi ambao si wamiliki wa mashamba katika maeneo hayo yaliyohusika na malipo ya fidia na wamelipwa malipo hayo.
Jadweli lifuatalo linaonesha orodha ya baadhi ya majina ya wananchi ambao hawamiliki miti au vipando na wamelipwa fidia:-

| Namba | Jina Kamili | Fedha zilizolipwa (Tshs.) |
|---|---|---|
| 1. | Kombo Khamis Vuai | 10172,550.00 |
| 2. | Kombo Khamis Msago | 1,278,000.00 |
| 3. | Ali Suleiman Nassor | 11,640,000.00 |
| 4. | Mwanajuma Mzee Abdulla | 14,701,550.00 |
| 5. | Masoud Rashid Msabah | 1,755,000.00 |
| 6. | Moh'd Silima Machano | 15,411,000.00 |
| 7. | Kheir Rubea | 10,071,400.00 |
| **JUMLA** | | **65,029,550.00** |

**Majibu ya Mamlaka**
Katika hoja hii Uongozi wa ZURA umebaini kuwa kuna waathirika walichukuliwa fedha hizo, wengine ni wamiliki halali wa vipando na miti, pamoja na wengine kutumia hesabu (accounts) za wahusika ambao sio wamiliki (watu wa karibu au jamaa zao).

**Uchunguzi wa Kamati**
Katika kufuatilia hoja hii, Kamati ya LAAC ilifanya mahojiano na baadhi ya wananchi walioorodheshwa kwenye hoja hiyo na imebaini yafuatayo:

i. Sio kweli kwamba wananchi walioorodheshwa kwenye hoja hii hawakumiliki miti/vipando.

ii. Baadhi ya wananchi walikuwa hawamiliki mashamba, isipokuwa kwamba, walikuwa wanamiliki miti/vipando baada ya kuridhiwa na wamiliki wa mashamba kulima ndani ya mashamba hayo. Mfano, Ndugu Moh'd Silima Machano.

Baada ya uchunguzi huo Kamati ya LAAC ilitaka kupata kauli kwa Watendaji wa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali juu ya maelezo ya wananchi hao, hata hivyo, Watendaji hao hawakuwa na maelezo zaidi kwa madai kwamba wao sio waliosimamia shughuli au zoezi hilo.

Kwa mnasaba huo, Kamati ya LAAC haikubaliani na hoja hiyo iliyoelezwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

**Mapendekezo ya Kamati**

Kutokana na matokeo ya uchunguzi huo uliofanywa na Kamati ya LAAC, Kamati hii inaitaka Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhakikisha kuwa inapata ushahidi wa kutosha juu ya hoja inazozitoa ili kulinda hadhi na heshima ya wananchi, Taasisi husika pamoja na Taasisi zote zilizohusika.

### 4.5.6 Malipo ya fedha za fidia kwa waathirika wa mradi zaidi ya makisio waliyopaswa kulipwa shilingi 63,135,020.00

Ukaguzi ulipitia taarifa mbali mbali za malipo ya fidia kwa waathirika wa mradi wa ujenzi wa bandari ya mafuta Mangapwani na kubaini malipo yamezidi kiwango cha makisio kwa kila muathirika. Kiwango cha malipo kilichofanyika ni kikubwa ukilinganisha na makisio ya malipo yaliyokusudiwa kufanyika.

| Nam | Jina Kamili | Kiasi alichopangiwa kulipwa (Tshs.) | Kiasi alicholipwa (Tshs.) | Tofauti (Tshs.) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Ali Pande Tabu | 3,960,000.00 | 11,376,000.00 | 7,416,000.00 |
| 2. | Khatib Khamis Nuru | 1,550,000.00 | 21,985,000.00 | 20,435,000.00 |
| 3. | Haji Haji Haji | 25,862,000.00 | 27,292,970.00 | 1,430,970.00 |
| 4. | Mwanajuma Mzee Abdulla | 709,500.00 | 14,701,550.00 | 13,992,000.00 |
| 5. | Fatma Ali Khamis | 6,873,000.00 | 18,349,000.00 | 11,476,000.00 |
| 6. | Khamis Nuru Khamis | 1,800,000.00 | 11.800,000.00 | 10,620,000.00 |
| **JUMLA** | | **42,989,500.00** | **105,504,000.00** | **63,135,020.00** |

#### Majibu ya Mamlaka

Uongozi ulifanya uhakiki kwa watu waliotajwa na kujiridhisha ya kwamba malipo kwa wahusika hao yapo kwa usahihi kwa watu wote.

#### Uchunguzi wa Kamati

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC ilifanya majadiliano na baadhi ya waathirika na imebaini yafuatayo:

1. Ndugu Khatib Khamis Nuru anamiliki eneo lake, lakini pia, ni mtoto wa Ndugu Khamis Nuru Khamis ambaye alikuwa anamiliki maeneo mawili, hivyo, alipokea fedha kwa niaba ya baba yake, hali hiyo imepelekea kuonekana kulipwa zaidi ya kiwango cha awali.
2. Ndugu Khatib Khamis Nuru alipokea fedha hizo kwa niaba ya marehemu baba yake, hata hivyo, hakukuwa na hati yoyote ya uwakala kama taratibu za kisheria zinavyoelekeza.
3. Kwa mujibu wa maelezo ya Ndugu Khatib Khamis Nuru zoezi la kuorodhesha miti na vipando limefanyika bila ya kuwepo wenye mali hizo.
4. Ndugu Fatma Ali Khamis hakumbuki alilipwa kiasi gani kwa kuwa siku nyingi zimepita na hana nyaraka yoyote, isipokuwa kwamba, kwenye hati ya uwakala imeoneshwa kuwa amewachukulia fedha Ndugu Mosi Badru (Tsh. 361,000)

na Ndugu Sikudhani Abdalla (Tsh. 1,962,000).

Kitendo cha Ndugu Fatma Ali kuwachukulia fedha na watu wengine kinaweza kuonesha kuwa amelipwa fedha za ziada.

5. Kwa mujibu wa Ripoti ya Tathmini, Ndugu Mwanajuma Mzee Abdulla alilipwa Tsh. 709,500 tu na sio kama ilivyoelezwa kwenye hoja hii. Fedha hizo zilichukuliwa kwa niaba yake na Ndugu Moh'd Silima Machano ambaye ni mume wa Ndugu Mwajuma ingawa kulikuwa na ridhaa ya mdomo tu.
6. Ndugu Fatma Ali Khamis baadhi ya waathirika hawakuorodheshwa kwenye nyaraka yoyote ingawa maeneo yao yamechukuliwa. Miongoni mwa waathirika hao ni Ndugu Mtakavyo Khamis Ghulam.

**Mapendekezo ya Kamati**

Baada ya uchunguzi huo Kamati ya LAAC ilipendekeza yafuatayo:

1. Serikali ihakikishe kuwa inatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria.
2. Watendaji wa Serikali wawe makini wakati wa kutekeleza majukumu yao ili kuepusha dosari.
3. Kamati ya LAAC ilishindwa kufanya mahojiano na baadhi ya walalamikiwa kutokana na sababu mbali mbali kama ifuatavyo:

| NAM. | JINA | SABABU |
|---|---|---|
| 1. | Ndugu Ali Pandu Tabu | Amefariki |
| 2. | Ndugu Khamis Nuru Khamis | Amefariki |
| 3. | Ndugu Haji Haji Haji | Mgonjwa |

Hata hivyo, kwa mujibu wa mahojiano iliyofanya na baadhi ya walalamikiwa walioorodheshwa kwenye hoja hii na kwa kuzingatia Ripoti ya Mtathmini, Kamati hii imeridhika kuwa hakuna mwananchi aliyelipwa fedha zaidi ya kiwango kilichoelezwa kwenye Ripoti ya Mtathmini, isipokuwa kwamba, baadhi ya wananchi walichukua fedha hizo kwa niaba ya wenzao bila ya kufuatwa utaratibu wa kisheria.

4. Zoezi la kuorodhesha vitu (miti na vipando) lifanyike mbele ya mmiliki wa eneo husika au mrithi/warithi wake ili kuepusha malalamiko yasiyo na msingi.
5. Baraza la Wawakilishi kuziamuru Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati na Kamati ya LAAC kufuatilia kwa kina suala hili kwani kutokuorodheshwa kwenye waraka baadhi ya waathirika ni kuwanyima haki yao.

Kamati ya LAAC baada ya kupokea taarifa kuwa wapo baadhi ya waathirika ambao hawakuorodheshwa kwenye orodha ya malipo na walikuwa na haki ya kulipwa iliandaa kikao cha pamoja tarehe 14 Februari, 2023 na kumuomba Ndugu Mtakavyo Khamis Ghulam ambae ni muathirika wa suala hilo kufika katika kikao hicho, hata hivyo, mhusika hakupewa ruhusa ya kuhudhuria kikao

hicho na mume wake.

Vile vile, katika kikao hicho Ndugu Hassan Hamid Hassan aliieleza Kamati kuwa yeye ni miongoni mwa waathirika wa mradi huo, isipokuwa kwamba, hakuzipokea fedha za fidia kwa kuwa ni kidogo ingawa kuna taarifa kuwa fedha zilizotengwa kwa ajili yake ziliingizwa kwenye hesabu ya benki na zimeshatolewa.

Aidha, Ndugu Hassan aliielezea Kamati kuwa kwa mtazamo wake alitarajia kulipwa sio chini ya Tsh. 200,000,000 badala ya Tsh. 1,000,000 aliyopangiwa kupewa.

Pamoja na hayo, Ndugu Hassan alizidi kueleza kuwa muathirika mwengine ambaye alitajwa kuwa hakupokea fedha ni Ndugu Ali Salum Ali ambae amefariki hivi karibuni.

### 4.5.7 Tofauti iliyobainika baina ya makisio ya fedha za malipo ya fidia na malipo halisi shilingi 774,548,646

Ukaguzi umebaini kwamba ZURA imelipa fedha zaidi ya zilizotathminiwa awali shilingi 1,288,380,665.00 ambazo pia zilikuwa haziko sahihi kutokana na mapungufu mengi yaliyojitokeza wakati wa kufanya tathmini.

Jumla ya shilingi 2,062,929,311.00 zimelipwa ikiwa ni malipo ya fidia kwa wananchi walioathirika katika eneo lililotengwa kwa ajili ya Ujenzi wa Miundombinu ya Mafuta na gesi hadi kufikia juni 2020 ambapo kuna ongezeko la shilingi 774,548,646.00 sawa na asilimia 60 ya fedha zilizotathminiwa kulipwa awali. Aidha baadhi ya malipo ya fidia yamelipwa zaidi ya mara moja kwa mtu mmoja kutokana na sababu zisizoeleweka.

**Majibu ya Mamlaka**

Uongozi wa ZURA unakubaliana ya kuwa makisio ya awali ni kweli yalikuwa Shilingi 1,288,380,665 lakini makisio halisi ni Shilingi 1,614,208,940 na kilicholipwa hakifikii kiasi cha Shilingi 2,062,929,311.00. Tofauti iliyobainika kwa Wakaguzi imetokana na kurejeshwa kwa malipo (miamala) kutoka benki kutokana na kasoro mbali mbali zikiwemo kukosewa kwa majina, namba za hesabu, kupelekwa kwa malipo mara mbili kwa mtu mmoja na kutofautiana kwa majina ya hesabu na nambari za hesabu husika.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**
Kamati ya LAAC baada ya kupitia nyaraka mbali mbali ilikubaliana na maelezo yaliyotolewa na watendaji wa ZURA, hivyo, imewashauri watendaji wa ZURA kuwa makini wakati wanatekeleza majukumu yao ili kuepuka hoja zisizo na msingi.

**4.5.8 Malipo ya fidia yenye utatanishi Shilingi 121,580,308**
Ukaguzi umebaini kuwa baadhi ya wananchi walioathirika na mradi wa ujenzi wa Bandari ya mafuta ya Mangapwani malipo yao ya fidia yalipokelewa na watu wengine bila ya kuwepo kwa hati ya uwakili 'Power of Attorney' kinyume na taratibu za fedha zinavyoelekeza.

Aidha, ukaguzi ulifanya mahojiano na baadhi ya wananchi ambao ni waathirika waliopisha mradi ili kutaka kujua kiasi cha fedha ambacho wameshalipwa na kuthibitisha kwamba hawajalipwa, lakini kumbukumbu za malipo ya ZURA zinaonesha tayari fedha hizo wamelipwa watu wengine akiwemo Sheha wa Shehia ya Misufini (Khamis Ussi Mlinde) kwa niaba yao bila ya kufuata utaratibu wa kisheria.

Jadweli lifuatalo linaonesha baadhi ya malipo ya fidia yaliyolipwa kwa niaba ya watu wengine bila ya kufuata taratibu za fedha:-

| Nam | Waliooneshwa kwenye orodha ripoti ya Mtathmini | Waliopokea fedha kwa niaba | Fedha zilizolipwa (Tshs.) | Hesabu ya Benki |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Maryam Kombo Msabah | Moh'd Silima Machano | 2,604,000.00 | 021206023195 PBZ |
| 2. | Mwanajuma Ali Kombo | Mtumweni Juma Vuai | 2,020,000.00 | 0722752001 PBZ |
| 3. | Maryam Kombo Msabah | Mwanajuma Ali Kombo | 3,095,900.00 | 0713526001 PBZ |
| 4. | Ali Kombo | Mwanajuma Ali Kombo | 1,428,000.00 | 0713526001 PBZ |
| 5. | Sija Jadi Haji | Khamis Ussi Mlinde | 24,002,529.00 | 0369430000 PBZ |
| 6. | Kombo Khamis Kombo | Khamis Ussi Mlinde | 5,266,000.00 | 0369430000 PBZ |
| 7. | Salum Zubeir Salum | Khamis Ussi Mlinde | 4,012,500.00 | 0369430000 PBZ |
| 8. | Ame Khamis | Khamis Ussi Mlinde | 3,050,850.00 | 0369430000 PBZ |
| 9. | Khamis Kheir Hamad | Khamis Ussi Mlinde | 1,744,000.00 | 0369430000 PBZ |
| 10. | Ame Makame Machano | Khamis Ussi Mlinde | 1,744,000.00 | 0369430000 PBZ |
| 11. | Ali Mbarouk Haji | Khamis Ussi Mlinde | 3,904,000.00 | 0369430000 PBZ |
| 12. | Shaaban Hamid | Khamis Ussi Mlinde | 1,704,000.00 | 0369430000 PBZ |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 13. | Alawi Haji Kirosa | Khamis Ussi Mlinde | 33,378,000.00 | 0369430000 PBZ |
| 14. | Sija Jadi Haji | Khamis Ussi Mlinde | 24,002,529.00 | 0369430000 PBZ |
| 15. | Shehe Msabah Kombo | Zubeir Zununi Omar | 9,624,000.00 | 0712842001 PBZ |
| **JUMLA** | | | **121,580,300.00** | |

Kufanya malipo ya fidia na kupokelewa na mtu mwengine kwa niaba ya muhusika pasipokuwepo na hati ya uwakili "Power of Attorney" kunapelekea kukosa uhalali wa malipo husika kwa mujibu wa sheria. Aidha kunapelekea kutoweza kutbibitisha ikiwa fedha hizo zimewafikia walengwa wa fidia waliokusudiwa.

**Majibu ya Mamlaka**

Kabla ya kuidhinisha malipo kwa waliopendekezwa na wahusika, ZURA ilikuwa na kikao cha pamoja na wote ili kujua maridhiano yaliyofikiwa juu ya kuwasilishwa kwa fedha hizo bila ya dosari yoyote. Ruhusa ya malipo iliidhinishwa baada ya kuridhika kwa uongozi wa ZURA. Vithibitisho vyote vilivyofanikisha uhalali wa malipo hayo kwa walioidhinishwa vipo.

Hati Maaluum za uthibitisho wa kulipa fedha (power of attorney) zimekalimishwa pamoja na barua za utambuzi za masheha.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC imeridhika na maelezo ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Hii ni kutokana na kuwa ZURA ilifanya malipo hayo kwa kuzingatia barua ya sheha pekee na hati za uwakala ziliandaliwa baada ya kutoka kwa Ripoti ya Mkaguzi. Hivyo, hoja hii imebaki kama ilivyo.

Pamoja na maelezo hayo, Kamati ya LAAC inazitaka Taasisi za Serikali kutekeleza majukumu yao kama Sheria zinavyoelekeza ili kuepusha dosari.

### 4.5.9 Manunuzi ya vifaa vya ujenzi yaliyokosa uthibitisho wa mapokezi shilingi 327,260,847

Katika kufuatilia ufanisi wa ujenzi wa nyumba za wanakikjiji Gongoni Mangapwani walioathirika kwa kupisha mradi wa ujenzi wa Bandari ya mafuta na gesi. Ukaguzi ilibaini kwamba Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar ilifanya manunuzi ya vifaa vya ujenzi vyenye thamani ya shilingi 327,260,847 vilivyokosa uthibitisho wa mapokezi katika eneo husika la mradi.

Kukosekana kwa kumbukumbu za mapokezi ya vifaa na jinsi vifaa hivyo vilivyotumika ukaguzi hauwezi kujua matumizi sahihi ya vifaa vilivyonunuliwa.

**Majibu ya Mamlaka**

Wakati wa utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa nyumba za Gongoni Mangapwani Wakandarasi wa ujenzi wa nyumba hizo ambao ni KMKM na Chuo cha Mafunzo kila mmoja kati yao alikabidhiwa daftari maalum la kurikodi (kupokelea) vifaa vyote vya kazi vilivyonunuliwa. Madaftari hayo yaliyotumika kupokelea na kurikodia vifaa vya ujenzi vilivyonunuliwa yapo katika ghala (store) ya Mamlaka na yanapatikana kwa ajili ya kujiridhisha.

### Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Baada ya kufanya majadiliano na Watendaji wa ZURA Kamati hii ilibaini kuwa vifaa hivyo viliingizwa kwenye madaftari baada ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuibua dosari hiyo. Hivyo, hoja hii imebaki kama ilivyo.

### 4.5.10 Dosari Zilizobainika Katika Ujenzi wa Nyumba za Wanakijiji Gongoni Zilizojengwa na Vikosi vya SMZ

Ukaguzi umebaini kwamba nyumba 31 zilizojengwa na vikosi hivyo ziko chini ya kiwango kutokana na nyumba hizo kufanya nyufa na zinaeza kuhatarisha maisha ya wakaazi wanaoishi ndani ya nyumba hizo. Jumla ya Tsh. 1,471,375,247 zimetumika kwa ajili ya ujenzi huo.

ZURA ilifunga mikataba miwili tofauti kwa siku tofauti na Kikosi cha KMKM na chuo cha Mafunzo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba 31 za makaazi katika kijiji cha Gongoni Mangapwani kwa kulipwa gharama za ufundi na malipo ya ununuzi wa vifaa vidogo vidogo.

Hata hivyo, ukaguzi umebaini dosari mbali mbali katika ujenzi huo kama zifuatazo:

1. Nyumba zote zilizojengwa na vikosi zimefanyika nyufa kwenye kuta na chini katika sakafu (floor).
2. Sehemu za vikuta vya nyuma vya kuingia mlango wa nyuma zimebomoka kutokana na uhaba wa saruji iliyotumika.
3. Kupinda kwa milango kunapelekea milango kushindwa kufunga vizuri.
4. Baadhi ya sehemu za nyumba zimeanza kubomoka.
5. Karo za maji machafu nne (4) zilizojengwa tayari zina athari za kupasuka kutokana na saruji hafifu iliyotumika.

Ujenzi wa nyumba hizo ulifanywa chini ya kiwango, ingawa, ulitumia gharama kubwa na kupelekea kukosekana kwa ufanisi hali inayoweza kusababisha nyumba hizo kushindwa kudumu kwa muda mrefu na kupelekea hasara kwa Serikali.

### Majibu ya Mamlaka

Ushauri ulipokelewa kwa ZURA kuwasiliana na Mshauri Elekezi pamoja na Wakandarasi kwa kuchukuwa hatua dhidi ya hoja hiyo iliyoibuliwa na Wakaguzi, uthibitisho ni barua zilizotumwa kwa Wakala wa Majengo pamoja na majibu husika

yaliyowasilishwa.

Katika ujenzi wa nyumba zaidi ya moja, Mshauri Elekezi anaweza kusanifu namna ya ujenzi wa karo kwa ajili ya upokeaji wa maji machafu kwa idadi ya nyumba maalum.

### Uchunguzi wa Kamati

Ili kujiridhisha na kilichoelezwa na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Kamati ya LAAC ilifanya ziara katika nyumba hizo na kuridhika na maelezo ya Mkaguzi Mkuu. Pamoja na maelezo hayo Kamati ya LAAC baada ya kufanya mahojiano na Wajenzi na Wakaazi wa nyumba hizo imebaini yafuatayo:

1. Nyumba hizo zilijengwa kwa gharama kati ya Tsh. 53 Milioni hadi Tsh. 43 Milioni gharama ambazo hazikuwa na uhalisia kwa mujibu wa nyumba husika, kitendo kilichopelekea kutopatikana ufanisi uliotarajiwa katika ujenzi wa nyumba hizo. Hii ni kutokana na kuwa Wajenzi wa nyumba hizo (Vikosi vya SMZ) walipendekeza nyumba hizo kujengwa kama ifuatavyo:
    a. Makisio ya awali ya ujenzi wa nyumba hizo walipendekeza kujengwa kwa gharama ya Tsh. 120 Milioni, isipokuwa kwamba, gharama hizo zilionekana kuwa ni kubwa sana na Serikali aliwataka wapunguze.
    b. Makisio ya pili wakapendekeza Tsh. 93 Milioni ambazo pia zilionekana gharama hizo kuwa ni kubwa.
    c. Makisio ya tatu wakapendekeza Tsh. 75 Milioni nazo zikaonekana ni nyingi.
2. Kati ya nyumba 31 zilizojengwa, nyumba tatu hazijahamiwa na zipo chini ya uangalizi wa Afisi ya Mkoa.
3. Baadhi ya karo zipo juu na nyumba zipo chini jambo linalopelekea uchafu kushindwa kutiririka vizuri na hivyo, karo hizo huziba.
4. Karo 1 inatumiwa na jumla ya nyumba 8 kitu ambacho ni kinyume na uratibu za kijenzi.
5. Masafa ya zilizopo karo na nyumba ni marefu sana, hivyo, uchafu hushindwa kutiririka vizuri na hatimae karo huziba.
6. Wajenzi walikuwa wanatoa ushauri juu ya mambo mbali mbali, isipokuwa kwamba, ushauri wao ulikuwa hausikilizwi na Mshauri Elekezi ambae ni Wakala wa Majengo.
7. Mshauri Elekezi alipelekwa na Baraza la Mapinduzi, hivyo, ZURA walikuwa hawana fursa ya kufuatilia au kuhoji chochote, kazi yao ilikuwa ni kutoa vifaa tu.

### Mapendekezo ya Kamati

Kutokana na uchunguzi huo Kamati ya LAAC imependekeza yafuatayo:

1. Serikali iwe na utaratibu wa kuwasilikiza Wataalamu wake na sio kufanya kazi kwa mazoea.
2. Kwa kuwa Taasisi inayolipa gharama juu ya jambo husika ndio inayokaguliwa na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na dosari yoyote itakayobainika inabebwa na Taasisi hiyo, hivyo, Taasisi hiyo ipewe nafasi kubwa ya kusimamia na kutoa ushauri katika jambo husika na isibakie kama Mtazamaji tu.
3. Kasoro zote zilizobainika kuchukuliwa hatua haraka iwezekanavyo kabla ya athiri kubwa kutokea na kuitia hasara Serikali.

## II. RIPOTI YA UKAGUZI MAALUM KUHUSU MALIPO YA NAULI YA WALIMU "BUS FARE" KWA SERIKALI ZA MITAA – PEMBA KWA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2020

Kwa mujibu wa barua ya tarehe 02 Disemba, 2011 kutoka kwa Katibu Mkuu (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora iliyofafanua kuhusu malipo ya posho la nauli kwa walimu na baadhi ya wafanyakazi nje ya kada ya ualimu. Lengo kuu la ulipwaji wa nauli za walimu ni kuwapunguzia gharama za usafiri pamoja na kuwawezesha kufika katika kituo cha kazi kwa wakati na kupelekea kuweza kufikia malengo yaliyopangwa.

## 8.4 MAMBO YALIYOBAINIKA KATIKA UKAGUZI MAALUM WA NAULI ZA WALIMU PEMBA (BUSFARE)

### BARAZA LA MJI MKOANI

### 8.4.1. Posho la nauli ambalo halikulipwa Tsh. 52,117,200.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa Jumla ya Tsh 52,117,200 nifedha za posho la nauli za walimu kwa miezi sita ambayo ni Januari 2020, Febuari 2020, Marchi 2020, Septemba 2020, Oktoba 2020 na Novemba 2020 ambazo hazikulipwa.

Kutokulipwa kwa posho la nauli kwa walimu ni kwenda kinyume na barua ya tarehe 2/12/2011 kutoka kwa Katibu Mkuu (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora inayofafanua kuhusu malipo ya posho hilo. Aidha inapelekea kutokufikia kwa malengo yaliyopangwa yanayohusiana na utolewaji wa posho hilo.

**Jadweli hapo chini linaonyesha idadi ya miezi pamoja naposho la nauli ambazo hazikulipwa.**

| S/N | Mwezi | Siku za kazi | Idadi ya Skuli | Idadi ya Walimu | Fedha ambazo hazikulipwa |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Januari 2020 | 22 | 27 | 137 | 6,725,000 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 2. | Febuari 2020 | 20 | 27 | 137 | 6,725,000 |
| 3. | Machi 2020 | 22 | 27 | 137 | 6,725,000 |
| 4. | Septemba 2020 | 22 | 27 | 137 | 10,647,400 |
| 5. | Oktoba 2020 | 20 | 27 | 137 | 10,647,400 |
| 6. | Novemba 2020 | 21 | 27 | 137 | 10,647,400 |
| | JUMLA | | | | 52,117,200 |

**Majibu**

Ukweli juu ya hoja ni kwamba Malipo ya nauli kwa waalimu yanalipwa kutokana na kupatikana kwa fedha za matumizi mengineyo (O.C) kutoka serikali kuu, kwa hiyo miezi ambayo posho hilo halikulipwa ni ile miezi ambayo fedha za matumizi mengineyo hazikupatikana ambapo kwa mnasaba wa hoja hii mwaka huu ulikua ni mwaka ambao changamoto ya upatikanaji wa fedha za OC ulitokana na kuliibuka kwa janga la maradhi ya COVID 19. Hivyo basi upatikanaji wa fedha za OC kwa kipindi hicho haukua nzuri.

Hatua zilizochukuliwa na Ofisi ya Baraza la Mji Mkoani:

- Baraza limekua likitoa mapendekezo katika kipindi cha uandaaji wa bajeti kwamba fedha za malipo ya nauli kwa waalimu ziambatanishwe na mishahara ili kuepusha kutokupatikana kwa posho hilo, hata hivyo mpaka kumalizika kwa ugatuzi bado pendekezo hilo halijafanyiwa kazi, jambo ambalo linapelekea kutokupatikana kwa fedha hizo kwa uhakika na hatimaye waalimu kukosa nauli.
- Baraza la Mji Mkoani lilichukua hatua ya kuziorodhesha fedha hizo katika orodha ya madeni ambayo yalitakiwa kuwasilishwa Wizarani.

**Uchunguzi wa Kamati**

Kamati katika uchunguzi wake imebaini kuwa Baraza la Mji Mkoani limetenga bajeti kwa upande wa Shughuli za Elimu ya Maandalizi na Msingi ya Tzs 362,723,000 na kuweza kutumia jumla ya Tzs Tzs 330,260,000 sawa na asilimia 91 ya makadirio.

Aidha, Kamati imejirizisha katika bajeti ya kuwalipa walimu posho la nauli imewekwa katika kifungu cha Kusimamia na kuhuduma Skuli za maandalizi na msingi ambayo imetengewa jumla ya TZS 20,000,000 na kuweza kupatiwa jumla ya Tzs 19,500,000 sawa na asilimia 97.5.

Kutokana na hali hiyo Kamati imebaini ni kweli mapato ya matumizi mengineyo hayakuingizwa kikamilifu kama bajeti ilivyopangwa kwa mwaka huo wa fedha 2019/2020. hata hivyo hakukuwa na sababu ya kutolipa posho la nauli kwa

walimu hao kwani wangeliweza kupunguza matumizi katika baadhi ya shughuli za elimu ya maadalizi na msingi, badala yake kuliongeza fungu la bajeti ya posho la nauli ili kuweza kuwalipa walimu posho la nauli kwa kipindi kilichokosekana fedha hizo kutokana ulipaji wa posho hilo kuwa ni agizo maalum hivyo ilikua ni busara kulipa kipaombele agizo hilo

Vile vile, Baraza la Mji Mkoani wangeliweza kupunguza shughuli za Baraza na kuweza kulipa fedha hizo kwa wakati kwa vile Mamlaka hizi zimeweza kuvuka malengo ya makusanyo kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kwa kukadiria kukusanya jumla ya Tzs 340,000,000 na kufanikiwa kukusanya jumla ya Tzs 341,944,368 sawa na asilimia 101.

**Mapendekezo ya Kamati**

Kamati inapenda kusisitiza kuwa maagizo yanayotolewa na Serikali sijambo la kupuuzwa ni vyema taasisi zinapopewa maagizo hayo kuyatekeleza kwa ufanisi mkubwa.

Aidha kamati inasisitiza kwa vile walimu hao tayari wamesharudishwa wizarani kutokana na kuondolewa kwa Ugatuzi hivyo hivyo Baraza la Mji Mkoani inatakiwa iwasilishe deni hilo Wizara ya Elimu na wizara ifanye uhakiki wa madai ya madeni ambayo hayakulipwa kwa kipindi hicho ili wahusika waweze kupatiwa stahiki zao.

**8.4.2 Walimu ambao hawakuingizwa katika orodha ya malipo ya posho la nauli.**

Kwa mujibu wa barua ya tarehe 02/12/2011 kutoka kwa Katibu Mkuu wa (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora linalohusu muongozo wa ulipaji wa posho la nauli kwa walimu na baadhi ya wafanyakazi nje ya kada ya Ualimu linafafanua kigezo cha masafa (kuanzia kilomita tano) ambacho kinastahiki kutumika ili kuweza kulipa posho la nauli.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba kuna idadi ya Walimu kumi “10” ambao wamekidhi kigenzo hicho lakini hawakuweza kuingizwa katika orodha ya malipo ya walimu wanaostahiki kulipwa posho hilo.

Kutokuwaingiza katika orodha ya malipo ya posho la nauli walimu waliokidhi kigenzo cha masafa ni kwenda kinyume na barua ya tarehe 02/12/2011 kutoka kwa katibu Mkuu (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora Zanzibar.

**Jadweli lifuatalo hapo chini linaonyesha walimu ambao hawakuingizwa katika orodha ya kulipwa posho la nauli.**

| Jina la Mwalimu | Anapoishi | Anaposomesha | Mwezi wa Ajira |
|---|---|---|---|
| Salma Rashid Suleiman | Ngwachani | Mtuhaliwa Msingi | Sept. 2020 |
| Makame Bakar Faki | Kiuyu Minungwini | Mtuhaliwa Msingi | Julai 2020 |
| Salma Said Sultan | Mbuguwani | Mtuhaliwa Msingi | Julai 2020 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Ali Mtumwa Abdalla | Muambe Jombwe | Muambe Shamiani | Julai 2020 |
| Abeida Amir Abdalla | Jonza Mtambile | Tumbi Msingi | Sept.2020 |
| Zuhura Khamis Ali | Ukutini Tuwatugawe | Chambani Msingi | Januari 2020 |
| Bidia Moh'd Juma | Minazini Msingi | Mjini Ole | Juni 2020 |
| Khamis Othmani Pandu | Mwambe Msingi | Sipwese | 2010 |
| Bikombo Suleiman Hamad | Mwambe Msingi | Kengeja | 2020 |
| Mpaji Mali Iddi | Mwambe Msingi | Kengeja | 2010 |

**Majibu**
Baraza la Mji Mkoani lilikuwa na utaratibu wa kuwaingiza katika mfumo wa kuwalipa posho la nauli waalimu wote ambao wamekidhi vigezo vya kulipwa posho hilo. Kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa kutoka wizara ya elimu na mafunzo ya amali Zanzibar, Mwalimu anaestahiki kulipwa posho la nauli ni yule anaetembea kwa umbali usiopunguwa kilomita tano (5) kutoka sehemu anayoishi.

Ili Baraza liweze kulipa posho la nauli kwa wale waalimu wanaostahiki baada ya kuajiriwa, muajiriwa anatakiwa kuomba posho hilo kwa kuandika barua kwa Mkurugenzi, impitie mwalimu mkuu, impitie afisa elimu wilaya na kuainisha mwezi alioajiriwa, anapoishi, anapofanya kazi na nauli sahihi anayotumia kwenda na kurudi kazini, baada ya Mwalimu Mkuu na afisa elimu wilaya kujiridhisha na kuweka mapendekezo yao katika barua hiyo na kuleta kwa Mkurugenzi kwa ajili ya kuidhinisha malipo hayo kwa kuchambua na kulinganisha nauli iliyotajwa na muhusika. Kwa hivyo kwa wale ambao hawajalipwa ni kwamba Baraza halikupokea barua ya kuomba kulipwa stahiki hizo jambo ambalo inakua vikugumu kiutaratibu wa fedha kuanza kulipa posho hizo.

Pamoja na hayo Baraza mara zote tuliwakumbusha waalimu wakuu wa Skuli za msingi na maandalizi wanapopata waajiriwa wapya au wale wenye vigezo vya kulipwa nauli, wawakumbushe kuomba nauli hizo ili kuepusha malimbikizo ya madeni ya nauli kwa waalimu.

Hatua zilizochukuliwa na Baraza la Mji Mkoani.

Baraza la Mji Mkoani liliendelea kuwasisitiza walimu na wafanyakazi nje ya kada

ya ualimu na maafisa husika ambao wamekamilisha vigezo vya kuingizwa katika mfumo wa malipo ya posho la nauli kuhakikisha wanakamilisha taratibu zitakazowezesha kuingizwa katika mfumo wa posho la nauli kwa lengo la kupatiwa stahiki hii bila usumbufu.

**Uchunguzi wa Kamati**

Kamati katika kufuatilia ukweli wa majibu ya hoja hii iliomba kukutana na baadhi ya walimu ambao hawakuingizwa katika orodha ya malipo ili kuihakikisha Kamati iwapo waliwasilisha barua za kuomba nauli hizo au hawakuwasilisha kwa kuwa walikidhi vigezo vya masafa na walistahikii kupatiwa posho hilo.

Hata hivyo Kamati ilifanikiwa kuitisha kikao cha tarehe 18/08/2022 katika ukumbi wa Baraza la Mji Chake Chake kwa kuwahoji walimu wawili ambao ni Ndugu Abeida Amir Abdalla na Ndugu Makame Bakari Faki ambao wamethibitisha mbele ya Kamati kuandika barua hizo lakini Kamati haikuweza kupatiwa barua hizo kwa vile wahusika hawakuweza kuja nazo kutokana na kutopewa taarifa ya mapema ya kuja na barua hizo.

**Mapendekezo ya Kamati**

Kamati inaungana na hoja ya Mkaguzi hata hivyo inaziomba taasisi za Serikali ikiwemo Mabaraza ya miji na Halmashauri kutii maagizo ya Serikali na kuyaweka kipao mbele katika utekelezaji wa Shughuli zake.

Aidha, Kamati inaliomba Baraza la Mji Mkoani kufanya uhakiki wa madeni yote ya walimu ambao walikuwa wanakidhi kupatiwa posho la nauli kwa mwaka wa fedha 2019/2020 na hawakuweza kupatiwa posho hilo kwa kisingizio cha kutowasilishwa Barua za maombi ya nauli katika Baraza la Mji Mkoani, na kuwasilisha madeni hayo Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa ajili ya kulipwa madeni hayo ili walimu hao waweze kupatiwa stahiki haki zao.

### 8.4.3 Posho la nauli ambalo halilipwi kwa kila mwezi kwa wastani wa shilingi 1,632,400.

Baraza la Mji Mkoani –Pemba linawajibu wa kusimamia na kuendesha shughuli za Baraza ikiwa ni pamoja na kuwalipa walimu posho la nauli stahiki kulingana na kigezo cha masafa kama ilivyofafanuliwa katika barua ya tarehe 02/12/2011 kutoka kwa katibu Mkuu (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Ukaguzi umebaini kwamba Baraza la Mji Mkoani –Pemba halipangi viwango stahiki vya nauli kwa walimu kulingana na vigezo vya masafa ambapo kiwango cha posho la nauli kinacholipwa kwa baadhi ya walimu ni kidogo ukilinganisha na uhalisia wa masafa wanayotoka walimu hao. Aidha kulingana na taarifa za malipo za posho la nauli zinaonyesha kuwepo kwa tofauti baina ya malipo stahiki na malipo halisi yanayolipwa kwa wastani wa jumla ya shilingi 1,623,600 kwa mwezi.

Kutokulipwa walimu posho la nauli stahiki ni kwenda kinyume na toleola tarehe 02/12/2011 kutoka kwa katibu Mkuu (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Aidha, idadi na taarifa za walimu ambao hawalipwi posho la nauli stahiki zinaonekana katika kiambatanisho nambari 8(A).

**Majibu**
Baraza la Mji Mkoani lilikuwa likifuata miongozo na barua na matoleo mbali mbali yanayotolewa na (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora iliyohusiana na utaratibu wa kulipa posho la nauli kwa walimu na baadhi ya wafanyakazi nje ya kada ya Ualimu.

Inawezekana yakawepo mapungufu ya ulipaji wa posho la nauli kwa waalimu, Lakini Baraza limechukua juhudi kubwa kufanya marekebisho ya malipo ya nauli kulingana na nauli sahihi ya mwalimu anayotumia. Naomba ikumbukwe kwamba wakati Baraza linapokea ugatuzi waalimu walikua wanalipwa nauli kwa kiwango sawa kwa kilomita, Baraza limechukua juhudi ya kuangalia nauli kusika zinatotozwa na daladala pamoja na boda boda kwa yale masafa ambayo gari hazifiki na kuweka nauli hizo stahiki.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**
Kwa vile Baraza la Mji Mkoani limekiri kuwepo kwa mapungu ya ulipaji wa nauli kulingana na masafa wanaoishi walimu hao hata hivyo kamati inaendelea kulishauri Baraza la Mji Mkoani katika kufuata Sheria na kutekeleza maagizo mbalimbali yanayotolewa na Serikali kama yalivyo.
Aidha Kamati inaendelea kulishauri Baraza la Mji kufanya uhakiki wa deni hilo ambalo halikupwa kwa kila mwezi na kuwasilisha deni hilo Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa ajili ya kupatiwa stahiki wanazodai walimu hao.

### 8.4.4 Kutokufanyiwa kwa makisio ya posho la nauli
Baraza la Mji Mkoani – Pemba linawajibu wa kufanya makisio (Bajeti), kusimamia na kulipa posho la nauli kwa walimu na baadhi ya wafanyakazi nje ya kada ya ualimu.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kutokufanya kwa makisio ya gharama inayostahiki kwa ajili ya malipo ya posho la nauli kwa walimu na baadhi ya wafanyakazi wa Baraza la Mji Mkoani ambapo fedha za malipo ya posho hilo hulipwa kupitia fungu la elimu.

Kutokufanywa kwa makisio ya gharama za posho la nauli katika kipindi cha mwaka husika ni kwenda kinyume na kifungu nambari 41(2) cha sheria ya usimamizi ya fedha za umma nambari 12 ya mwaka 2016 ya Zanzibar.

**Majibu**
Kufuatia mabadiliko ya Serikali (UGATUZI) yaliyopelekea kuingizwakwa sekta ya

elimu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa Baraza la Mji Mkoani lilikuwa linapokea miongozo mbali mbali kuhusu kuweka bajeti ya sekta zilizogatuliwa. Hivyo basi kila mwaka Baraza.

Kwa mwaka wa kwanza bajeti ya sekta ya elimu ilitayarishwa katika wizara husika na baadae Baraza likapokea bajeti hizo na kuzifanyia kazi, kwa miaka iliyofuatia bajeti ya sekta hiyo ilitayarishwa katika bajeti kuu ya Ofisi ya Baraza la Mji Mkoani ambapo Makisio ya kifungu cha posho la nauli kwa walimu na maafisa pamoja na posho la TU-TU yalikuwa yakiingizwa katika mipangoya Ofisi.

**Uchunguzi wa Kamati**
Kamati katika uchunguzi wake imebaini kuwa Baraza la Mji Mkoani limepanga bajeti ya kuwalipa walimu posho la nauli imewekwa katika kifungu cha Kusimamia na kuhuduma Skuli za maandalizi na msingi ambayo imetengewa jumla ya TZS 342, 723,000 na kuweza kupatiwa jumla ya Tzs 310,760,000 sawa na asilimia 91.

Dosari iliyobainika ni kuwa bajeti hiyo haikuingizwa katika taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka jambo ambalo limepelekea kutoonekana bajeti hiyo ya posho la nauli na Mkaguzi.

**Mapendekezo ya Kamati**
Kamati inalishauri baraza la Mji Mkoani kufuata taratibu zote za ufungaji wa hesabu za mwisho wa mwaka kwa kuingiza bajeti za vifungu vyote vya mapato na matumizi kama vile miongozo unavyotutaka ili kukidhi viwango sahihi vya ufungaji wa mahesabu ya taasisi kitaifa na kimataifa.

### 8.4.5 Dosari katika utaratibu wa malipo ya posho la nauli
Baraza la Mji Mkoani-Pemba linawajibu wa kufanya malipo ya posho la nauli kwa walimu na baadhi ya wafanyakazi nje ya kada ya ualimu kwa kuzingatia mfumo madhubuti katika ulipaji wa posho hilo.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwepo kwa udhibiti usioridhisha wa ulipaji wa fedha za posho la nauli kwa walimu ambapo imebainika malipo hayo hulipwa kwa njia ya fedha taslimu kupitia walimu wakuu wa skuli husika kinyume na sheria ya usimamizi wa fedha za umma no.12 ya mwaka 2016 ya Zanzibar.

Aidha, imepelekea kuwepo kwa malalamiko kwa baadhi ya Walimu ambao hawakulipwa malipo ya posho la nauli licha ya kwamba walimu hao wameonekana katika malipo hayo.

**Jadweli lifuatalo hapo chini linaonesha orodha ya skuli pamoja na walimu wakuu wanaokabidhiwa fedha taslimu kwa ajili ya posho la nauli**

| NAMBA | JINA LA MWALIMU | SKULI HUSIKA |
|---|---|---|
| 1 | Ilyasa Fadhili Shaka | Tironi Msingi |
| 2 | Makame Bakari Haji | Mtuhaliwa msingi |
| 3 | Daudi Shamata Makame | Shamiani Mwambe |
| 4 | Omar Ali Muhammed | Tumbi Msingi |
| 5 | Halima Mohd Abdalla | Minazini Msingi |
| 6 | Mohd Haji Mohd | Mizingani Msingi |
| 7 | Ali Mohd Omar | Mwambe Msingi |
| 8 | Ali Khamis Mali | Chambani Msingi |
| 9 | Bakari Omar Mohd | Jambang'ome |
| 10 | Mwaka Abdalla Shamte | Mtambile Msingi |
| 11 | Hamadi Haji Makame | Kangani Msingi |

**Majibu**

Ukweli juu ya hoja hii ni kwamba wakati Baraza la Mji Mkoani linapokea ugatuzi lilikuta utaratibu wa kuwalipa waalimu fedha taslimu kupitia kwa waalimu wakuu, baada ya kuona hivyo Baraza likabadilisha mfumo wa ulipaji huo na likawaamuru waalimu walete akaunti zao za Benki ili posho za nauli zilipwe kupitia benki.

**Uchunguzi wa Kamati**

Kamati katika kufuatilia hoja hii kamati imeomba kukutana na walimu ambao hawakupokea malipo ya posho la nauli zao na wameonekana katika vocha za malipo kwa ajili ya kuwafanyia mahojiani ili kupata ufafanuzi wa kadhia hii.

Kamati ilifanikiwa kuitisha kikao cha tarehe 18/08/2022 katika ukumbi wa Baraza la Mji Chake Chake kwa kuwahoji walimu watatu ambao Walimu hao Ndugu Sakina Ali Makame na Ndugu Amina Said Mohd kutoka Skuli ya Msingi Mizingani wote wamekiri kuwa fedha zao zote wamepewa na walimu wakuu wao na saini zote ni za kwao tofauti na alivyoripoti Mkaguzi katika kitabu chake.

Aidha, Kamati ilifanikiwa kufanya mahojiano na Ndugu Juma Abbas Mjawir kutoka Skuli ya Tironi yeye amekiri kutopokea fedha zake licha ya kuonekana katika orodha ya malipo kuwa ameshachukua malipo hayo na amekiri kuona saini sio ya kwake.

**Mapendekezo ya Kamati**

Kamati inaishauri Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali wakati wanapochukua maelezo kwa watu ambao wameathiriwa na hoja Fulani ni vyema kuweka mifumo ya kurikodi maelezo hayo ili kubaini wahusika ambao

watakaotoa maelezo tofauti kwa Mkaguzi mkuu wakati wa uchunguzi na kuyabadili maelezo hayo pindi wanapohojiwa na Kamati za Baraza la Wawakilishi ili hatua za kisheria ziweze kuchukuliwa kwa wote watakao husika kuzidanganyaa taasisi hizi mbili za Serikali.
Aidha Kamati inalishauri Baraza la Mji kufuatilia kwa karibu na kubaini wahusika wote waliojihusishwa na vitendo hivyo ili kukomesha vitendo hivyo ambavyo havileti tija katika nchi yetu.

**8.4.6. Kutokufanyiwa marekebisho orodha ya malipo kwa baadhi ya walimu baada ya kuhamishwa**

Baraza la Mji Mkoani –Pemba inawajibu wa kusimamia uhamisho wa walimu pamoja na mafao yao kutoka skuli moja kwenda nyengine.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwepo walimu waliohamishwa kutoka skuli moja kwenda skuli nyengine bila kufanyiwa marekebisho ya uhamisho wa malipo ya posho za nauli zao, kufanya hivyo inapelekea usumbufu kwa walimu kusomesha Skuli moja na kupokea posho la nauli Skuli nyengine.

Kutokufanyiwa marekebisho ya malipo ya posho la nauli la walimu baada ya uhamisho ni kwenda kinyume na taratibu za kiutumishi.

**Jadweli lifuatalo hapo chini linaonyesha walimu waliohamishwa bila ya kufanyiwa marekebisho ya posho za nauli**

| NAM. | JINA LA MWALIMU | SKULI ALIOTOKA | SKULI ALIYOPO SASA |
|---|---|---|---|
| 1 | Zainab Omar Haji | Mkanyageni shidi msingi | Mwambe Msingi |
| 2 | Huda Maisara Kombo | Mkanyageni Shidi Msingi | Mwambe Msingi |
| 3 | Semeni Moh'd Abeid | Mtambile Msingi | Mwambe Msingi |

**Majibu**

Baraza la Mji Mkoani lilikuwa na utaratibu wa kuwafanyia marekebisho ya taarifa za uhamisho wa walimu kila inapotokea kuhamishwa kwa walimu kutoka skuli moja kwenda Skuli nyengine, kila inapozipokea taarifa hizo kutoka kwa mamlaka husika, kwa lengo la kurahisisha kufanyika kwa malipo ya stahiki zote wanazostahiki kulipwa walimu hao ikiwemo posho la nauli.

Walimu waliotajwa katika orodha ya jadweli hapo juu marekebisho ya taarifa za uhamisho wao kutoka skuli zao za awali kwenda kuendelea na kazi katika skuli nyengine ulikuwa bado hazijawasilishwa katika ofisi za Baraza la Mji Mkoani

wakati ukaguzi huo unafanyika.

**Uchunguzi na mapendekezo ya Kamati**

Kamati imebaini kuwa utaratibu wa kuwasilisha barua za uhamisho wa walimu kwenda kwa Mkurugenzi wa Baraza la Mji Mkoani Ulikuwa hauna utaratibu mzuri kwani Kamati ilipozihitaji barua hizo kwa ukaguzi zilikosekana na huenda hii ndio ikawa sababu ya kucheleweshа kufanya marekebisho ya ulipaji wa posho la nauli katika skuli husika ambayo walimu hao wanafanyakazi.

**Mapendekezo ya Kamati**

Kamati inaushauri uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni juu ya utekelezaji wa Sheria mbalimbali za kiutumishi ikiwemo sheria ya ambazo inazitaka taasisi za Serikali kuhakikisha kuwa indapo mtumishi atahamishwa kutoka sehemu moja kwenda nyengine ni vyema maslahi yake yote yaweze kuhamishwa mara moja iwezekanavyo.

BARAZA LA MJI CHAKE CHAKE

**8.4.7 Posho la nauli ambalo halikulipwa shilingi 41,735,800**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa jumla ya shilingi 41,735,800 ni fedha za posho la nauli za walimu kwa miezi mitano”5” ambayo ni Januari 2020, Machi 2020, Septemba 2020, Oktoba 2020 na Novemba 2020 ambazo hazikulipwa.

Kutokulipwa kwa posho la nauli kwa walimu ni kwenda kinyume na barua ya tarehe 02/12/2011 kutoka kwa Katibu Mkuu (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora inayofafanua kuhusu malipo ya posho hilo.

Aidha, inapelekea kutokufikia kwa malengo yaliyopangwa yanayohusiana na utolewaji wa posho hilo.

Jaduweli lifuatalo linaonyesha idadi ya miezi pamoja na fedha za posho la nauli ambazo hazikulipwa.

| Nam | Mwezi | Siku za kazi | Idadi ya Skuli | Idadi ya walimu | Fedha ambazo hazikulipwa |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Januari, 2020 | 20 | 28 | 237 | 7,589,000 |
| 2 | Machi, 2020 | 13 | 28 | 236 | 5,217,400 |
| 3 | Septemba, 2020 | 22 | 30 | 289 | 10,741,000 |
| 4 | Oktoba, 2020 | 16 | 30 | 289 | 7,911,000 |
| 5 | Novemba, 2020 | 21 | 30 | 289 | 10,277,200 |

| | |
|---|---|
| Jumla | 41,735,800 |

**Majibu ya Baraza la Mji Chake Chake**

Kwa kipindi hichi kuna baadhi ya miezi ambayo walimu hawakulipwa nauli, hii ni kutokana na kutokea kwa janga la taifa la ugonjwa wa COVID-19 kwa baadhi ya miezi ambayo hatukuingiziwa bajeti zao za nauli. Miezi ambayo hutakupata ni kama tajwa kwenye taarifa ya CAG isipokua mwezi wa Oktoba 2020 tulipata fedha na tulilipa ada ya nauli kwa walimu kwa deni la posho la mwezi wa Agosti 2020. Hivyo, tunashauri nauli za walimu zingelipwa moja kwa moja kwenye mishahara yao kama maposho mengine ili kundosha usumbufu huu.

**Uchunguzi wa Kamati**

Kamati katika uchunguzi wake imebaini kuwa Baraza la Mji Chake Chake imetenga bajeti kwa upande wa Shughuli za Elimu ya Maandalizi na Msingi ya Tzs 225,430,000 na kuweza kutumia jumla ya Tzs 186,520,000 sawa na asilimia 91 ya makadirio.

Aidha, Kamati imejirizisha katika bajeti ya kuwalipa walimu posho la nauli imewekwa katika kifungu cha Kusimamia na kuhuduma Skuli za maandalizi na msingi ambayo imetengewa jumla ya TZS 222,600,000 na kuweza kutumia jumla ya Tzs 183,520,000 sawa na asilimia 82.

Aidha, kwa vile taasisi hizo zinakusanya mapato yao wenyewe na kwa mwaka wa fedha 2019/2020 Baraza la Mji Wete limekadiria kukusanya jumla Tzs 600,000,000 katika vyanzo vyake mbali mbali na kuweza kukusanya jumla ya Tzs 523,137,240 sawa na asilimia 87

Kutokana na hali hiyo Kamati imebaini ni kweli mapato ya matumizi mengineyo hayakuingizwa kikamilifu kama bajeti ilivyopangwa kwa mwaka huo wa fedha 2019/2020. hata hivyo hakukuwa na sababu ya kutolipa posho la nauli kwa walimu hao kwani wangeliweza kupunguza matumizi katika baadhi ya shughuli za elimu ya maadalizi na msingi, badala yake kuliongeza fungu la bajeti ya posho la nauli ili kuweza kuwalipa walimu posho la nauli kwa kipindi kilichokosekana fedha hizo kutokana na jambo hilo kuwa ni agizo maalum hivyo ilikua ni busara kulipa kipaombele

Vile vile, Baraza lingeweza kupunguza shughuli zake mbalimbali na kuweza kulipa fedha hizo kwa wakati kwa vile wameweza kukusanya mapato yao ya ndani kwa asilimia 87.2% ya malengo waliyojiwekea,

**Mapendekezo ya Kamati**

Kamati inasititiza kuyapa vipao mbele maagizo yote yanayotolewa na viongozi wetu wa ngazi za juu kwa lengo la kuleta ufanisi na uwajibikaji wa majukumu yetu ya kila siku. Aidha, kamati inaliomba baraza la Mji Chake Chake kuwasilisha

barua za madai ya madeni hayo kwenda Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar ili kufanyiwa uhakiki wa madeni hayo na kuweza kupatiwa walimu stahiki zao kwa kila mwenzi ambao hawakupatiwa wakati walipokuwa katika mamlaka za Serikali za Mitaa kipindi cha Ugatuzi.

### 8.4.8 Walimu ambao hawakuingizwa katika orodha ya malipo ya posho la nauli

Kwa mujibu wa barua ya tarehe 02/12/2011 kutoka kwa Katribu Mkuu (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora linalohusu muongozo wa ulipwaji wa posho la nauli kwa walimu na baadhi ya Wafanyakazi nje ya kada ya ualimu linafafanua kigezo cha masafa (kuanzia kilomita tano) ambacho kinastahiki kutumika ili kuweza kulipa posho la nauli.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba kuna idadi ya walimu arobaini na tisa "49" ambao wamekidhi kigezo hicho lakini hawakuweza kuingizwa katika orodha ya malipo ya walimu wanaostahiki kulipwa posho hilo.

Kutokuwaingiza katika orodha ya malipo ya posho la nauli walimu waliokidhi kigezo cha masafa ni kwenda kinyume barua ya tarehe 02/12/2011 kutoka kwa Katibu Mkuu (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora Zanzibar.

**Jadweli lifuatalo hapo chini linaonyesha walimu ambao hawakuingizwa katika orodha ya kulipwa posho la nauli.**

| Nam | Jina la Mwalimu | Anaposhi | Anaposomesha | Mwezi wa Ajira |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Shuwekha Said Rashid | Wesha | Karume | Nov,2018 |
| 2 | Muhamed Suleiman Salim | Wete | Ziwani | Jan,2020 |
| 3 | Mariam Salum Moh'd | Mkoroshoni | Pondeani | Feb,2020 |
| 4 | Tahria Hamza Suleiman | Wesha | Pondeani | Nov,2019 |
| 5 | Fadhila Said Hamad | Madungu | Ziwani | Julai,2020 |
| 6 | Mgeni Khamis Moh'd | Machomane | Furaha | Feb,2020 |
| 7 | Khairat Juma Abdulla | Mtambwe | Ziwani | Mei,2020 |
| 8 | Mgeni Seif Kombo | Wete Selemu | Ziwani | Machi,2020 |
| 9 | Mgeni Juma Kassim | Msingini | Furaha | Julai,2020 |
| 10 | Mgeni Omar Said | Wawi Ditia | Pondeani | Juni,2020 |
| 11 | Mariam Ali Nassor | Pondeani | Furaha | Machi,2020 |
| 12 | Khairat Kassim Shaaban | Mkungu Malofa | Pondeani | Juni,2020 |
| 13 | Asha Omar Juma | Wesha | Pondeani | Juni,2020 |
| 14 | Zuhura Zahor Massoud | Wesha | Pondeani | Juni,2020 |
| 15 | Fatma Khamis Amour | Minazini | Pondeani | Sept,2020 |
| 16 | Khadija Hussein Faki | Chanjamjawiri | Pujini | Feb,2020 |
| 17 | Fathiya Rashid Abeid | Mkoroshoni | Furaha | Juni,2020 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 18 | Maryam Khatib Hamad | Madungu | Pujini | Nov,2019 |
| 19 | Rabia Hamad Manja | Machomane | Pujini | Juni,2020 |
| 20 | Thabit Said Khamis | Mbuzini | Pujini | Mei,2020 |
| 21 | Asila Hamad Othman | Kilimni | Pujini | Juni,2020 |
| 22 | Khalfan Salu Suleiman | Wete Kizimbani | Mbuzini | Machi,2020 |
| 23 | Shuwena Nassor Abeid | Kiuyu Micheweni | Mbuzini | Machi,2020 |
| 24 | Fadhila Hamad Suleiman | Mavungwa | Mbuzini | Oktoba,2017 |
| 25 | Fatma Moh'd Ali | Wawi | Ng'ambwa | Machi,2020 |
| 26 | Aziza Haji Khamis | Kangagani | Mbuzini | Oktoba,2019 |
| 27 | Nachia Juma Bakar | Machomane | Vikunguni | Nov. 2013 |
| 28 | Tatu Moh'd Haji | Machomane | Vikunguni | 2018 |
| 29 | Tamima Moh'd Said | Machomane | Vikunguni | 2001 |
| 30 | Fatma Amour Mbarouk | Machomane | Vikunguni | Feb,2003 |
| 31 | Zuwena Abdulla Ali | Vitongoji | Uwandani | Mei,2018 |
| 32 | Mafunda Masoud Ali | Wete Kipangani | Mbuzini | Nov,2019 |
| 33 | Zainab Moh'd Jadi | Mwane | Mbuzini | Nov,2019 |
| 34 | Rahma Mbwana Makame | Kiuyu Micheweni | Mbuzini | Mei,2019 |
| 35 | Zuhura Moh'd Said | Mkanjuni | Ng'ambwa | April,2018 |
| 36 | Moza Haji Kassim | Vitongoji | Uwandani | Juni,2020 |
| 37 | Missi Masoud Shamte | Mchangamdogo | Vitongoji | Machi,2020 |
| 38 | Kombo Sheha Rashid | Wingwi | Uwandani | April,2020 |
| 39 | Shaina Suleiman Ali | Kangagani | Uwandani | April,2020 |
| 40 | Bimkubwa Khamis Ali | Wete | Mbuzini | Nov,2019 |
| 41 | Fatma Mbarouk Saleh | Vikunguni | Vitongoji | Sept,2020 |
| 42 | Asha Choumu Ngwali | Vikunguni | Vitongoji | Machi,2020 |
| 43 | Amina Sheha Bakar | Machomane | Vikunguni | Nov,2018 |
| 44 | Maryam Mussa Hamad (Muhudumu) | Kiuyu Minungwini | Vikunguni | Juni,2020 |
| 45 | Asha Omar Suleiman | Ole | Uwandani | Nov,2011 |
| 46 | Khadija Hafidh Juma | Ole | Uwandani | Nov,2019 |
| 47 | Jabu Faki Hassan (Muhudumu) | Chanjaani | Wawi | Julai,2020 |
| 48 | Sauda Khamis Said (Muhudumu) | Furaha | Wawi | Julai,2020 |
| 49 | Amina Muhsini Abdulrahman | Mkoroshoni | Vitongoji | Juni,2020 |

**Majibu**
Kuna baadhi ya idadi ya walimu kwa mwaka huu wa fedha kweli hawakuingizwa katika orodha ya malipo, hii ni kutokana na uhamisho wa walimu kutoka eneo dogo ambalo alikua analifanyia kazi na kwenda eneo kubwa ambalo alistahiki sasa kupewa nauli pamoja na ajira mpya za walimu kwamba mwalimu anafikia kigezo sasa cha kupewa nauli lakini bajeti ya nauli hua imeshapitishwa, sasa inakua ni vigumu kuweza kuwaingiza wote kwa mwaka husika hivyo wanakua wanaingia kidogo kidogo kwa utaratibu.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**
Kamati katika kuthibitisha hoja hii iliomba kupatiwa barua ya uhamisho kwa baadhi ya walimu inayoonesha walimu hao kutolewa katika mfumo wa malipo kutokana na kuhamishiwa katika eneo dogo ambalo halistahili kulipwa posho la nauli lakini barua hizo hazikupatika kwa ukaguzi.

Aidha, Kamati iliomba kupatiwa kibali cha uajiri wa walimu wapya ili kuthibitisha kama iwapo ni kweli kuwa walimu ambao wametajwa katika ripoti ya Mkaguzi miongoni mwao ni wapya na hawakuingizwa katika orodha ya malipo kwa sababu ya kuwa hakuemo katika bajeti ya mwaka 2019/2020 na Kamati iliweza kupatiwa orodha hiyo ya walimu wapya ambao wameajiriwa na kamati imeridhika na majibu hayo.

Hata hivyo, Kamati inalishauri Baraza la Mji Chake Chake kuyapa vipao mbele maagizo yote yanayotolewa na viongozi wetu wa ngazi za juu kwa lengo la kuleta ufanisi na uwajibikaji wa majukumu yetu ya kila siku kwa vile Baraza la Mji linaogozwa kwa sheria namba 7 ya mwaka 2014 na kanuni zake ambazo inazipa Mamlaka hizi uwezo wa kuhaulisha vifungu vya matumizi na kufanya ongezeko la Bajeti kupitia Baraza lake la Madiwani.

Aidha, Kamati inaliomba Baraza la Mji Mkoani kuwasilisha madeni ya posho la nauli Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar kwa ajili ya kufanyiwa uhakiki wa madeni hayo na kuweza kupatiwa walimu stahiki zao kwa kila mwenzi ambao hawakupatiwa wakati walipokuwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kipindi cha Ugatuzi.

**8.4.9 Posho la nauli ambalo halilipwi kwa kila mwezi kwa wastani wa shilingi 224,400**
Baraza la Mji Chake Chake – Pemba lina wajibu wa kusimamia shughuli za Baraza ikiwa ni pamoja na kuwalipa walimu posho la nauli stahiki kulingana na kigezo cha masafa kama ilivyofafanuliwa katika barua ya tarehe 02/12/2011 kutoka kwa Katibu Mkuu (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Ukaguzi umebaini kwamba Baraza la Mji Chake Chake – Pemba halipangi viwango stahiki vya posho la nauli kwa walimu kulingana na vigezo vya masafa

ambapo kiwango cha posho la nauli kinacholipwa kwa baadhi ya walimu ni kidogo ukilinganisha na uhalisia wa masafa wanayotoka walimu hao. Aidha kulingana na taarifa za malipo za posho la nauli zinaonyesha kuwepo kwa tofauti baina ya malipo stahiki na malipo halisi yanayolipwa kwa wastani wa jumla ya shilingi 224,400/= kwa mwezi.

Kutokuwalipa walimu posho la nauli stahiki ni kwenda kinyume na toleo la tarehe 02/12/2011 kutoka kwa Katibu Mkuu (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora Zanzibar.

Aidha, idadi pamoja na taarifa za walimu ambao hawalipwi posho la nauli stahiki ni kama zinavyonekana katika Jadweli:

| NAM | JINA LA MWALIMU | SKULI ANAYOFUNDISHA | PAHALA ANAPOISHI | POSHO ANAZOSTAHIKI KULIPWA KWA SIKU | POSHO LINALOLIPWA KWA SIKU | POSHO AMBALO HALILIPWI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Unguja Juma Moh'd | Ziwani | Mkoroshoni | 1400 | 2000 | 600 |
| 2 | Salma Ali Muhidini | Ziwani | Mbuzini | 1400 | 2000 | 600 |
| 3 | Pili Hafidh Juma | Ziwani | Mbuzini | 1400 | 2000 | 600 |
| 4 | Jamila Khamis Said | Ziwani | Mkoroshoni | 1400 | 2000 | 600 |
| 5 | Asha Saleh Juma | Ziwani | Mkoroshoni | 1400 | 2000 | 600 |
| 6 | Farashuu Abdalla Khamis | Ziwani | Machomanne | 1400 | 2000 | 600 |
| 7 | Halima Rashid Masoud | Ziwani | Gombani | 1400 | 2000 | 600 |
| 8 | Asha Juma Moh'd | Ziwani | Mbuzini | 1400 | 2000 | 600 |
| 9 | Fatma Ali Adam | Ziwani | Mkoroshoni | 1400 | 2000 | 600 |
| 10 | Dina Shaibu Kheir | Ziwani | Mkanjuni | 1400 | 2000 | 600 |
| 11 | Hassan Shariff Salum | Ziwani | Kangangani | 2,400 | 3000 | 600 |
| 12 | Fatma Khamis Othman | Ziwani | Kaole | 2,800 | 3000 | 200 |
| 13 | Maryam Suleiman Khalfan | Ziwani | Gombani | 1,400 | 2000 | 600 |
| 14 | Ali Hafidhi Juma | Vitongoji | Ole | 1,400 | 2000 | 600 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 15 | Zakia Moh'd Said | Pondeani | Mkungu Malofa | 1000 | 1400 | 600 |
| 16 | Zuwena Moh'd Issa | Pondeani | Kichungwani | 1000 | 1600 | 600 |
| 17 | Mchumi Hassan | Uwandani | Kangagani | 1200 | 2000 | 800 |
| 18 | Zulfa Suleiman Said | Uwandani | Ole | 1200 | 1400 | 200 |
| | **JUMLA KWA SIKU** | | | **26,400** | **36,400** | **10,200** |
| | **JUMLA KWA MWEZI** | | | | | **224,400** |

**Majibu**

Kutokana na kubadilika ada ya nauli kwa gari za abiria ndio hupelekea utofauti huo. Lakini kama ofisi ilifanya jitihada ya kufanya mapitio ya nauli halisi kwa mujibu wa masafa husika ili kuona kuwa mwalimu analipwa nauli yake stahiki. Ila tuelewe kuwa hii itatokea mara kwa mara kutokana na mabadiliko ya nauli.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kwa vile Baraza la Mji Chake Chake limekiri kuwepo kwa dosari hii hata hivyo Baraza la Mji Chake Chake lilikuwa na uwezo wakufidia malipo hayo kwa kutumia fedha za mapato ya ndani hasa kwa vile waliweza kukusanya mapato ya ndani kwa asilimia 91 kwa vile jambo hilo lilikuwa ni agizo maalum la Serikali.

Kamati inasisitiza juu ya umuhimu wa utekelezaji wa maagizo yanayotolewa na viongozi wetu hasa maagizo maalum la kuonesha utii na uwajibikaji kwa viongozi wetu Aidha uongozi wa Baraza la Mji Chake Chake unatakiwa kuwasilisha kwa barua ya madeni yote yanayotokana posho la nauli kwa walimu kwenda Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar kwa ajili ya kufanya uhakiki wa madeni hayo ambayo hayajalipwa katika miezi iliyotaja hapo juu ili yapatiwe ufumbuzi.

**8.4.10 Kutokufanywa kwa makisio ya posho la nauli.**

Baraza la Mji Chake Chake – Pemba linawajibu wa kufanya makisio (bajeti), kusimamia na kulipa posho la nauli kwa walimu na baadhi ya wafanyakazi nje ya kada ya ualimu kulingana na kigezo cha masafa wanaoishi mbali na eneo la kazi.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kutokufanywa kwa makisio ya gharama zinazostahiki kwa ajili ya malipo ya posho la nauli kwa walimu na baadhi ya wafanyakazi wa Baraza la Mji Chake Chake ambapo fedha za malipo ya posho hilo hulipwa kupitia fungu la Elimu.

Kutokufanywa kwa makisio ya gharama za posho la nauli katika kipindi cha mwaka husika ni kwenda kinyume na kifungu nambari 41(2) cha Sheria ya

Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016 ya Zanzibar.

**Majibu**
Baraza la Mji Chake lina sekta tofauti ikiwemo Sekta ya Elimu na kila sekta hio inatakikana iwe na bajeti yake tofauti, hivyo malipo ya nauli za walimu zinapangiwa bajeti kupitia sekta husika ya elimu na inatakiwa ilipwe kupitia fungu hilo hilo la elimu lakini kutokana na ongezeko kubwa la uajiri kwa mwaka huu wa fedha uliofanyika serikalini ilipelekea fungu hili kuzidiwa na kuonekana halitoshelezi.

**Uchunguzi wa Kamati**
Kamati katika kufuatilia hoja hii imejiridhisha kwa kuangalia mpango kazi pamoja na Bajeti ya Elimu ya Maandalizi na Msingi na imebaini kwamba Baraza la Mji Chake Chake ilikua inapanga bajeti maalum kwa ajili ya kulipa posho la nauli bajeti changamoto iliyo bainika ni kuwa kifungu hicho cha bajeti kilikua hakioneshwi katika taarifa za mwisho za hesabu za mwaka (financial statement).

**Mapendekezo ya Kamati**
Kamati inalishauri baraza la Mji Chake Chake kufuata taratibu zote za ufungaji wa hesabu za mwisho wa mwaka kwa kuingiza bajeti za vifungu vyote vya mapato na matumizi kama vile miongozo unavyotutaka ili kukidhi viwango sahihi vya ufungaji wa mahesabu ya taasisi kitaifa na kimataifa.

**8.4.11 Dosari katika utaratibu wa malipo ya posho la nauli.**
Baraza la Mji Chake Chake – Pemba lina wajibu wa kufanya malipo ya posho la nauli kwa walimu na baadhi ya wafanyakazi nje ya kada ya ualimu kwa kuzingatia mfumo madhubuti katika ulipaji wa posho hilo.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainia kuwepo kwa udhibiti usioridhisha wa ulipaji wa fedha za posho la nauli kwa walimu ambapo imebainika malipohayo hulipwa kwa njia ya fedha taslim kupitia kwa walimu wakuu wa skuli husika kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016 ya Zanzibar.

Aidha, imepelekea kuwepo kwa malalamiko kwa baadhi ya walimu ambao hawakulipwa malipo ya posho la nauli licha ya kwamba walimu hao wameonekana katika orodha ya malipo hayo.

**Jadweli hapo chini linaonyesha orodha ya skuli pamoja na walimu wakuu wanaokabidhiwa fedha taslim kwa ajili ya posho la nauli.**

| NAM | JINA LA MWALIMU | SKULI HUSIKA |
|---|---|---|
| 1 | ASHA MSEMA BWANGALA | VITONGOJI |
| 2 | SALMA A. MUHDINI | ZIWANI |
| 3 | MKUBWA J. SEIF | VIKUNGUNI |

| | | |
|---|---|---|
| 4 | CHUMU H. JUMA | FURAHA |
| 5 | SABAH SEIF SAID | PUJINI |
| 6 | OMAR YAHYA JUMA | WAWI |
| 7 | ASHA ALI KHAMIS | MBUZINI |
| 8 | HALIMA SAID ALI | UWANDANI |
| 9 | MOH'D JUMA KHAMIS | PONDEANI |
| 10 | **JUMA AMOUR JUMA** | **NG'AMBWA** |

**Majibu**
Kwa kipindi hichi kweli malipo yakifanyika kwa njia taslim kwa kupitia walimu wakuu wa skuli husika, tulifanya hivo kwa nia safi ya kuwarahisishia walimu wetu kupata nauli zao kwa wakati lakini pia kuwapunguzia masafa na usumbufu wa kuzifuata benki. Lakini dosari hii tumeshaifanyia kazi kwani kwa sasa posho la nauli za walimu tunazilipa kupitia benki akaunti ya muhusika moja kwa moja.

**Uchunguzi wa Kamati**
Kamati katika kufuatilia hoja hii kamati imeomba kukutana na walimu ambao hawakupokea malipo ya posho la nauli na wameonekana katika vocha za malipo kwa ajili ya kuwafanyia mahojiani ili kupata ufafanuzi wa kadhia hii.

Kamati ilifanikiwa kuitisha kikao cha tarehe 18/08/2022 katika ukumbi wa Baraza la Mji Chake Chake kwa kuwahoji walimu wanne ambao ni ndugu Mchumi Hassan Ali kutoka Skuli ya Msingi Uwandani, ndugu Bimkubwa Omar Salim, ndugu Zubeda Haroub Mussa na ndugu Fatma Abeid Shaame wote kutoka Skuli ya Msingi Furaha.

Aidha, Kamati ilifanikiwa kufanya mahojiano na walimu hao na wote wamekiri kutopokea fedha za malipo ya nauli kwa miezi tofaut licha ya kuonekana katika orodha ya malipo kuwa wameshachukua malipo hayo na wamethibitisha saini sio za kwao.

**Mapendekezo ya Kamati**
Kamati inalishauri Baraza la Mji kufuatilia kwa karibu vocha za malipo za Skuli ya msingi ya Furaha, Skuli ya msingi Mbuzini na Skuli ya msingi Uwandani ili kubaini wahusika wote waliojihusishwa na vitendo vya kughushi saini na kuchukua posho la nauli la walimu hao ili waweze kuchukuliwa hatua stahiki kwa mujibu wa Sheria kwa lengo la kukomesha vitendo hivyo ambavyo havileti tija katika nchi yetu.

**8.4.12 Kutokufanyiwa marekebisho orodha ya malipo kwa baadhi ya walimu**

**baada ya kuhamishwa.**

Baraza la Mji Chake Chake – Pemba linawajibu wa kusimamia uhamisho wa walimu pamoja na mafao yao kutoka skuli moja kwenda nyengine.

Katika ukaguzi ulifanyika imebainika kuwepo walimu waliohamishwa kutoka skuli moja kwenda skuli nyengine bila ya kufanyiwa marekebisho ya uhamisho wa malipo ya posho la nauli zaoambapo kufanya hivyo kunapelekea usumbufu kwa walimu kusomesha skuli moja na kupokelea posho lao la nauli nyengine.

Kutokufanyiwa marekebisho ya malipo ya posho la nauli za walimu baada ya uhamisho ni kwenda kinyume na taratibu za kiutumishi.

**Jadweli lifuatalo hapo chini linaonyesha walimu waliohamishwa bila ya kufanyiwa marekebisho ya malipo ya posho la nauli.**

| NAM | JINA LA MWALIMU | SKULI ALIYOTOKA | SKULI ALIYOPO KWA SASA |
|---|---|---|---|
| 1 | Makame Haji Vuai | Pujini | Baraza la Mji Chake Chake |
| 2 | Saumu Khamis Rashid | Furaha | Unguja |
| 3 | Salma Rashid Abdallah | Furaha | Unguja |
| 4 | Asha Nassor Sultan | Ziwani | Unguja |
| 5 | Azrad Muhsin Ali | Wawi Msingi | Alkhamis Camp |
| 6 | Choumu Moh’d Mkubwa | Uwandani Msingi | Vitongoji |
| 7 | Ali Khamis Mali | Pujini | Chambani |

**Majibu**

Matokezeo haya ni makosa ya kibinaadamu kwa kwa kutokufanyiwa uhamisho wa nauli kwa mwalimu aliyehamishiwa skuli moja kwenda nyengine na bado ikawa yupo wilaya hio hio. Lakini kwa mujibu wa taratibu za ulipaji wa posho la nauli kwa walimu ni kua mwalimu anapopewa tu uhamisho kutoka wilaya moja kwenda wilaya nyengine ni kua posho hilo la nauli limeishia hapo. Sasa atapewa posho hilo tu kule anakokwenda ikiwa skuli aliyopangiwa na anapoishi itafikia kigezo cha kupewa posho la nauli. Hivyo hakutokuwa na kulipwa posho la nauli sehemu ambayo mwalimu kashahamishwa.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kwa vile Baraza la Mji Chake Chake limekiri kutokea kwa dosari hii hata hivyo Kamati inaushauri uongozi wa Baraza la Mji Chake Chake katika utekelezaji wa Sheria mbalimbali za kiutumishi ikiwemo sheria ya ambazo inazitaka taasisi za Serikali kuhakikisha kuwa indapo mtumishi atahamishwa kutoka sehemu moja kwenda nyengine ni vyema maslahi yake yote yaweze kuhamishwa mara moja iwezekanavyo.

### 8.4.13 Malipo yaliyolipwa zaidi ya mara moja shilingi 253,000/=

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwepo kwa malipo ya shilingi 253,000/= ambayo yamelipwa mara mbili (double payment) kwa mwalimu Bi Fatma Khamis Othman katika Skuli ya Mbuzini na Ziwani kuanzia mwezi wa April 2019 hadi Agosti 2019.
Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na muongozo kutoka kwa Katibu Mkuu (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora pamoja na sheria ya usimamizi wa fedha za umma ya Zanzibar nambari 12 ya mwaka 2016.

**Jadweli lifuatalo hapo chini linaonyesha mchanganuo wa malipo hayo kwa kila skuli kwa mwezi.**

| Mwezi/Skuli | Aprili | Mei | Juni | Julai | Agosti | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Skuli ya Ziwani | 25,300 | 25,300 | 25,300 | 25,300 | 25,300 | 126,500 |
| Skuli ya Mbuzini | 25,300 | 25,300 | 25,300 | 25,300 | 25,300 | 126,500 |
| Jumla | 50,600 | 50,600 | 50,600 | 50,600 | 50,600 | 253,000 |

### Majibu

Malipo haya ya mwalimu kulipwa mara mbili inawezakana ni majina yamefanana au ni makoseo ya kibinadamu kua jina lake halijaondoshwa skuli aliyohama. Lakini hata hivyo jitihada zilichukuliwa kwa kufanyiwa uhakiki zaidi na kufanya marekebisho ya ulipaji wa posho la nauli mara tu baada ya mwalimu kupewa uhamisho kwenda skuli nyengine. Kwani kwa mwaka mwengine wa fedha halitojitokeza tena tatizo hili.

### Uchunguzi wa Kamati

Kamati katika kufuatilia hoja imeomba kukutana na mwalimu Bi Fatma Khamis Othman kwa lengo la kupata ufafanuzi wa kadhia hii.

Kamati ilifanikiwa kuitisha kikao cha tarehe 18/08/2022 katika ukumbi wa Baraza la Mji Chake Chake na ilifanikiwa kukuta na mwalimu Bi Fatma Khamis Othman na kuiambia Kamati kuwa ni kweli Alichukua uhamisho kutoka Skuli ya msingi Mbuzini na kwenda Skuli ya msingi Ziwani ambapo baada uhamisho huo posho lake la nauli alikuwa anachukulia Skuli ya Ziwani tu ambapo amehamishiwa na wala hakuwahi kuchukua fedha hizo hata mara moja katika

Skuli ya Mbuzini licha ya kuonekana katika orodha ya malipo ya vocha ya Skuli ya Mbuzini

Aidha, Kamati ilifanya mazungumzo na mwalimu mkuu wa Skuli ya Mbuzini na kuilezea Kamati kuwa kazi hiyo ilikuwa inafanywa na msaidizi mwalimu mkuu, hivyo basi Kamati ilipofanikiwa kuzungumza na Msaidizi Mwalimu mkuu alikiri kuwa Bi Fatma alikuwa hachukui fedha hizo Badala yake vocha hiyo hurudishwa Baraza la Mji bila ya kuwa na saini ya mwalimu Bi Fatma.

**Mapendekezo ya Kamati**

Kamati inaushauri uongozi wa Baraza la Mji Chake Chake juu ya utekelezaji wa Sheria mbalimbali za kiutumishi ikiwemo sheria ya ambazo inazitaka taasisi za Serikali kuhakikisha kuwa indapo mtumishi atahamishwa kutoka sehemu moja kwenda nyengine ni vyema maslahi yake yote yaweze kuhamishwa mara moja iwezekanavyo.

Hata hivyo, Kamati inalishauri Baraza la Mji Chake Chake kufuatilia kwa karibu vocha za malipo za Skuli ya msingi ya Ziwani na Skuli ya msingi Mbuzini ili kubaini wahusika wote waliojihusishwa na vitendo vya kughushi saini na kuchukua posho la nauli la Skuli ya Mbuzini ambako mwalimu huyo alikuwa amepata uhamiosho ili waweze kuchukuliwa hatua stahiki kwa mujibu wa Sheria kwa lengo la kukomesha vitendo hivyo ambavyo havileti tija katika nchi yetu.

BARAZA LA MJI WETE

**8.4.14 Posho la nauli ambalo halikulipwa kwa idadi ya miezi 8 Shilingi 25,367,600/=**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa Jumla ya Tsh 25,367,600 nifedha za posho la nauli za walimu kwa miezi ‘8’ ambayo ni Julai 2019, Septemba 2019, Disemba 2019, Januari 2020, Machi 2020 hadi Juni 2020 ambazo hazikulipwa.

Kutokulipwa kwa posho la nauli kwa walimu ni kwenda kinyume na barua ya tarehe 2/12/2011 kutoka kwa Katibu Mkuu ( OR ) Utumishi wa Umma na Utawala Bora inayofafanua kuhusu malipo ya posho hilo.

Aidha, inapelekea kutokufikia kwa malengo yaliyopangwa yanayohusiana na utolewaji wa posho hilo.

**Jadweli hapo chini linaonyesha idadi ya miezi pamoja naposho la nauli ambazo hazikulipwa.**

| NAM | MWEZI | POSHO LA NAULI KWA MWEZI (Tshs) |
|---|---|---|

| | | |
|---|---|---|
| 1 | Julai 2019 | 7,348,800 |
| 2 | Septemba 2019 | 4,756,400 |
| 3 | Disemba 2019 | 0 |
| 4 | Januari 2020 | 8,175,200 |
| 5 | Machi 2020 | 5,087,200 |
| 6 | April 2020 | 0 |
| 7 | Mei 2020 | 0 |
| 8 | Juni 2020 | 0 |
| **JUMLA** | | **25,367,600** |

**Majibu**

Posho la nauli kwa walimu wa msingi hulipwa kupitia bajeti na upatikanaji wa fedha za matumizi mengineyo katika sekta ya elimu, hivyo basi kiasi cha fedha kilichotajwa hapo juu hakikulipwa kutokana na kukosekana kwa fedha za ruzuku katika miezi yote tajwa hapo juu.

**Uchunguzi wa Kamati**

Kamati katika uchunguzi wake imebaini kuwa Baraza la Mji Wete imetenga bajeti kwa upande wa Shughuli za Elimu ya Maandalizi na Msingi ya Tzs 227,054,000 na kuweza kutumia jumla ya Tzs 159,439,000 sawa na asilimia 70 ya makadirio.

Aidha, Kamati imejirizisha katika bajeti ya kuwalipa walimu posho la nauli imewekwa katika kifungu cha Kusimamia na kuhuduma Skuli za maandalizi na msingi ambayo imetengewa jumla ya TZS 64,000,000 na kuweza kutumia jumla ya Tzs 61,991,400 sawa na asilimia 97.

Aidha, kwa vile taasisi hizo zinakusanya mapato yao wenyewe na kwa mwaka wa fedha 2019/2020 Baraza la Mji Wete limekadiria kukusanya jumla Tzs 325,000,000 katika vyanzo vyake mbali mbali na kuweza kukusanya jumla ya Tzs 359,468,990 sawa na asilimia 111% ya makadirio

Kutokana na hali hiyo Kamati imebaini ni kweli mapato ya matumizi mengineyo hayakuingizwa kikamilifu kama bajeti ilivyopangwa kwa mwaka huo wa fedha 2019/2020. hata hivyo hakukuwa na sababu ya kutolipa posho la nauli kwa walimu hao kwani wangeliweza kupunguza matumizi katika baadhi ya shughuli za elimu ya maadalizi na msingi, badala yake kuliongeza fungu la bajeti ya posho la nauli ili kuweza kuwalipa walimu posho la nauli kwa kipindi kilichokosekana fedha hizo kutokana na jambo hilo kuwa ni agizo maalum hivyo ilikua ni busara kulipa kipaombele.

Vile vile, Baraza lingeweza kupunguza shughuli zake mbalimbali na kuweza kulipa fedha hizo kwa wakati kwa vile wameweza kupindukia malengo ya makusanyo ya ndani kwa kuweza kukusanya mapato ya ndani kwa asilimia 111.

**Mapendekezo ya Kamati**
Kamati inasititiza kuyapa vipao mbele maagizo yote yanayotolewa na viongozi wetu wa ngazi za juu kwa lengo la kuleta ufanisi na uwajibikaji wa majukumu yetu ya kila siku. Aidha, kamati inaiomba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar kwa vile walimu hawa kwa sasa wamerudishwa katika mamlaka zao baada ya kuondoshwa kwa Ugatuzi ni vyema basi kufanyika kwa uhakiki wa madeni hayo na kuweza kupatiwa walimu stahiki zao kwa kila mwezi ambao hawakupatiwa wakati walipokuwa katika mamlaka za Serikali za Mitaa kipindi cha Ugatuzi.

**8.4.15 Walimu ambao hawakuingizwa katika orodha ya malipo ya posho la nauli**
Kwa mujibu wa barua ya tarehe 02/12/2011 kutoka kwa Katibu Mkuu wa (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora linalohusu muongozo wa ulipaji wa posho la nauli kwa walimu na baadhi ya wafanyakazi nje ya kada ya Ualimu linafafanua kigezo cha masafa (kuanzia kilomita tano) ambacho kinastahiki kutumika ili kuweza kulipa posho la nauli.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba kuna idadi ya Walimu watano “5” ambao wamekidhi kigenzo hicho lakini hawakuweza kuingizwa katika orodha ya malipo ya walimu wanaostahiki kulipwa posho hilo.

Kutokuwaingiza katika orodha ya malipo ya posho la nauli walimu waliokidhi kigenzo cha masafa ni kwenda kinyume na barua ya tarehe 02/12/2011 kutoka kwa katibu Mkuu (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora Zanzibar.

**Majibu**
Malipo ya posho la nauli yanalipwa kwa mujibu wa bajeti kwa mwaka wa fedha husika pamoja na kuzingatia vigezo vya masafa, ikiwa malipo ya nauli yamefikia ukomo wa bajeti hakuna uwezekano wa kulipa malipo Zaidi ya idadi na kiasi kilichopangwa. Hata hivyo ofisi ya Baraza la Mji Wete ilifanya mapitio ya kina kwa walimu ambao wanafundisha masafa ya mbali na makaazi yao na kuweza kuwahamishia katika skuli jirani ili kuweza kupunguza na kuondoa madai ya nauli na usumbufu kwa walimu.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**
Kwa vile Baraza la Mji Wete limekiri kufanyika kwa dosari hii kutoka na ukomo wa bajeti kwa matumizi hayo.

Kamati inakubaliana na majibu hayo hata hivyo Kamati imeona hakukuwa na sababu za kutolipa posho hilo kwa Vile Baraza la Mji linaogozwa kwa sheria

namba 7 ya mwaka 2014 na kanuni zake ambazo inazipa Mamlaka hizi uwezo wa kuhaulisha vifungu vya matumizi na kufanya ongezeko la Bajeti kupitia Baraza lake la Madiwani kwa ajili ya kutii agizo hilo kutoka Serikalini.

Kamati inalishauri Baraza la Mji Wete kuyapa vipao mbele maagizo yote yanayotolewa na viongozi wetu wa ngazi za juu kwa lengo la kuleta ufanisi na uwajibikaji wa majukumu yetu ya kila siku.

Aidha, Kamati inaliomba Baraza la Mji Mkoani kuwasilisha madeni yote ya posho la nauli za walimu kwenda Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar kwa ajili ya kufanyiwa uhakiki madeni hayo na kuweza kupatiwa walimu stahiki zao kwa kila mwenzi ambao hawakupatiwa wakati walipokuwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kipindi cha Ugatuzi.

**8.4.16 Malipo ya Posho la nauli kwa walimu ambao si waajiriwa Tsh.594,000**

Kwa mujibu wa barua ya tarehe 02/12/2011 kutoka kwa Katibu Mkuu wa (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora linalohusu muongozo wa ulipaji wa posho la nauli kwa walimu na baadhi ya wafanyakazi nje ya kada ya Ualimu ambao ni waajiriwa wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwepo kwa jumla ya walimu saba “7” ambao hawajaajiriwa wanasomesha katika skuli mbalimbali na kulipwa posho la nauli la shilingi 594,000 kwa kila mwezi.

Kufanya malipo ya fedha za posho la nauli kwa walimu wasioajiriwa ni kwenda kinyume na Sheria ya usimamizi wa fedha za Umma ya Zanzibar ya mwaka 2016.

**Jadweli lifuatalo hapo chini linaonyesha mchanganuo wa walimu wanaolipwa posho la nauli ambao hawajaajiriwa.**

| Nam | Jina la mwalimu | Anapoishi | Skuli anayofundisha | Fedha anayolipwa kwa mwenzi |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Abeid Hendia Hinga | Wete | Fundo | 110,000 |
| 2. | Suleiman Ali Suleiman | Wete | Fundo | 110,000 |
| 3. | Subira Khamis Abeid | Fundo | Fundo Msingi | 110,000 |
| 4. | Nadhira Zahor | Fundo | Uvinje | 66,000 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Mustari | | | |
| 5. | Wanu Ussi Makame | Fundo | Uvinje | 66,000 |
| 6. | Mamboto Haji Khamis | Fundo | Uvinje | 66,000 |
| 7. | Amina Ame Juma | Fundo | Uvinje | 66,000 |
| **JUMLA** | | | | **594,000** |

**Majibu**
Ni kweli jumla ya Fedha zilizotajwa hapo juu zilikuwa zikilipwa kwa walimu ambao si waajiriwa ambao walikuwa wakifundisha katika skuli za visiwa vya Fundo, Uvinje na Kojani hii ilitokana na uhitaji mkubwa wa walimu ka1ika visiwa hivyo ambavyo vilikosa walimu wa kutosha hivyo basi ofisi ya Baraza la mji Wete iliweza kuwalipa posho la nauli kupitia bajeti yake ya matumizi mengineyo (Ruzuku) nje ya bajeti ya sekta ya elimu ili kuweza kukidhi mahitaji ya wanafunzi katika visiwa hivyo.

**Uchunguzi wa Kamati**
Kamati katika uchunguzi zaidi wa hoja hii ilijiridhisha vyema juu ya uwepo wachangamoto kubwa ya ukosefu wa walimu katika Skuli ya Fundo, Uvinje na Kojani hivyo ni jambo la busara kuwaajiri walimu hao katika kusaidia kufundisha masomo mbalimbali katika Skuli hizo.
Hata hivyo utaratibu uliotumika kuwalipa nauli walimu hao ulikua na mapungufu kwa vile ilitakikana Baraza la Madiwani likae na kuridhia viwango maalum vya ulipaji wa posho hilo kwa kutumia fedha za makusanyo ya ndani ya Baraza la Mji Wete na sio fedha za matumizi mengineyo (OC) ambazo zimewekewa bajeti maalum kwa ajili ya kuwalipa walimu posho la nauli ambao wameajiriwa na wanatambulikana na Serikali.

**Mapendekezo ya Kamati**

Kamati inashauri uongozi wa Baraza la Mji Wete kuhakikisha matumizi ya fedha za matumizi mengineyo O/C yanatumika kama yalivyopangwa katika bajeti husika Aidha kwa jambo lolote lile la dharura ambalo halimo katika Bajeti na linahitaji kutekelezwa kwa umuhimu wake ni vyema basi Halmashauri kuitisha baraza la madiwani la dharura kwa ajili ya kupata rizaa ya matumizi ya jambo hilo aidha kwa vile mamlaka hizi zinahaki ya kisheria kukusanya mapato na kufanya matumizi basi waweze kutumia fedha zinazotokana na mapato ya ndani na si vyenginevyo.

**8.4.17 Posho la nauli ambalo halilipwi kwa kila mwczi kwa wastani wa Tsh. 215,600/=**

Baraza la Mji Wete –Pemba linawajibu wa kusimamia na kuendesha shughuli za Baraza ikiwa ni pamoja na kuwalipa walimu posho la nauli stahiki kulingana na kigezo cha masafa kama ilivyofafanuliwa katika barua ya tarehe 02/12/2011 kutoka kwa katibu Mkuu (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Ukaguzi umebaini kwamba Baraza la Mji Wete –Pemba halipangi viwango stahiki vya nauli kwa walimu kulingana na vigezo vya masafa ambapo kiwango cha posho la nauli kinacholipwa kwa baadhi ya walimu ni kidogo ukilinganisha na uhalisia wa masafa wanayotoka walimu hao. Aidha kulingana na taarifa za malipo za posho la nauli zinaonyesha kuwepo kwa tofauti baina ya malipo stahiki na malipo halisi yanayolipwa kwa wastani wa jumla ya shilingi 215,600 kwa mwezi.

Kutokulipwa walimu posho la nauli stahiki ni kwenda kinyume na toleola tarehe 02/12/2011 kutoka kwa katibu Mkuu (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Aidha, idadi na taarifa za walimu ambao hawalipwi posho la nauli stahiki zinaonekana katika Ripoti husika ya Mdhibiti.

**Majibu ya Baraza la Mji Wete**

Tofauti iliyojitokeza katika ulipaji wa posho hizo ulitokana na mabadiliko ya kuhama makaazi na kituo cha kufanyia kazi kwa walimu husika ambapo marekebisho ya kulipa nauli katika hali kama hiyo yanachukua muda (hayafanyiki kwa mwezi husika) kuweza kufanyika lakini ofisi ya Baraza la Mji Wete ilijitahidi kuweza kufanya marekebisho ya nauli kwa kila inapopokca taarifa za mabadiliko hayo.

Pia, taarifa za awali zilizopokelewa kutoka kwa walimu husika ambazo zilitumika kundaa bajeti ya mwaka ndio hizo hizo ambazo hutumika kufanya malipo ya nauli kwa walimu husika.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kwa vile Baraza la Mji Wete limekiri kuwepo kwa mapungufu ya ulipaji wa nauli kulingana na masafa wanaoishi walimu hao hata hivyo kamati inaendelea kulishauri Baraza la Mji Wete katika kufuata Sheria na kutekeleza maagizo mbalimbali yanayotolewa na Serikali kama yalivyo.

Aidha, Kamati inaendelea kulishauri Baraza la Mji kufanya uhakiki wa deni hilo ambalo halikupwa kwa kila mwenzi na kuwasilisha deni hilo Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa ajili ya kupatiwa stahiki wanazodai walimu hao.

### 8.4.18 Kutokufanywa kwa makisio ya posho la nauli.

Baraza la Mji Wete – Pemba linawajibu wa kufanya makisio (Bajeti), kusimamia

na kulipa posho la nauli kwa walimu na baadhi ya wafanyakazi nje ya kada ya ualimu.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kutokufanya kwa makisio ya gharama inayostahiki kwa ajili ya malipo ya posho la nauli kwa walimu na baadhi ya wafanyakazi wa Baraza la Mji Wete ambapo fedha za malipo ya posho hilo hulipwa kupitia fungu la elimu.

Kutokufanywa kwa makisio ya gharama za posho la nauli katika kipindi cha mwaka husika ni kwenda kinyume na kifungu nambari 41(2) cha sheria ya usimamizi ya fedha za umma nambari 12 ya mwaka 2016 ya Zanzibar.

**Majibu**

Makisio ya posho la nauli kwa walimu na wafanyakazi wengine wa sekta ya elimu hufanyika kila mwaka kwa kuzingatia mahitaji ila kutokana na ongezeko kubwa la uajiri uliofanywa na Serikali Kuu katika mwaka wa fedha 2019/2020 ilipelekea bajeti ya sekta ya elimu kuzidiwa na kupelekea uhaba wa fedha katika malipo ya posho la nauli.

**Uchunguzi wa Kamati**

Kamati katika kufuatilia hoja hii imejiridhisha kwa kuangalia mpango kazi pamoja na Bajeti ya Elimu ya Maandalizi na Msingi na imebaini kwamba Baraza la Mji Wete ilikua inapanga bajeti maalum kwa ajili ya kulipa posho la nauli bajeti changamoto iliyo bainika ni kuwa kifungu hicho cha bajeti kilikua hakioneshwi katika taarifa za mwisho za hesabu za mwaka (financial statement).

**Mapendekezo ya Kamati**

Kamati inalishauri baraza la Mji Chake Chake kufuata taratibu zote za ufungaji wa hesabu za mwisho wa mwaka kwa kuingiza bajeti za vifungu vyote vya mapato na matumizi kama vile miongozo unavyotutaka ili kukidhi viwango sahihi vya ufungaji wa mahesabu ya taasisi kitaifa na kimataifa.

### 8.4.19 Dosari katika utaratibu wa malipo ya poshola nauli.

Baraza la Mji Mkoani-Pemba linawajibu wa kufanya malipo ya posho la nauli kwa walimu na baadhi ya wafanyakazi nje ya kada ya ualimu kwa kuzingatia mfumo madhubuti katika ulipaji wa posho hilo.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwepo kwa udhibiti usioridhisha wa ulipaji wa fedha za posho la nauli kwa walimu ambapo imebainika malipo hayo hulipwa kwa njia ya fedha taslimu kupitia walimu wakuu wa skuli husika kinyume na sheria ya usimamizi wa fedha za umma no.12 ya mwaka 2016 ya Zanzibar.

Aidha, imepelekea kuwepo kwa malalamiko kwa baadhi ya Walimu ambao

hawakulipwa malipo ya posho la nauli licha ya kwamba walimu hao wameonekana katika malipo hayo.

**Jadweli lifuatalo hapo chini linaonesha orodha ya skuli pamoja na walimu wakuu wanaokabidhiwa fedha taslimu kwa ajili ya posho la nauli**

| NAMBA | JINA LA MWALIMU | SKULI HUSIKA |
|---|---|---|
| 1 | Asaa Hamad Salim | Kokota |
| 2 | Azan Mussa Hamad | Uvinje |
| 3 | Hamad Sharif Azan | Finya |
| 4 | Hassan Bakar Haji | Chwale |
| 5 | Ali Rashid Ali | Minugwini |
| 6 | Beda Khamis Juma | Shengejuu |
| 7 | Amour Hamad Moh'd | Daya |
| 8 | Mshangi Haji Hassan | Mz/ Takao |
| 9 | Said Omar Hassan | Maziwani |
| 10 | Ali Khamis Omar | Fundo |
| 11 | Rukia Moh'd Othman | Kinyasini. |

**Majibu**

Ni kweli malipo ya posho za nauli kwa walimu yalikuwa yanafanyika kwa njia ya fedha taslimu badala ya kulipwa katika benki, hii ilitokana na kiasi cha nauli ambacho kilikuwa kinalipwa hakikutosha kulipwa kupitia hesabu zao na pia ilikuwa inasababisha usubufu wa kuzifata pesa hizo za nauli benki.

Vile vile, malipo ya posho hizo za nauli zikilipwa kupitia kwa walimu wakuu wa shule husika kutokana na kupunguza gharama za malipo na kuendana na wakati wa malipo hayo kwa sababu skuli ni nyingi na wahusika wanaosytahiki kufanya malipo ya nauli kwa mujibu wa sheria ya fedha ni mmoja tu ambayo ni mshika fedha (Cashier) hivyo basi, njia rahisi ambayo ikitumika ni kuwakabidhi walimu wakuu na baadac kuleta marejesho ya malipo ya nauli baaada ya kufanya malipo.

**Uchunguzi wa Kamati**

Kamati katika kufuatili hoja hii ilifanikiwa kuitisha kikao cha tarehe 18/08/2022 katika ukumbi wa Baraza la Mji Chake Chake kwa kuwahoji walimu wanne ambao ni ndugu Amina Shehe Dadi, ndugu Bimkubwa masoud Aley na ndugu Ahmed Juma Massoud hawa wote walikuta majina yao yameshasainiwa kwa kiwango cha elfu 30 na wakalazimishwa kuchukuwa elfu kumi tano na ndugu Arafa Ali Rashid hakupokea fedha hizo nauli hata siku moja licha ya kuonekana katika orodha ya malipo kuwa ameshapatiwa malipo hayo.

**Mapendekezo ya Kamati**

Kamati inalishauri Baraza la Mji kufuatilia kwa karibu vocha za malipo za Skuli ya msingi ya Furaha, Skuli ya msingi Mbuzini na Skuli ya msingi Uwandani ili kubaini wahusika wote waliojihusishwa na vitendo vya kughushi saini na kuchukua posho la nauli la walimu wenzao ili waweze kuchukuliwa hatua stahiki kwa mujibu wa Sheria kwa lengo la kukomesha vitendo hivyo ambavyo havileti tija katika nchi yetu.

**8.4.20 Kukosekana kwa uthibitishowa halali wa malipo ya fedha za posho la nauli za walimu kwa mwezi wa (June 2019) shilingi 5,144,400/=**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwepo kwa jumla ya shilingi 5,144,000 ambazo zimetumika kwa malipo ya posho la nauli kwa walimu ambapo uthibitisho wa fomu ya mapokezi ya fedha hizo kwa walimu mkuu imekosekana kwa ukaguzi. Aidha, orodha za malipo ya posho hilo kwa mwenzi Juni, 2019 zimekataliwa na walimu husika.

Kutokuwepo kwa uthibitisho wa malipo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha sheria ya usimamizi wa fedha za umma ya Zanzibar nambari 12 ya mwaka 2016.

**Jadweli lifuatalo hapo chini linaonyesha taarifa za uthibitisho wa malipo zilizokosekana kwa ukaguzi**

| NAM | UTHIBITISHO | MAELEZO |
|---|---|---|
| 1. | Fomu za malipo kwa walimu wakuu | Zimekosekana |
| 2. | Orodha za malipo ya posho la nauli kwa mwenzi wa Juni, 2019 | Walimu wamezikata |

**Majibu**

Ofisi ya Baraza la Mji Wete ilifanya malipo ya Tsh. 4,923,000/= kwa posho la nauli kwa walimu wa msingi kwa mwezi June - 2019 katika vocha no. 48/6 ya tarehe 25/06/2019 yenye thamani ya Tsh. 4,923,000/= na vielelezo vya malipo hayo vimeambatanishwa katika vocha hiyo.

Kwa hivyo malipo yaliyotajwa na ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi mkuu wa hesabu za serikali kwa mwezi June 2019 yenye thamani ya Tsh. 5,144,400/= sio kwa ofisi ya Baraza la Mji Wete.

**Uchunguzi wa Kamati**

Katika kufuatilia hoja hii Kamati imemtaka mwakilishi kutoka Ofisi ya Mkaguzi ambae amefuatana na Kamati ili kutoa uthibitisho wa malipo ya Tsh. 5,144,400 kiwango ambacho kimekataliwa na Baraza la Mji wete na kubainisha kuwa kiwango sahihi walicholipa jumla ya Tzs 4,923,000 kwa mwezi wa June -2019 katika vocha no. 48/6 ya tarehe 25/06/2019.

Kamati imebaini kuwa Baraza la Mji Wete limekiri kufanya matumizi ya Tsh, 5,144,400 kwa mwezi wa June-2019 Katika barua walioiwasilisha ya majibu ya hoja kwa mkaguzi "Financial Management" hivyo ni wazi kuwa Mkaguzi amewalisha kiwango hicho cha fedha ambacho baraza la mji walikiri kukulipa ila wakati wa ukaguzi wa Kamati wa kupata majibu ya hoja hiyo wamekanusha kulipa kiwango hicho.

Sambamba na hayo Kamati imeomba kupatiwa daftari la fedha taslim "Cash book" kwa lengo la kukagua kiwango sahihi cha malipo yaliyolipwa katika vocha hiyo, Kamati imebaini kuwa daftar hilo lilikua na alama nyingi kutoka kwa Mkaguzi ambazo ziliashiria kuwa daftari hilo lilikuwa na mapungufu kadhaa ya utunzaji sahihi wa taarifa za kifedha ambapo Baraza la Mji wete limekiri kuwepo kwa dosari hiyo.

**Mapendekezo ya Kamati**

Kamati inaziomba taasisi za Serikali zikiwemo Mabaraza ya Miji kuhakikisha wanatoa taarifa za usahihi wakati wanapowasilisha majibu ya hoja kwa mkaguzi mkuu kwa vile kumekuwa na baadhi ya taasisi hupingana na taarifa za hoja ambazo zimewasilishwa katika kitabu cha mdhibiti na Mkaguzi mkuu wa Hesabu

za Serikali lakini Kamati inapofanya uhakiki wa barua walizojibu kumpelekea Mkaguzi inabaini taarifa za mkaguzi zipo sawa sawa na majibu yaliyomo katika barua za majibu ya hoja yani 'Financial Management" walizoziwasilisha kwa Mkaguzi.
Aidha, Kamati inasisitiza kuwepo kwa umakini mkubwa wa utunzaji wa taarifa za kifedha katika daftari la fedha taslim "Cash book" ili taarifa hizo ziwe sahihi na zilete uhalisia wa mapato na matumizi yanayofanywa na Baraza la Mji Wete.

HALMASHAURI YA WILAYA YA MICHEWENI

### 8.4.21 Posho la nauli ambalo halikulipwa shilingi 18,071,199.00

Kwa mujibu wa barua ya tarehe 02/12/2011 kutoka kwa Katibu Mkuu wa (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora linalohusu muongozo wa ulipaji wa posho la nauli kwa walimu na baadhi ya wafanyakazi nje ya kada ya Ualimu linafafanua kigezo cha masafa (kuanzia kilomita tano) ambacho kinastahiki kutumika ili kuweza kulipa posho la nauli.

Katika ukaguzi uliobainika kuwa jumla ya shilingi 18,071,199 ni fedha za posho la nauli za Walimu kwa miezi saba "7" ambayo ni Julai 2019, Disemba 2019, Januari 2020, Machi 2020 hadiJuni 2020 ambazo hazikulipwa.

Kutokulipwa kwa posho la nauli kwa walimu ni kwenda kinyume na barua ya tarehe 2/12/2011 kutoka kwa Katibu Mkuu (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora inayofafanua kuhusu malipo ya posho hilo.

Aidha, inapelekea kutokufikia kwa malengo yaliyopangwa yanayohusiana na utolewaji wa posho hilo.
**Jadweli hapo chini linaonyesha idadi ya miezi pamoja naposho la nauli ambazo hazikulipwa.**

| NAM | MWEZI | POSHO LA NAULI KWA MWEZI (Tshs) |
|---|---|---|
| 1 | Jul - 2019 | 4,292,800 |
| 2 | Dec - 2019 | - |
| 3 | Jan - 2020 | 4,292,800 |
| 4 | Mar - 2020 | 2,536,654 |
| 5 | Apr - 2020 | - |
| 6 | May - 2020 | - |
| 7 | Jun - 2020 | 6,948,945 |
| **JUMLA** | | **18,071,199** |

**Majibu**
Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni inakiri kwamba ni kweli Jumla ya Shilingi 18,071,199.00 za posho la nauli hazikulipwa kama inavoonekana katika hoja hapo juu, hii ni kutokana na uchachewa upatikanaji wa fedha za matumizi mengineo.

Hata hivyo, kwa sasa madeni ya fedha hizo yameshawasilishwa Serekali kuu ili kuweza kuwapatia walimu hao stahiki zao.

**Uchunguzi wa Kamati**

Kamati katika uchunguzi wake imebaini kuwa halmashauri ya Wilaya ya Micheweni imetenga bajeti kwa upande wa Shughuli za Elimu ya Maandalizi na Msingi ya Tzs 143,105,000 na kuweza kutumia jumla ya Tzs 103,567,962 sawa na asilimia 72 ya makadirio.

Aidha, Kamati imejirizisha katika bajeti ya kuwalipa walimu posho la nauli imewekwa katika kifungu cha Kusimamia na kuhuduma Skuli za maandalizi na msingi ambayo imetengewa jumla ya TZS 30,000,000 na kuweza kutumia jumla ya Tzs 21,880,000 sawa na asilimia 73.

Aidha, kwa vile taasisi hizo zinakusanya mapato yao wenyewe na kwa mwaka wa fedha 2019/2020 Baraza la Mji Wete limeweza kuvuka malengo ya Ukusanyaji wa mapato kwa kukadiria jumla ya Tzs 240,000,000 na Kuweza kukusanya Tzs 264,333,477.34 sawa na asilimia 110.0.

Kutokana na hali hiyo Kamati imebaini ni kweli mapato ya matumizi mengineyo hayakuingizwa kikamilifu kama bajeti ilivyopangwa kwa mwaka huo wa fedha 2019/2020. hata hivyo hakukuwa na sababu ya kutolipa posho la nauli kwa walimu hao kwani wangeliweza kupunguza matumizi katika baadhi ya shughuli za elimu ya maadalizi na msingi, badala yake kuliongeza fungu la bajeti ya posho la nauli ili kuweza kuwalipa walimu posho la nauli kwa kipindi kilichokosekana fedha hizo kutokana na jambo hilo kuwa ni agizo maalum hivyo ilikua ni busara kulipa kipaombele

Vile vile, wangeliweza kupunguza shughuli za halmashauri na kuweza kulipa fedha hizo kwa wakati kwa vile wameweza kufikia malengo ya makusanyo kwa asilimia 111%.

**Mapendekezo ya Kamati**

Kamati inapenda kusisitiza kuwa maagizo yanayotolewa na Serikali sijambo la kuupuuzwa ni vyema taasisi zinapopewa maagizo hayo kuyatekeleza kwa ufanisi mkubwa.

Aidha, kamati inasisitiza kwa vile walimu hao tayari wamesharudishwa wizarani kutokana na kuondolewa kwa Ugatuzi na kwa vile Halmashauri ya wilaya ya micheweni imeshawasilisha madeni hayo Serikali kuu basi ni vyema Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar wafanye uhakiki wa madeni hayo ili wahusika waweze kupatiwa stahiki zao ambazo wamezikosa kwa kipindi hicho.

### 8.4.22 Walimu ambao hawakuingizwa katika orodha ya malipo ya posho la nauli

Kwa mujibu wa barua ya tarehe 02/12/2011 kutoka kwa Katibu Mkuu wa (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora linalohusu muongozo wa ulipaji wa posho la nauli kwa walimu na baadhi ya wafanyakazi nje ya kada ya Ualimu linafafanua kigezo cha masafa (kuanzia kilomita tano) ambacho kinastahiki kutumika ili kuweza kulipa posho la nauli.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba kuna idadi ya Walimu kumi na moja "11" ambao wamekidhi kigezo hicho lakini hawa kuweza kuingizwa katika orodha ya malipo ya walimu wanaostahiki kulipwa posho hilo.

**Jadweli lifuatalo hapo chini linaonyesha walimu ambao hawakuingizwa katika orodha ya kulipwa posho la nauli.**

| Jina la Mwalimu | Anapoishi | Anaposomesha | Masafa (km) | Mwezi wa Ajira |
|---|---|---|---|---|
| Ridhwan Naomba Kombo | Kiuyu Mbuyuni | Karume | 8 | Feb. 2020 |
| Raya Ali Abdalla | Shumba viamboni | Micheweni Msingi A | 8 | Feb.2020 |
| Shariff Khamis Ali | Wingwi | Micheweni Msingi A | 6 | - |
| Jaffar Juma Sharifu | Maziwang'ombe | Micheweni Msingi A | 5 | Machi,2020 |
| Shemsa Ali Rashid | Shumba | Micheweni Msingi A | 8 | Juni, 2020 |
| Amina Faki Ali | Kiuyu | Micheweni Msingi A | 6 | Machi, 2020 |
| Bijuma Khator Chande | Kiuyu Mbuyuni | Micheweni Msingi A | 6 | Feb, 2020 |
| Suleiman Rashid Khatib | Kiuyu Mbuyuni | Maziwang'ombe | 4 | Machi, 2020 |
| Hamad Hija Khatib | Kiuyu Mbuyuni | Maziwang'ombe | 4 | Machi, 2020 |
| Bijine Suleiman Daudi | Kiuyu Mbuyuni | Maziwang'ombe | 4 | Machi, 2020 |
| Sharifa Rashid Khamis | Mchanga Mdogo | Mtemani Msingi | 8 | Oktoba, 2019 |

**Majibu**

Halmashauriya Wilaya ya Micheweni inakiri kwamba ni kweli Jumla ya walimu kumi na moja (11) hawakuingizwa katika orodha ya malipo ya posho la nauli, hii ni kutona na wakati wa malipo hayo yanafanyika watumishi ukweli wa jambo hilo

hivyo ni wazi kuwa walimu hao wapya walistahiki kulipwa posho la nauli kwa kigezo cha masafa licha ya kuwa bado hawa kuthibitishwa kazini.

**Uchunguzi wa Kamati**

Kamati katika kufuatilia hoja hii imeelezwa kuwa baadhi ya walimu hao walikuwa wapya na bado walikuwa hawajathibitishwa kazini, Kamati ilipoomba muongozo wa ulipaji wa posho hilo kutoka Wizara ya Elimu iligundua kuwa hakuna kifungu kilichoonesha kuwa mwalimu ambae hajathibitishwa kazini hastahiki kulipwa posho licha ya kuwa amekidhi kigezo cha masafa.

Aidha, Kamati imebaini kuwa Halmashauri ya wilaya ya Micheweni ingeliweza kuwalipa walimu hao kwa vile imetenga bajeti kwa upande wa Shughuli za Elimu ya Maandalizi na Msingi ya Tzs 143,105,000 na kuweza kupata jumla ya Tzs 103,567,962 sawa na asilimia 72 ya makadirio kwa kulipa kipao mbele agizo la Serikali kwa kupunguza fedha katika shughuli nyengine za elimu na kuongeza fedha katika kifungu cha malipo ya posho la nauli

**Mapendekezo ya Kamati**

Kamati inaziomba taasisi za Serikali ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni kutii maagizo yanayotolewa na Serikali na kuyaweka kipao mbele katika utekelezaji wake.

Aidha kamati inaiomba halmashauri ya Wilaya Micheweni kufanya uhakiki wa madeni yote ya walimu ambao walikuwa wanakidhi kupatiwa posho la nauli kwa mwaka wa fedha 2019/2020 na hawakuweza kupatiwa posho hilo kwa sababu tofauti, kuwasilisha madeni hayo Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa ajili ya kufanyiwa utaratibu wa malipo ili walimu hao waweze kupatiwa stahiki haki zao.

### 8.4.23 Malipo ya posho la nauli kwa walimu ambao hawaja ajiriwa ya shilingi 88,000.00

Kwa mujibu wa barua ya tarehe 02/12/2011 kutoka kwa Katibu Mkuu wa (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora linalohusu muongozo wa ulipaji wa posho la nauli kwa walimu na baadhi ya wafanyakazi nje ya kada ya Ualimu ambao ni waajiriwa wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwepo kwa jumla ya walimu wawili (2) ambao hawaja ajiriwa wanasomesha katika skuli mbalimbali na kulipwa posho la nauli shilingi 88,000 kwa kila mwezi.

Kwa mujibu wa barua ya tarehe 02/12/2011 kutoka kwa Katibu Mkuu wa (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora linalohusu muongozo wa ulipaji wa

posho la nauli kwa walimu na baadhi ya wafanyakazi nje ya kada ya Ualimu ambao ni waajiriwa wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Kufanya malipo ya fedha za posho la nauli kwa walimu wasioajiriwa ni kwenda kinyume na Sheria ya usimamizi wa fedha za Umma ya Zanzibar ya mwaka 2016.

**Jadweli lifuatalo hapo chini linaonyesha mchanganuo wa walimu wanaolipwa posho la nauli ambao hawajaajiriwa.**

| Namba | Jina la mwalimu | Anapoishi | Skuli anayofundisha | Fedha anayolipwa kwa mwenzi |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Halima Saleh Nassor | Konde | Kipanga Msingi | 44,000 |
| 2. | Halima Abdalla Hamad | Konde | Kipanga Msingi | 44,000 |
| **Jumla** | | | | **88,000** |

Majibu
Halmashauriya Wilaya ya Micheweni inakiri kwamba ni kweli Jumla ya Shilingi 88,000 zimelipwa kwa walimu wawili ambao hawajaajiriwa wa Skuli ya Kiuyu Kipanga ni hii ni kutoka na na upungufu mkubwa wa walimu katika Skuli ya Kiuyu Kipangani, uongozi ulifanya jitihada ya kutafuta vijana wakusaidiana kupatikana nje ya eneo la Kiuyu Kipangani (Konde) na kuwasaidia angalau nauli kwa ajili ya kuwawezesha kufika katika sehemu husika, vyenginevyo watoto wa Skuli hio wangekosa haki yao ya msingi.

Uchunguzi wa kamati
Kamati katika uchunguzi Zaidi wa hoja hii ilijiridhisha vyema juu ya uwepo wachangamoto kubwa ya ukosefu wa walimu katika skuli ya Kiuyu Kipangani hivyo ni jambo la busara kuwaajiri walimu hao katika kusaidia kufundisha masomo mbalimbali katika Skuli hizo
Hata hivyo utaratibu uliotumika kuwalipa nauli walimu hao ulikua na mapungufu kwa vile ilitakikana Baraza la Madiwani likae na kuridhia viwango maalum vya ulipaji wa posho hilo kwa kutumia fedha za makusanyo ya ndani ya Halmashauri na sio fedha za matumizi mengineyo (OC) ambazo zimewekewa bajeti maalum kwa ajili ya kuwalipa walimu posho la nauli ambao wameajiriwa na wanatambulikana na Serikali.

Mapendekezo ya Kamati

Kamati inashauri uongozi wa Halmashauri ya Micheweni kuhakikisha matumizi ya fedha za matumizi mengineyo O/C yanatumika kama yalivyopangwa katika bajeti husika Aidha kwa jambo lolote lile la dharura ambalo halimo katika Bajeti na linahitaji kutekelezwa kwa umuhimu wake ni vyema basi Halmashauri kuitisha baraza la madiwani la Dharura kwa ajili ya kupata rizaa ya matumizi ya jambo hilo aidha kwa vile mamlaka hizi zinahaki ya kisheria kukusanya mapato na kufanya matumizi basi waweze kutumia fedha zinazotokana na mapato ya ndani na si vyenginevyo.

### 8.4.24 Posho la nauli ambalo halilipwi kwa kila mwezi kwa wastani wa shilingi 1,150,600

Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni–Pemba linawajibu wa kusimamia na kuendesha shughuli za Baraza ikiwa ni pamoja na kuwalipa walimu posho la nauli stahiki kulingana na kigezo cha masafa kama ilivyofafanuliwa katika barua ya tarehe 02/12/2011 kutoka kwa katibu Mkuu (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Ukaguzi umebaini kwamba Halmashauriya Wilaya ya Micheweni – Pemba haipangi viwango stahiki vya posho la nauli kulingana na vigezo vya masafa ambapo kiwango cha posho la nauli kinacholipwa kwa baadhi ya walimu ni kidogo ukilinganisha na uhalisia wa masafa wanayotoka walimu hao. Aidha kulingana na taarifa za malipo za posho la nauli zinaonesha kuwepo kwa tofauti baina ya malipo stahiki na malipo halisi yanayolipwa kwa wastani wa Jumlaya shilingi 1,150,600 kwa mwezi

Kutokulipwa walimu posho la nauli stahiki ni kwenda kinyume na toleola tarehe 02/12/2011 kutoka kwa katibu Mkuu (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

**Majibu**

Halmashauriya Wilaya ya Micheweni inakiri kwamba ni kweli Jumla ya Shilingi 1,150,600.00 zimekuwa hazilipwi kwa kila mwezi kutokana na uchache wa upatikanaji wa fedha za matumizi mengineyo na inaahidi kutokwenda tena kinyume na mapungufu hayo na kuweza kulipa nauli stahiki ila hata hivyo walimu hao kwasasa wameshaondoka baada ya kuondoka kwa ugatuzi

**Uchunguzi wa Kamati**

Kamati katika kufuatilia hoja hii imejirizisha kuwa kwa kipindi hicho fedha za OC kutoka Serikali hazikuwa zinaingizwa kwa wakati kutokana Changamoto ya mripuko wa maradhi ya UVIKO 19 licha ya kuwepo Changamoto hii uongozi wa Halmashauri ulikua na uwezo wakufidia malipo hayo kwa kutumia fedha za mapato ya ndani kwa vile Halmashauri ya Wilaya Micheweni imeweza kuvuka malengo ya ukusanyi wa mapato kwa kukadiria kukusanya jumla ya Tzs 240,000,000 na kufanikiwa kukusanya Jumla ya Tzs 264,936,247.00 sawa na

asilimia 110.

**Mapendekezo ya Kamati**
Kamati inasisitiza juu ya umuhimu wa utekelezaji wa maagizo yanayotolewa na viongozi wetu hasa maagizo maalum la kuonesha utii na uwajibikaji kwa viongozi wetu Aidha kwa vile uongozi wa Halmashauri umekiri kuwasilisha kwa barua madeni yote yanayotokana posho la nauli kwa walimu kamati inaisisitiza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar kufanya uhakiki wa madeni hayo ambayo hayajalipwa katika miezi iliyotaja hapo juu ili walimu hao waweze kupatiwa stahiki zao ambazo wanadai wakati walipokuwa katika usimamizi wa Halmashauriya Wilaya ya Micheweni katika kipindi cha Ugatuzi.

**8.4.25 Kutokufanywa kwa makisio ya posho la nauli**

Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni – Pemba linawajibu wa kufanya makisio (Bajeti), kusimamia na kulipa posho la nauli kwa walimu na baadhi ya wafanyakazi nje ya kada ya ualimu.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kutokufanywa kwa makisio ya gharama zinazostahiki kwa ajili ya malipo ya posho la nauli kwa walimu na baadhi ya wafanyakazi wa Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni ambapo fedha za malipo ya posho hilo hulipwa kupitia fungu la Elimu.

Kutokufanywa kwa makisio ya gharama za posho la nauli katika kipindi cha mwaka husika ni kwenda kinyume na kifungu nambari 41(2) cha sheria ya usimamizi ya fedha za umma nambari 12 ya mwaka 2016 ya Zanzibar.

**Majibu**
Halmashauriya Wilaya ya Micheweni haipingani moja kwa moja na hoja za mdhibiti na mkaguzi mkuu wahesabu za serekali, ila makisio ya posho za nauli kwa walimu ilifanywa kulingana na walimu ambao walikuwepo na waliku wa wanastahiki kulipwa nauli hizo.

**Uchunguzi wa Kamati**
Kamati katika kufuatilia hoja hii imejiridhisha kwa kuangalia mpango kazi pamoja na Bajeti ya Elimu ya Maandalizi na Msingi na imebaini kwamba halmashauri ya Wilaya ya Micheweni ilikua inapanga bajeti maalum kwa ajili ya kulipa posho la nauli bajeti changamoto iliyo bainika ni kuwa kifungu hicho cha bajeti kilikua hakioneshwi katika taarifa za mwisho za hesabu za mwaka (financial statement).

**Mapendekezo ya Kamati**

Kamati inalishauri baraza la Mji Chake Chake kufuata taratibu zote za ufungaji wa hesabu za mwisho wa mwaka kwa kuingiza bajeti za vifungu vyote vya mapato na matumizi kama vile miongozo unavyotutaka ili kukidhi viwango sahihi vya ufungaji wa mahesabu ya taasisi kitaifa na kimataifa.

### 8.4.26 Dosari katika utaratibu wa malipo ya posho la nauli

Baraza la Mji Mkoani-Pemba linawajibu wa kufanya malipo ya posho la nauli kwa walimu na baadhi ya wafanyakazi nje ya kada ya ualimu kwa kuzingatia mfumo madhubuti katika ulipaji wa posho hilo.

Katika ukaguzi uliofanyika imebaini kakuwepo kwa udhibiti usioridhisha wa ulipaji wa fedha za posho la nauli kwa walimu ambapo imebainika malipo hayo kwa njia ya fedha taslim kupitia walimu wakuu wa skuli husika kinyume na sheria ya usimamizi wa fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016 ya Zanzibar.

Aidha, imepelekea kuwepo kwa malalamiko kwa baadhi ya Walimu ambao hawakulipwa malipo ya posho la nauli licha ya kwamba walimu hao wameonekana katika malipo hayo.

**Jadweli lifuatalo hapo chini linaonyesha orodha ya Skuli pamoja na walimu wakuu wanaokabidhiwa fedha taslim za posho la nauli.**

| NAM | JINA LA MWALIMU | SKULI HUSIKA |
|---|---|---|
| 1 | Mahindi Hamad Chumu | Kipangani |
| 2 | Kombo Rashid Hilal | Maziwa Ngo'mbe |
| 3 | Fatma Kombo Faki | Micheweni |
| 4 | Mohd' Ali Rubea | Wingwi |
| 5 | Wahida Saleh Hamad | Mtemani |
| 6 | Salim Hemed Salim | Shumba |
| 7 | Khamis Shaame Said | Karume |
| 8 | Abdalla Khamis Suleiman | Mkiang'ombe. |

Mchanganuo wa idadi ya walimu ambao hawakupokea malipo ya posho la nauli unaonekana katika Ripoti husika ya Mdhibiti.

#### Majibu

Halmashauriya Wilaya ya Micheweni inakiri kwamba ni kweli kumekuwa na ulipwaji wa fedha za posho la nauli kwa walimu kwa njia ya fedha taslim, ila kwa sasa malipo yote yanayoendelea yanafanywa kupitia system na fedha za kila mtu kuwekewa katika hesabu namba yake.

#### Uchunguzi wa Kamati

Kamati katika uchunguzi wake ilielezwa kuwa uongozi wa halmashauri wa

Wilaya ya Micheweni uliona ni busara kwa fedha hizo kuwakabidhi walimu wa kuu wa Skuli husika ili kuepuka usumbufu kwa walimu hao kutoka kuacha kusomesha na kufuata posho zao katika ofisi za Halmashauriya Wilaya ya Micheweni.

Hata hivyo Kamati imeona ipo haja ya kukutana na walimu ambao wametajwa katika kiambatanisho nambari 8 (I) kuwa wamelalamika hawakulipwa malipo ya posho la nauli licha ya kwamba wameonekana katika orodha ya malipo.

Kamati ilifanikiwa kuitisha kikao cha tarehe 18/08/2022 katika ukumbi wa Baraza la Mji Chake Chake kwa kuwahoji walimu hao ni Ndugu Jaffar Omar Juma ambae amekiri kukuta saini siyo yake katika vocha ya malipo na wala hakupokea fedha hizo.

Aidha, Kamati imefanya mahojiano na ndugu Issa Kai Hamad yeye alikiri mbele ya Kamati kuwa saini zote ambazo zipo katika vocha ya malipo ni zake lakini alipohojiwa na wakaguzi kutoka Afisi ya Mkaguzi Mkuu alikataa kuwa saini sio zake na Kamati ilipotaka kujua kwanini alipohojiwa na Mkaguzi amekanusha na ameijibu Kamati kuwa Siku hiyo hakuwa timamu kiakili kwa iyo hakuweza kuitambua saini yake.

**Mapendekezo ya Kamati**

Kamati inasisitiza juu ya utaratibu wa kufuata sheria mbalimbali za fedha ikiwemo suala la utolewaji wa fedha za malipo na posho zitolewe na wahasibu na si vyenginevyo ili kuepusha changamoto mbalimbali ambazo zimejitokeza katika utaratibu huu uliotumika zikiwemo malalamiko kwa baadhi ya walimu kukosa nauli zao.

Kamati inaishauri Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali wakati wanapochukua maelezo kwa watu ambao wameathiriwa na hoja Fulani ni vyema kuweka mifumo ya kurikodi maelezo hayo ili kubaini wahusika ambao watakaotoa maelezo tofauti kwa Mkaguzi mkuu wakati wa uchunguzi na kuyabadili maelezo hayo pindi wanapohojiwa na Kamati za Baraza la Wawakilishi ili hatua za kisheria ziweze kuchukuliwa kwa wote watakao husika kuzidanganyaa taasisi hizi mbili za Serikali.

Aidha, Kamati inalishauri Baraza la Mji kufuatilia kwa karibu na kubaini wahusika wote waliojihusishwa na vitendo hivyo ili kukomesha vitendo hivyo ambavyo havileti tija katika nchi yetu.

### 8.4.27 Kutokufanyiwa marekebisho orodha ya malipo kwa baadhi ya walimu baada ya kuhamishwa

Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni- Pemba linawajibu wa kusimamia uhamisho wa walimu pamoja na mafao yao kutoka skuli moja kwenda nyengine.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwepo walimu waliohamishwa kutoka skuli moja kwenda skuli nyengine bila kufanyiwa marekebisho ya uhamisho wa malipo ya posho la nauli zao, kufanya hivyo kunapelekea usumbufu kwa walimu kusomesha skuli moja na kupokea posho la nauli skuli nyengine.

**Jadweli lifuatalo hapo chini linaonyesha walimu waliohamishwa bila ya kufanyiwa marekebisho ya posho za nauli.**

| NAMBA | JINA LA MWALIMU | SKULI ALIOTOKA | SKULI ALIYOPO SASA |
|---|---|---|---|
| 1 | Jafar Omar Juma | Wingwi Secondary | Wingwi Msingi |
| 2 | Hamad Massoud Hamad | Wingwi Msingi | Mtemani Msingi |
| 3 | Kassim Omar Said | Tumbe | Mtemani Msingi |

Majibu

Halmashauriya Wilaya ya Micheweni inakiri kwamba ni kweli kuna walimu watatu (3) ambao wamehamishwa kutoka Skuli moja kwenda Skuli nyengine bila ya kutolewa katika orodha ya malipo na kuhamishiwa katika Skuli waliokwenda ila suali hilo lilishafanyiwa marekebisho mara tu baada ya kuligunduliwa na uongozi na kwa sasa walimu hao wameshaondoka baada ya kuondoka kwa ugatuzi.

Uchunguzi wa Kamati

Kamati ilihoji juu ya ucheleweshaji wa kufanya marekebisho ya posho la nauli kwa walimu ambao wamehamishiwa kutoka Skuli moja kwenda Skuli nyengine na kuelezwa kuwa kwa wakati huo shughuli za ugatuzi zilikua na changamoto nyingi kiutendaji jambo ambalo limepelekea kuchelewesha marekebisho hayo lakini baada ya suala hilo kugundulikana na uongozi limeweza kufanyiwa kazi na walimu hao wakawa wanapokea nauli zao katika Skuli ambazo wamehamishiwa.

Mapendekezo ya Kamati

Kamati inaushauri uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni juu ya utekelezaji wa Sheria mbalimbali za kiutumishi ikiwemo sheria ya ambazo inazitaka taasisi za Serikali kuhakikisha kuwa indapo mtumishi atahamishwa kutoka sehemu moja kwenda nyengine ni vyema maslahi yake yote yaweze kuhamishwa mara moja iwezekanavyo.

## 5.2 SHIRIKA LA NYUMBA

### Taarifa ya Mapato

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 Shirika la Nyumba lilikadiriwa kupata mapato jumla ya shilingi 3,035,000,000 kutoka vyanzo vyake mbalimbali vya mapato. Hadi kufikia tarehe 30, Juni 2021 Shirika limeweza kufanikiwa kupata mapato ya shilingi 3,046,500,971.99 sawa na asilimia 100.3 ya makadirio.

### Majibu

Ongezeko hilo la mapato limetokana kuwashajihisha wapangaji kwa mikutano ya mara kwa mara kwenye redio na kuwatumia ujumbe mfupi wa simu wapangaji kwa ajili ya kuwakumbusha kuhusu kulipa kodi pamoja na kuwaandikia barua za ukumbusho wa madeni yao. Pia, Shirika limechukua hatua ya kuwafungia milango na nyumba za wadaiwa sugu ambao walikaidi kulipa kodi zao kwa wakati.

Mlinganisho wa mapato kwa mwaka fedha 2020/2021 na 2019-2020 ni kama inavyoonekana katika jadweli la hapo chini:

| Mwaka 2019/2020 (Tsh.) | Mwaka 2020/2021 (Tsh.) | Asilimia ya Ongezeko |
|---|---|---|
| 2,800,961,602.17 | 3,046,500,971.99 | 8.7% |

### Uchunguzi wa Kamati

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC ilitaka kujua sababu zilizopelekea Shirika kukusanya mapato yake zaidi ya lilivyokadiriwa na lilieleza kuwa mapato hayo yameongezeka kutokana na sababu zifuatazo:

i. Kuendelea kuwashajihisha Wakodishwaji kulipa fedha ya kodi husika: na

ii. Wameanza kuifanyia kazi ipasavyo Sheria yao kwa kuwachukulia hatua Wakodishwaji wote wanaokwenda kinyume na Sheria hiyo. Hivyo, katika mwaka huo wa fedha walilazimika kuwafutia mkataba Wakodishwaji wanne walioshindwa kulipa deni la kodi ya nyuma.

iii. Baadhi ya Wakodishwaji walilipa kodi zao kabla (in advance) ambapo katika mwaka wa fedha 2020/2021 jumla ya Tsh. 252,524,540.50 zililipwa

ukilinganisha na mwaka wa fedha 2019/2020 ambapo Tsh. 120,000,000 zililipwa.

Vile vile, Kamati ya LAAC ilibaini kuwa ada ya kodi inayotozwa na Shirika ni ndogo sana ukilinganisha na bei halisi ya soko, hali hii inaitia hasara Shirika kwani hutumia gharama kubwa kuzifanyia nyumba ukarabati wakati Shirika linapokea kidogo.

**Mapendekezo ya Kamati**

Kutokana na hatua hiyo iliyofikiwa Kamati ya LAAC ililishauri Shirika la Nyumba mambo yafuatayo:

1. Kuzidi kuisimamia vyema Sheria yake na kuwachukulia hatua zaidi Wapangaji wasiolipa kodi pamoja na kuwachukulia hatua Wapangaji wanaopangisha watu wengine kitendo ambacho ni kwenda kinyume na Sheria za Shirika hilo.
2. Kuwa makini katika matumizi yake, kwani endapo Wakodishwaji watalipa kodi zao kabla kuna uwezekano mkubwa katika mwaka unaofuata Shirika kutokuwa na mapato ya kutosha.
3. Mchakato wa kubadilisha bei za nyumba kukamilishwa haraka iwezekanavyo ili Shirika liweze kupunguza kutumia gharama kubwa wakati tija inayopatikana ni ndogo.

**Taarifa ya Matumizi**

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 Shirika la Nyumba Zanzibar lilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 1,775,209,040 kwa kazi za kawaida pamoja na kazi za maendeleo. Hadi kufikia tarehe 30, Juni 2021 shirika lilitumia jumla ya shilingi 1,600,991,251.70 sawa na asilimia 90.2 ya makadirio.

**Majibu**

Sababu za kutofikia matumizi yaliyopangwa kwa kipindi husika ni kuchelewa kuanza kwa kazi za matengenezo za nyumba zifuatazo:

a. Nyumba 24 ngazi ya pili Maendeleo Michenzani.

b. Matengenezo ya nyumba namba 1699/1705- Mkunazini (Mnadani).

Kuchelewa huko kumetokana na kuchelewa kuanza kwa taratibu za manunuzi.

Ulinganisho wa matumizi kwa mwaka fedha 2020/2021 na mwaka wa fedha uliopita 2019/2020:

| **Mwaka 2019/2020 (Tsh.)** | **Mwaka 2020/2021 (Tsh.)** | **Asilimia ya mapungufu ya matumizi** |
|---|---|---|

| | | |
|---|---|---|
| 2,263,313,153.00 | 2,253.241,509 | 0.4% |

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Kamati ya LAAC ilibaini kuwa maelezo ya "Note" namba 7 kwenye Taarifa ya Hesabu ya Mwisho wa Mwaka yanatofautiana kwenye ukurasa wa 19 na ukurasa wa 27 kitendo ambacho ni kwenda kinyume na taratibu za ufungaji wa hesabu.

Kutokana na kasoro hiyo, Kamati ya LAAC imelishauri Shirika kuwa makini wakati wa kuandaa taarifa hiyo ili kuondosha utata kwa Mtumiaji yeyote wa taarifa hiyo.

MATOKEO YA UKAGUZI

### 5.2.1.1 Kutokufanyiwa maboresho kwa daftari la Mali za kudumu za Shirika

Wakati wa ukaguzi wa mali za kudumu za Shirika la Nyumba nilibaini kuwa Shirika halikuwa na daftari sahihi na lililoboreshwa la kutunzia taarifa za mali za kudumu. Ukaguzi ulibaini daftari hilo halikuwa na taarifa muhimu zinazosaidia katika kuimarisha udhibiti wa ndani na utayarishaji wa hesabu za mwisho wa mwaka. Miongoni mwa taarifa zilizokosekana ni thamani ya mali za kudumu zilizonunuliwa katika mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2021, gharama za uchakavu wa mali hizo, ardhi na majengo zimerekodiwa kama kitu kimoja, mali zimerekodiwa bila kuonyesha thamani, kuwapo kwa mali ambazo hazikuonyweshwa kwenye regista, kutoonyesha taarifa muhimu kama vile eneo mali ilipo pamoja na tarehe ya manunuzi.

Aidha, ukaguzi wangu umebaini kwamba Shirika la Nyumba halina mamlaka ya moja kwa moja ya uboreshaji wa taarifa za mfumo wa uwekaji wa kumbukumbu za mali za kudumu katika daftari la kutunzia mali ikiwemo uwezo wa kufanya maboresho ya uingizaji wa mali mpya ziilizo nunuliwa pamoja na uondoshaji wa taarifa za mali zilizouzwa au mali chakavu ambazo hazitumiki.

Kukosekana kwa daftari la mali za Kudumu lililofanyiwa maboresho katika Shirika, kutaendelea kukwaza uandaaji wa taarifa za kifedha ambazo zinakidhi viwango vya uhasibu. Kushindwa kuweka taarifa za Mali za Kudumu kwa usahihi kunasababisha ugumu katika kusimamia Mali za Kudumu zisiibiwe au kutumika isivyopaswa.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Shirika la Nyumba kuhakikisha unaboresha daftari la Mali za Kudumu na kurekodiwa kwa usahihi kuanzia mali inaponunuliwa, matumizi yake na mpaka kuondoa mali kwenye rejista pamoja na kuhakikisha ina

mfumo mzuri wa uwekaji wa taarifa za mali za kudumu.

**Majibu**

Ni kweli wakati wa ukaguzi daftari la mali za kudumu la Shirika lilikuwa na mapungufu yaliyoorodheshwa na Mkaguzi Mkuu. Hata hivyo, Shirika limeshachukua hatua ya kulifanyia maboresho daftari hilo na kwa sasa daftari hilo la Mali za kudumu (Fixed Asset Register) za Shirika lina taarifa zote za thamani ya mali za kudumu zilizonunuliwa, gharama za uchakavu, ardhi na majengo zimerekodiwa tofauti, thamani ya mali nae neo mali ilipo, pamoja na tarehe ya manunuzi husika.

Vile vile, Shirika limeshawapatia mafunzo baadhi ya watendaji wa Shirika mafunzo juu ya uingizaji wa taarifa kwa ajili ya uboreshaji wa daftari la mali za Shirika kila inapohitajika ili kuhakikisha hapatokei tofauti baina ya taarifa zinazoingizwa au kutolewa katika daftari.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya LAAC inaunga mkono hoja ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, hata hivyo, Kamati imeifuta hoja hiyo kwa kuwa Shirika limeanza kutekeleza kasoro hiyo kwa asilimia kubwa.

Pamoja na hilo, Kamati ya LAAC imelishauri Shirika kubadilisha muundo wake ili kuanzisha Kitengo cha Usimamizi wa Mali kwa lengo la kuzisimamia vyema mali zake.

**SHIRIKA LA NYUMBA – PEMBA**

### 4.2.1.2 Malipo fedha kwa watoa huduma ambao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za umma shilingi 12,228,861.8

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(1) cha Sheria ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma kinaeleza kulingana na masharti ya sheria hii mtu, kampuni au taasisi haitawasilisha zabuni au vyenginevyo kushiriki katika manunuzi ya Umma isipokua chombo kiwe kimesajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi.

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(2), zabuni kutoka kwa mtu, kampuni au chombo ambacho hakijasajiliwa haifai na hakitazingatiwa na taasisi ya ununuzi.

Ukaguzi umebaini kwamba Shirika la Nyumba - Pemba limefanya manunuzi na watoa

huduma mbali mbali ambapo watoa huduma hao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi kwa mujibu wa sheria ambapo kumepelekea kushindwa kujiridhisha uhalali wa malipo hayo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na vifungu vya Sheria nilivyovinakili hapo juu vya Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Shirika la Nyumba - Pemba kufanya manunuzi kwa kuzingatia kanuni, sheria pamoja na miongozo mbali mbali iliyopo.

**Majibu**
Ni kweli kwamba Shirika limewahi kufanya manunuzi kwa baadhi na watoa huduma wasiosajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma katika baadhi ya wakati kwa mazingira yafuatayo:

- Kwenye manunuzi ya kazi za dharura kama vile vifaa vya ujenzi na usafishaji wa mashimo ya vyoo, inapotokea kuharibika au kujaa na kuhatarisha usalama na wapita njia, wakaazi, wananchi kwa ujumla au kuharibu mazingira kwa ujumla.

Hata hivyo, Shirika limepokea ushauri wa Mkaguzi Mkuu wa Serikali kuanzia sasa manunuzi yote ya vifaa na huduma hata zile za dharura zinafuata utaratibu kwa mujibu wa Sheria ya Manunuzi. Kwa upande wa watoa huduma Shirika sasa hivi linatumia mafundi waliosajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi Zanzibar.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**
Kamati ya LAAC inaunga mkono hoja ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, hata hivyo, Kamati imeifuta hoja hiyo kwa kuwa Shirika limeanza kutekeleza kasoro hiyo.

#### 4.2.1.3 Madeni yatokanayo na kodi za nyumba za Shirika shilingi 270,085,500

Jumla ya shilingi 270,085,500 ni madeni ambayo Shirika la Nyumba – Pemba linadai kutoka kwa baadhi ya wapangaji wake wa nyumba za maendeleo na milango ya biashara. Baada ya kupitia mikataba ya upangishaji, ukaguzi umebani kwamba wapangaji wanaodaiwa wamekwenda kinyume na makubaliano ya mkataba na uongozi wa Shirika la Nyumba - Pemba umeshindwa kuchukua hatua zinazostahiki.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu namba 7(i) cha mkataba wa ukodishaji wa nyumba za maendeleo na milango ya biashara.

Ukaguzi unashauri Shirika la Nyumba - Pemba kuhakikisha linafanya ufuatiliaji wa haraka kwa upatikanaji wa malipo kwa wapangaji wote wanaodaiwa pamoja na

kuweka usimamizi mzuri wa mikataba ya ukodishwaji. Aidha shirika linapaswa kuweka Sera madhubuti ikiwemo kuweka adhabu (penalty) kwa kampuni, taasisi, shirika au mpangaji yoyote kushindwa kulipa malipo yake kwa wakati.

**Majibu**

Shirika linakubali kuwepo kwa madeni hayo, pamoja na mambo mengine Shirika limechukua hatua zifuatazo katika kukabiliana na tatizo hili:

1. Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika iliunda kamati ya kufuatilia madeni na kuwaita wapangaji wenye madeni makubwa ili kuwahimiza kulipa madeni yao.
2. Shirika linaendelea kupeleka barua za ukumbusho wa kulipa madeni kwa wapangaji wote wenye madeni.
3. Shirika linafunga nyumba na milango ya biashara ya wadaiwa sugu ili kuhakikisha wanakamilisha madeni yao.
4. Shirika limeanzisha mfumo wa kuwatumia wapangaji bili zao kila mwezi na pia kuwakumbusha madeni yao kila mara kwa njia ya ujumbe mfupi.

Shirika linatumia dalali wa mahkama (Kumekucha) ambaye limefunga nae mkataba kwa kuwatoa kwa mujibu wa sheria wapangaji walioshindwa kabisa kukamilisha madeni yao ya muda mrefu.

**Uchunguzi wa Kamati**

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC imebaini yafuatayo:

1. Deni la Shirika la Nyumba la Tsh. 270,085,500 limejumuisha deni lote la kodi ya nyumba tangu lilivyoanzishwa Shirika hilo mwaka 2016.
2. Deni hilo limewajumuisha hadi Watendaji wa Serikali ambao hulipwa fedha na Taasisi zao kwa ajili ya kodi ya nyumba, isipokuwa kwamba, fedha hizo wanazitumia kwa shughuli zao nyengine na kubakia na deni kwa upande wa kodi ya nyumba. Kwa mujibu wa Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka 2020/2021 jumla ya Tsh. 24,462,500 zinadaiwa na Shirika kwa Watendaji wa Serikali wanaofanya kazi katika Taasisi mbali mbali zilizopo Pemba.
3. Kwa mujibu wa Taarifa ya Hesabu ya Mwisho wa Mwaka deni halisi la Shirika ni Tsh. 193,852,000 na sio Tsh. 270,085,500 kama ilivyoandikwa kwenye Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

   Kamati ya LAAC imejiridhisha hilo kupitia ukurasa wa 33 wa Taarifa ya Hesabu ya Mwisho wa Mwaka ya 2020/2021. Hii ni kutokana na kuwa Shirika la Nyumba kwa upande wa Pemba limekusanya Tsh. 269,310,000 na deni halisi kwa mwaka huo ni Tsh. 75,458,000.

   Kutokana na kasoro hiyo iliyobainika Kamati ya LAAC iliomba kupatiwa

maelezo kutoka kwa Afisa wa Afisi ya Mdhibiti anayefuata na Kamati na alieleza kuwa, kasoro hiyo imejitokeza kwa kuwa Afisi ya Mdhibiti ikifanya ukaguzi kwa upande wa Pemba huwa haiangalii Taarifa ya Hesabu ya Mwisho wa Mwaka. Hii ni kutokana na kwa kuwa hakuna taarifa zinazoonesha taarifa za Pemba pekee na badala yake huangalia zaidi kwenye nyaraka zilizokuwepo Afisini hapo.

4. Shirika la Nyumba hivi sasa limeanza kuchukua hatua ya kuwatoa ndani ya majengo hayo Wapangishwaji waliovunja mkataba kama kifungu cha 33 na 34 cha Sheria Namba 6 ya mwaka 2014 kinavyoelekeza.
5. Baadhi ya Wapangaji wa nyumba hukimbilia kwa Viongozi wa Serikali endapo Shirika linataka kuchukua hatua za kutekeleza masharti ya kifungu cha 33 na 34 Sheria hiyo.

   Viongozi hao wa Serikali wamekuwa wakitoa amri mbali mbali kwa Watendaji wa Shirika hili kwa lengo la kuwalinda Wapangaji hao. Kitendo cha Viongozi hao kutoa amri hizo kinaviza juhudi za Watendaji wa Shirika hilo na kulikosesha Shirika mapato ambayo ndio chanzo kikuu cha Shirika.

6. Tarehe 14 Novemba, 2022 Mtendaji wa Shirika la Nyumba Pemba amepigwa na mwananchi wa kawaida wakati anatekeleza majukumu yake kitendo kilichopelekea Mtendaji huyo kushindwa kuhudhuria kazini kwa muda wa siku mbili mfululizo kutokana na maumivu makali aliyoyapata.

Mapendekezo ya Kamati

Ili kasoro kama hizo zisijotokeza tena Kamati ya LAAC ilipendekeza yafuatayo:

1. Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika kutekeleza shughuli zake azingatie Taarifa ya Hesabu ya Mwisho wa Mwaka ili kuwa na taarifa sahihi.
2. Serikali ianzishe utaratibu wa kufunga hesabu za mwisho wa mwaka kwa upande wa Pemba pekee (segment report) ili kupima utendaji wa Taasisi pamoja na kuwa na taarifa sahihi kwa Pemba.
3. Viongozi wa Serikali wasiwabughudhi Watendaji wa Shirika la Nyumba endapo watachukua au wanachukua hatua ya kuwatoa katika majengo Wapangishwaji wanaovunja mkataba au wanavyochukua hatua nyengine yoyote ili mradi hawavunji Sheria za nchi.
4. Viongozi wa Serikali kusimamia kwa dhati mapato ya Serikali na wasiwe chanzo cha kuzuia mapato hayo kwa kuzingatia kuwa Shirika la Nyumba linamilikiwa kwa asilimia mia moja na Serikali, lakini pia, Shirika hilo lina kazi kubwa ya kukarabati nyumba za maendeleo na ujenzi wa nyumba mpya katika maeneo mbali mbali Zanzibar.
5. Vyombo vinavyohusika na ulinzi na usalama vitoe mashirikiano kwa Shirika hili wakati wa zoezi la kuwatoa katika majengo Wapangishwaji waliovunja mkataba ili kuepusha kutokea vitendo viovu dhidi ya Watendaji wa Shirika.

6. Taasisi za Serikali kuanzia mwezi wa Machi, 2023 zihakikishe kuwa zinawakata moja kwa moja kwenye mishahara yao Watendaji wao waliokodi katika nyumba za Shirika kama mikato mengine inavyofanywa, kwa mfano; Mkato wa Income Tax, ZSSF na kadhalika ili Shirika liweze kupata kodi yake kwa wakati kwa maendeleo ya Shirika hili. Kwani endapo hatua za haraka zisipochukuliwa kuna uwezekano mkubwa wa deni hilo kuongezeka kwa kiwango kikubwa siku hadi siku.
7. Taasisi za Serikali ambazo Watendaji wake wana deni la kodi ya nyumba zihakikishe kuwa deni hilo linalipwa na Watendaji hao ndani ya miezi mitatu kuanzia mwisho wa mwezi wa Machi, 2023 kwa kuwa Baraza la Wawakilishi liliidhinisha fedha hizo kwa madhumuni hayo.
8. Wapangaji wote wa Shirika la Nyumba ambao ni Watu Binafsi wahakikishe kuwa wanakamilisha kulipa deni hilo ndani ya miezi sita kuanzia mwezi wa Machi, 2022.
9. Vyombo vya Ulinzi na Usalama vihakikishe kuwa vinawachukulia hatua wananchi wote waliohusika na kitendo kiovu cha kumjeruhi Mtendaji wa Shirika la Nyumba, tarehe 14 Novemba, 2022 alivyokuwa akitekeleza wajibu wake ili iwe fundisho kwa wengine na hasa ikizingatiwa kuwa hadi tunawasilisha taarifa hii tarehe 23 Februari, 2023 hakuna mtu yeyote aliyekamatwa dhidi ya kitendo hicho.

### 5.2.3 SHIRIKA LA MAGAZETI

#### Taarifa ya Mapato

Shirika la Magazeti ya Serikali Zanzibar lilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 857,500,000 katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 kupitia vyanzo vyake vya ndani vya mapato na shilingi 621,000,000 ikiwa ni ruzuku kutoka Serikalini. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya shilingi 877,311,882.06 zilikusanywa kutokana na vyanzo vya ndani vya mapato ambapo ni sawa na asilimia 102.3 ya makadirio na shilingi 610,605,854 ikiwa ni ruzuku iliyopokelewa kutoka Wizara ya Habari, Vijana Utamaduni na Michezo sawa na asilimia 98.3 ya makadirio.

#### Majibu

Ongezeko hili la shilingi 19,811,882.45/= ambalo ni sawa na asilimia 2 za makadirio lilitokana na ongezeko la mauzo ya magazeti mapya ya Zanzibar Mail na ZASPORT pamoja madeni ambayo yalikuwepo kipindi cha mwaka 2019/2020 kwa taasisi mbali mbali hasa taasisi za Serikali.

#### Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Katika kufuatilia hoja hii, Kamati ya LAAC ilibaini kuwa fedha yoyote inayoingia ndani ya Shirika inachukuliwa kuwa ni mapato hata kama ni deni, kitendo hicho kinainyima Shirika kuweza kujua mapato halisi yaliyokusanywa katika mwaka husika.

Kutokana na hali hiyo, Kamati ya LAAC imelitaka Shirika hili kuendelea na utaratibu iliouanzisha kuanzia mwezi wa Oktoba, 2021 wa kuzigawanya fedha zinazoingia katika Shirika hilo kwa kuweka malipo ya deni mbali na malipo ya kawaida mbali ili kupatikana mapato halisi ya mwaka husika.

Vile vile, Kamati ya LAAC inaishauri Serikali kukifanyia marekebisho kifungu cha 35 cha Sheria ya Kuanzisha Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar Namba 12 ya mwaka 2018 ili Shirika la Magazeti liweze kupatiwa mtambo wake na kuweza kutoa huduma mbali mbali za uchapaji kwa lengo la kukuza mapato yake pamoja na kuchapisha gazeti kwa gharama nafuu zaidi.

### Taarifa ya Matumizi

Shirika la Magazeti ya Serikali Zanzibar lilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 1,683,005,426.83 kwa matumizi ya kazi za kawaida kwa mwaka wa fedha 2020/2021, hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya shilingi 1,639,909,576 zilitumika ambazo ni sawa na asilimia 97.4 ya makadirio.

### Majibu

Matumizi ya Shirika la Magazeti ya Serikali Zanzibar yameonekana kupungua kutoka shilingi 1,683,005,426.83/= iliyoidhinishiwa kwa kazi za kawaida, hadi kufikia shilingi 1,639,909,575.99/= sawa na asilimia 97 ya makadirio, kukiwa na upungufu wa shilingi 43,095,850.84/= sawa na asilimia 3 ya mapungufu. Hii ni kutokana na kupungua kwa ruzuku kutoka Serikalini tuliyoingiziwa haikuweza kufikia gharama zetu za matumizi yaliyopangwa.

### Uchunguzi wa Kamati

Katika kufuatilia hoja hii, Kamati ya LAAC ilibaini yafuatayo:

1. Baadhi ya ununuzi ulifanywa na Mhariri Mtendaji bila ya kuhusishwa Afisa wa Ununuzi.
2. Kwenye Taarifa ya Hesabu ya Mwisho wa Mwaka baadi ya "Note" zina jina zaidi ya moja kitendo ambacho ni kinyume na taratibu za kihasibu.
3. Baadhi ya shughuli zimepangwa kinyume na uhalisia wake. Hatua hii imefikiwa ili makisio ya bajeti yaendane na ukomo (ceiling) wa bajeti uliopewa Shirika wakati wa uandaaji wa bajeti. Kwa mfano, Huduma ya Bima ya Afya (NHIF) ilikadiriwa kutumia Tsh. 9,026,000 ingawa mwaka wa fedha 2019/2020 wametumia Tsh. 15,114,180,000 na mwaka wa fedha 2020/2021 wametumia kiwango hicho hicho.

### Mapendekezo ya Kamati

Ili kasoro kama hizo zisijitokeze tena katika siku zijazo, Kamati ya LAAC ilipendekeza yafuatayo:

1. Taasisi za Serikali zipange bajeti zao kulingana na uhalisia uliopo.
2. Shirika la Magazeti lihakikishe kuwa linatekeleza majukumu yake kama Sheria

za nchi zinavyolekeza.

## MATOKEO YA UKAGUZI

### 5.2.3.1 Manunuzi yaliyofanyika nje ya mpango wa manunuzi shilingi 107,382,500

Mapitio ya mpango wa manunuzi wa mwaka 2020/21 wa Shirika la Magazeti ya Serikali yalibaini kwamba Shirika la Magazeti ya Serikali lilifanya manunuzi ya gari mbili (2) aina ya Suzuki Vitara GLX yenye thamani ya shilingi 107,382,500 nje ya mpango wa manunuzi kinyume na kifungu cha 42(7) cha Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa mali za Umma namba 11ya mwaka 2016.

Manunuzi nje mpango wa manunuzi yanaweza kupelekea kutotekelezwa kwa mipango mingine na kunaweza kukwamisha shughuli stahiki zilizopangwa kwa mujibu wa bajeti iliyoidhinishwa.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Shirika la Magazeti ya Serikali Zanzibar uingize shughuli zote muhimu katika bajeti na mpango wa manunuzi wa kila mwaka ili kuepuka kufanya manunuzi nje ya mpango ambayo yanaweza kusababisha gharama za ziada au zisizo za lazima kwa Shirika.

Aidha, ukaguzi unashauri Shirika kufuata muongozo nambari BLM/97/M/C.5/VOL.V/27 wa tarehe 27 Septemba 2021 kutoka Serikalini uliotolewa na Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi kuwaagiza Wakuu wote wa Taasisi kuwasilisha maombi ya ununuzi wa gari kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Fedha na Mipango na kuacha kununua magari yaliyotumika (Used Car) pamoja na kuacha kununua magari kwa wazabuni binafsi kwa lengo la kununua gari kwa thamani kubwa kuliko bei ya sokoni.

**Majibu**

Shirika la Magazeti ya Serikali lilifanya ununuzi wa gari mbili (2) mpya aina ya SUZUKI VITARA kwa ajili ya matumizi ya Shirika yenye thamani ya shilingi 107,382,500/=. Manunuzi haya yalishawekwa katika mpango wa manunuzi wa mwaka wa fedha 2019/2020. Hata hivyo, kutokana na uhaba wa fedha, ambazo Shirika la Magazeti ya Serikali ilipatiwa kutoka Serikalini zilikuwa chini ya mahitaji na ilibidi Shirika la Magazeti ya Serikali kutafuta fedha za kuongezea ili kuweza kununua gari hizo ambapo ilipelekea manunuzi hayo kufanyika kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Shirika limepokea ushauri wa Mkaguzi wa Hesabu za Serikali wa kuingiza shughuli zote muhimu katika mpango wa manunuzi wa kila mwaka ili kuepusha kufanya manunuzi nje ya mpango.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**
Kamati haikuridhika na majibu ya Shirika hivyo, hoja hii imebaki kama ilivyo.

### 5.2.3.2 Manunuzi yaliyofanywa kwa kutokufuata njia sahihi ya ununuzi katika manunuzi ya umma shilingi 140,149,332

Kifungu cha 66(1)(a) cha Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma namba 11 ya mwaka 2016 kimeelezea utaratibu wa kuchagua njia ya ununuzi ambapo taasisi za ununuzi wa Umma zimeelekezwa kutumia utaratibu ulioelezwa katika kifungu cha 65 hadi 71 pamoja na masharti yaliyoelezwa katika jadweli la tatu la sheria hii.

Aidha, kifungu cha 66(2) cha Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa mali za Umma kimeeleza kuwa Taasisi ya ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Italazimika kupata ruhusa ya Mamlaka kabla ya kutumia utaratibu mwengine mbali ya ule ulioelezwa katika sehemu hii ya Sheria hii.

Ukaguzi umebaini kwamba Shirika la Magazeti ya Serikali limefanya manunuzi kinyume na miongozo ya Sheria pasi na kuomba ruhusa ya Mamlaka ya ununuzi katika ununuzi gari na Samani za Shirika zenye thamani ya jumla ya shilingi 140,149,332.

Kutokufuata taratibu sahihi za manunuzi kunaweza kupelekea kukosekana kwa bidhaa zenye ubora na bidhaa kununuliwa kwa bei ambayo haitalinufaisha Shirika.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Shirika la Magazeti ya Serikali Zanzibar kufanya manunuzi kwa mujibu wa taratibu na miongozo iliyotolewa na Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa mali za Umma ya mwaka 2016.

**Majibu**
Ununuzi wa gari mbili (2) mpya aina ya SUZUKI VITARA na ununuzi wa samani kwa ajili ya matumizi ya Shirika la Magazeti ya Serikali katika ofisi za Dodoma.

Shirika limefanya manunuzi ya gari 2 ambazo thamani yake ilikuwa ya kawaida na zilipata msamaha wa kodi. Katika hili, Shirika la Magazeti ya Serikali limefuata Sheria ya Manunuzi, Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016, kifungu cha 73 (a, b, c, na d). Kutokana na uhitaji wa mahitaji ya magari kwaajili ya shughuli za uendeshaji na usambazaji wa magazeti na Shirika la Magazeti ya Serikali kukosa hata gari ya kuweza kuendesha shughuli zake ilitumia kifungu hicho cha sheria katika ununuzi wa magari hayo.

Pia, ununuzi wa gari hizi ulifanywa kwa dharura (emergency) kutokana na uhalisia wa tatizo la usafiri katika Shirika la Magazeti ya Serikali. Ikumbukwe kuwa Shirika la

Magazeti ya Serikali linazalisha magazeti manne kwa wiki (Zanzibar Leo, ZaSpoti, Zanzibar Mail na Zanzibar Leo Wanawake) ambayo yote haya yanahitaji kutayarishwa (kwa maana ya usafiri wa uhakika kwa waandshi wa habari) na kusambazwa kwa magazeti katika sehemu mbali mbali za Zanzibar wakati huo shirika halikuwa na hata gari moja inayofanya kazi kwa uhakika. Katika hili pia Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016, kifungu cha 67 (1) (2) (3) kimefuatwa.

Aidha, Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016, kifungu cha 75 (1) (2) imetumika kwa kuichagua Kampuni ya CFAO ambao ndio pekee waliokuwa na uhakika wa uuzaji wa gari mpya ambazo zinakidhi kiwango kwa mahitaji ya shirika pamoja na kuweza kuzifikisha Zanzibar kwa wakati stahiki.

Uchunguzi umebainisha kuwa kwa njia nyengine yoyote ambayo ingelitumika ingeweza kugharimu fedha nyingi zaidi na pia kushindwa kufika gari hizo kwa wakati ili kuweza kufanikisha maendeleo kasi ya Shirika la Magazeti ya Serikali, Zanzibar.

Kwa kuwa suala hili ni la haraka (emergency), pia suala hili lilisharidhiwa na kupitishwa na Wizara ya Habari na Bodi ya Shirika la Magazeti ya Serikali. Pia katika manunuzi haya ushauri wa Waziri wa Fedha ambaye alikuwa na taarifa za kutosha kuhusu manunuzi hayo ya gari zilifuatwa na pia ameridhia kuruhusu msamaha wa gari hizo kwa kupata punguzo kubwa la bei na kodi.

Gari hizo mpya na zenye kiwango zilifika kwa wakati na kupunguza tatizo la usafiri pamoja na usambazaji wa magazeti katika sehemu mbali mbali za Zanzibar.

Pia, Shirika lilifanya manunuzi ya samani za Ofisi kwa ajili ya matumizi ya Shirika katika ofisi ndogo ya Dodoma, zenye thamani ya Tsh. 16,550,000. Kwenye mchakato huu katika hatua za awali Shirika la Magazeti ya Serikali ilishirikisha kitengo cha Manunuzi cha Shirika ili kuelekeza takwa pamoja na njia sahihi ya manunuzi ya samani hizo kwa upande wa ofisi ya Dodoma.

Hata hivyo, suala hili lilikumbana na changamoto na lilishindwa kuendelezwa na Maafisa Manunuzi wa Shirika la Magazeti ya Serikali kwa sababu zifuatazo:-

a. Msaidizi Afisa Manunuzi alitoa dharuara ya kuwa ananyonyesha na hatoweza

kwenda Dodoma.

b. Afisa Manunuzi pia alitoa dharura ya kuwa kutokana na kuwepo kwa UVIKO 19 (Corona) hatoweza kusafiri.

Ili kazi isikwame na Shirika liendelee kutoa huduma zake kwa upande wa Mkoa wa Dodoma kwa ufanisi zaidi na kwa vile tayari tulishapata jengo la Ofisi, Shirika kupitia Afisa Masuuli (Mhariri Mtendaji) iliona ipo haja ya kuwa na vitendea kazi na kulazimika kufanya maamuzi ya kununua fanicha hizo kwa maendeleo ya Shirika.

Hata hivyo, Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016, kifungu cha 72 (1) (2) (3) kilifuatwa kwa kuitisha quotation tatu (3) kabla ya kumchagua mtoa huduma.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**
Kamati ya LAAC haikuridhika na majibu ya Shirika, hivyo, hoja hii imebaki kama ilivyo.

**5.2.3.3 Mikataba iliyosainiwa bila kupata ridhaa ya Mwanasheria Mkuu**
Kifungu cha 27(3) cha Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa mali za Umma ya mwaka 2016 na kanuni za manunuzi kifungu 47(1) kinaelezea kwamba, "Mikataba yote inayohusiana zabuni baadaa ya kukubaliwa kwa zabuni, ombi au pendekezo lililoandaliwa chini ya sheria hii, ni lazima iridhiwe na Afisi ya Mwanasheria Mkuu kabla ya kusainiwa na pande mbili husika katika mkataba".

Ukaguzi umebaini kwamba mkataba uliosainiwa baina ya Shirika la Magazeti ya Serikali Zanzibar na Kampuni ya Cfao Motors Tanzania Limited wa tarehe 5 Novemba 2020 kwa ajili ya ununuzi wa gari mbili (2) aina ya SUZUKI VITARA zenye thamani ya Shilingi 107,383,050 ulisainiwa bila kupelekwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kwa ajili ya kupatiwa ridhaa ya kuendelea na ununuzi.

Shirika la Magazeti ya Serikali Zanzibar kusaini mikataba bila ya kupata ridhaa ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni Kwenda kinyume na kifungu cha 27(3) ya Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa mali za Umma ya mwaka 2016 ambapo kunaweza kupelekea Shirika kuingia makubaliano ambayo hayatalinufaisha Shirika.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Shirika la Magazeti ya Serikali Zanzibar linapotaka kuingia mikataba na kampuni lihakikishe kwamba linazingatia kikamilifu Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa mali za Umma ya mwaka 2016 ili kuweza kuboresha zaidi mchakato mzima wa manunuzi katika Shirika.

**Majibu**
Shirika la Magazeti linakiri kwamba mkataba uliosainiwa baina ya Shirika na CFAO

Motors Tanzania Limited haukuwasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kwa njia ya kuidhinishwa.

Hata hivyo, uharaka wa uhitaji wa upatikanaji wa gari hizo kutokana na uhitaji (kwa waandishi pamoja na usambazaji wa magazeti) imepelekea kwa uongozi wa Shirika la Magazeti ya Serikali, Wizara ya Habari, Waziri wa Fedha pamoja na Bodi ya Shirika la Magazeti ya Serikali 'kukengeuka' kidogo na kushindwa kuwasilisha mkataba kati ya Shirika la Magazeti ya Serikali na CFAO.

Hata hivyo, Shirika linaahidi kutekeleza takwa la Kifungu cha Nambari 11 cha Sheria ya Ununuzi na Uondoaji Mali za Umma kwa Mikataba yote inayoingiwa na Shirika. Na kwa sasa Mikabata yote inapitia kwa Mwanasheria Mkuu.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya LAAC haikuridhika na majibu ya Shirika, hivyo, hoja hii imebaki kama ilivyo.

### 5.2.3.4 Manunuzi ambayo hayakupita katika kitengo cha ununuzi na uondoshaji wa mali za umma yenye thamani ya shilingi 153,445,942

Kwa mujibu wa kifungu nambari 29(a) cha Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa mali za Umma ya mwaka 2016, kimeelezea kazi za kitengo cha Ununuzi na Uondoshaji wa mali za Umma moja wapo ikiwa ni , "Kusimamia kazi zote za ununuzi na uondoshaji wa mali za umma katika Taasisi ya ununuzi na uondoshaji wa mali isipokua maamuzi na utoaji wa Zabuni".

Ukaguzi umebaini kwamba baadhi ya manunuzi yaliyofanywa na Shirika la Magazeti ya Serikali hayakufanywa na kitengo cha ununuzi na uondoshaji wa mali za umma na hivyo kupelekea manunuzi hayo kufanyika bila ya kuzingatia misingi na miongozo iliyowekwa na Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa mali za Umma ya mwaka 2016.

Kufanya manunuzi bila ya kushirikisha kitengo cha manunuzi cha Shirika ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa mali za Umma ya mwaka 2016, ambapo kunaweza kupelekea manunuzi kufanyika bila kuzingatia taaluma na taratibu za manunuzi zilizowekwa chini ya Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma. Aidha, upo uwezekano wa kufanyika kwa manunuzi yasiyokuwa na tija.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Shirika la Magazeti ya Serikali Zanzibar kuhakikisha kwamba, manunuzi yote yanafanywa na kusimamiwa na Kitengo cha ununuzi na uondoshaji wa mali za umma kama ambavyo imeelezwa na Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa mali za Umma ya mwaka 2016.

**Majibu**

Ni kweli Shirika lilifanya manunuzi mbali mbali na manunuzi yote ya Shirika

hushirikisha Kitengo cha Manunuzi katika hatua zote. Aidha, inapotokezea changamoto za kibinaadamu kutoka kwa watendaji wa kitengo cha manunuzi ikiwemo dharura za ugonjwa na kupelekea kuzorota ama kukwama kabisa kwa shughuli hizo Afisa Masuuli (Mhariri Mtendaji) huchukua hatua ili Shirika liweze kufanikisha shughuli zake.

Kwa mfano, Watendaji wa Kitengo cha Manunuzi waliposhindwa kwenda Dodoma kwa ajili ya manunuzi ya samani za ofisi ndogo ya Dodoma, Mhariri Mtendaji alichukua hatua katika kufanikisha suala hilo.

Pia, tunaishukuru Mamlaka ya Ununuzi kwa kutuletea Afisa manunuzi mwenye uzoefu na ambae hufuata miongozo, taaluma na taratibu na maelekezo sahihi ya manunuzi, na kwa sasa shughuli za Shirika zinaendelea kwa ufanisi zaidi.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya LAAC haikuridhika na majibu ya Shirika, hivyo, hoja hii imebaki kama ilivyo.

SHIRIKA LA MAGAZETI YA SERIKALI – PEMBA

### 5.2.3.5 Kukosekana kwa mapato yatokanayo na malimbikizo ya madeni ya magazeti shilingi 48,002,170

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Shirika la Magazeti – Pemba linadai madeni ya muda mrefu yenye jumla ya shilingi 48,002,170 yatokanayo na huduma za uuzwaji wa magazeti kwa taasisi na mashirika mbali mbali ya yanayopewa huduma hiyo kwa njia ya mkopo.

Kujitokeza kwa uwepo wa wadaiwa waliopatiwa huduma na Shirika la Magazeti – Pemba kunapelekea kudumaza shughuli za uendeshaji wa shirika jambo ambalo linapekelea kwa baadhi ya miezi shirika kushindwa kuchapisha magazeti kutokana na uhaba wa fedha.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Shirika la Magazeti - Pemba kuhakikisha linafanya ufuatiliaji wa haraka wa urejeshwaji wa madeni hayo kwa lengo la kuweza kujiendesha pamoja na kuandaa taratibu na sera imara ya tozo ya adhabu kwa wale watakaoshindwa kulipa malipo kwa wakati.

**Majibu**

Shirika la Magazeti ya Serikali linakiri kuwepo kwa madeni ya matangazo na mauzo ya magazeti kutoka kwa wadau mbali mbali kisiwani Pemba yenye jumla ya shilingi 48,002,170. Madeni hayo ni madeni ambayo huchelewa kulipwa hususani na Taasisi za Serikali ambao hupata huduma mwanzo na baadae kufanya malipo. Deni hili

huongezeka kila siku kutkana na ucheleweshaji wa kulipwa madeni hayo kwani taasisi hizo huendelea kupokea huduma.

Kutokana na hali hiyo Shirika linaendelea kudai madeni hayo kwa kuziandikia barua taasisi zinazodaiwa, ufuatiliaji wa ana kwa ana na pia kuiandikia barua Ofisi ya Rais Fedha na Mipango wazikate Taasisi hizo katika fedha zao za OC moja kwa moja ili kuepusha mrundikano na engezeko la madeni hayo. Pia kupitia kauli ya Mheshimiwa Dkt, Hussein Ali Mwinyi Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mpinduzi katika kilele cha miaka 20 ya Gazeti la Zanzibar Leo kuzitaka taasisi hizo kulipa madeni yao wanayodaiwa, imesaidia sana Shirika kuendelea kulipwa kiasi cha shilingi 7,913,500.00 kutoka kwa baadhi ya taasisi hizo ingawaje kwa upate wa Pemba pia hutoa changamoto ya ufinyu wa Fedha za OC wanazopatiwa.

**Uchunguzi wa Kamati**

Katika kufuatilia hoja hii yafuatayo yamebainika:

1. Gharama ya kununua gazeti sio kubwa ila Taasisi hazitoi kipaumbele kulipa matumizi hayo jambo linalopelekea fedha hizo kujirundika na kuwa nyingi na hatimae Taasisi kushindwa kulipa.
2. Shirika la Magazeti linajitahidi kutoa barua za ukumbusho wa deni kwa Taasisi husika hata hivyo, muitikio ni mdogo sana.

**Mapendekezo ya Kamati**

Ili kasoro hiyo isizidi kuendelea Kamati ya LAAC ilipendekeza kuwa fedha za ununuzi wa magazeti zikatwe moja kwa moja kwenye fedha za matumizi mengine ya Taasisi husika ili deni hilo lisiongezeka. Pendekezo hilo lilitakiwa kuanza kazi kuanzia mwezi wa Machi, 2023.

Vile vile, Kamati ya LAAC inapendekeza kurekebishwa kwa Sheria ya Kuanzishwa Shirika la Magazeti Zanzibar Namba 11 ya mwaka 2008 ili Taasisi itakayoshindwa kulipa fedha hizo kwa wakati kutozwa na faini.

### 5.2.3.6 Kutokuwepo kwa hesabu ya matumizi ya kawaida

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Shirika la Magazeti ya Serikali - Pemba linafanya matumizi mbali mbali ya Shirika lakini halina hesabu ya kupokea na kutoa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa shuhuli za Shirika kwa matumizi ya kawaida.

Aidha, imebainika kuwa fedha huhaulishwa kutoka ofisi kuu ya Shirika Zanzibar na kuingizwa katika hesabu ya mtu binafsi kwa ajili ya matumizi ya Shirika au fedha hizo hurushwa kwa njia ya miamala ya simu ya mtu binafsi na kufanya matumizi kwa shirika jambo ambalo ni kinyume na miongozo ya fedha za Umma. Hali hii inaweza kupelekea upotevu wa fedha za Serikali.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Shirika la Magazeti – Pemba kuharakisha ufunguaji

wa hesabu ya matumizi ya kawaida kwa lengo la kuepuka kujitokeza kwa hasara ya upotevu wa fedha pamoja na kukosekana kwa kumbukumbu za mapokezi na matumizi ya fedha.

**Majibu**

Shirika la Magazeti ya Serikali linakiri kutokuwepo kwa Hesabu ya Matumizi kwa upande wa Pemba. Hali hii imetokana na kukosekana kwa mhasibu, Mshika fedha au Karani Hesabu na kukosekana kwa muundo wa shirika. Kwa vile Shirika bado kwa wakati huo lilikuwa Muundo wake haujakamilika, hivyo upande wa Pemba walikuwa wanapatiwa Fedha za matumizi madogo madogo kuanzia shilingi 100,000/= hadi 200,000/=, kwa mujibu ya maombi yao na kuhakikiwa na afisa masuuli wanapokamilisha matumizi hayo. Fedha hizi(Petty Cash) alikua akipatiwa mkuu wa shirika la magazeti Pemba.

Shirika ingefungua Hesabu nyengine Pemba, ingelipelekea kupata gharama za utunzaji wa hesabu za kila mwezi ambapo hesabu hio ilikuwa haina matumizi makubwa na matumizi yote makubwa kwa upande wa Pemba yalikuwa yanafanywa na kusimamiwa katika Ofisi kuu ya Shirika Unguja.

Kwa sasa shirika imeshakamilisha ufunguaji wa hesabu Pemba na Kupatiwa Akaunti nambari 0833640001 na inaendelea kufuatilia ombi la kupatiwa mhasibu. Aidha muundo wa shirka umeshakamilika, muundo huu utatoa fursa kwa ofisi za Pemba kufanya matumizi yao yote.

**Uchunguzi wa Kamati**

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC ilielezwa yafuatayo:

1. Shirika la Magazeti lilitumia njia hiyo baada ya Wizara ya Fedha na Mipango kuwaelekeza wasifungue hesabu kwa kuwa kiwango cha fedha ni kidogo, hivyo, sio busara kuwa na hesabu nyingi za benki kwa lengo la kuepusha udanganyifu.

   Kamati ya LAAC ilitaka kuthibitishiwa hilo kwa kupatiwa barua husika, hata hivyo, Shirika la Magazeti liliieleza Kamati kuwa maelekezo hayo yalitolewa kwa njia ya mdomo jambo ambalo ni kinyume na taratibu za kiofisi.
2. Utaratibu wa kurusha fedha kwa kutumia simu ya Mkuu wa Taasisi hiyo ulianza kutumika tokea mwaka 2014. Kamati ya LAAC ilishtushwa na taarifa hiyo kwa kuwa ni miaka mingi imepita bila ya Mkaguzi Mkuu kubaini jambo hilo.
3. Matumizi ya Shirika kwa upande wa Pemba hujumuishwa kwenye kifungu cha "Sundry" ndio maana hayaonekani moja kwa moja kwenye Taarifa ya Hesabu za Mwisho wa Mwaka.

**Mapendekezo ya Kamati**

Ili kasoro kama hizo zisijitokeze tena Kamati ya LAAC ilipendekeza yafuatayo:

1. Shirika la Magazeti kuhakikisha kuwa wanaandaa “petty cash” kwa ajili ya matumizi ya Pemba na hatimae kupatiwa fedha hizo mhusika mkononi na sio kurushiwa kwenye simu.
2. Taasisi za Serikali ziwasiliane kwa maandishi na sio kwa mdomo ili kuwa na kumbukumbu ya kudumu kwa kile kilichoamulika.

### 5.3.3 MAMLAKA YA UNUNUZI NA OUNDOSHAJI WA MALI ZA UMMA ZANZIBAR (ZPPDA)

#### Taarifa ya Mapato

Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kupokea jumla ya shilingi 1,936,300,000 kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina kwa ajili ya kazi za kawaida. Aidha, Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma Zanzibar ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 325,000,000 kutoka vyanzo vyake vya ndani vya mapato.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma Zanzibar ilipokea jumla ya shilingi 1,033,555,223 kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina kwa ajili ya kazi za kawaida sawa na asilimia 47 wa makadirio. Aidha, Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma Zanzibar ilikusanya jumla ya shilingi 182,145,003 kutoka vyanzo vyake vya ndani vya mapato sawa na asilimia 56 ya makadirio.

#### Majibu
Mamlaka ilikuwa na kianzio kimoja tu cha mapato ambacho ni usajili wa wafanyabiashara usajili ambao ni wa hiari na kutokana na maradhi ya Uviko 19 shughuli nyingi zilisita.

#### Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati
Kamati ya LAAC iliridhika na majibu ya Mamlaka kwa kuwa kitendo cha Mfanyabiashara kujiandikisha ni cha hiari na ulazima wake hujitokeza endapo Mfanyabiashara husika ataamua kufanya biashara na Serikali.

#### Taarifa ya Matumizi

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma Zanzibar ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 2,261,300,000 kwa ajili ya kazi za kawaida. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma Zanzibar ilitumia jumla ya shilingi 1,219,933,862 kwa ajili ya kazi za kawaida sawa na asilimia 53.95 ya makadirio.

#### Majibu

Kutokana na ufinyu wa fedha Mamlaka ilishindwa kutekeleza mambo yafuatayo:

1. Uzinduzi wa mkataba wa huduma;
2. Mafunzo ya kupambana na rushwa;
3. Kukosa usafiri;
4. Mchakato wa ajira;
5. Kufanya mafunzo ya Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma kwa Taasisi nunuzi;
6. Kufanya mafunzo ya Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi;
7. Kuzipitia nyaraka za ukaguzi na uchunguzi wa manunuzi; na
8. Kutayarisha vipindi vya TV.

## 5. MAFANIKIO

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kutokana na ufinyu huo wa fedha zilizoingizwa Mamlaka ilishindwa kutekeleza shughuli zake ipasavyo, hivyo, Kamati ya LAAC inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa inaziingizia Taasisi zake fedha za kutosha ili ziweze kufikia malengo iliyojipangia.

MATOKEO YA UCHUNGUZI

### 5.3.3.1 Kasoro katika malipo ya muda wa ziada (overtime) shilingi 8,169,036

Kwa mujibu wa kifungu nambari 57(2) cha Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2014, kazi itakayolazimika kufanywa katika muda wa saa za ziada na ikapelekea kulipwa posho la kufanya kazi hiyo lazima ipatikane idhini ya Katibu Mkuu au Mkuu wa Taasisi kabla ya kazi hiyo kufanyika.

## 6. CHANGAMOTO

Ukaguzi umebaini kwamba Mamlaka imefanya malipo ya posho la muda wa ziada (overtime) kwa ajili ya kuwalipa watumishi mbalimbali wa Mamlaka ambapo taratibu za kiutumishi hazikuthibitika kukamilika ikiwemo kupatikana kwa idhini ya Mkuu wa taasisi (Mkurugenzi Mtendaji) kabla ya kazi hizo kufanyika pamoja na idhini ya Mkuu wa Kitengo kuthibitisha muda na siku kazi hizo zimefanyika.

Uwepo wa kasoro zilizobainika hapo juu kunapelekea udhibiti dhaifu katika malipo ya posho la muda wa ziada.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma kuhakikisha kuwa wanafuata Sheria Nambari 2 ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2011 pamoja na kanuni zake katika malipo yanayohusu stahiki za watumishi wa Mamlaka.

**Majibu**

Taratibu zote za ulipaji wa malipo ya ziada zilifuatwa isipokuwa idhini ya Mkuu Idara/Kitengo na ya Mkuu wa Taasisi kabla ya kufanyika kazi hizo. Hii ni kutokana na

uelewa mdogo waliokuwa nao watendaji juu ya taratibu hizo.

Mamlaka inakiri kutokea dosari hii, inahakikisha kuiondoa dosari hiyo na Sheria za Utumishi zitafuatwa kikamilifu. Miongozo imeshatolewa kwa wafanyakazi kuhusu utaratibu wa kufutwa wakati wa kufanyakazi katika muda wa ziada.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**
Katika kufuatilia hoja hii, Kamati ya LAAC iliyapitia Madokezo mbali mbali na kujiridhisha kuwa hakukuwa na ombi la ruhusa ya kufanya kazi husika, isipokuwa kwamba, madokezo hayo moja kwa moja yaliomba kuidhinishwa kwa posho.

Kutokana na kasoro hiyo Kamati ya LAAC imewataka Watendaji wa Mamlaka kuhakikisha kuwa wanafuata taratibu zilizopo ili kuepuka hoja zisizo na msingi.

## MAMLAKA YA UNUNUZI NA OUNDOSHAJI WA MALI ZA UMMA ZANZIBAR (ZPPDA) – PEMBA

### 5.3.3.2 Malipo kwa Watoa huduma ambao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma shilingi 1,520,000

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(1) cha Sheria ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma kinaeleza kulingana na masharti ya sheria hii mtu, kampuni au taasisi haitawasilisha zabuni au vyenginevyo kushiriki katika manunuzi ya Umma isipokua chombo kiwe kimesajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi.

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(2), zabuni kutoka kwa mtu, kampuni au chombo ambacho hakijasajiliwa haifai na hakitazingatiwa na taasisi ya ununuzi.

Ukaguzi umebaini kwamba Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Pemba imefanya manunuzi na watoa huduma mbali mbali ambao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya Zanzibar.

Kufanya hivyo kunapelekea kuikosesha Serikali mapato ambapo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

**Majibu**
Mfanyabiashara huyu wa chakula alisajiliwa kisheria lakini lilitokea tatizo la kimfumo wa malipo jambo ambalo lilikuwa liko nje ya uwezo wa Mamlaka na kupelekeza kutoonekana kwenye orodha kwa wakati huo, lakini tayari alikuwa keshajisajiliwa Mamlaka.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**
Katika kufuatilia hoja hii, Kamati ya LAAC ilijiridhisha kuwa Mfanyabiashara huo

alisajiliwa na Mamlaka. Kamati hii ilijiridhisha hilo baada ya kukagua Cheti cha Usajili cha Mfanyabiashara huyo kilichotolewa na Mamlaka pamoja na kukagua barua ya tarehe 02 Februari, 2020 yenye kumbukumbu Namba BG.89/403/03/30 inayohusiana na maombi ya Mamlaka kuomba mhusika kuingizwa katika mtandao wa IFMs wa Wizara ya Fedha, kwa mnasaba huo, Kamati ya LAAC imeifuta hoja hiyo.

#### 5.3.3.3 Hati za Malipo zenye vielelezo pungufu shilingi 2,230,000

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 2,230,000 zimelipwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Pemba kwa matumizi mbali mbali lakini baadhi ya vielelezo husika havikupatikana kwa ukaguzi ili kuweza kuthibitisha uhalali wa matumizi hayo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

**Majibu**

Mamlaka ya ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma Pemba ilifanya malipo kwa wafanyakazi na yote yalikuwa yana vielelezo husika vikiwemo orodha za mahudhurio inawezekana wakati wa ukaguzi muhusika hakuviona.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Baada ya majadiliano ya kina na Watendaji wa Mamlaka, Kamati ya LAAC ilikagua hati za malipo na kutokuridhika na hati hizo pamoja na maelezo ya Mamlaka, hivyo, hoja hii imebaki kama ilivyo.

#### 5.3.3.4 Kutokuthibitishwa kwa mtumishi aliyekaimu nafasi kwa kipindi kirefu

Kwa mujibu wa kifungu nambari 20(6) cha kanuni za utumishi wa Umma ya Zanzibar ya mwaka 2014 inasema kuwa “Kwa kuzingatia masharti ya kifungu hiki hakuna nafasi ya kukaimu zaidi ya muda wa miezi kumi na mbili (12) mfululizo kutoka tarehe ya uteuzi wa kukaimu isipokuwa muhusika atathibitishwa katika wadhifa huo au mwenye dhamana atakaporejea”.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba kwa mujibu wa barua yenye kumbukumbu namba AC.161/383/01/70 ya tarehe 22/07/2019 kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka Unguja ambayo inamtaka Mratibu wa Ofisi ya Mamlaka Pemba kukaimu nafasi hiyo, lakini uthibitisho wa nafasi anayoikaimu haujatolewa hali ambayo inayopelekea uwezekano wa kukosekana kwa haki za mtumishi huyo katika kipindi kirefu cha kukaimu kwake.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu cha Kanuni ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2014 nilichokinakili hapo juu.

**Majibu**
Kutothibitishwa kwa mfanyakazi huyo ni kutokana na kutokuwepo kwa Bodi ya Wakurugenzi kwa muda mrefu. Bodi mpya imeshatangazwa na miongoni mwa vipaumbele ni kuthibitishwa kwa Mtumishi huyo.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**
Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC imebaini kuwa Mamlaka ilikuwa haina Bodi ya Wakurugenzi kwa muda wa miaka miwili Bodi ambayo pamoja na mambo mengine ndio yenye mamlaka ya kutekeleza suala hilo. Hivyo, Kamati ya LAAC imekubaliana na majibu ya Mamlaka na hoja hii imefutwa.

Pamoja na kufutwa kwa hoja hii, Kamati ya LAAC inapendekeza kwa Serikali kuhakikisha kuwa inateua Bodi mpya mara tu inapokamilisha muda wake Bodi iliyopo ili kuepusha hoja zisizo na msingi.

Vile vile, Kamati ya LAAC inazishauri Taasisi za Umma kutoa taarifa za kukamilisha muda Bodi husika mapema kunakohusika ili mamlaka husika iweze kuchukua hatua haraka iwezekanavyo.

### 5.3.3.5 Dosari katika orodha ya wasambazaji na watoa huduma waliosajiliwa

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Pemba inasimamia utaratibu wa ununuzi na usajili wa wasambazaji pamoja na kuhakikisha kwamba taasisi zinapata orodha halisi na sahihi za watoa huduma pamoja na wasambazaji waliosajiliwa katika kipindi cha mwaka husika. Dosari zilizobainika ni kama ifuatavyo:-

- Baadhi ya watoa huduma na wasambazaji wa bidhaa kutokuonekana katika orodha iliyotolewa na mamlaka pamoja na kwamba wasambazaji hao wamekamilisha utaratibu wa usajili.

- Baadhi ya watoa huduma na wasambazaji wa bidhaa ambao hawakukamilisha taratibu za usajili kuonekana katika orodha halisi iliyotolewa na Mamlaka katika kipindi cha mwaka husika.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

**Majibu**
Mamlaka haikuwa na uwezo wa kuwaingiza watoa huduma hao katika mfumo wa malipo. Ililazimu majina ya watoa huduma yapelekwe Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango Unguja ili kuingizwa katika mfumo wa malipo jambo ambalo lilichelewesha kutolewa kwa orodha watoa huduma hao. Mamlaka inathibitisha kwamba tatizo hili

limeshatatuliwa na usajili wa watoa huduma katika mfumo wa malipo unafanyika kwa haraka katika Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango Pemba.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya LAAC imekubaliana na hoja ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, hata hivyo, Kamati iliifuta hoja hii kwa kuwa Mamlaka ya Manunuzi ilitekeleza wajibu wake kwa kuwasilisha maombi ya kuingizwa kwenye mfumo wa IFMs Wafanyabiashara huko Wizara ya Fedha na Mipango. Isipokuwa kwamba, Wizara ya Fedha na Mipango haikutekeleza wajibu wake huo kwa wakati na kupelekea kubainika kwa hoja hii.

Pamoja na juhudi zilizochukuliwa na Mamlaka za kubadilisha utaratibu wa usajili wa Wafanyabiashara, Kamati ya LAAC inapendekeza kwa Serikali kuhakikisha kuwa inapoanzisha jambo inaweka utaratibu mwepesi wa utekelezwaji wa jambo husika ili kuepusha usumbufu wa Watendaji wa Serikali pamoja na Wadau wake.

#### 5.3.3.6 Kutokufikia malengo ya ukusanyaji wa mapato ya shilingi 85,250,000

Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Pemba ilikadiriwa kukusanya shilingi 85,250,000 kupitia katika vyanzo vyake mbali mbali vya mapato kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30, Juni 2021.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba mapato halisi hadi kufikia tarehe 30 Juni 2021 ofisi iliweza kukusanya shilingi 17,643,000 tu ambazo ni sawa na asilimia 20.70 ya fedha zilizokadiriwa ikiwa na upungufu wa shilingi 67,607,000 ambapo ni kushindwa kufikia malengo ya ukusanyaji wa mapato kama ilivyokusudiwa.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

**Majibu**

Lengo la ukusanyaji wa mapato halikufikiwa kutokana na janga la maradhi ya Uviko 19 lililosababisha kupungua kwa mzunguko wa biashara nchini, na hivyo kukosa watoa huduma wa kutosha wa kujisajili.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya LAAC ilikubaliana na hoja ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, hata hivyo, Kamati hii imeifuata hoja hiyo kwa kuwa iliridhika na majibu ya Mamlaka. Hii ni kutokana na kuwa katika mwaka huo wa fedha Mamlaka ilikuwa na kianzio kimoja tu cha mapato ambacho sio cha kuaminika sana kwa kuwa kitendo cha Mfanyabiashara kujiandikisha ni cha hiari na ulazima wake hujitokeza endapo Mfanyabiashara husika ataamua kufanya biashara na Serikali.

### 5.4.2 MAMLAKA YA USAFIRI BAHARINI (ZMA)

**Taarifa za Mapato**
Mamlaka ya Usafiri wa Baharini kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 3,350,419,962 kutoka kwenye vyanzo vyake vya ndani vya mapato. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Mamlaka ya Usafiri wa Baharini ilikusanya jumla ya shilingi 2,519,379,366.8 kutoka vyanzo vyake vya mapato ya ndani sawa na asilimia 75.2 ya makadirio.

**Majibu**
**a. Vyanzo vya Mapato**
Mamlaka ya Usafiri Baharini imekusanya mapato kupitia vyanzo mbali mbali ambavyo ni; Mapato yanayotokana na vyanzo vya usajili wa meli za ndani, Mapato yanayotokana na masuala ya bahari, na Mapato yanayotokana na vyanzo vya usajili wa meli za kimataifa.

**b. Makusanyo ya Mapato kupitia Vyanzo Mbalimbali**

Katika mwaka wa fedha 2020/2021, Mamlaka ya Usafiri Baharini ilipanga kukusanya jumla ya TZS 3,350,419,962 ambapo hadi kufikia Juni, 2021 Mamlaka imekusanya jumla ya TZS 2,519,379,366.80. Fedha hizo zilipatikana kutoka vianzio mbali mbali sawa na asilimia 75 ya makadirio.

Kutofikia malengo ya kukusanya mapato hayo, kulisababishwa na kuibuka kwa ugonjwa wa UVIKO 19 ambapo shughuli nyingi za kiuchumi zilisimama kwa dunia nzima ikiwemo visiwa vya Zanzibar.

**MAPATO YALIYOKUSANYWA KWA KIPINDI CHA JULAI, 2020 – JUNI, 2021 KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021**

| Nam. | Vyanzo vya makusanyo | Makisio ya Mapato kwa Mwaka | Makusanyo halisi kwa Mwaka | Asilimia ya Makusanyo kwa Mwaka |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Mapato yanayotokana na vyanzo vya usajili wa meli za ndani | 592,867,806 | 428,986,265 | 72 |
| 2. | Mapato yanayotokana na masuala ya bahari | 1,768,552,156 | 906,148,149 | 51 |

| Nam. | Vyanzo vya makusanyo | Makisio ya Mapato kwa Mwaka | Makusanyo halisi kwa Mwaka | Asilimia ya Makusanyo kwa Mwaka |
|---|---|---|---|---|
| 3. | Mapato yanayotokana na vyanzo vya usajili wa meli za kimataifa | 989,000,000 | 1,184,244,953 | 120 |
| **JUMLA KUU** | | **3,350,419,962** | **2,519,379,367** | **75** |

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC ilibaini kuwa bado Mamlaka hii haijaanza kukusanya tozo ya mafuta kwa meli zinazoingia Zanzibar kama kanuni ya 4 ya Kanuni za Tozo zilizotungwa chini ya kifungu cha 491 cha Sheria Namba 5 ya mwaka 2006 kinavyoelekeza.

Kwa kuwa Serikali inajitahidi kubuni vianzio mbali mbali vipya vya mapato ili Zanzibar iondokane na tabia ya kuwa na bajeti tegemezi. Hivyo basi, Kamati ya LAAC inapendekeza kwa Serikali kuiruhusu Mamlaka hii kuanza kukusanya tozo hiyo kwa kuwa Mamlaka ya Usafiri Baharini ndio Taasisi yenye jukumu la kuhifadhi mazingira ya bahari na zipo baadhi ya meli hutokea kuchafua mazingira kwa kudondosha mafuta baharini, lakini pia, suala la kukusanya tozo hiyo lipo Kisheria na Kikanuni.

Sambamba na hilo, Kamati ya LAAC imependekeza kwa Mamlaka hii kulifanyia marekebisho jina la kianzio cha mapato yanayotokana na usajili wa meli za kimataifa kwa kuwa kianzio hicho kinahusisha pia na huduma zinazotolewa kwa meli hizo ili kiendane na uhalisia huo.

**Taarifa za Matumizi**

Mamlaka ya Usafiri wa Baharini kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 3,335,462,280.00 kwa ajili ya kazi za kawaida. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Mamlaka ya Usafiri wa Baharini ilitumia jumla ya shilingi 2,387,364,747.00 kwa ajili ya kazi za kawaida sawa aslimia 71.58 makadirio.

**Majibu**

Mamlaka ya Usafiri Baharini ilifanya matumizi kupitia shughuli mbali mbali ambazo ni; Kuwapatia maslahi wafanyakazi, kusimamia huduma za utawala na fedha, kuwepo kwa Usalama wa Usafiri wa baharini Kitaifa na Kimataifa na kuwepo kwa usalama na ulinzi wa mazingira ya baharini.

MATUMIZI YALIYOFANYIKA KWA KIPINDI CHA JULAI, 2020 – JUNI, 2021

| Nam. | Shughuli Makhsusi | Makisio ya Fedha kwa Mwaka | Fedha zilizopatikana | Asilimia ya Fedha kwa Mwaka |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Kuwapatia maslahi wafanyakazi | 1,828,761,720 | 1,463,773,689 | 80 |
| 2. | Kusimamia huduma za utawala na fedha | 1,198,123,060 | 711,916,850 | 59 |
| 3. | Kusimamia Usalama wa Usafiri wa baharini Kitaifa na Kimataifa | 204,792,500 | 138,988,318 | 68 |
| 4. | Kusimamia usalama na ulinzi wa mazingira ya baharini | 103,785,000 | 72,685,890 | 70 |
| **JUMLA KUU** | | **3,335,462,280** | **2,387,364,747** | **72** |

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC iliridhika na maelezo ya Mamlaka juu ya matumizi mbali mbali iliyofanywa na Mamlaka. Hata hivyo, Kamati hii haikuridhishwa na Muundo wa Mamlaka ya Usafiri Baharini na katika kupata maelezo ya kina juu ya suala hili Kamati ya LAAC ilielezwa kuwa Mamlaka iliufanyia marekebisho Muundo huo na kuuwasilisha Kamisheni ya Utumishi wa Umma ambapo Kamisheni hiyo ilitoa mapendekezo yake na kufanyiwa kazi na Mamlaka. Cha kusikitisha, tarehe 15 Agosti, 2022 Mamlaka ilipokea barua yenye kumbukumbu Namba OR/UT/KUU/36/56/VOL.1/17 kutoka kwa Kamisheni hiyo na kueleza kuwa Mamlaka iendelee kutumia Muundo ulioidhinishwa na Serikali.

Kamati ya LAAC haikuridhishwa na maelekezo hayo kwa kuwa Muundo wa Mamlaka ya Usafiri Baharini uliopo hivi sasa hauendani na hali halisi iliyopo jambo linalopelekea kuwa na tofauti kubwa ya ulipaji wa stahiki baina ya Watendaji wa Mamlaka.

Kutokana na dosari hiyo, Kamati ya LAAC inapendekeza kwa Serikali kuliangalia tena suala hilo ili haki iweze kutendeka.

MATOKEO YA UKAGUZI

### 5.4.2.1 Kutokukusanywa kwa Mapato yanayotokana na tozo za Meli za mafuta na abiria

Kwa mujibu wa Jadweli nambari 33 la kanuni za "Maritime Transport (Fees and Charges)" za mwaka 2020, Mamlaka ya Usafiri Baharini inatakiwa kukusanya mapato yanayotokana na tozo ya meli za abiria na mafuta kwa mujibu wa viwango vilivyowekwa katika kanuni hizo. Ukaguzi umebaini kwamba Mamlaka haikusanyi mapato hayo kwa mujibu wa matakwa ya kanuni hizo.

Kutokukusanywa kwa mapato ya Mamlaka kwa mujibu wa sheria kunaweza kupelekea Mamlaka kushindwa kufikia malengo yake ya muda mfupi na muda mrefu iliyojiwekea.

Ukaguzi unashauri kwamba Mamlaka ya Usafiri Baharini ichukuwe hatua na juhudi kuhakikisha kwamba mapato yanakusanywa kwa mujibu sheria na kanuni husika ili kuisaidia kuongeza mapato ya Mamlaka na hatimae kufikia malengo yake. Aidha ukaguzi unashauri uongozi wa Mamlaka kufikiria kuzipitia tena kanuni za tozo mbalimbali za Mamlaka ili iweze kuzirekebisha kulingana na uwezekano wa utekelezaji wake.

#### Majibu

Kwa mujibu wa Sheria na Kanuni ya Ada na Tozo ya Mamlaka ya mwaka 2020 inaonesha kuwa Mamlaka inatakiwa ikusanye USD 3 kwa kila tani moja ya mafuta yanayoingizwa nchini na USD 0.6 kwa kila abiria anaesafiri kutoka ZNZ/DAR au UNGUJA/PBA/UNGUJA.

Katika kushindwa kutekeleza suala hili mambo yafuatayo yalijitokeza: -

i. Kupitia mashauriano baina ya Mamlaka pamoja na Kamishna wa ZRB, Waziri Ofisi Rais, Fedha na Mipango na Waziri wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi pamoja na Wadau wengine wa sekta ya Usafiri Baharini ambapo ilikubalika kuwa tozo ya abiria iendelee kama ilivyo, TZS 500 kwa ZNZ/DAR na TZS 250 UNGUJA/PBA/UNGUJA, licha ya Mamlaka kuomba itoze kwa mujibu wa Kanuni. Serikali ilitaka kuendelea na tozo hiyo kwa ajili ya kuwapunguzia wananchi mzigo.
ii. Kwa upande wa Tozo za Meli za mafuta, Mamlaka haijaruhusiwa kukusanya tozo hiyo.

#### Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Hoja hii imebaki kama ilivyo kwa kuwa tozo hizo hazikusanywi kama Kanuni inavyoelekeza. Hivyo, Kamati ya LAAC inapendekeza kwa Serikali kuiruhusu Mamlaka kukusanya tozo hizo kama Kanuni zinavyoelekeza na endapo itaendelea

kuona kuwa hakuna haja ya kutoza tozo hizo basi ni busara ikafidia tofauti ya fedha iliyopo ili Mamlaka iweze kupata mapato yake kamili kwa mujibu wa Kanuni yao.

#### 5.4.2.2 Tofauti kati ya kiasi cha mapato kilichorikodiwa katika daftari la mapato na kiasi kilichorikodiwa katika vitabu vya risiti.

Ukaguzi wa taarifa za mapato ya Mamlaka ya Usafiri Baharini kwa mwaka wa fedha 2020/2021 umebaini uwepo wa tofauti kati ya taarifa za mapato zilizorikodiwa katika daftari la fedha taslim (cash book) na taarifa zilizomo katika vitabu vya risiti vya Mamlaka.

Kutofautina kati ya kiasi cha mapato kilichorikodiwa katika daftari la mapato na kiasi kilichorikodiwa katika vitabu vya risiti kunatia shaka juu ya usahihi wa taarifa za mapato za Mamlaka na kunaweza kupelekea upotevu wa fedha za Mamlaka.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Mamlaka ya Usafiri Baharini kupitia na kulinganisha taarifa za mapato zilizorikodiwa katika daftari la mapato na zile zilizomo katika vitabu vya risiti ili kuweza kubaini tofauti baina yao na kufanyia kazi.

**Majibu**

Katika kupitia daftari la fedha, vitabu vya risiti pamoja na taarifa za benki, tuligundua kuwa ni kweli tatizo hili lilijitokeza kwa wakati huo, kwa upande wa daftari la fedha kurudiwa viwango ambavyo si sahihi kimakosa.

Mamlaka ilishafanya marekebisho hayo na kiwango ambacho ni sahihi ni USD 1000 badala ya USD 50 kwa upande wa hesabu nambari 0400660000 na TZS 359,000 badala ya TZS 615,000 kwa upande wa hesabu nambari 0404380000.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya LAAC imekubaliana na matokeo ya uchunguzi ya Mkaguzi Mkuu, pamoja na hayo, Kamati ya LAAC imewashauri Watendaji wa Mamlaka kuwa makini wakati wanatekeleza majukumu yao ili kuepusha hoja zisizo na msingi.

#### 5.4.2.3 Risiti za Mapato zilizorikodiwa zaidi ya mara moja katika daftari la fedha taslim

Ukaguzi wa taarifa za mapato ya Mamlaka ya Usafiri Baharini kwa mwaka wa fedha 2020/2021 umebaini uwepo risiti za mapato zilizorikodiwa zaidi ya mara moja katika daftari la fedha taslim ambapo baadhi ya risiti hizo zimejirudia rudia katika kiasi tofauti katika tarehe tofauti.

Kurikodi risiti moja zaidi ya mara moja katika daftari la fedha taslim kwa kiasi tofauti cha fedha kunatia shaka juu ya usahihi wa taarifa za mapato za Mamlaka na kunaweza kupelekea upotevu wa fedha za Mamlaka.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Mamlaka ya Usafiri Baharini kupitia taarifa za mapato

zilizorikodiwa katika daftari la mapato ili kuweza kurekebisha kasoro zilizobainika.

**Majibu**
Mamlaka illipitia daftari la fedha taslim na kurekebisha kasoro zote ambazo zilijitokeza kimakosa.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**
Kamati ya LAAC imekubaliana na matokeo ya uchunguzi ya Mkaguzi Mkuu, pamoja na hayo, Kamati ya LAAC imewashauri Watendaji wa Mamlaka kuwa makini wakati wanatekeleza majukumu yao ili kuepusha hoja zisizo na msingi.

#### 5.4.2.4 Kasoro zilizobainika Katika Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Mpango Mkakati Wa Mamlaka

Ukaguzi ulipitia mpango Mkakati wa Mamlaka ya Usafiri Baharini Zanzibar wa mwaka 2016/2017 hadi 2020/2021 pamoja na ripoti mbalimbali za uongozi za Mamlaka. Mpango Mkakati huo wa Mamlaka pamoja na mambo mengine ulikuwa na malengo Mkakati Makuu (Grand Strategic Objectives) ya aina mbili yaliyopangwa kwa ajili ya kusaidia Mamlaka kutekeleza na kufanikisha majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

Ukaguzi umebaini kutokufikiwa kwa baadhi ya malengo mkakati ambayo ni muhimu kwa ajili ya kuboresha ufanisi wa utendajii kazi wa Mamkala ikiwemo:-

1. Kukosekana kwa mfumo wa kielektroniki kwa ajili ya kazi za kiuhasibu.
2. Kukosekana kwa wa daftari la vihatarishi (risk mitigation na management register).
3. Kutokuwepo kwa miongozo inayoelekeza utoaji elimu za mabaharia iliyotayarishwa.
4. Kutokufanya ukaguzi wa miradi inayoendeshwa baharini ili kuhakikisha kwamba. inafuata kanuni na taratibu za ulinzi wa mazingira ya bahari.
5. Kutokuanzisha sera na mkakati mawasiliano.
6. Kutokufanyika kwa tathmini ya utendaji kazi na upatikanaji wa huduma kwa wateja (customer satisfaction survey).
7. Kutokuanzishwa kwa mfumo wa usimamizi wa viwango (Quality management system).

Kutokufikiwa kwa malengo yaliyomo katika Mpango Mkakati wa Mamlaka kunapelekea Mamlaka kukosa ufanisi katika utekelezaji wa mpango mkakati wake na kunaweza kuathiri kufikia malengoyake ya muda mrefu.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Mamlaka ya Usafiri Baharini kuhakikisha kuwa unafuatilia kwa karibu utekelezaji wa malengo yaliyomo katika mpango mkakati wa

Mamlaka ili kuweza kufikia malengo yake ya muda mrefu kwa ufanisi.

**Majibu**

Mamlaka inajitahidi kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa mpango mkakati kwa mujibu wa malengo iliyojiwekea sambamba na kuyapitia malengo hayo kila mwaka. Juhudi za utekelezaji wa malengo hayo ni kama ifuatavyo: -

1. **Kukosekana kwa Mfumo wa Kieletroniki kwa ajili ya kazi za kiuhasibu**
   Mamlaka inatumia Mfumo wa Kielectroniki kwa ajili ya kazi za kiuhasibu ikiwemo Biling System, Vocha payment na Salary Payment System. Aidha ipo katika taratibu za kutafuta mfumo bora wa kisasa wa kiuhasibu.
2. **Kukosekana kwa daftari la Vihatarishi**
   Mamlaka ilichukua juhudi ya kuwapatia mafunzo watendaji na bodi ya wakurugenzi yanayohusiana na vihatarishi na kwa sasa Mamlaka ipo katika hatua ya kutafuta mtaalam wa kutayarisha daftari la vihatarishi.
3. **Kutokuwepo kwa miongozo inayoelekeza utoaji wa elimu za mabaharia iliyotayarishwa**
   Mamlaka tayari inayo miongozo ya mabaharia inayoelekeza masuala yote ya mabaharia ambayo ni; ''The Inquiry of Conduct of Seafarers Regulations'', ''Safe Manning Regulations,'' '' The Repatriation and Relief of Seafarers Regulations,'' Seafarers Medical Examination Regulations; and The Seafarers Engagement Regulations.
4. **Kutokufanya ukaguzi wa miradi inayoendeshwa baharini ili kuhakikisha kwamba inafuata kanuni na taratibu za ulinzi wa mazingira ya bahari**
   Kwa hivi sasa, miradi yote inayohusu sekta ya bahari tunashirikishwa kikamilifu na ZIPA na kuitolea miongozo kuhusiana na suala la usalama, ulinzi na udhibiti wa mazingira. Aidha Mamlaka inafanya ukaguzi kwa miradi hiyo.
5. **Kutokuanzisha sera na mkakati wa mawasiliano**
   Mamlaka ipo katika taratibu ya kumtafuta mtaalamu wa kuifanya kazi, na tayari tuliishaipangia bajeti kwa mwaka huu wa fedha 2022/2023.
6. **Kutokufanyika kwa tathmini ya utendaji kazi na upatikanaji wa huduma kwa wateja**
   Mamlaka inafanya tathmini za utendaji na kuhusu upatikanaji wa huduma kwa wateja tayari tumeshaweka kisanduku cha maoni. Na kwa sasa maoni tunayapata kwa kupitia kisanduku hicho.
7. **Kutokuanzishwa kwa mfumo wa usimamizi wa viwango (Quality Management System)**
   Mamlaka ipo katika hatua ya kutafuta mtaalamu wa kuifanya kazi hiyo, pia itategemea upatikanaji wa fedha na kuingizwa katika mpango mkakati mpya unaotayarishwa 2023/2024.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya LAAC imekubaliana na matokeo ya uchunguzi ya Mkaguzi Mkuu, hata hivyo, Kamati ya LAAC imeifuta hoja hiyo kwa kuwa Mamlaka imeanza kuchukua

hatua mbali mbali dhidi ya hoja hii.

Pamoja na hayo, Kamati ya LAAC imeishauri Mamlaka kuhakikisha kuwa inatekeleza shughuli zake kwa mujibu wa mpango mkakati wake ili kuepusha hoja zisizo za lazima.

### 5.4.2.5 Dosari katika daftari la kuhifadhia Mali za kudumu

Kwa mujibu wa kifungu nambari 29(2) cha sheria nambari 12 ya Usimamizi wa fedha nambari 12 ya mwaka 2016, Afisa masuuli anahusika na kusimamia mali za Taasisi ya Umma ikiwemo kutunza daftari la mali zote zilizopo chini ya udhibiti wa taasisi yake.

Daftari la kuhifadhia mali za kudumu huonyesha taarifa muhimu kuhusiana na mali za kudumu za taasisi husika ikiwemo aina ya mali, sehemu ilipo, tarehe iliyonunuliwa au kuuzwa, thamani ya mali, pamoja na mambo mbali mbali yanayohusiana na mali (assets).

Ukaguzi umebaini kuwa jengo la Mamlaka linalotumiwa kama ofisi kuu halikuorodhoreshwa katika daftari la mali za kudumu la Mamlaka.

Kutokuliingiza jengo la Mamlaka katika orodha ya mali za kudumu za Mamlaka kunapelekea taarifa ya fedha ya mwisho wa mwaka ya Mamlaka kutokuonyesha sura sahihi na halisi.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Mamlaka kuingiza jengo hilo linalotumiwa kama ofisi kuu katika orodha ya mali za kudumu za Mamlaka kwa vile limekidhi sifa ya kutambuliwa kama ni mali ya kudumu ya Mamlaka.

**Majibu**
Mamlaka tayari imeshaliingiza jengo lake katika orodha ya mali za kudumu.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**
Kamati ya LAAC imekubaliana na matokeo ya uchunguzi ya Mkaguzi Mkuu, hivyo, hoja hii imebaki kama ilivyo na imeishauri Mamlaka kuendelea kufuatilia hati miliki ili kuwa na umiliki halali wa jengo hilo.

### 5.4.2.6 Kuwepo kwa uhaba wa vitendea kazi
Ukaguzi umebaini kwamba Mamlaka ya Usafiri Baharini haina vifaa vya kutosha kwa ajili ya kusaidia Mamlaka kutekeleza majukumu yake ya msingi. Baadhi ya vifaa ambavyo Mamlaka haina ni kama ifuatavyo:-

- Vituo vya uokozi (Marine operating center) vyenye vifaa vya kutosha.
- Patrol boat.

- Vifaa na wataalam wa kupambana na uchafuzi wa mazingira (mfano umwagikaji wa mafuta baharini).

Kuwepo kwa uhaba wa vitendea kazi kunapelekea kupunguza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Mamlaka ya Usafiri Baharini kuhakikisha kunapatikana vitendea kazi muhimu kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya Mamlaka kwa ufanisi.

**Majibu**

1. Mamlaka ya Usafiri Baharini haihusiki na majukumu ya Utafutaji na Uokozi (Search and Rescue-SAR) majukumu haya yanasimamiwa na Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM) ambapo hadi sasa kuna vituo 3 vya Utafutaji na Uokozi (Search and Rescue Centres). Vituo hivyo kwa Unguja vipo Kibweni na Nungwi na kwa upande wa Pemba kipo Mkoani.

2. Mamlaka ya Usafiri Baharini inahusika na Kituo cha Ufuatiliaji wa Nyenendo za Vyombo Baharini (Marine Operating Centre - MOC) ambapo, moja kati majukumu ya Kituo hicho ni kufuatilia mwenendo wa meli (Identification and Tracking) na tayari kimeshaanza kutumia mfumo wa 'Fleet Moon' kwa kufungwa vifaa vyake katika minara iliyopo Makunduchi, Kigomasha, Nungwi na Chumbe.

   Aidha, kwa kituo mahsusi, Mamlaka inatarajia kuanza ujenzi wa chumba cha kufuatilia mwenendo za vyombo vya baharini (MOC) katika robo ya tatu ya mwaka wa fedha wa 2022/2023.

3. Kwa upande wa 'Patrol Boat', Mamlaka imepanga kununua boti kwa mwaka wa fedha wa 2022/2023 ili kusaidia mambo mbali mbali yanayotokea katika bahari zetu.

   Boti hiyo inapendekezwa kuwa na vigezo 'specifications' zifuatazo:
   Type: Patrol, Safety na Rescue
   Material: Fiber Reinforced Plastic
   Length: 12m
   Breadth: 4m
   Propulsion/Engine Type: Propeller driven - HP
   Speed: 12 Knots Maximum
   Area of Operation: 24nm
   Cost: Tsh. 345,000,000

4. Mamlaka mpaka sasa haina vifaa vya kujikinga na kuzuia uchafuzi wa mazingira ya bahari kutokana na umwagikaji wa mafuta baharini ingawa imejiunga na taasisi binafsi iliyoundwa iitwayo 'OSMAG – Oil Spill Mutual Aid Group' inayohusisha wadau wote wa masuala ya baharini pamoja na Kampuni za mafuta ikiwa na lengo la kuunganisha nguvu ya pamoja kwa ajili ya ununuzi wa vifaa husika.

   Aidha, Serikali ilipata ufadhili wa Serikali ya Norway kupitia Mamlaka yake ya bahari ya 'NovuMare' na ulitayarishwa mpango wa kujikinga na kuzuia umwagikaji wa mafuta baharini (Zanzibar Marine Oil Spill Response Contingency Plan - ZMORCP) ambao hatukuwahi kukabidhiwa kutokana na kuzuka kwa maradhi ya Uviko 19.

   Sambamba na hayo, Mamlaka inaendelea na mpango wa kuajiri na kufundisha Wataalam, kwa kuwa idadi ya Wataalamu iliopo hivi sasa ni chache. Huu ni sehemu ya mpango wa utekelezaji wa urekebishaji wa mapungufu yaliyobainika katika ukaguzi wa IMO uliofanyika nchini mnamo mwezi wa Machi, 2019.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya LAAC imeifuta hoja hiyo kwa kuwa Mamlaka imeanza kuchukua hatua mbali mbali dhidi ya hoja hii.

Aidha, Kamati ya LAAC ilibaini kuwa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ameandika hoja ya Utafutaji na Uokozi kwa Mamlaka hii wakati Mamlaka haina jukumu hilo. Hivyo, Kamati ya LAAC inaishauri Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuwa makini inavyotekeleza majukumu yake ili iweze kutoa ambayo ni sahihi.

Pamoja na hayo, Kamati ya LAAC imeishauri Mamlaka kuhakikisha kuwa inafuata taratibu zote za ununuzi wa boti ya doria 'Patrol Boat' pamoja na kuzingatia vigezo vyote vilivyowekwa ili ipatikane tija iliyokusudiwa.

## MAMLAKA YA USAFIRI BAHARINI (ZMA) – PEMBA

### 5.4.2.7 Kutokuwepo kwa hesabu ya matumizi ya kawaida

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Mamlaka inawajibu wa kuendesha na kusimamia shughuli za Mamlaka kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Miongozo mbali mbali lakini Mamlaka haina hesabu ya matumizi ya kawaida hali inayopelekea kutumiwa fedha kwa njia isiyo rasmi.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma

nambari 12 ya mwaka 2016.

**Majibu**
Mamlaka imeona ni vyema matumizi yote yafanyike Ofisi Kuu Unguja ili kuimarisha udhibiti na usimamizi mzuri wa matumizi hayo.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**
Kamati ya LAAC imekubaliana na matokeo ya uchunguzi ya Mkaguzi Mkuu, hivyo, hoja hii imebaki kama ilivyo. Pamoja na hayo, Kamati hii imependekeza kwa Mamlaka kutumia njia ya hundi “Cheque” au “Transfer” kwa kuwa matumizi ya Afisi ya Pemba sio makubwa, hivyo, kufungua hesabu ya matumizi ni kuitia hasara zisizo na msingi Mamlaka kwa kuwa italazimika kuajiri baadhi ya Watendaji.

### 5.1.2 SHIRIKA LA BIMA ZANZIBAR (ZIC)

**Ufanisi katika Uendeshaji wa Shirika (Operating Performance)**

Katika ukaguzi uliofanyika umeweza kupima ufanisi katika shughuli za uendeshaji wa shirika kwakufanya tathmini kwa kipindi cha miaka miwili kwanzia mwaka wa fedha unaoishia tarehe 31 Disemba 2019 hadi tarehe 31 Disemba 2020 mambo yafuatayo yamebainika.

Ukaguzi umebaini mapato ya Shirika la Bima Zanzibar yameongezeka kutoka shilingi 19,853,482,000 kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 31 Disemba 2019 hadi kufikia shilingi 20,020,553,000 kwamwaka wa fedha unaoishia tarehe 31 Disemba 2020 kukiwa na ongezeko la shilingi 167,071,000 sawa na asilimia 0.8. Aidha, ukaguzi umebaini gharama za uendeshaji ziliongezeka hadi kufikia shilingi 17,661,618,000 kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 31 Disemba 2020 ukilinganishana shilingi 16,914,469,000 kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 31 Disemba 2019 ambayo ni ongezeko la shilingi 747,149,000 sawa na asilimia 4.4.

Kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 31 Disemba 2020 Shirika la Bima Zanzibar limepata faida ya shilingi 2,358,935,000 ukilinganisha na faida iliyopatikana kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe

31 Disemba 2019 ambayo ni shilingi 2,939,013,000 kukiwa na upungufu wa shilingi 580,078,000 sawa na asilimia 19.7, faida iliyoonekana hapo ilipatikana kabla ya kulipa ushuru.

Kwa upande wa faida baada ya tozo ya kodi imeonekana kupungua na kufikia shilingi 1,608,935,000 kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 31 Disemba 2020 ukilinganisha na faida ya shilingi 2,519,013,000 iliyopatikana kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 31 Disemba 2019 ambapo imefanya upungufu wa shilingi 910,078,000 sawa na asilimia 36.1.

Ukaguzi umebaini kujitokeza kwa ongezeko kubwa la gharama za uendeshaji kwa wastani wa asilimia 4.4 ikilinganishwa na ongezeko la mapato la wastani wa asilimia 0.8.

Kutokana na ongezeko la gharama za uendeshaji ikiwa vyanzo vya mapato vya shirika havikubainishwa vizuri na kuibua vyanzo vipya vya mapato na kushindwa kudhibiti matumizi yasiyoya lazima kunaweza kupelekea shirika kutofikia malengo waliyojipangia.

Aidha, kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 31 Disemba 2020 Shirika la Bima Zanzibar limefanyamalipo ya kodi kwa mujibu wa Sheria ya Kodi yenye thamani ya shilingi 750,000,000 ukilinganishana mwaka wa fedha unaoishia tarehe 31 Disemba 2019 ambapo Shirika la Bima lilifanya malipo ya shilingi 420,000,000 kukiwa na tofauti ya shilingi 330,000,000 sawa na asilimia 79.

Uwepo wa ongezeko la asilimia 79 la malipo ya kodi limepelekea kupunguza faida ya Shirika kwaasilimia 36.1 kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 31 Disemba 2020.

Vile vile, kwa mujibu wa taarifa za hesabu za Shirika la Bima la Zanzibar zinabainisha Shirika linatarajia kulipa gawio la faida kwa Serikali lenye thamani ya shilingi 804,467,000 kwa mwaka wa fedha unaoshia tarehe 31 Disemba 2020 ukilinganisha na gawio la shilingi 406,069,000 kwa mwaka wa fedha ulioshia tarehe 31 Disemba, 2019 ambapo ni sawa na wastani wa asilimia 98.1 ya ongezeko.

### Majibu

Ongezeko la matumizi limesababishwa na kuongezeka kwa Ujira wa mwaka na “Staff cost” ambazo ziliongezeka kwa mwaka wa 2020.

Ujira wa mawakala na madalali kwa mwaka 2020 inaonekana ulipanda na kusababisha matumizi kuwa juu hali hii ilitokana na kwamba biashara nyingi kwa mwaka 2020 zilifanywa kupitia madalali na mawakala na ndio sababu ambayo imepelekea kupanda kwa gharama za matumizi za afisi.

“Staff cost” gharama za mishahara na stahiki za wafanyakazi ziliongezeka kutokana na kupanda kwa mishahara ya wakurugenzi na mameneja hali ambayo imepelekea kuzidisha matumizi ya Shirika ukilinganisha na mwaka 2019 kwa asilimia ambayo imeoneshwa na mkaguzi.

Kupungua kwa faida kwa mwaka 2020 ukilinganisha na mwaka 2019 kumetokana na kuongezeka kwa yafuatayo:-

i. Uendeshaji na gharama nyenginezo (Operating and other expense).

ii. Gharama za wafanyakazi

iii. Uchakavu wa thamani (Depreciation of asset)
iv. Kodi za ada za bima na leseni (Premium tax and License).

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC ilibaini yafuatayo:

1. Ujira wa Mawakala na Madalali katika mwaka husika ulipanda kwa kuwa shughuli nyingi zenye mapato makubwa zilifanywa na Mawakala na Madalali badala ya Shirika la Bima.
2. Ripoti ya Mkaguzi wa Hesabu za Ndani haioneshi taarifa ya mapato na matumizi ya Shirika jambo ambalo litapelekea kushindwa kupima utendaji wa Shirika kwa mujibu wa kanuni ya 141(a) na (j) ya Kanuni za Usimamizi wa Fedha za mwaka 2021.

   Hii ni kutokana na kuwa kifungu cha 116 cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha ya mwaka 2016, kimempa mamlaka Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Ndani kupitia, kutathmini na kutoa mapendekezo juu ya mfumo wa mapato na matumizi ya Serikali kwa uwajibikaji.

3. Shirika la Bima haliwasilishi Ripoti ya Mkaguzi wa Hesabu za Ndani ya kila mwaka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kama kifungu cha 117(6) cha Sheria ya Fedha kinavyoelekeza.

Kutokana na dosari hizo zilizojitokeza Kamati ya LAAC ililishauri Shirika la Bima kufuata masharti ya Sheria zilizopo ili kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria na kuepuka kupata hoja zisizo na msingi.

**Ufanisi katika Utendaji wa Kifedha (Financial Performance)**

Katika kupima ufanisi wa utendaji katika masuala ya kifedha, ukaguzi umeangalia mlinganisho wa msimamo wa mtaji (Position of Working Capital) wa Shirika la Bima Zanzibar kwa muda wa miaka miwili ambapo mambo yafuatayo yamebainika.

Ukaguzi umebaini utendaji wa kifedha wa Shirika la Bima Zanzibar umeimarika ingawa haujakidhi vigezo vinavyotakiwa kiuhasibu vya uwezo wa shirika kumudu madeni ya muda mfupi kwa uiwano wa 2:1 ambapo imeonekana uwezo wa shirika kumudu dhima za mpito umefikia 1.14 : 1 kwa mwaka unaoshia tarehe 31 Disemba 2020 ukilinganisha na uwiano wa 1.06 : 1 kwa mwaka wa fedha unaoshia tarehe 31 Disemba 2019.

Hata hivyo, kutokuimarika kwa vigezo vinavyotakiwa kiuhasibu vya uwezo wa shirika kumudu madeni ya muda mfupi kunaweza kukapelekea Shirika kushindwa kulipa madai ya Bima (Insurance Claims) kwa wakati kwa mujibu wa sheria.

Ukaguzi unashauri jitihada za makusudi zichukuliwe ili kuboresha uwiano wa

shirika kumudu madeni ya muda mfupi kwa kuzingatia Mawakala na Madalali kuweza kufuata sheria za Bima ikiwemo kuwasilisha malipo yaliyokusanywa kwa wakati pamoja na kupunguza fedha nyingi za shirika kuwepo katika mikono ya wadaiwa.

**Majibu**

Shirika limeathiriwa kwa kiasi kikubwa kwa maamuzi ya Serikali ambapo kupitia kwa agizo la Serikali kuamuru Shirika kumlipa Shirika la Meli kiasi cha dola za kimarekani 345,000 ambapo iliathiri kwa kiasi kikubwa ufanisi wa kifedha ambapo mpaka leo hii Shirika bado halijarudisha kiasi chote cha fedha kutoka kwa Re-insurer (UAP).

Hata hivyo, kupitia changamoto hii Shirika limeendelea kuweka mikakati ya uwekezaji ili kuimarisha ufanisi katika utendaji wa kifedha. Kwa mwaka wa fedha 2021, ufanisi wa utendaji wa kifedha ulipanda kutoka 1.14:1 mpaka 1.24:1 kama inavoonekana kwenye vitabu vya hesabu. Kwa mwaka wa fedha 2022, mpaka kufikia mwezi September 2022 Shirika lilikua na uwekezaji wa 10.2 bilioni tofauti na 8.1 bilioni kwa mwaka wa fedha 2021. Hii itasaidia kuhakikisha Shirika linakua na mitaji mikubwa kwenye uwekezaji na kupelekea ufanisi mzuri katika utendaji wa kifedha.

**Mapendekezo ya Kamati**

Katika kuondoa dosari hiyo Kamati ya LAAC ilipendekeza kwa Serikali kufuata masharti ya mikataba inayofungwa ili kuepusha hasara baina ya Taasisi zake.

Hii ni kutokana na kuwa maamuzi yaliyotolewa na Serikali ya kulitaka Shirika la Bima kulipa kiwango chote cha fedha ya fidia kwa Shirika la Meli hakikuwa sahihi kwa kuwa bima iliyokatwa ni Bima Mtawanyo. Hivyo, fidia hiyo kulipaswa kulipwa na Shirika la Bima na Kampuni ya UAP kwa pamoja na sio kama utaratibu uliofanyika wa kulitaka Shirika la Bima kulipa fedha zote na baadae Kampuni ya UAP kulipa kidogo kidogo ni kwenda kinyume na masharti ya mkataba waliofunga.

#### 5.1.2.1 Kutokulinganisha matokeo ya zoezi la kuhakiki mali za Shirika na kumbukumbu zilizopo kwenye vitabu vya mali za kudumu shilingi 260,986,000

Katika ukaguzi wa kuhakiki mali za kudumu za Shirika uliofanyika mwishoni mwa mwaka kama inavyotakiwa kwa mujibu wa utaratibu, ukaguzi umebaini kulikuwa hakuna ushahidi wa kuonyesha kwamba matokeo ya zoezi hilo yalioanishwa na kumbukumbu za kwenye vitabu, na kupelekea uwepo wa dosari ya kushindwa kuthibitisha usahihi wa thamani ya mali za kudumu za Shirika (zinazohamishika na zisizohamishika) iliyoonyeshwa kwenye taarifa ya fedha kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Disemba 2020 kama kweli inaonyesha sura sahihi na halisi.

Kushindwa kuthibitisha usahihi wa thamani za mali za kudumu za Shirika

kunaweza kupelekea kujitokeza kwa hesabu za Shirika zilizowasilishwa kutokuonesha sura sahihi na halisi.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Shirika la Bima Zanzibar kuhakikisha kwamba zoezi la kuhakiki mali za shirika likishakamilika matokeo ya zoezi hilo yanalinganishwa na rejista ya Shirika yamali za kudumu ili kuhakikisha hali halisi ya mali za Shirika na usahihi wa thamani ya mali hizo itakayoonyeshwa kwenye taarifa za kifedha kwa mwaka husika.

**Majibu**

Shirika kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango linafanya zoezi la kupitia upya na kuhakiki mali zote za Shirika ili kuweza kupata daftari (Register) lililosahihi la mali zote za Shirika. Kwa kupitia barua ya tarehe 05/07/2022 yenye kumbukumbu namba BA.26/454/01/25/79 tayari tushapatiwa wataalamu wa kushirikiana katika kazi hiyo na kwa sasa zoezi linaendelea ambapo tayari mali zote za Shirika zimesha hakikiwa, Shirika linasubiria kupatiwa ripoti ya daftari hilo kutoka Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya LAAC imekubaliana na matokeo ya uchunguzi ya Mkaguzi Mkuu, hata hivyo, Kamati ya LAAC imeifuta hoja hiyo kwa kuwa Mamlaka imeanza kuchukua hatua mbali mbali.

Aidha, Kamati ya LAAC imebaini kuwa daftari hilo linahifadhiwa na Msajili wa Hazina kufuatia kutungwa kwa Sheria ya Namba 6 ya mwaka 2021.

Sambamba na hayo, Kamati ya LAAC imebaini kuwa baadhi ya miongozo inayotolewa na Serikali haiwezi kutekelezwa na Taasisi zote za umma kwa kuwa baadhi ya Taasisi kama vile Shirika la Bima linaongozwa na miongozo mingine.

Kwa msingi huo, Kamati ya LAAC inapendekeza yafuatayo:

1. Kufanyiwa marekebisho kifungu cha 57(1)(b) cha Sheria ya Namba 6 ya mwaka 2021 ili Daftari liwe mali ya Taasisi husika na sio kama utaratibu uliopo hivi sasa na Msajili wa Hazina asimamie "balance sheet" pekee.
2. Serikali iache tabia ya kutoa miongozo ya aina moja kutekelezwa na kila Taasisi ya Umma iweze kwa kuwa baadhi ya Taasisi hukwazika kiutendani, hivyo basi, ni vyema kila Taasisi ikatekeleza shughuli zake kwa mujibu wa mipaka yake ili kuepuka kupata hoja zisizo na msingi.

**5.1.2.2 Uwekezaji usiyo na tija shilingi 711,000,000**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Shirika la Bima la Zanzibar zilimefanya uwekezaji wa shilingi 711,000,000 kati ya hizo jumla ya shilingi 261,000,000 ni uwekezaji katika kampuni ya ZAFICO naTZS 450,000,000 katika kampuni ya MWANI

ulitokana na maagizo ya Serikali ya kuchangia katikamaendeleo ya taasisi za Serikali ambapo uhakika wa upatikanaji wa mapato hayo kutokana na uwekezaji huo ni jambo lisilo na uhakika.

Aidha, kwa mujibu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania "TIRA" namna ya uwekezaji huo hauwezi kukubalika kwa kuzingatia ya kwamba hauna tija kwa Shirika wakati wa Upimaji wa Uwezo wa Shirika wa kulipa madeni ya bima (Solvency Margin Test). Katika suala hili, uwekezaji ambao hauna tija unachangia kuzidi kuporomoka kwa kiwango cha uwezo wa Shirika cha kulipa madai ya bima na inaweza kusababisha Shirika kushindwa kufanya kazi katika tasnia ya bima kulingana na kanuni za Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA).

Ukaguzi unashauri uongozi wa Shirika la Bima Zanzibar kupitia Kitengo cha uwekezaji unapaswa kuwa makini katika kuchagua uwekezaji unaofaa na wenye tija. Kwa uwekezaji unaotokana na maagizo ya Serikali uongozi wa Shirika unapaswa kuwasiliana na Serikali kwa lengo la kupendekeza aina ya uwekezaji ambao utakuwa na tija na utaweza kutambulika na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA), hata hivyo ukaguzi unapendekeza ya kwamba ni vyema michango iwe midogo midogo badala ya kuwekeza kiasi kikubwa cha fedha katika maeneo ambayo hayana tija.

**Majibu**

Uwekezaji huu kwenye Kampuni hizi mbili ulitokana na maagizo kutoka Serikalini, Shirika la Bima pamoja na kuwa linatakiwa kuwajibika kwa kufuata Kanuni zilizowekwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Biashara ya Bima (TIRA) pia tunawajibu wa kufata maagizo yanayotolewa na Serikali.

Uwekezaji huu unaweza ukawa unakinzana na taratibu za Mamlaka (TIRA) lakini una manufaa kwa watu wa Zanzibar na Serikali kwa ujumla na tunategemea kuwa siku za usoni marejesho ya uwekezaji huu utapatikana.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya LAAC imekubaliana na matokeo ya uchunguzi ya Mkaguzi Mkuu, hivyo, hoja hii imebaki kama ilivyo ingawa miradi ya aina kama hii huchukua muda mrefu faida yake kuonekana.

Kwa kuwa fedha nyingi zimewekezwa kwenye miradi hii na kwa kuwa miradi ya aina kama hii huchukua muda mrefu faida yake kuonekana, hivyo basi, Kamati ya LAAC imelitaka Shirika hili kufuatilia kwa karibu mwenendo wa Kampuni hizo ili Shirika liweze kurudisha fedha zake pamoja na kupata faida.

Aidha, Kamati ya LAAC imekubaliana na matokeo ya uchunguzi ya Mkaguzi Mkuu,

hivyo, hoja hii imebaki kama ilivyo na inapendekeza kwa Serikali kuachana na tabia ya kuzilazimisha Taasisi za Umma kutekeleza mambo ambayo hayaendani na malengo na dhamira ya kuanzishwa kwa Taasisi husika kwani kuendelea kufanya hivyo kutazitia hasara Taasisi hizo.

### 5.1.2.3 Kuendelea kushuka kwa Uwezo wa Shirika wa Kulipa Madai ya Bima (Solvency Margin)

Kulingana na Kanuni ya Bima namba 21 (1) na Sheria ya Bima namba 10 ya 2009, kifungu cha 20 (1) Shirika linatakiwa kuandaa Jaribio la Upimaji Uwezo wa Shirika wa Kulipa Madai ya Bima (Solvency Margin Test) kwa madhumuni ya kupima uwezo halisi wa Shirika haswa wakati wa kutathmini uwezo wa kulipa kiasi kikubwa cha madai mara moja.

Ukaguzi umebaini uwezo wa Shirika wa kulipa madeni ya bima unaendelea kushuka kwa kipindi cha miaka minne mfulululizo kuanzia mwaka 2017 hadi mwaka 2020 jambo ambalo linapelekea uwepowa hali ngumu kuweza kutimiza majukumu yake ya kimkataba na hatimae linaweza kufilisika kamahali hii haitabadilika.

Hata hivyo upo uwezekano mkubwa wa Shirika kufungiwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima kufanya kazi katika tasnia ya bima kulingana na kanuni za TIRA.

Uwezo wa Shirika wa kulipa madeni ya bima umeonekana kupungua mwaka hadi mwaka. Kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Disemba 2020 uwezowa Shirika umepungua kwa shilingi 1,034,269,000 sawa na asilimia 109 ukilinganisha na mwaka ulioishia tarehe 31 Disemba 2019.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Shirika kuhakikisha kuwa uwezo wa Shirika wa ulipaji madeni ya bima (Solvency Margin Test) unaboreshwa na kuwa na mwelekeo mzuri kwa kuhakikisha kuwa vizuizi vyote vinavyochangia kuzorota kwa mwenendo vinatambuliwa kwa wakati na kutatuliwa ipasavyo.

#### Majibu

Kwa mujibu wa jadweli ambalo limeoneshwa na Mkaguzi ni kweli kumekuwa na ongezeko la ukwasi katika Shirika na hali hii ilisababishwa na maagizo ya mara kwa mara ambayo hutolewa na Serikali ambayo yanaathiri "cash position" ya Shirika. Mfano Shirika lilitakiwa kuwekeza jumla ya Tsh. 711,000,000.00 katika Mwani na ZAFICO fedha hizo ziliathiri kwa kiwango kikubwa "solvency margin" ya Shirika.

Pia, Serikali kupitia Wizara ya Miundombinu na Wizara ya Fedha ilitutaka kulipa deni la Kampuni ya UAP USD 324,166.17 kulilipa Shirika la Meli, fedha hizi zilichangia kwa kiwango kikubwa uwepo wa kuongezeka "solvency margin" katika Shirika.

#### Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Kamati ya LAAC imekubaliana na matokeo ya uchunguzi ya Mkaguzi Mkuu, hivyo, hoja hii imebaki kama ilivyo na inapendekeza kwa Serikali kuachana na tabia ya kuzilazimisha Taasisi za Umma kutekeleza mambo ambayo hayaendani na malengo na dhamira ya kuanzishwa kwa Taasisi husika kwani kuendelea kufanya hivyo kutazitia hasara Taasisi hizo.

### 5.1.2.4 Uwepo wa Ongezeko la Madeni yatokanayo na ukodishwaji wa Nyumbaza Shirika shilingi 363,692,298

Katika uhakiki wa akaunti za wapangaji wa nyumba za Shirika umeonyesha kwamba kuna wapangaji wenye madeni makubwa ya muda mrefu kati ya mwaka mmoja (1) hadi sita (6) ikimaanisha kuwa Kifungu Namba 2 cha makubaliano ya ukodishwaji wa nyumba hizo hakijazingatiwa (kutokulipa kodi mapema). Ukaguzi umebaini kwamba Wapangaji wengi wenye madeni ya muda mrefu ni taasisi za Serikali pamoja na Taasisi binafsi.

Aidha, juhudi za ufuatiliaji zilizofanywa na Shirika za kukusanya madeni hayo zimeonekana kutokuzaa matunda. Wapangaji wengine walionekana kuwa wamesitisha mikataba yao na Shirika, kitendo ambacho kinatia shaka kuhusu upatikanaji wa fedha hizo zinazodaiwa na Shirika.

Kwa mujibu wa kifungu Nambari 16 cha makubaliano ya kukodisha nyumba za Shirika kinampa mamlaka mwenye nyumba (ZIC) kudai riba kwa kiwango cha aslimia kumi (10%) ya kodi ya pango iliyocheleweshwa.

Hata hivyo, ukaguzi haukupata ushahidi wa kuonyesha kwamba kifungu hiki kilizingatiwa.
Kutokuzingatia kwa makubaliano ya mkataba kunapelekea uwepo wa usimamizi mbovu wa mikataba ya kukodisha nyumba za Shirika ambayo inaweza kusababisha hasara kwa Shirika kutokana na kodi isiyoweza kukusanywa.

Ukaguzi unashauri ni vyema kwa uongozi wa Shirika la Bima Zanzibar kuhakikisha ya kwamba wapangaji wote wanatii sheria na masharti yaliyowekwa katika mikataba ya kukodisha nyumba, ikiwa ni pamoja na kulipa kwanza kabla ya kukabidhiwa nyumba na wasiolipa kwa wakati bila sababu watozwe riba inayostahiki ili kuokoa Shirika kupata hasara inayotokana na kodi isiyolipika.

Vile vile ukaguzi unashauri uongozi wa Shirika la Bima Zanzibar kuangalia uwezekano wa kufanya muda wa upangaji uwe wa muda mfupi kama vile kwa kila robo mwaka ili kuwezesha hatua za kukusanya kodi mapema kwa wale ambao watashindwa kulipa kwa wakati.

**Majibu**

Kuna baadhi ya wapangaji hasa taasisi na wizara za Serikali ni miongoni mwa

wapangaji wa nyumba za Shirika la bima la Zanzibar, lakini zipo na Kampuni binafsi chache ambazo pia ni Wapangaji wa Shirika.
Maendeleoyamadenihayo ni kama ifuatavyo:-

1. Black Artist

Tumepitia kumbukumbu na tumebaini kwamba Black Artist hakuwa Mpangaji bali alikuwa ni Mtoa Huduma (Supplier), hata hivyo, deni lipo na tayari hatua za kulifuatilia deni hili zimechukuliwa.

2. Mass Global Investment

Shirika limefungua shauri la madai Mahakamani na kuifuatilia kesi hiyo kwa ukaribu sana na hivi sasa Shirika linasubiri maamuzi ya Mahakama. Pamoja na taarifa hiyo naambatanisha hati ya madai NAM 3/2018.

3. DhowandJeep

Shirika liliendelea kulifuatilia deni hilo kwa aliyekuwa Mpangaji wa Shirika ambapo, Mpangaji huyu aliweza kupunguzi deni hilo kwa kulipa kiasi cha Tsh. 400,000/= na hivi sasa Shirika limepeleka indhari ya kufungua shauri la madai Mahakamani baada yakuonekana Mpangaji huyo bado anasuasua kulipa deni hilo. Ninaambatanisha na barua ya indhari ya kufungua shauri la madai Mahakamani yenye kumbu kumbu namba ZIC/A.351/D&J/14/2021.

4. Swahili Soft Technology

Jitihada kubwa Shirika iliendelea kuchukuwa ikiwa ni pamoja na kumuandikia ‘reminding letter’ kwa lengo la kumkumbushia deni lake ikiwa ni pamoja na kumuandikia indhari ya kufungua shauri la madai Mahakamani. Ninaambatanisha shauri hilo lenye kumbukumbu namba ZIC/G261/SSST/11/2021.

5. Green Light Foundation

Kampuni hii ilifanikiwa kupunguza deni lake kwa kulipa kiasi cha Tsh. 3,000,000 na Shirika halijaishia hapo liliendelea kumfuatilia ili akamilishe deni lake.

6. Afisi ya Rais, Fedha na Mipango na ‘Zanzibar Tourism Commission’

Hatua kadhaa zimechukuliwa na Shirika ili kuhakikisha fedha hizo zinalipwa na Wadaiwa ikiwemo kufuatilia, kuzikumbusha kwa barua Taasisi hizo pamoja na kukaa vikao vya pamoja ili tuweze kumaliza kadhia hii. ZIC/G.59/NYS/11/2021 na ZIC/A.98/OR-FM/VOL. XIV/65/2021 ni kumbu kumbu namba za barua za kukumbushia kwa ‘Zanzibar Tourism Commission’ na Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango zimeambatanishwa.

7. NIDA

Taasisi hii imekamilisha kulipa deni lake siku ya tarehe 27/01/2022 na Stakabadhi ya Malipo namba 220100080 imeambatanishwa.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**
Kamati ya LAAC imekubaliana na matokeo ya uchunguzi ya Mkaguzi Mkuu, hivyo, hoja hii imebaki kama ilivyo na imelitaka Shirika hili kuendelea kufuatilia madeni hayo ili wahusika waweze kulipa ndani ya kipindi kifupi.

Vile vile, Kamati ya LAAC imelitaka Shirika la Bima kuwatoza Wapangaji wake asilimia kumi (10%) ikiwa ni adhabu ya kushindwa kulipa kodi kwa wakati kwa kuwa sharti hilo limo ndani ya makubaliano yao, lakini pia, fedha hizo zitasaidia kuongeza mapato ya Shirika.

Aidha, Kamati ya LAAC haikukubaliana na ushauri uliotolewa na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusiana na kupunguzwa muda wa kukodisha majengo hayo hadi kila baada ya miezi mitatu (robo mwaka) kwa kuwa muda wa mwaka mmoja sio mrefu.

Sambamba na hayo, Kamati ya LAAC inaishauri Afisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuwa makini wakati inatekeleza shughuli zake ili kuandika taarifa sahihi kwa lengo la kuondosha usumbufu kwa Wadau wake.

### 5.1.2.5 Ununuzi wa vifaa na kuonyesha kwamba vimetumika bila kuzingatia utaratibu wa kihasibu

Ukaguzi umefanya mapitio ya kumbukumbu zinazohusiana na vifaa vilivyonunuliwa katika kipindi cha mwaka ulioishia tarehe 31 Disemba 2020 na kubainika kuwa vifaa vyote vilivyopokelewa vilionyeshwa kwenye hesabu za Shirika kama matumizi ya mwaka huo (Direct Expensing) bila kuzingatia kuwa vifaa vyote vimetumika kwa kipindi hicho au havikutumika.

Aidha jukumu la kudhibiti na kuweka hesabu za vifaa vilivyonunuliwa, vilivyotumika na vilivyobaki kwenye ghala liliachwa chini ya usimamizi wa mtunza ghala pamoja na kutokuwa na udhibiti kutoka kitengo cha uhasibu na fedha (finance department) ili kulinganisha kumbukumbu za mtunza ghala na za mhasibu hasa katika uhakiki wa vifaa vya Shirika.

Utaratibu huo wa kuonyesha gharama za vifaa vyote vilivyonunuliwa kama matumizi (direct expensing) hausaidii kubaini mapungufu ambayo yanaweza kusababishwa na wizi, udokozi, upokeaji hafifu wa vifaa, utunzaji mbaya wa kumbukumbu, ununuzi hewa na kadhalika. Kwa hivyo ukaguzi haukuweza kujiridhisha kwamba ununuzi wa vifaa uliofanywa katika kipindi chote cha mwaka wa ukaguzi vilipokelewa na kutumika kwa faida ya Shirika.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Shirika la Bima Zanzibar kuhakikisha manunuzi na matumizi ya vifaa vyote yanakuwa na viambatanisho vyote vya ununuzi na vya

kutolea vifaa ghalani. Kumbukumbu zote hizo zinatakiwa kuingizwa kwenye vitabu vya Shirika kila mwezi kwa upande wa mtunza ghala na upande wa uhasibu na fedha.

Mwisho wa mwaka kufanyike mlinganisho kati ya kumbukumbu za uhasibu na ghala na kama kuna mapungufu yoyote yachunguzwe ili kuboresha udhibiti wa ndani juu ya utumiaji wa vifaa vya Shirika.

**Majibu**

Ni kweli changamoto hii ilikuwepo lakini kwa sasa Shirika limeongeza ufanisi wa mfumo wake wa Smart ERP ambapo kwa sasa masuala yote ya utunzaji na uhakiki wa mali za Shirika yanafanywa moja kwa moja kwenye mfumo na kuwezesha kupata ripoti hizo sahihi na kwa wakati unaohitajika.

Mfumo huo wa ‘Stock and Inventory Management’ unafanya kazi kama ilivyokusudiwa na tayari umeanza kutoa ripoti kwa ajili ya kutolea maamuzi sahihi.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya LAAC imekubaliana na matokeo ya uchunguzi ya Mkaguzi Mkuu, hata hivyo, Kamati ya LAAC imeifuta hoja hii kwa kuwa Shirika la Bima limeanza kuchukua hatua juu ya kasoro zilizobainika.

#### 5.1.2.6 Uwepo wa deni la muda mrefu linalodaiwa kwa kampuni ya Bima Mtawanyo ya UAP shilingi 564,882,415 na Shirika la Meli la Zanzibar shilingi 344,275,825

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika uwepo wa deni la shilingi 564,882,415 pamoja na deni la shilingi 344,275,825 ambapo kwa ujumla linafanya uwepo wa deni la shilingi 909,158,240 ambapo Shirika la Bima linadai kwa kampuni ya Bima ya UAP linalotokana na biashara ya Bima Mtawanyo pamoja na Shirika la Meli MV Mapinduzi II deni ambalo limedumu tangu mwaka 2018.

Ukaguzi umebaini Urejeshaji wa deni hili kwa sasa umesimama kutokana na ukweli kwamba wafanyabiashara wengine katika Bima ya Mtawanyo chini ya UAP walisita kulipa deni hilo kwa sababu malipo ya bima (premium) yalipokelewa na Kampuni ya (UAP) baada ya kutokea kwa ajali ya MV Mapinduzi II kinyume na kanuni 35 (a) ya Kanuni za Bima ambazo zinaeleza ya kwamba “Mikataba ya bima (insurance policy) itakua haifai tena hadi tarehe ya kuanzishwa ikiwa malipo kamili ya ada ya Bima (premium) hayatatolewa ndani ya siku saba tangu tarehe ya kuanza kwa mkataba wa bima (insurance policy), isipokuwa ikiwa bima ya gari italipwa wakati wa kusainiwa mkataba wa bima.”

Kwa kuzingatia matakwa ya kifungu hicho, kwa kuwa mkataba wa Bima ya

Mtawanyo uliingiwa kati ya Shirika la Bima Zanzibar na Shirika la Meli Zanzibar inayomiliki MV Mapinduzi II Shirika la Bima Zanzibar lililazimika kulipa deni lote kwa Shirika la Meli Zanzibar na kuanzisha juhudi za kufuatilia deni lake kutoka Kampuni ya UAP ambayo urejeshwaji wake ni wa mashaka.

Katika ufuatiliaji wa ulipwaji wa deni hilo imebainika kupitia Kumbukumbu zilizopo zinaonyesha kwamba kuna kiasi cha shilingi 344,275,825 ambazo Shirika la Bima (Makao Makuu) linalidai Shirika la Meli Zanzibar tangu Julai, 2020. Deni hilo linahusu bima ya mali hiyo hiyo ( MV Mapinduzi II). Juhudi zilizofanywa na Shirika la Bima Zanzibar katika kufuatilia ulipwaji wa deni hili hazikuonekana.

Katika suala hili Shirika linakiuka kanuni za TIRA na kusababisha mkusanyiko wa madeni makubwa mikononi mwa wadaiwa, hali ambayo inachangia kupunguza uwezo wa Shirika wa kulipa madai ya Bima pindi yanapotokea.

**Ukaguzi unashauri uongozi wa Shirika la Bima kufanya mambo yafuatayo:-**

1. Kuimarisha hatua za kurejeshewa madeni kutoka kwa Kampuni ya UAP na Shirika la Meli Zanzibar.

2. Kabla ya kukubali biashara ya bima kwa Meli zinazomilikiwa na Serikali au mali nyingine yoyote Uongozi wa Shirika la Bima unapaswa kukaa na maafisa wenye dhamana chini ya Wizara ya Miundombinu, Usafirishaji na Mawasiliano kujadili kwa kina mambo yote muhimu yanayohusiana na kuandikisha mali kama hizo na mashaka ya maisha ya Shirika la Bima kuendelea kuwepo ikiwa bima mtawanyo itashindikana.

3. Shirika lijitahidi kuwa na mwelekeo wa kibiashara zaidi badala ya huduma zaidi kuzingatia sheria na kanuni zinazosimamia biashara ya bima.

**Majibu**

Uongozi wa Shirika ulichukuwa hatua na kuufanyia kazi ushauri wa Mkaguzi na kupelekea Shirika la Meli kulipa jumla ya USD 77,243.86 kwa Bima na jumla ya USD 71,600.00 zimelipwa kwa njia ya kufanya “netoff” kupitia madai yao ambayo Shirika ilitakiwa kulipa jumla ya USD 71,600 kwa dai la ajali ya Meli ya MT. Ukombozi I na kwa sasa hatuna madeni na Shirika la Meli na uhusiano wetu umeimarika.

Kwa upande wa deni la Kampuni ya UAP lilikuwa ni jumla ya USD 324,166.17 na hadi kufikia leo Shirika limeweza kupokea kiwango cha USD 78,569.36 kutoka kwa UAP na jumla ya USD 245,601.82 zimebaki bado hazijalipwa kutoka kwa kampuni hiyo ya bima, hatahivyo hatua mbali mbali zimeshachukuliwa ili kuhakikisha deni hilo linalipwa kama ifuatavyo:-

i. Kumuandikia barua Kamishna kumtaka aingilie kati suala hili ili Shirika kupata haki yake.

ii. Kumefanyika makubaliano baina ya Kampuni ya UAP na Shirika la Bima kwa bima ya mtawanyo kwamba Shirika halitalipa malipo kwa Kampuni ya UAP badala ya malipo hayo yatalipwa kwa kupunguza deni wanalodaiwa, kwa sasa deni hili ni USD 227,375.98.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya LAAC imekubaliana na matokeo ya uchunguzi ya Mkaguzi Mkuu, hata hivyo, Kamati ya LAAC imeifuta hoja hii kwa kuwa deni hili linaendelea kulipwa kwa kasi kubwa.

Vile vile, Kamati ya LAAC imelitaka Shirika la Bima kuendelea kuusimamia utaratibu iliouanzisha wa kuikata moja kwa moja Kampuni ya UPA kwenye "premium" kwa dhamira ya kuhakikisha kuwa deni hilo linalipwa ndani muda mfupi ujao.

#### 5.1.2.7 Kutokuoanisha madeni wanayodaiwa mawakala/madalali wa Bima na madeni ambayo Shirika la Bima linadaiwa kutokana na biashara ya bima (lack of reconciliations and confirmation statements)

Katika ukaguzi wa madeni wanayodaiwa mawakala na madalali wa bima na madeni mengine mbali mbali ambayo shirika la bima linadaiwa kutokana na biashara ya bima mtawanyo imebainika ya kuwa kuna baadhi ya mawakala/madalali wenye madeni makubwa na ya muda mrefu zaidi ya miaka miwili na mengine ambayo shirika linadaiwa kwenye bima mtawanyo.

Aidha, ukaguzi hakuweza kupatiwa ushahidi wa kuonyesha kwamba kumbukumbu za Shirika na za madalali/ mawakala husika zimekuwa zikioanishwa (zikilinganishwa) mara kwa mara.

Aidha hakukuwa na uthibitisho kwamba wadaiwa walikuwa wanapelekewa taarifa za madeni yao (statements of account) mara kwa mara ili kuhakikisha uwepo wa deni, usahihi wa deni na kuwezesha uoanishaji wa kumbukumbu na kurahisisha ukusanyaji wa madeni hayo.

Kutokulinganishwa kwa kumbukumbu za Shirika na za wadaiwa mara kwa mara na kutokuwapelekea wadaiwa taarifa za madeni yao (statements of account) mara kwa mara kunaweza kupelekea Shirika kuwa na madeni hewa na wadaiwa hewa kwenye vitabu vya Shirika.

Ukaguzi unashauri kwa Uongozi wa Shirika uwe na utaratibu wa kuwapelekekea wadaiwa wake taarifa za madeni yao kila robo mwaka kwa ajili ya kutambua uwepo

wa deni, usahihi wake na njia rahisi ya kuweza kuyakusanya kwa wakati. Utaratibu huu utarahisisha zoezi la kuoanisha kumbukumbu za Shirika na za wadaiwa wake.

**Majibu**

Shirika baada ya ukaguzi huu liliainisha madeni ambayo linawadai Mawakala na baadae kuwasilina na Mawakala hao kwa uhakiki wa madeni haya ili kuweka kumbukumbu sawa pamoja na uhakiki huu na kuthibitisha madeni haya.

Pia, Shirika lilifunga mikataba na Mawakala hawa jambo ambalo iliwawezesha Mawakala kulipa madeni wanayodaiwa kwa kukatwa kidogo kidogo kwenye ujira wao kila mwezi mpaka deni litakapo kwisha.

Naambatanisha mkataba wa makubalino ya kukata deni kwenye ujira wa wakala na kwa sasa hali inazidi kuwa nzuri baada ya kufanya uhakiki wa madeni na kufanya ufuatiliaji wa karibu kufuatia ripoti ya mkaguzi.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya LAAC imekubaliana na matokeo ya uchunguzi ya Mkaguzi Mkuu, hata hivyo, Kamati ya LAAC imeifuta hoja hii kwa kuwa Shirika hili limeanza kuchukua hatua dhidi ya kasoro zilizobainika.

#### 5.1.2.8 Kushindwa Kuwasilisha Taarifa ya Mapato na Matumizi kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa Mwaka wa Fedha 2020.

Kwa mujibu wa kifungu cha 91 (1) cha Sheria ya Kodi SURA 332 (R.E.2019) kinasema kwamba kulingana na kifungu cha 92 na 94 cha Sheria hii na 39 na 48 cha Sheria ya Usimamizi wa Ushuru, kila mtu atawasilisha kwa Kamishna taarifa ya mapato na matumizi ndani ya miezi sita baada ya mwaka wa mapato kuisha.

Mapitio ya taarifa ya ukaguzi wa ushuru iliyofanywa na TRA kwa mwaka wa mapato 2017 ulibaini kuwa Shirika lilipata hasara kwa sababu ya riba na adhabu ya ushuru (corporate tax) ya shilingi 113,690,515 kwa kutowasilisha taarifa ya mapato kwa wakati. Ukaguzi uliofanywa katika eneo hili kwa mwaka wa ukaguzi haujaonyesha kwamba Shirika limewasilisha taarifa ya mwisho wa mwaka 2020 inayohusu mapato na matumizi ya Shirika kwa TRA ambayo ilipaswa kuwasilishwa mnamo au kabla ya tarehe 30 Juni, 2021 licha ya idhini ya kuongezewa muda iliyotolewa na TRA hadi tarehe 3 Julai, 2021.

Kwa hali hii Shirika litaendelea kupoteza fedha kupitia riba na adhabu kwani hali ya kutotii bado inaendelea kutoka mwaka 2018 hadi 2020 kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Ushuru ya 2013 (R.E 2019).

Ukaguzi unashauri uongozi wa Shirika la Bima Zanzibar kuzingatia Sheria zote za

kodi na Kanuni zake kikamilifu.

**Majibu**
Kuchelewa kwa taarifa kwa kwenda kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) yalichangiwa na uchelewaji wa ufungaji wa hesabu za Shirika kwa wakati ambapo Shirika lilikuwa awali likifunga hesabu zake kwa njia ya "manual", kwa sasa Shirika limeweka mikakati kuhakikisha hesabu zinafungwa kwa wakati na kuwasilisha kwa Mamlaka husika kwa wakati. Kama ilivyoainishwa awali, Shirika linahakikisha hesabu za kila mwezi zinapatikana kwa wakati kusaidia upatikanaji wa hesabu za mwaka.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**
Kamati ya LAAC imeridhika na maelezo ya Shirika la Bima, hivyo, hoja hii imefutwa.

#### 5.1.2.9 Uwepo wa matumizi ya gharama kubwa za maegesho ya Masalia ya Magari (Substantial Parking Costs of Salvages)

Katika ukaguzi wa uhakiki wa kumbukumbu za malipo yaliyofanyika kwa ajili ya masalia ya magari ulibaini ya kwamba kulikuwepo na baadhi ya magari mengine ambayo yalilipwa chini ya madai yote (total loss). Kumbukumbu za masalia ya magari kwa mwaka 2020 ulionyesha kwamba kulikuwepo magari kadhaa ambayo yalitengwa kwa ajili ya kuuzwa. Wakati wa mahojiano nilielezwa kwamba masalia hayo ya magari huwa yanahifadhiwa katika karakana binafsi ambazo watoa huduma wanalitoza Shirika shilingi 70,000 kila siku (Dar es Salaam) kwa idadi ya magari yaliyokuwa yameegeshwa kwa siku na shilingi 2,000,3,000 kwa siku kwa gari katika ofisi za kanda. Kwa maelezo hayo utaona kwamba Shirika linatumia wastani wa shilingi 2,100,000 kwa mwezi (sawa na shilingi 25,200,000 kwa mwaka kwa Dar es Salaam) na shilingi 720,000 hadi shilingi 1,080,000 kwa mwaka (kwa ofisi za kanda). Gharama hizi ni kubwa ukilinganisha na mapato yanayoweza kupatikana kwa mauzo ya masalia hayo ya magari.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Shirika kushughulikia changamoto hii na kuchukua hatua za haraka.

**Majibu**
Utaratibu wa uuzaji na uondoaji wa mali za Serikali uko chini ya Mamlaka ya Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango Zanzibar. Shirika linaingia gharama za kulaza masalia ya gari kutokana na kuchelewa kwa watendaji kutoka Afisi ya Rais, Fedha na Mipango kwenda Ofisi za Dar es Salaam au Ofisi zetu za Kanda kwa ajili ya kuweka thamani. Shirika limekuwa likihifdhi masalia hayo katika karakana binafsi kwa sababu hatuna eneo la kuweka masalia hayo na kuepuka hasara ya uharibifu.

Shirika imechukuwa hatua ya kuondosha changamoto hiyo kwa kuwasiliana na Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuturuhusu kumtumia Mtia Thamani wetu ambaye

amethibitishwa ili masalia hayo yauzwe kwa haraka na kuepuka gharama hizo. Wizara ilitujibu tufate taratibu na miongozo inayotolewa na Ofisi hiyo kama tulivyoelezwa kwenye barua namb B.26/454/01/20/108 ya tarehe 23/08/2021.

### Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Kamati ya LAAC imekubaliana na matokeo ya uchunguzi ya Mkaguzi Mkuu kwa kuwa Sheria ya Ununuzi iliyopo hivi sasa inaelekeza hivyo. Hata hivyo, Kamati ya LAAC inaishauri Taasisi inayohusika na Sheria hiyo kuifanyia marekebisho Sheria hiyo kwa kuwa masharti yaliyowekwa kwenye Sheria hiyo utekelezaji wake unakwaza baadhi ya Taasisi. Hivyo, ni busara ikatungwa Sheria ambayo masharti yake yataziwezasha Taasisi kuitekeleza Sheria hiyo kwa mujibu wa majukumu yao.

### 5.1.2.10 Ukosefu wa Ujuzi wa Kuachiana Madaraka (Lack of Delegation Skills)

Kuachiana madaraka kiofisi maana yake ni kukabidhi mamlaka kutoka kwa mtu mmoja wa kiwango cha juu kwenda kwa mtu wa kiwango cha chini.

Ukaguzi umebaini kuwa wafanyakazi kadhaa wa Shirika wenye nyadhifa za juu walikosa ustadi katika kuwaachia wafanyakazi wenzao madaraka wakati walipoenda likizo kwani waliwaachia wafanyakazi waliopo kwenye safu sawa (same level) kinyume na utaratibu bora wa kuachiana madaraka.

Aidha, ukaguzi umebaini kwa baadhi ya meneja/wakurugenzi wa idara hawana ujuzi wa usimamizi ambao ungesaidia wafanyakazi wenzao katika makabidhiano na pia kushughulika vizuri na walio chini yao, kitendo ambacho kinaruhusu mtiririko rahisi wa shughuli katika Shirika. Katika mahojiano yaliyofanyika kwa maafisa mbali mbali katika idara tofauti yalionyesha kwamba wafanyakazi wa ngazi za chini walikuwa na utegemezi mkubwa kwa viongozi wao katika kushughulikia masuala mengi kwani hawakuwa na majibu ya moja kwa moja kwa maswali waliyoulizwa.

Kukosekana kwa ustadi katika kugawana kazi za kiofisi ni dhahiri kwamba maafisa wa ngazi za juu wanazidiwa na majukumu huku wafanyakazi wengine wakiwa hawana kazi au wakikata tamaa. Aidha, kukosekana kwa uwezo wa kutoa mwelekeo na kufundisha wafanyakazi wa chini kunasababisha kushuka kwa motisha ya kazi na kusababisha Shirika kutofikia malengo yake.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Shirika la Bima Zanzibar kuhakikisha unafanya jitihada ya kuwafundisha wasimamizi/wakurugenzi kuhusu ustadi wa usimamizi, mfano jinsi ya kugawana kazi za ofisi (delegation skills), kufuatilia na kufundisha walio chini yao ili kustawisha ujuzi wao unaolenga kuongeza ufanisi wa kazi na tija na hivyo kufikia malengo ya shirika.

### Majibu

Shirika linatekeleza taratibu za kukasimu kazi kwa watumishi wa ngazi za chini kwa

lengo la kuongeza ufanisi. Katika kuimarisha “Delegation skills”, Shirika la Bima la Zanzibar imeandaa muongozo wa uandaaji Uongozi utakaowezesha watumishi wa ngazi ya chini wenye uwezo, sifa na utayari wa kujifunza kukasimiwa madaraka ya nafasi za juu itakapotokezea Mkuu wa Idara/Meneja hayupo kazini kwa sababu za kisheria.

Muongozo huo unamuezesha mtumishi kujengewa uwezo wa kujiamini na kumudu dhamana atakazokabidhiwa kwa kushirikishwa kwa kila hatua ya kazi zilizopo katika Idara husika muongozo huo upo kwa sasa.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya LAAC imekubaliana na matokeo ya uchunguzi ya Mkaguzi Mkuu, hata hivyo, Kamati ya LAAC imeifuta hoja hii kwa kuwa Shirika la Bima limeanza kuchukua hatua juu kasoro zilizobainika.

#### 5.1.2.11 Kuchelewa kuwasilisha taarifa za fedha kwa ajili ya ukaguzi

Kulingana na miongozo ya ukaguzi wa hesabu Shirika linatakiwa kuwasilisha taarifa za fedha kwa mkaguzi kwa ajili ya ukaguzi ndani ya miezi mitatu baada ya kumalizika kwa mwaka wa fedha. Pia, Kanuni namba 39 ya Kanuni za Kifedha za Shirika la Bima Zanzibar inasema kwamba ukaguzi wa kila mwaka unapaswa kuanza wiki ya kwanza ya Februari.

Hata hivyo, ukaguzi ulibaini kuwa rasimu ya taarifa za fedha ya mwaka ulioishia tarehe 31 Disemba, 2020 iliwasilishwa kwa ukaguzi tarehe 17 Juni, 2021, kwa hivyo ilicheleweshwa kwa zaidi ya miezi mitano. Aidha, Shirika halikufuata miongozo ya ukaguzi na kanuni zake za kifedha na kanuni za Bima. Zaidi ya hayo, kuchelewa kuwasilisha hesabu kwa ukaguzi kunaathiri Shirika kwa njia ya malipo ya riba, adhabu na faini kutokana na Shirika kuchelewa kulipa kodi (Corporate Tax).

Ukaguzi unashauri uongozi wa uongozi wa Shirika la Bima Zanzibar kuhakikisha kuwa rasimu za taarifa za fedha zinaandaliwa na kuwasilishwa kwa wakaguzi ndani ya miezi mitatu baada ya mwaka kumalizika kulingana na miongozo ya ukaguzi na mihimili mingine ya udhibiti.

**Majibu**

Shirika linatumia jitihada kubwa kuhakikisha hesabu za mwaka zinatumwa kwa wakati kama sheria na taratibu zinavyotaka ambapo hesabu za mwaka 2021 ziliwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi mwanzoni mwa mwezi Machi, 2022.

Mbali na hivyo, Shirika limeweka mikakati madhubuti ikiwemo kufunga hesabu zake kila mwezi ili kuhakikisha hesabu za mwisho wa mwaka zinapatikana mwanzoni mwa mwaka unaofuata kama taratibu zinavyoeleza.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**
Kamati ya LAAC imeridhika na maelezo ya Shirika la Bima, hivyo, hoja hii imefutwa.

### 5.1.3 SHIRIKA LA BANDARI ZANZIBAR (ZPC)

**Taarifa ya mapato**

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 Shirika la Bandari Zanzibar limefanikiwa kupata mapato ya kiasi cha shilingi 39,897,236,524.39 kutokana na vyanzo vyake mbalimbali vya makusanyo ukilinganisha na makusanyo ya shilingi 34,848,390,345.80 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kukiwa na ongezeko la shilingi 5,048,846,178.59 ambalo ni sawa na asilimia 14.5 ya ongezeko.

**Majibu ya Shirika la Bandari Zanzibar (ZPC)**

Katika mwaka wa Fedha 2020/2021, ni kweli mapato yaliongezeka kwa sababu mzigo mchanganyiko uliohudumiwa ni tani 717,305.2 ikiwa ni ongezeko la asilimia 78.9 ukilinganisha na ilivyokadiriwa tani 400,918. Ongezeko hilo limesababishwa na upokeaji mzigo (saruji sukari ) mwingi kutoka nje ya nchi uliotokana na athari za Covid ikiwemo upungufu wa makontena matupu, hali hiyo limepelekea kupata mapato yanayotokana na "Cargo" Tshs.2,586,952,429.2 ukilinganisha na Tshs.1,561,150,647 zilizokadiriwa.

Aidha, kwa upande wa mzigo wa meli za ndani na a majahazi kumekuwa na ongezeko la mizgo unaotokana na usafirishaji wa mchanga na kokoto kwa wingi kunakotokana na kuongezeka kwa mahitaji ya ujenzi Unguja. Ni ongezeko la asilimia 64 ambapo tani 184,382.47 zilihudumiwa ukilinganisha na tani 112,741 zilizokadiriwa. Ongezeko hilo limepelekea kupata mapato yanayotokana na "Wharfage Dhow" Tshs. 482,612,331.01 ukilinganisha na makadirio ya mapato ya Tshs. 322,580,186.25

**Uchunguzi wa Kamati**

Kamati katika uchunguzi wake imebaini kuwepo kwa taarifa tofauti za mapato baina ya ripoti ya Mkaguzi wa ndani, na Taarifa ya mwisho wa hesabu za mwaka kama ifuatavyo.

Kwa mujibu wa ripoti ya Mkaguzi wa ndani Shirika kwa mwaka wa fedha 2020/2021 limepanga kukusanya jumla ya Tzs 37,348,628,090.42 na kufanikiwa kukusanya jumla ya Tzs 36,153,047,783.08 sawa na asilimia 98

Aidha Kamati imebaini mamlaka kuwa na kiwango kuzuri cha ukusanyaji wa mapato kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kwa kuwa na ongezeko la shilingi 5,048,846,178.59 ambalo ni sawa na asilimia 14.5 ya ongezeko, hata hivyo kamati imebaini kuwepo kwa udhibiti mdogo wa ukusanyaji mapato ambapo Shirika lilikuwa linatumia mfumo wa utoaji wa stakabadhi za malipo ambazo hazikuwa na ufanisi na kuhofiwa uwezekano mkubwa ya kughushi stakabadhi hizo na kupelekea baadhi ya mapato ya

Shirika kuvuja.

### Mapendekezo ya Kamati

Kamati Inaliomba Shirika la Bandari kuweka sawa taarifa zake za ndani za mapato na matumizi ili ziweze kufanana baina ya taarifa zinatolewa na Mkaguzi wa ndani, na taarifa za mwisho wa hesabu ya mwaka kwa pamoja zitoe sura sahihi za upangaji na utekelezaji wa Shughuli za Shirika ili kutoipa kazi kamati ya kubaini ipi ni taarifa sahihi kwa ajili ya kufanyiwa kazi.

Aidha Kamati inaendelea kusisitiza juu ya udhibiti wa ukusanyaji wa mapato ya Shirikia kwa kuendelea kutumia mifumo ya ki- elektroniki katika ukusanyaji wa vyanzo vyake mbalimbali vya mapato ili shirika liweze kuhudumia meli mbalimbali ambazo zinatia nanga katika bandari ya Zanzibar kwa ufanisi mkubwa na Shirika liweze kutekeleza miradi yake mbalimbali ambayo imepanga kuitekeleza.

### Taarifa ya matumizi

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 Shirika la Bandari Zanzibar limefanikiwa kutumia jumla ya shilingi 14,488,527,271.93 kwa kazi za kawaida ukilinganisha na matumizi ya shilingi 16,903,525,233.17 ya mwaka wa fedha 3 2019/2020 kukiwa na upungufu wa matumizi ya shilingi 2,414,997,961.24 sawa na asilimia 14.3 ya upungufu.

### Majibu

Ni kweli matumizi yamepungua katika mwaka fedha 2020/2021kama ukaguzi ulivyobaini ukilinganisha na Makadiro ya matumizi ya mwaka huo, mapungufu haya yamesabishwa na kutolipwa mishahara ilioyopangwa kwasababu ya kutopita kwa muundo mpya wa mishahara ambao kwa mwaka huu bajeti yake ilipangwa, sababu nyengine ni kupungua kwa gharama za shughuli mbali za upakiaji na upakuzi katika Bandarini ambayo inatokana na kupungua kwa ujaji wa meli kubwa. Matumizi hayo hayajumuishi malipo ya Corporate Tax na Gawio iliyolipwa Serikalini.

### Uchunguzi wa Kamati

Kamati imebaini Shirika la Bandari limetekeleza shughuli zake za kawaida na Shughuli za miradi ya mandeleo kwa kiwango kidogo sana tofauti na walivyojipangia hii ni kutokana na kupungua kwa upakiaji na upakuzi wa mizigo katika bandari ya Zanzibar kuliko sababiswa na kupungua kwa ujaji wa meli kubwa katika kipindi hicho jambo ambalo limeathiri matumizi ya Shirika kwa vile utoaji wa huduma za shirika umeweza kupungua.

Aidha Kamati imebaini deni linalotokana na mikopo kwa wafanyakazi wa bandari ambapo kwa mwaka wa fedha 2020/2021 deni hilo lilikuwa na thamani ya Tzs 602,800,000 hadi kufikia 30 june 2021 deni hilo lilikuwa na bakaa ya Tzs 374,074,700.00 hata hivyo Kamati imebaini kutokuwepo kwa sera na mikakati madhubuti ya ukopeshaji na ulipaji wa mikopo hiyo kwa wafanyakazi wa Shirika la

Bandari.

**Mapendekezo ya Kamati**

Kamati inalishauri Shirika Kuongeza juhudi na ufanisi katika shughuli zake mbalimbali kwa lengo la kuliongezea Shirika mapato, ambapo upatikanaji wa mapato hayo kwa kiwango kikubwa kutapelekea kuimarika kwa shughuli za bandari katika kuhudumia meli mbalimbali na kuwezesha utekelezaji wa miradi mbalimbali ya Shirika.

Aidha kamati haipingani na utoaji wa mikopo kwa wafanyakazi wa Shirika kinachotakiwa Shirikiwa kuwa na Sera na mikakati madhubuti ya utoaji wa mikopo hiyo kwa lengo la kupatikana kwa wakati marejesho ya mikopo hiyo.

### 5.1.3.1 Manunuzi yaliyofanyika nje ya mpango wa manunuzi shilingi 100,280,180

Mapitio ya mpango wa manunuzi wa mwaka 2020/21 wa Shirika la Bandari yalibaini kwamba Shirika la Bandari Zanzibar lilifanya manunuzi "iPads" 13 zenye thamani ya shilingi 100,280,180 ambapo ni sawa shilingi 7,713,860 kwa kila moja.

Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kufanya matumizi nje ya mpango wa manunuzi na kinyume na kifungu cha 42(7) cha Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa mali za Umma ya mwaka 2016 pamoja na kutokushirikishwa kwa watendaji wa kitengo cha TEHAMA ili kuweza kutoa vigezo kwa mujibu wa mahitaji ya ununuzi wa "iPads" hizo.

Manunuzi nje mpango wa manunuzi yanaweza kupelekea utotekelezwa kwa mipango mingine na kunaweza kukwamisha shughuli stahiki zilizopangwa kwa mujibu wa bajeti iliyoidhinishwa.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Shirika la Bandari Zanzibar kuandaa shughuli zote muhimu katikabajeti na mpango wa manunuzi wa kila mwaka ili kuepuka kufanya manunuzi nje ya mpango ambayo yanaweza kusababisha gharama za ziada au zisizo za lazima kwa Shirika.

**Majibu ya Shirika la Bandari Zanzibar (ZPC)**

Uongozi wa Shirika ulifanya mapitio ya mpango wa manunuzi baada ya kupokea maombi ya manunuzi tofauti ikiwemo mfumo wa eport na hatimae kuja na mpango mpya ambao ulianisha aina mbili ya manunuzi, aina ya kwanza kupitia Zabuni SMZ/F.123/G.NCB/2020.2021/ 24 ambayo ilikusudiwa ununuzi wa vitendea kazi vya Tehama, vitendea kazi hivyo vinajumuisha ununuzi wa IPAD 13, CCTV 10 kwa ajili ya eneo la Idara ya ufundi na CCTV kamera 5 kwa ajili ya kubadilisha za Bandari ya abiria. na antvirus 200pcs. Na zabuni ya pili ya mfumo wa E port SMZ/F.123/CS/QSBS/2020.2021/02.

Katika kuhakikisha Ushauri uliotolewa na Ukaguzi unafuatwa, Uongozi wa Shirika

umehakikisha taarifa zote zinazohusu manunuzi zinapatikana kwa wakati na kwa uhakika, Shirika limerekebisha kosoro zote zilizopo kwa kufanya zoezi maalum la kutambuana kuorodhesha mikataba yote iliyofungwa na Shirika, manunuzi yote yaliyofanyika kuhakikisha yanazingatia matakwa ya Sheria ikiwemo kuonekana ndani ya mpango huo. Aidha, matumizi yote yatazingatia bajeti iliyopitiswa na kuridhiwa na bodi ya Wakurugenz.

Aidha, kwa upande wa kitengo cha TEHAMA kilishirikiswa kikamilifu katika kutoa sifa za iPad hizo, kwa kuwa wao ndio waliopewa dhamana na Shirika kwa mujibu wa Muundo kusimamia masuala yote ya Tehama.

**Uchunguzi wa Kamati ya LAAC**

Kamati katika kufuatilia hoja hii imeelezwa kuwa Mamlaka baada ya kuja na mfumo wa e port kwa lengo la kurahisisha utoaji wa huduma kwa wateja wake, Shirika limeamua kununua vifaa vya Tehama kama vile IPAD, CCTV kamera na mfumo wa e-port. hata hivyo Kamati inakubaliana na hoja ya Mkaguzi kwa vile manunuzi hayo hayakuwepo kwenye mpango wa manununzi wa mwaka 2020/2021 Aidha kamati iliomba kupatiwa mikataba ya shirika na mzabuni ambae amenunua vifaa hivyo na mikataba wa kampuni uliyopewa kazi ya kutengeneza mfumo wa e port na kamati imeweza kupatiwa mikataba hiyo.

**Mapendekezo ya Kamati ya LAAC**

Kamati inapenda kusisitiza kutekelezwa kwa ushauri uliotolewa na mdhibiti na mkaguzi mkuu wa Hesabu za Serikali juu ya kuhakikisha Shirika linafanya manunuzi ambayo yamo ndani ya mpango kwa lengo la kukamilisha kutekeleza mipango ya taasisi kama ilivyojipangia ili kuepusha baadhi ya shughuli za taasisi kuzorota au kutofanyika kabisa hali ya kuwa zimo katika utekelezaji wa mpango wa Shirika kwa mwaka husika. Aidha ni vyema kuwashirikisha wahusika katika manunuzi ya vifaa mbalimbali kwa vile wao ndio wenyekujua ubora na sifa (specification) wa vifaa hivyo ili kuepuka ununuzi wa vifaa ambavyo havina sifa wala kuleta tija katika matumizi yake na kuepusha kuingizia Serikali hasara.

### 5.1.3.2 Manunuzi yaliyofanyika bila ya kuzingatia thamani ya fedha (VFM) 588,920,179.54

Kwa mujibu wa kifungu cha 37(c), (e) cha Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa mali za Umma ya mwaka 2016 kinaeleza kuwa ununuzi na uondoshaji wa mali za umma unatakiwa kufanywa kwa mujibu wa misingi ya kuwepo kwa ushindani na kuzingatia thamani ya fedha inapatikana pamoja na kuzingatia hali ya uchumi na ufanisi.

Ukaguzi umebaini kuwa Shirika la Bandari Zanzibar limefanya manunuzi ya vifaa kwa ajili ya uekaji wa mfumo wa mawasiliano kwa upande Shirika la Bandari Pemba (LAN)

pamoja na ununuzi wa “iPad” 13 bila ya kuzingatia thamani ya fedha (uchumi, uwekevu na ufanisi) kuhusiana na matumizi ya iPads hizo.

Aidha, lengo lililokusudiwa la kuanzishwa kwa mfumo wa mawasiliano wa Shirika la Bandari “LAN “kisiwani Pemba halikufikiwa kutokana na kutokuwepo kwa vifaa vya TEHAMA vitakavyotumika katika mfumo huo ikiwemo kompyuta, n.k ambapo ikizingatiwa kiasi kikubwa cha fedha kimetumika katika mradi huo. Kwa hivyo, Shirika la Bandari Zanzibar limetumia gharama kubwa zaidi kuliko thamani halisi ya mradi huo na kuisababishia Serikali hasara.

Kutokuzingatia hali ya uchumi, ufanisi na thamani halisi ya fedha katika manunuzi ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa mali za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Shirika la Bandari Zanzibar kuzingatia tija itakayopatikana kabla ya utekelezaji wa miradi. Mchanganuo wa manunuzi hayo pamoja na gharama zake ni kama inavyoonekana katika Jadweli hapo chini:

**Jadweli Nambari 18: Manunuzi yaliyofanyika bila ya kuzingatia thamani ya fedha**

| Jina la Kampuni | Kiasi cha fedha kilichotumika (Tshs.) | Maelezo |
|---|---|---|
| PC Solution ltd | 100,280,179.54 | Supply of full iPads Pro 12.9 |
| Zan IT Solutions Co. | 488,640,000 | Installation of LAN phase 3 |
| **Jumla** | **588,920,179.54** | |

**Majibu ya Shirika la Bandari Zanzibar**

Uongozi wa Shirika unapenda kuifahamisha Kamati kuwa, katika bajeti ya 2020/2021 haukupanga matumizi ya uwekaji wa LAN kama hoja ya mkaguzi inavyojieeleza, matumizi hayo yalikuwa mwaka 2019/2020. Hata hivyo suala la uwekaji wa LAN limetumia jumla ya Tshs. 488,920,179.54 badala ya Tshs. 588,920,179.54 zilizoripotiwa.

Uongozi wa Shirika ulifanya ushindani katika kumpata mzabuni wa uwekaji wa LAN ambapo jumla ya Kampuni 2 zilishiriki na Kampuni M/s ZanIT solution ilibarikiwa kazi hiyo.

Kazi hiyo haikuwa ya uwekaji wa mfumo wa mawasiliano pekee bali uwekaji wa miundombinu ya TEHAMA iliyojumisha Vifaa vifuatavyo:-

a) Ununuzi na ufungaji wa vifaa vya Local Area Network (LAN)

b) Uwekaji wa miundombinu ya kamera 64 za CCTV.

c) Usambazwaji na uungwaji wa mkonga (National Fiber Backbone) Kazi hizi zilifanyika katika Bandari zote za Pemba (Mkoani, Wete na Wesha).

Hivyo, kwa kuwa kulikuwa na ushindani wa Wazabuni, Shirika lilizingatia thamani halisi ye fedha kwa mujibu wa Sheria ya manunuzi. Kwa upande wa iPad, Uongozi wa Shirika ulizingatia mambo yafuatayo wakati wa ununuzi wa IPAD 13:-Usalama (security mechanism).

Shirika lipo katika maandalizi ya uwekaji wa mfumo wa kielektroniki wa kuendesha vikao vya bodi (Diligent Board) ambapo mfumo huo unatumika vizuri katika bidhaa za apple. Ufanisi na umadhubuti wa kifaa hicho. "Unique Features" zinazotoka na iPad hizo.

iPad hizi zilinunuliwa kutoka kwa wakala pekee wa iStore Tanzania (PC Solution) kwa wakati huo lengo ni kudhibiti thamani halisi ya fedha

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati ya LAAC**

Kamati imebaini Ucheleweshaji wa matumizi wa mfumo wa mawasiliano ya Bandari (LAN) katika Bandari ya Pemba ambapo mfumo huo ili uweze kufanya kazi hutegemea vifaa vyengine vya Tehama kama vile kompyuta, ipad, miundo mbinu ya CCTV kamera n.k ambavyo vilichewa katika ufungaji wake na kusababisha mfumo huo kuchelewa kufanya kazi na kupelekea kukosekana kwa thamani ya fedha iliyotolewa kwa ajili ya ununuzi wa mfumo huo.

Hata hivyo Kamati imeelezwa kuwa kwa sasa Shirika limeshaanza na utaratibu wa uwekaji wa mfumo wa Eport ambao utaenda kutumia miundombinu iliyopo katika Bandari za Pemba.

Kamati inalishauri Shirika kuzingatia thamani ya matumizi ya fedha kwa kutekeleza miradi mbalimbali katika muda uliopangwa ili tija iliyokusudiwa katika miradi hiyo iweze kupatikana katika kipindi kifupi na thamani ya matumizi ya fedha hizo yaweze kuonekana. Aidha Kamati inasisitiza juu ya ukamilishaji wa mfumo wa LAN na E-port ambao utakaopelekea kurahisisha shughuli mbalimbali za Bandari zikiwemo mawasiliano ndani ya Bandari, ili kuongeza ufanisi wa Shughuli za Bandari jambo ambalo litasaidia kuongezeka kwa mapato ya Shirika la Bandari

**\5.1.3.3 Kutokukusanywa kwa shilingi 732,348,980.00 kutokana na tozo ya uhifadhi wa bidhaa Bandarini**

Kifungu cha 57 (3) cha Sheria ya Usimamizi wa kodi ya forodha ya Afrika Mashariki

ya mwaka 2004 kinataka bidhaa zinazouzwa kwa mnada wa hadhara au mkataba wa kibinafsi, kisha mapato yatajumuisha ushuru, gharama za mauzo, kodi na tozo zozote zinazodaiwa za ulinzi wa ghala, gharama za bandari na bidhaa na malipo mengine yoyote.

Katika ukaguzi wetu wa Shirika la Bandari Zanzibar nimebaini kwamba shirika limeshindwa kudai tozo mbalimbali za Bandari ikiwemo tozo za gharama za uhifadhi wa bidhaa bandarini kwa mizigo iliyopitiliza muda wa kisheria wa kuhifadhiwa katika maghala ya bandari na kupelekea bidhaa hizo kuuzwa kwa mnada na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) pasi na Shirika la Bandari kudai gharama za awali za bidhaa hizo baada ya kuuzwa.

Kutokudai gharama za awali za tozo za Bandari kwa bidhaa zilizopigwa mnada na Mamlaka ya Mapato Tanzania kumepelekea Shirika la Bandari kupoteza mapato ya tozo ya forodha kutokana na hifadhi ya bidhaa (Storage charge).

Ukaguzi unashauri uongozi wa Shirika la Bandari Zanzibar kukaa pamoja na uongozi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa lengo la kujadili na kukubaliana bidhaa yoyote itakayouzwa kwa njia ya mnada kuhakikisha tozo zote za bandari zinalipwa kabla ya bidhaa hizo kupewa mnunuzi ili kudhibiti upotevu wa mapato Serikalini.

### Majibu ya Shirika la Bandari Zanzibar (ZPC)

Uongozi wa Shirika unakiri huko nyuma ulikuwa ukifatilia malipo yake ya bidhaa kutoka TRA kupitia vikao mbalimbali ambavyo vinahusisha watendaji wa TRA na Shirika la Bandari bila mafanikio. Barua tofauti ziliwasilishwa mamlaka ya lengo la kukumbushia malipo hayo. Hata hivyo hakuna fedha iliyopatikana baada ya Hivyo Uongozi wa Shirika kwa hatua Zaidi uliwaandikia Barua Uongozi wa Mamlaka ya mapato Tanzania (TRA)

Shirika la Bandari lilifanya utaratibu wa kuwaandikia madai TRA mwezi wa Ogasti 2022 na kuhusiana na makontena yaliyopelekwa kwao kwa ajilio ya kutulipa fedha za lifting charges na Storage charges hadi sasa Taasisi hiyo haijalipa wala kutoa mrejesho wa deni hilo na badala yake wanakumbushia makontena zaidi yapelekwe kwa ajili yam nada. Shirika kwa sasa lipo kwenye hatua ya kukaa pamoja na TRA kulitatua jambo hili.

### Uchunguzi wa Kamati ya LAAC

Kamati imeelezwa jitihada mbalimbali ambazo zinafaywa na Shirika katika kufuatilia deni hilo katika Mamlaka ya Mapato Tanzania TRA lakini bado jitihada zaidi zinahitajika katika kuhakikisha deni hilo linalipwa kwani ni miongoni mwa chanzo kikubwa cha mapato kwa upande wa Shirika

### Mapendekezo ya kamati

Kamati inaomba wizara kuingilia kati suala hili kwa kufanya vikao vya pamoja baina Wizara, Uongozi wa Shirika la Bandari pamoja na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ili kulipatia ufumbuzi suala hili ili deni hilo la Shirika liweze kulipwa Aidha Kamati

inalishauri shirika la Bandari kutafuta mfumo madhubuti utakaosaidia kutoza tozo zote bandari bila ya usumbufu wowote kabla ya kontena kutolewa Bandarini na Kukabidhiwa TRA kwa ajili ya kupiga mnada kwa lengo la kuliongezea mapato Shirika.

#### 5.1.3.4 Kutokufanyika kwa zoezi la utambuzi na uthibitisho wa mali za kudumu za Shirika shilingi 90,039,232,318.7

Shirika la Bandari Zanzibar lina wajibu wa kufanya zoezi la utambuzi na uthibitishaji wa mali za kudumu mara moja kila mwaka. Matokeo yataoanishwa na daftari la kumbukumbu za mali ya Shirika ambalo litawekwa ili kurekodi na kufuatilia mienendo ya mali zote za kudumu za Shirika.

Ukaguzi umebaini kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni 2021, Shirika la Bandari liliripoti mali za kudumu zenye thamani ya shilingi 90,039,232,318.7, dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kutokufanyika kwa zoezi la uhakiki na utambuzi wa mali za kudumu ili kuhakikisha miongoni mwa mali zilizopo na hali halisi ya ufanyaji kazi wa mali hizo.

Kukokufanyika kwa zoezi la uhakiki na utambuzi wa mali za kudumu za Shirika kunapelekea kukosekana kwa usahihi wa taarifa ya thamani ya mali za kudumu za Shirika katika hesabu za mwisho wa mwaka jambo ambalo linaweza kusababisha uwezekano mkubwa wa taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka za Shirika kutokuonesha sura sahihi na halisi.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Shirika la Bandari kuhakikisha unafanya zoezi la utambuzi na uhakiki wa mali za kudumu kila mwaka kwa mujibu wa utaratibu ili kuenda sambamba na zoezi la ufungaji wa hesabu za mwisho wa mwaka ambazo zitaonesha sura sahihi na halisi.

#### Majibu

Shirika la Bandari limeomba kwa Afisi ya Rais Fedha na Mipango kupitia idara yake ya Hazina kuhusiana na zoezi hili kazi ilianza kwa kutia code kwa kila mali ya Shirika na taarifa zote zimekusanywa kwa ajili ya kuzitunza kwenye Taarifa za Mali ya Kudumu ambapo saivi tupo katika hatua hiyo bado taarifa hizo hazijawasilishwa kwenye Shirika.

Kwa sasa zoezi limeshakamilika ya kuhakiki mali za Kudumu na tupo katika hatua ya kuweka kumbukumbu katika vitabu vya Mali Za kudumu (Fixed Asset Register)

#### Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Kamati imebaini kuwa Shirika lilikuwa linafanya tathmini ya mali zake za kudumu bila ya kuzikagua nakuzitembelea ili kubaini hali halisi ya uchakavu wake jambo ambalo linakwenda kinyume na sheria na kupelekea kushidwa kupata thamani halisi ya mali za kudumu za Shirika.

Kamati inaendelea kuishauri Ofisi ya Rais fedha na Mipango kuharakisha zoezi la

uundwaji wa kitengo cha Usimamizi wa mali za kudumu (Asset Management Unit) kwa kila Taasisi, Mamlaka na Mashirika ya Serikali ili Shughuli za Kuhakiki mali za kudumu zifanywe ndani ya taasisi husika ili Changamoto za kuhakiki taarifa za mali za kudumu ambazo kwa sasa taasisi na Mashirika zinakumbana nazo ziweze kuondoka moja kwa moja.

### 5.1.3.5 Mazingira yasiyoridhisha ya utendaji kazi katika chumba cha mawasiliano ya kuongozea meli cha Bandari Malindi

Katika ukaguzi wa shirika la Bandari uliofanyika imebainika kuwa chumba cha mawasiliano ya kuongozea vyombo vya baharini katika Bandari ya Malindi kinafanya kazi katika mazingira magumu kama ifuatavyo:-

- Kuna Redio mbili za VHF MARINE ambazo hazipo vizuri kwa ajili ya mawasiliano kati ya Operetawa chumba cha mawasiliano na Meli inayoingia. Redio zilizopo ni za kizamani ambazo zina uwezo mdogo wa kiutendaji na ambazo hazina ufanisi katika kufanya mawasiliano ya masafa marefu ambapo kama ikitokezea tatizo, janga au uharibifu wa bahari hakutakuwa na uwezo wa kufanya mawasiliano kutokana na udhaifu wa mawimbi ya sauti ya vifaa hivyo kutokufika katika sehemu husika.
- Uwepo wa rada ambayo haifanyi kazi kwa muda mrefu na inahitaji ukarabati mkubwa au ununuzi wa rada mpya jambo ambalo linasababisha ugumu sana kwa watu wa mawasilano ya Bandari au waongozaji wa vyombo vya baharini kutambua (detect) vyombo vidogo kama vile mashua na jahazi vinavyopita maeneo ya mipaka ya Bandari hali inayopelekea kuhatarisha usalama wa vyombo, maisha ya mabaharia pamoja na kushindwa kubaini vitendo vya Uharamia(Pirates) vinavyoweza kufanyika.
- Ukosefu wa mafunzo ya mara kwa mara ya usalama kwa watendaji wa chumba cha mawasiano ya Bandari katika kipengele cha usalama wa Bandari.
- Kukosekana kwa mazingira sahihi ya chumba cha mawasiliano ya kuongoza meli jambo ambalolinapelekea Waongozaji wa meli kupata taarifa kutoka kwa mabaharia wanaofanya kazi katikavyombo vya Tagi.
- Kutokuwaekea mazingira bora watendaji wa Chumba cha Mawasiliano ya Kuongozea Meli jambo ambalo linapelekea kupungua kwa ufanisi wa kazi na hatimae kupelekea kupungua kwamakusanyo ya mapato ya Shirika.

Kukosekana kwa vifaa vya kisasa vya kuongozea meli katika chumba cha mawasiliano kunapelekea ugumu wa kuhudumia Meli zilizopo masafa marefu na ya kati zinazohitaji kuingia Bandarini Zanzibar.

Aidha, kukosekana kwa vyombo vya kisasa vya mawasiliano ya Tehama

kunahatarisha usalama wa Bandari na pia kukosekana kwa mafunzo sahihi ya mara kwa mara ya usalama kwa watendaji wa kitengo cha mwasiliano ya kuongozea Meli cha Bandari kunaweza kupelekea watendaji hao kushindwa kujilinda pindi madhara yanapotokea.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Shirika la Bandari Zanzibar kuhakikisha kwamba unaboresha mazingira ya chumba cha mawasiliano ya kuongozea meli, kuimarisha maslahi ya watendaji wa kitengo cha mawasiliano ya kuongozea meli pamoja na uwepo wa vitendea kazi vya kisasa.

**Majibu ya Shirika la Bandari Zanzibar (ZPC)**

Uongozi utaanzisha mfumo wa e-port ambao utakuwa na vifaa mbalimbali vya kufuatilia mwenendo wa meli.

Ni kweli kwa sasa chumba cha kuongozea meli hakipo katika hali nzuri, Shirika limejipanga kujenga chumba cha kuongozea meli cha kisasa katika eneo la Bandarini ndani eneo la Scanner ya TRA. Ni kweli Shirika la Bandari linasumburi na tatizo la kuviona vyombo pamoja na kujua mwendo kasi wake wakati wa kuingia na kutoka. Hii inatokana na vifaa viliopo hivi sasa vinaudhaifu. Shirika limeshafungiana mkataba na kampunzi ya FOTRIS na WATSILAT kwa ajili ya kufanya kazi Ujenzi wa zifuatazo:

- Mnara wa kuongozea meli ambapo maopereta wataweza kuona vyombo vyote vinavyoingia na kutika kwa macho.
- Uwekaji waVTS ambao utakuwa na mambo yafuatayo:
- CCTV Camera¬ ambapo itaweza kurekodi picha pamoja na video katika mfumo wa 3D.
- Ufungaji wa¬ mfumo wa hali ya hewa ambapo utasaidia vyombo vyote vya Zanzibar na maeneo ya karibu kupata taarifa ya hali ya hewa.
- Ufunguji wa¬ Rada kwa ajili ya kuona vyombo vyote ambavyo vinafanyakazi katika bandari yetu.
- Kufungwa AIS¬ kwa ajili ya kuthibiti mwendo kasi wa vifaa GMDS kwa¬ ajili ya hali ya dharura.
- MF na HF kwa¬ ajili ya mawasiliano.

Wafanyakazi wamepatiwa mafunzo katika kipindi tofauti katika Nyanja mbalimbali za uendeshaji wa huduma

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kwa vile Shirika limekiri kuwepo kwa changamoto hiyo na kuilezea Kamati hatua

mbalimbali ambazo wanataka kuzitekeleza ili kuondoa changamoto hizo.

Hata hivyo Kamati inaliomba Shirika la Bandari Zanzibar kuchukua hatua za haraka katika kuboresha kituo hicho kwa kupatikana kituo chengine chenye mazingira mazuri ya utendaji kazi, vifaa vya kisasa vya mawasiliano n.k aidha mafunzo kwa watendaji wa kituo hicho yaendelee kutolewa kwa nyakati tofauti ili ufanisi na utendaji wa kituo hicho uweze kupatikana wa kunusuru na Kusaidia hali za hatari na majanga zinapotokea katika vyombo vya usafiri baharini.

SHIRIKA LA BANDARI - PEMBA

**5.1.3.6. Dosari zilizobainika katika mapokezi ya vitabu vya mapato.**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika uwepo wa dosari za mapokezi ya vitabu vya mapato katika Shirika la Bandari Pemba ambapo dosari hizo ni kama zifuatazo:-

- Kutokujulikana idadi kamili ya vitabu vilivyopokelewa.
- Kukosekana kwa uthibitisho wa mapokezi (Delivery Order).

Kukosekana kwa taarifa kamili ya vitabu vilivyowasilishwa kutoka makao makuu ya Shirika la Bandari Zanzibar na kujulikana idadi halisi ya vitabu vilivyopokelewa kunatia shaka juu ya ukusanyaji wa mapato kuwa umeendana na vitabu halisi vilivyopokewa jambo ambalo linaweza kupelekea upotevu wa mapato kwa kutumia vitabu ambavyo havikupokelewa na kuorodheshwa katika daftari maalum la kuwekea kumbukumbu za vitabu vya ukusanyaji wa mapato (counter foil register).

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Shirika la Bandari – Pemba kuhakikisha kwamba mapokezi yote yanayofanyika yanatakiwa kufuata utaratibu ikiwemo kuweka rikodi katika vitabu vya uthibitisho wa mapokezi na kuwasilisha hati ya mapokezi (delivery Order).

**Majibu ya Shirika la Bandari Zanzibar (ZPC)**

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 jumla ya vitabu 400 vya kukusanyia mapato Idadi ya vitabu vilivyotoka Unguja kwenda Shirika la Bandari Pemba kwa mwaka wa Fedha 2021 ilikua ni vitabu 400 vya kukusanyia mapato vilivyo rikodiwa kwenye counter foil namba 0801-0900 vilipokelewa kutoka Makao makuu ya Shirika kwa utaratibu wa makabidhiano kati ya watendaji kutoka makao makuu na watendaji wa Tawi. Vitabu hivyo vyote vilirekodiwa katika Counter Foil Register kabla ya kusambazwa katika vituo vya matumizi kwa ajili ya kufanyiwa kazi.

Kwa sasa utaratibu wa kupokea vitabu umeandaliwa, ambapo vitabu vinakuja

Pemba baada ya Mkurugenzi Tawi kuandika barua ya kuomba idadi ya vitabu vinakavyohitaji kwa matumizi ya Tawi Pemba na makabadhiano ya vitabu hivyo ni kupitia delivary Note

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati katika kufuatilia hojahii imeomba kupatiwa (Counter fail register) la Shirika ambapo kamati ilipatiwa daftari hilo ambalo lilikuwa limerodhosha vitabu vya mapato vilivyopokelewa kwa mwaka wa fedha 2020/2021 lakini halikua na alama yoyote inayotoa ishara ya kukaguliwa na Mkaguzi kwa maana Mkaguzi hakuliona katika ukaguzi wake, Aidha Kamati iliomba uthibitisho wa mapokezi ya vitabu hivyo yani (Delivery Oder) haikuweza kupatikana kwa ukaguzi.

Hata hivyo Kamati inakubalina na ushauri ulitolewa na Mkaguzi wa kulitaka Shirika katika Kufuata sheria wakati wanapopokea vitabu vya mapato kwa kurikodi vitabu hivyo katika vitabu vya mapokezi na kuwasilisha hati ya mapokezi ya vitabu hivyo yani (Delivery Oder), aidha Shirika kuwa na utaratibu mzuri wa kuhifadhi taarifa mbalimbali ili zinapohitajika na Mkaguzi ziweze kupatikana kwa wakati

### 5.1.3.7 Kukosekana kwa mapato yatokanayo na maegesho ya Meli na Tozo ya Mafuta shilingi 13,862,132.3

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Shirika la Bandari - Pemba linadai mapato yatokanayo na maegesho ya Meli (dockage) pamoja na mapato ya ardhia (wharfage) katika Bandari ya Wesha.

Ukaguzi umebaini kwamba kampuni ya GAPCO imetumia huduma ya Bandari kwa ajili ya Maegesho ya upakuzi wa mafuta kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 hawakuweza kulipia huduma zinazotolewa na Bandari ya Wesha yenye jumla ya shilingi 5,821,113.

Aidha, imebainika Shirika la Meli Zanzibar limetumia huduma zinazotolewa na Bandari ya Wesha kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 na kushindwa kulipia huduma hizo zenye thamani ya shilingi 8,041,019.3 jambo ambalo limepelekea kudhorotesha malengo ya Shirika waliyojipangia.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 29(3) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri Shirika la Bandari – Pemba kuhakikisha linafanya ufuatiliaji wa haraka kuhakikisha malipo hayo yanalipwa na kuweka Sera madhubuti ikiwemo kuweka adhabu (penalty) kwa kampuni, taasisi au shirika lolote litakaloshindwa kulipa malipo yake kwa wakati.

Mchanganuo wa mapato ya maegesho ya Meli na Tozo ya Mafuta yaliyokosekana ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 20 : Mapato yaliyokosekana yatokanayo na maegesho ya Meli na Tozo ya Mafuta**

| Nambari ya Ankara | Tarehe ya Ankara | Jina la mdaiwa | Jina la chombo | Kiasi cha mapato kinachodaiwa (Tshs.) |
|---|---|---|---|---|
| 0594 | 31/08/2020 | Zanzibar Shipping Corp | Mt. Ukombozi | 430,227.76 |
| 0595 | 31/08/2020 | Zanzibar Shipping Corp | Mt. Ukombozi II | 523,543.36 |
| 0603 | 25/09/2020 | Zanzibar Shipping Corp | Mt. Ukombozi | 763,497.76 |
| 0610 | 21/10/2020 | Zanzibar Shipping Corp | Mt. Ukombozi | 811,107.76 |
| 0612 | 21/10/2020 | Zanzibar Shipping Corp | Mt. Ukombozi | 717,411.10 |
| 0615 | 30/10/2020 | Zanzibar Shipping Corp | Mt. Ukombozi | 739,692.76 |
| 0644 | 29/01/2021 | Zanzibar Shipping Corp | Mt. Ukombozi | 906,327.76 |
| 1661 | 02/03/2021 | Zanzibar Shipping Corp | United spirit | 763,497.76 |
| 1679 | 21/05/2021 | Zanzibar Shipping Corp | Mt. Ukombozi | 858,717.76 |
| 1682 | 25/05/2021 | Zanzibar Shipping Corp | Mt. Ukombozi | 763,497.76 |
| 1689 | 29/06/2021 | Zanzibar Shipping Corp | Mt Ukombozi | 763,497.76 |
| 1654 | 16/02/2021 | GAPCO Zanzibar Ltd Pemba | Malipo ya Ardhia (Wharfage) | 166,350 |
| 1660 | 02/03/2021 | GAPCO Zanzibar Ltd Pemba | Malipo ya Ardhia (Wharfage) | 1,178,610 |
| 1685 | 21/05/2021 | GAPCO Zanzibar Ltd Pemba | Malipo ya Ardhia (Wharfage) | 1,205,133 |
| 1681 | 25/05/ 2021 | GAPCO Zanzibar Ltd Pemba | Malipo ya Ardhia (Wharfage) | 896,703 |
| 1699 | 21/05/ 2021 | GAPCO Zanzibar Ltd Pemba | Malipo ya Ardhia (Wharfage) | 1,205,133 |
| 1688 | 29/06/ 2021 | GAPCO Zanzibar Ltd Pemba | Malipo ya Ardhia (Wharfage) | 1,169,184 |
| **Jumla Ndogo** | | | | **5,821,113.0** |
| **Jumla Kuu** | | | | **13,862,132.3** |

**Majibu ya Shirika la Bandari**

Uongozi wa Shirika la Bandari Tawi la Pemba uliufanyia kazi ushauri wa Mkaguzi wa kufanya ufuatiliaji wa malipo hayo kutoka kwa GAPCO na tayari malipo hayo

yameshalipwa. Kwa upande wa Shirika la Meli Zanzibar bado malipo hayajafanyika pamoja na Shirika kufanya jitihada za kuwaandikia barua ya madai.

Kwa sasa Shirika limejiunga na mfumo wa TANCIS ambapo malipo yote ya Meli za nje na Mafuta yanalipwa moja kwa moja kupitia mfumo huo ambao unasismamiwa na Mamlaka ya Mapato (TRA)

**Uchunguzi wa Kamati**

Kamati inalipongeza Shirika kwa jitihada walizozichukua za kulipwa deni lote wanalodai katika Kampuni ya GAPCO Zanzibar Ltd Pemba, aidha kuongeza ufanisi wa ukusanyaji wa mapato ya mafuta kujiunga na mfumo wa TANCIS ambao utarahisisha ulipaji wa mafuta kwa meli zinatoka nje ya nchi hata hivyo kamati haijaridhika na jitihada za Shirika la Bandari za kufuatilia deni la Shirika la Meli kwa hadi kamati inapita katika uchunguzi wake deni hilo halijalipwa kabisa.

**Mapendekezo ya Kamati**

Kamati inalishauri Shirika la Bandari kukaa na Uongozi wa Shirika la Meli ili kulipatia ufumbuzi deni hilo kwani ni moja wapo ya chanzo cha mapato ya Shirika ambacho kinategemewa katika kuliendeleza Shirika katika Shughuli zake mbalimbali.

### 5.1.3.8 Upotevu wa mapato yatokanayo na tozo mbali mbali za Bandari shilingi 187,378,815.58

Shirika la Bandari tawi la Pemba lina wajibu wa kukusanya mapato kutoka katika vyanzo vyake mbali mbali vya bandari na maeneo mengineyo.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Shirika la Bandari - Pemba limekusanya kupitia ankara za mapato yenye jumla ya shilingi 23,766,907.20 kutokana na tozo mbali mbali bandarini, dosari iliyobainika na ukaguzi ni kukosekana kwa taarifa za kumbukumbu katika daftari la mapato pamoja na kukosekana kwa uthibitisho wa mapato hayo kuwasilishwa benki jambo ambalo limetia shaka juu ya mapokezi ya mapato hayo.

Aidha, imebainika uwepo wa upotevu wa mapato yenye thamani ya shilingi 163,611,908.38 yanayotokana na tozo mbali mbali ambapo imebainika kutokurikodiwa katika daftari la mapato kwa baadhi ya mapato hayo na kukosekana kwa uthibitisho kwa baadhi ya mapato hayo kuwasilishwa benki hadi ukaguzi unakamilika, **Kiambatisho Nambari 1 Kinahusika.**

Kutokurikodiwa kwa mapato na kukosekana kwa uthibitisho wa mapokezi ya mapato hayo katika taarifa za benki ni kwenda kinyume na kifungu nambari 30(1)(2)(3) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Shirika la Bandari – Pemba kuchukuwa hatua za kinidhamu kwa wale wote watakaobainika kufanya vitendo vya kusababisha upotevu wa mapato hayo.

**Majibu ya Shirika la Bandari (ZPC)**

Ni kweli kwamba utaratibu wa awali ambao ulikua umezoeleka katika uwekaji wa rikodi za makusanyo pamoja na uwasilishaji wa makusanyo hayo kunakohusika (benki) haukua mzuri na unapelekea mashaka, hata hivyo kupitia upekuzi wa nyaraka mbalimbali zilizotumika imebainika kuwa fedha hizo zimerikodiwa na kufikishwa kunakohusika kwa mujibu wa Sheria. Katika kuhakikisha kuwa suala hili la kutiliwa shaka halitokezei tena Shirika la Bandari limechukua hatua zifuatazo:- i) Kujiunga na mfumo wa ki-electronikiwa kukusanyia mapato wa Serikali (ZAN MALIPO) unaosimamiwa na (OR) Fedha na Mipango chini ya Wakala wa Serikali Mtandao (E- GOVERNMENT)

Katika kuhakikisha kuwa suala hili la kutiliwa shaka halitokezei tena Shirika la Bandari limechukua hatua zifuatazo:-

i) Kujiunga na mfumo wa ki-electronikiwa kukusanyia mapato wa Serikali (ZAN MALIPO) unaosimamiwa na (OR) Fedha na Mipango chini ya Wakala wa Serikali Mtandao (E- GOVERNMENT)

ii) ii)Mapato yote kulipwa kwa njia ya Benki kupitia Wakala wa Benki.

iii) iii)Mapato yote yatokanayo na meli za nje hulipwa moja kwa moja TRA kupitia mfumo wa TANCIS.

**Uchunguzi wa Kamati**

Katika kufuatilia hoja hii Kamati imebaini yafuatayo:

Mapato yaliyokusanywa katika Bandari ya Wete hayakuonekana katika taarifa za mwisho za hesabu yani “financial statement”

Ucheleweshaji wa upelekaji wa mapato benki baada ya kukusanywa, na kupelekea utofauti wa mahesabu ya mapato katika taarifa za mwisho za hesabu “financial statement”

Makusanyo ya mapato yalikusanywa kwa njia ya mkononi badala ya kutumia mifumo.

Hata hivyo Kamati inaifuta hoja hii kwa vile Shirika limekiri kutokea kwa dosari na tayari imeshachukua hatua kadhaa za kuimarisha ukusanyaji wa mapato na kudhibiti mianya ya upotevu wa mapato hayo kwa kuanza kutumia mifumo mbalimbali ya Ki-elektroniki ya ukusanyaji mapato ikiwemo mfumo wa (Zan

MALIPO) Wakala wa Benki na mfumo wa TANCIS.

**Mapendekezo ya Kamati**

Kamati inaishauri Mamlaka katika kuendelea kufuata sheria na miongozo mbalimbali inayotelewa na Serikali katika ukusanyaji wa mapato kwa njia ya Ki - elektroniki ili kudhibiti upotevu wa mapato ya Shirika,

Aidha Kamati inaushauri uongozi wa Shirika kufanya uchunguzi na kubaini watendaji wote waliohusika na upotevu wa Tzs 163,611,908.38 zinazotokana na tozo mbalimbali ili kuweza kuwachukulia hatua stahiki kwa mujibu wa Sheria na iwe fundisho kwa watendaji wengine watakaosababisha uzembe kama huo kutokea.

### 5.1.3.10 Shirika kushindwa kufikia lengo la ukusanyaji mapato shilingi 1,538,540,289.53

Jumla ya shilingi 1,538,540,289.53 zilikadiriwa kukusanywa na Shirika la Bandari tawi la Pemba kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Ukaguzi umebaini kwamba makadirio haya ni makubwa ukilinganisha na makusanyo halisi kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ambapo hadi kufikia 30 Juni 2021, jumla ya shilling 1,050,886,458.73 zilikusanywa sawa na asilimia 68.30 ya makadirio. Hali hii inaonyesha kuwepo kwa upungufu wa fedha za makusanyo zenye jumla ya shilingi 487,653,830.8 sawa na asilimia 31.6

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 32(1) (2) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Shirika la Bandari – Pemba ni vyema kuwa na makadirio halisi ya mapato kulingana na uwezo wa shirika pamoja na vyanzo vya mapato walivyonavyo ili kuweza kufikia malengo yaliyowekwa ya shirika kwa mwaka husika

**Majibu ya Shirika la Bandari (ZPC)**

Ni kweli kuwa makadirio ya ukusanyaji mapato kwa mwaka 2020/2021 haya kuweza kufikiwa hii ilitokana na kuzuka kwa ugonjwa wa COVID 19, ambao ulisababisha shughuli za usafiri na usafirishaji katika dunia kupungua kwa kiasi kikubwa, jambo ambalo lilipelekea mapato kushuka na kutofikia malengo yaliyokadiriwa kwa mwaka husika. Hata hivyo upungufu huu umetokana na kutopata kwa wakati mapato ya minara kwa robo ya tatu na robo ya nne

Hata hivyo Uongozi wa Shirika umeboresha huduma baada ya kupungua kwa COVID na kwa sasa Shirika linafikia malengo inayojipangia kwa mwaka.

Kuongeza udhibiti na ufanisi wa kukusanyia mapato kwa njia ya ki- eletroniki kama ZAN MALIPO,Wakala wa Benki na TANCIS, ili kuongeza ufanisi zaidi wa katika

ukusanyaji wa mapato

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati imebaini ni kweli ukosefu wa fedha za malipo ya minara kutoka bandari ya Tanzania TPA yamepelekea kwa kiasi kikubwa kushuka kwa mapato ya Shirika kwa upande wa Pemba hata hivyo kamati imepewa taarifa kuwa tayari mapato hayo yameshalipwa yenye jumla ya Tzs 209,084,916.

Kamati inalishauri Shirika kuongeza wigo wa ukusanyaji mapato kwa kusimamia vyema vyanzo mbalimbali vya mapato ya Shirika kwa lengo la kuweza kufikia makadirio ya mapato waliyojiwekea katika mwaka husika.

### 5.1.3.10 Malipo kwa watoa huduma ambao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za umma shilingi 64,523,945.4

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(1) cha Sheria ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma kinaeleza kulingana na masharti ya sheria hii mtu, kampuni au taasisi haitawasilisha zabuni au vyenginevyo kushiriki katika manunuzi ya Umma isipokua chombo kiwe kimesajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi.

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(2), zabuni kutoka kwa mtu, kampuni au chombo ambacho hakijasajiliwa haifai na hakitazingatiwa na taasisi ya ununuzi.

Ukaguzi umebaini kwamba Shirika la Bandari - Pemba limefanya manunuzi na watoa huduma mbali mbali ambao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya Zanzibar na kupelekea upotevu wa mapato ya Serikali.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na vifungu vya Sheria nilivyovinakili hapo juu vya Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Shirika la Bandari – Pemba kufanya manunuzi kwa kuzingatia kanuni,sheria pamoja na miongozo mbali mbali iliyopo.

Mchanganuo wa watoa huduma ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

**Jadweli Nambari 21: Malipo kwa watoa huduma ambao hawakusajiliwa**

| Hati Namba | Hundi Namba | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs.) | Alielipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 17/07<br>01/07/2020 | 002337 | 3,023,400 | Zanzibar Petroleum Ltd | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya Diesel na Petroli |
| 35/07 | 002355 | 821,318.40 | Mohammed Amour | Malipo ya fedha kwa ajili ya |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 17/07/2020 | | | Abdalla | upelekaji wa maji |
| 38/07<br><br>20/07/2020 | 002358 | 3,023,400 | Zanzibar Petroleum Ltd | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya Diesel na Petroli |
| 39/07<br><br>15/05/2020 | 002359 | 950,600 | Mohammed Amour Abdalla | Malipo ya fedha kwa ajili ya kukodi kijiko na gari ya kubebea udongo |
| 50/08<br><br>10/08/2020 | 002368 | 3,309,300 | Zanzibar Petroleum Ltd | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya Diesel na Petroli |
| 55/08<br><br>21/08/2020 | 002373 | 3,309,300 | Zanzibar Petro-<br><br>leum Ltd | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya Diesel na Petroli |
| 56/8<br><br>21/08/2020 | 002374 | 1,200,000 | Ahaabna restaurant | Malipo ya fedha kwa ajili ya chakula |
| 93/09<br><br>10/09/2020 | 002403 | 3,453,000 | Zanzibar Petroleum Ltd | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya Diesel na Petroli |
| 112/09<br><br>18/09/2020 | 002417 | 821,318 | Mohammed Amour Abdalla | Malipo ya fedha kwa ajili ya kupeleka maji |
| 119/09<br><br>28/09/2020 | 002424 | 3,468,600 | Zanzibar Petroleum Ltd | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya Diesel na Petroli |
| 130/09<br><br>18/09/2020 | 002428 | 2,211,600 | Ali Mohammed<br><br>Khamis | Malipo ya fedha kwa ajili ya fundi kwa kazi ya ujenzi wa choo |
| 137/10 | 002433 | 1,500,000 | Ahaabna Restaurant | Malipo ya fedha kwa ajili ya |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 12/10/2020 | | | | chakula |
| 140/10<br>16/10/20 | 002436 | 4,624,800 | Zanzibar Petroleum Ltd | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya Diesel na Petroli |
| 155/10<br>16/10/2020 | 002447 | 4,500,000 | Mbarouk Salim Ali | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi |
| 175/11<br>16/11/2020 | 002461 | 4,569,200 | Zanzibar Petroleum Ltd | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya Diesel na Petroli |
| 246/1<br>31/12/2020 | 002502 | 4,511,200 | Zanzibar Petroleum Ltd | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya Diesel na Petroli |
| 266/1<br>14/1/2021 | 002516 | 6,913,900 | Hamad Said Bakar | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi |
| 270/1<br>18/1/2021 | 002520 | 817,516 | Bai Sign Writer | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa mabango ya kuandikia habari |
| 311/02<br>19/02/2021 | 002548 | 475,300 | Mustafa Mohammed Zahoro | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa chokaa |
| 334/03<br>17/03/2021 | 002560 | 4,693,600 | Zanzibar Petroleum Ltd | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya Diesel na Petroli |
| 350/04<br>30/04/2021 | 002572 | 1,500,000 | Ahaabna Restaurant | Malipo ya fedha kwa ajili ya chakula |
| 381/04<br>16/04/2021 | 002590 | 821,318 | Mohammed Amour Abdalla | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa maji |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 384/04 16/04/2021 | 002593 | 783,275 | Ali Mohamed Khamis | Malipo ya fedha kwa ajili ya kazi ya ufundi |
| 403/5 18/5/2021 | 002602 | 3,222,000 | Zanzibar Petroleum Ltd | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya Diesel |
| **Jumla** | | **64,523,945.4** | | |

**Majibu ya Shirika la Bandari Zanzibar**

Ni kweli katika ukaguzi imebainika kua baadhi ya wafanyabiashara hawakusajiliwa na mamlaka ya Ununuzi hali ambayo ilisababishwa na ukosefu wa Afisa Ununuzi ambae angeweza kuwachunguza Wafanyabiashara alosajiliwa. Hivyo Shirika limechukua hatua ya kuhakikisha kitengo cha ununuzi kinakuepo pamoja na Afisa ununuzi, ili kusimamia na kufuatilia shughuli zote za manunuzi na ugavi kwa taratibu na kanuni zinazo kubalika.

Shirika limeacha kutumia mfumo wa zamani wa ununuzi (Manual Procurement System) na sasa unatumia mfumo mtandao wa Ununuzi (E- proZ) unaosimamiwa na Mamlaka ya Manunuzi Zanzibar.

Aidha Shirika limetoa elimu kwa wafanyabiashara wachache walio kua hawajasajiliwa na tuliwaeleza juu ya utaratibu unao takiwa ili waweze kufanya biashara na mashirika pamoja na taasisi za serikali miongoni mwa wafanya biashara hao ni Mbarouk Salim Ali, Tahfif Alluminium& and Glass Work Shop na Zanzibar Petrolium

Vile vile Shirika linachukua hatua ya kufanya biashara na wafanya biashara walio sajiliwa baada ya kujirizisha kuwa na uhalali na vigezo vyote vinavyo waruhusu kufanya biashara na Serikali

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kwa vile Shirika limekiri kufanya malipo kwa watoa huduma ambao hawakusajiliwa, hata hivyo Kamati inaifuta hoja hii kwa vile Shirika limeshachukua jitihada za kutosha na kuahidi haitopokea huduma yoyote kwa Kampuni au Taasisi ambazo hazijasajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi.

Kamati inalishauri Shirika kuendelea na utaratibu wa kufanya biashara na watoa huduma ambao tayari wameshasajiliwa na wameshaingizwa katika mfumo wa manunuzi ili kuepusha dosari kama hizi kutokea tena.

### 5.1.3.11 Kukosekana kwa marejesho ya malipo ya masurufu shilingi 7,085,000

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 7,085,000 zimelipwa kwa matumizi mbali mbali ya Shirika la Bandari Pemba kupitia malipo

ya masurufu lakini marejesho ya masurufu hayo yamekosekana kwa ajili ya ukaguzi ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya Zanzibar nambari 12 ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Shirika la Bandari – Pemba kufanya malipo kwa kuzingatia kanuni, sheria na miongozo ya fedha iliyopo. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 22: Marejesho ya malipo ya masurufu yaliyokosekana**

| Hati Namba | Hundi Namba | Kiasi cha Fedha kili- cholipwa (Tshs.) | Maelez o |
|---|---|---|---|
| 41/07 24/07/2020 | 002361 | 3,150,000 | Malipo ya fedha za imprest kwa kazi mbali mbali |
| 43B/07 28/07/2020 | 002366 | 1,800,000 | Malipo ya fedha za imprest kwa kazi mbali mbali |
| 248/1 14/1/2021 | 002504 | 1,600,000 | Malipo ya fedha za imprest kwa ajili ya kazi ya usafi |
| 373/04 16/04/2021 | 002586 | 535,000 | Malipo ya fedha za imprest kwa ajili ya kazi ya usafi |
| **Jumla** | | **7,085,000** | |

**Majibu ya Shirika la Bandari Zanzibar**
Baada ya ukaguzi kuisha Shirika la Bandari Tawi Pemba limefanya jitihada ya kudai marejesho na kwa sasa marejesho ya malipo ya masurufu yote tayari yamesharejeshwa na yameshakamilika.

Aidha malipo yote kwa sasa yanafanyiwa marejesho kwa wakati.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**
Kamati imerizika na majibu yaliyotolewa na Mamlaka na inaifuta hoja hii kwa vile tayari hatua zimeshachukuliwa za kukamilisha upatikanaji wa marejesho ya malipo ya masurufu ya Tzs 7,085,000 hata hivyo Kamati inaungana na Ushauri uliotolewa na Mkaguzi wa Kuhakikisha Shirika inafanya malipo kwa kuzingatia kanuni, sheria, na miongozi ya fedha iliyopo.

**Mapendekezo ya Kamati**

**5.1.3.12 Malipo ya mishahara kwa wafanyakazi wasiokuwa na mikataba ya kazi shilingi 16,070,098.6**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 16,070,098.6 zimelipwa kwa wafanyakazi wanne (4) wa muda wa Shirika la Bandari - Pemba

lakini mikataba yao ya kazi imekosekana kwa ukaguzi.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 135(1) cha Kanuni ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2014.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Shirika la Bandari – Pemba kuhakikisha kwamba kama kutakuwa na ulazima wa kutumia watumishi wa kutwa ni vyema Mkuu wa Taasisi kuomba kibali kwa Tume ya Utumishi husika kwa lengo la kumjazisha mkataba mtumishi huyo.

Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 23: Malipo ya mishahara kwa wafanyakazi wasiokuwa na mikataba ya kazi**

| Hati Namba | Hundi Namba | Kiasi cha Fedha kilicholipwa (Tshs.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 18/07 17/07/2020 | 002344 | 1,382,702 | Shirika la Bandari tawi la Pemba | Malipo ya fedha kwa ajili ya mishahara |
| 61/08 21/08/2020 | 002375 | 1,444,159.60 | Shirika la Bandari tawi la Pemba | Malipo ya fedha kwa ajili ya mishahara |
| 100/09 15/09/2020 | 002409 | 1,331,889 | Shirika la Bandari tawi la Pemba | Malipo ya fedha kwa ajili ya mishahara |
| 143/10 16/10/2020 | 002437 | 1,439,432 | Shirika la Bandari tawi la Pemba | Malipo ya fedha kwa ajili ya mishahara |
| 179/11 19/11/2020 | 002463 | 1,312,979.80 | Shirika la Bandari tawi la Pemba | Malipo ya fedha kwa ajili ya mishahara |
| 217/12 16/12/2020 | 002484 | 1,373,247 | Shirika la Bandari tawi la Pemba | Malipo ya fedha kwa ajili ya mishahara |
| 254/01 18/01/2021 | 002506 | 1,418,156 | Shirika la Bandari tawi la Pemba | Malipo ya fedha kwa ajili ya mishahara |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 300/02<br>19/02/2021 | 002537 | 1,295,252 | Shirika la Bandaritawi la Pemba | Malipo ya fedha kwa ajili ya mishahara |
| 353/04<br>17/03/2021 | 002573 | 1,465,432 | Shirika la Bandaritawi la Pemba | Malipo ya fedha kwa ajili ya mishahara |
| 372/04<br>16/04/2021 | 002580 | 1,229,072 | Shirika la Bandaritawi la Pemba | Malipo ya fedha kwa ajili ya mishahara |
| 409/5 | 002604 | 1,143,982 | Shirika la Bandaritawi la Pemba | Malipo ya fedha kwa ajili ya mishahara |
| 449/06<br>28/06/2021 | 002633 | 1,233,795.20 | Shirika la Bandaritawi la Pemba | Malipo ya fedha kwa ajili ya mishahara |
| **Juml a** | | **16,070,098.6** | | |

Majibu ya Shirika la Bandari Zanzibar

Uongozi wa Shirika unakubali kuwepo kwa hali hii, ila kwa ujumla malipo haya hayakuwa mishahara bali yalikuwa ni malipo ya wafanyakazi wa kutwa ambayo Shirika ilikuwa inayakusanya na kulipwa inapofika mwisho wa mwezi hii ni kutokana umbali wa wanapofanyia kazi vibarua hao na Makao makuu ya Shirika kwa Pemba ambapo vibarua 2 wanafanyakazi Wesha na 1 yupo kwenye mnara Matumbini.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Kwa vile Shirika limekiri kulipa mishahara bila ya kuwa na mikataba na Wafanyakazi hao na kwa vile bado shirika linahitaji wafanyakazi ili kuendelea na shughuli mbalimbali katika bandari hiyo basi ni vyema Shirika kuomba kibali cha uajiri kutoka Serikalini ili kuweza kuwaajiri wafanyakazi hao ili kuepuka kwenda kinyume na kifungu nambari 135 (1) cha kanuni ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2014

### 5.1.3.13 Kukosekana kwa Mpango wa Manunuzi wa Mwaka

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Shirika la Bandari - Pemba linafanya manunuzi ya vitu na huduma mbali mbali lakini hakuna mpango wa manunuzi ambao ni muhimu katika kutoa muelekeo wa mpango mzima wa manunuzi wa ofisi.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 29(e) cha Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Shirika la Bandari – Pemba kuhakikisha kwamba unaandaa na kuutumia mpango wake wa manunuzi na kuacha kutegemea mpango wa manunuzi uliopo Ofisi Kuu jambo ambalo linapelekea kutokuonesha muelekeo wa matumizi na bajeti kwa manunuzi yaliyofanywa.

**Majibu ya Shirika la Bandari Zanzibar**

Ni kweli katika ukaguzi imebainika kwamba Shirika la Bandari Pemba linafanya manunuzi ya vitu na huduma mbali mbali bila ya kuepo mpango wa manunuzi wa mwaka 2020-2021, Shirika la Bandari Tawi la Pemba linafuata mpango mkubwa wa manunuzi kutoka Makao Makuu ya Shirika (Procurement Plan for Goods, Works and Consultancy Services). Shirika la Bandari Tawi la Pemba hufanya manunuzi yake madogo madogo ambayo ni ya dharura, manunuzi makubwa hupangwa na kutekelezwa Makao Makuu ya Shirika, hivyo imepelekea Shirika la Bandari Tawi la Pemba kutegemea mpango wa manunuzi kutoka Ofisi kuu.

Kwasasa shirika la bandari Pemba lina mpango wa manunuzi ambao ni sehemu ya mpango wa manunuzi wa makoa makuu kama alivyoshauri mkaguzi wa nje

Uchunguzi wa Kamati

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati katika Uchunguzi wake imebaini ni kweli Shirika limefanya manunuzi mbalimbali pasi na kuwa na mpango wa manunuzi kwa upande wa Pemba na Kutegemea mpango mkuu wa manunuzi uliopo makao makuu ya shirika la Bandari Unguja jambo ambalo linapelekea kukosekana taarifa sahihi za manunuzi ya Shirika.

Hata hivyo Kamati inakubaliana na Ushauri uliotolewa na Mkaguzi wa kuliomba Shirika la Bandari- Pemba kuhakikisha kuwa inaandaa na kutumia mpango wake wa manunuzi na kuacha kutegemea mpango wa manunuzi uliopo ofisi kuu hali inayopelekea kutokuonesha mwelekeo wa matumizi na bajeti kwa matumizi yaliyofanywa.

### 5.1.3.14 Uwepo wa uchakavu wa mali za kudumu kwa muda mrefu.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Shirika la Bandari - Pemba inamiliki mali aina ya Crane iliyosajiliwa kwa nambari ya utambulisho ZPC/PBA/UF/CR/01 pamoja na gari Nissan SLS 150A ambazo zimekaa kwa muda mrefu bila ya kufanyiwa matengenezo au kuchukuliwa hatua za kuuzwa mali chakavu jambo ambalo linapelekea kuendelea kuchakaa kwa mali hizo na huwenda ikapelekea kukosekana kwa mapato ya Serikali pale itakapochukuwa jitihada za kuondoa mali

chakavu kutokana na kuchelewa kuchukuwa maamuzi hayo.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Shirika la Bandari – Pemba kuchukuwa jitihada za makusudi katika kuzifanyia matengenezo mali hizo au kuziuza kwa lengo la upatikanaji wa mapato.

**Majibu ya Shirika la Bandari Zanzibar**

Shirika linakubali juu ya hoja hii Mnamo tarehe 12/06/2022 Shirika la Bandari –Pemba lilifanya mnada wa hadhara ambapo mali chakavu (crane namba ZPC/PBA/UF/CR/01) iliuzwa kwa thamani ya Shillingi Milioni kumi na mbili na laki tano (12,500,000) kwa stakabadhi (Receipt) nambari A.1452 ya tarehe 13/06/2022. Gari aina ya Nissan SLS 150A imeuzwa kwa shillingi Millioni tatu na elfu Hamsini (3,050,000) kwa stakabadhi D.18382 ya tarehe 20/06/2022

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati imebaini kuwa Shirika limeweza kuondoa mali zake za kudumu ambazo zimechakaa na kuziuza kwa njia ya mnada, hivyo basi Kamati haioni haja ya kuendelea na hoja hii na inaifuta kwa vile tayari Shirika limeshachukua hatua. Hata hivyo Kamati inalishauri Shirika kutii sheria bila ya kushurutishwa kwa kuzitengeneza mali zake za kudumu zilichokaa au kuziuza kwa njia ya mnada endapo zitakaa kwa muda mrefu bila ya kufanya kazi ili kunusuru mapato ya Serikali kupotea endapo zikiathiriwa zaid na uchakavu na kupelekea kushuka thamani wakati wa kuuzwa kwa njia ya mnada.

### 5.1.3.15 Uendeshwaji wa nyumba ya wageni kwa hasara

Shirika la Bandari - Pemba linamiliki nyumba kwa ajili ya kulala wageni (BOMANI GUEST HOUSE) iliopo Wete Pemba.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba nyumba hio inaendeshwa kwa hasara kubwa ukilinganisha na mapato yanayokusanywa ambapo hadi kufikia30 Juni, 2021 jumla ya shilingi 7,672,802.12 zimekusanywa kutokana na huduma ya malazi wakati jumla ya shilingi 9,390,000 zimetumika kwa ajili ya gharama za uendeshaji kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Kuendelea kuitumia nyumba hio kwa kutoa huduma ya malazi kwa wageni ni kuitia Serikali hasara kwa kutokupatikana kwa faida.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Shirika la Bandari – Pemba kwa vile imebainika kila mwaka kuendelea kupata hasara itokanayo na uendeshaji wa Nyumba ya Kulala Wageni hiyo ni vyema shirika kuchukuwa jitihada za kumtafuta muekezaji ambae ataweza kuendesha biashara hiyo au kuamua kuiuza kuliko kuendelea kuingia hasara mwaka hadi mwaka.

**Majibu ya Shirika la Bandari Zanzibar (ZPC)**

Nyumba ya kulala wageni (BOMANI GUEST HOUSE) haiendeshwi kwa faida kutokana na idadi ndogo ya wageni ambao wanafikia mji wa Wete. Hivyo nyumba hiyo hubakia kipindi kirefu bila wageni

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati imebaini kwamba Nyumba ya kulala wageni (BOMANI GUEST HOUSE) haina usimamizi mzuri wa kibiashara jambo ambalo linapelekea kuikosesha mapato na kuliingizia hasara shirika kwa kutumia gharama kubwa za uendeshaji kuliko faida inayopatikana

Kamati inalishauri Shirika la Bandari kuwa na usimamizi mzuri katika Nyumba ya kulala wageni (BOMANI GUEST HOUSE) na ikishindikana kufuata ushauri wa Mkaguzi wa kuchukuwa jitihada za kumtafuta muekezaji ambae ataweza kuendesha biashara hiyo au kuamua kuiuza kuliko kuendelea kuingia hasara mwaka hadi mwaka.

## ZIARA YA KAMATI KATIKA MAMLAKA YA BANDARI TANZANIA (TPA)

Kamati ya LAAC imefanya ziara Tanzania Bara katika Mamlaka ya Bandari Tanzania Jijini Dar - es – Salaam kwa lengo la kujifunza Shughuli mbalimbali zinazofanywa na Mamlaka hiyo ili Kamati iweze kujionea, kujifunza, na kuishauri Serikali kupitia Shirika la Bandari Zanzibar katika kusimamia vyema majukumu ya bandari na kutekeleza shughuli zake kwa ufanisi mkubwa na kuweza kufikia malengo waliojiwekea.

Katika ziara hiyo imejifunza mambo yafuatayo;

Kamati imejionea na kujivunza namna ya Mamlaka inavyojitahidi katika kuimarisha huduza za Bandari kwa kufunga mashine za kisasa za upakuzi wa makontena ambapo Kamati imeelezwa itakapokamilika miradi hiyo mamlaka itaweza kuhudumia upakuzi wa makontena kwa meli kubwa tatu kwa wakati mmoja ili kupunguza muda wa meli hizo kukaa muda mrefu katika Bandari ya Dar - es – Salaam jambo ambalo hata Bandari yetu inakumbana na changamoto hiyo.

Aidha Kamati imejifunza namna ya mifumo ya Tehama inavyorahisisha katika ukaguzi na utoaji wa makontena Bandarini, ambapo kwa sasa makontena hayo hukaguliwa kwa mashine maalum inayoitwa ‘scanner’ badala ya kulifungua kontena

kwa njia ya manually, utumiaji wa mifumo hiyo imeleta ufanisi mkubwa katika uharakishaji wa utoaji wa makontena bandarini kwa muda mfupi na kupunguza mrundikano wa makontena Bandarini.

Aidha Kamati imejifunza namna ya mamlaka ya Bandari Tanzania kuruhusu Bandari bubu ICD kufanywa na watu binafsi, Kamati ilitembelea Bandari bubu ya Azam na imejionea namna bandari hiyo inavyoendesha kwa ufanisi mkubwa na kuweza kurahisisha shughuli za utoaji wa makontena hayo Bandarini na kusaidia kuongeza mapato ya Mamlaka

### 5.1.5 SHIRIKA LA BIASHARA LA TAIFA (ZSTC)

#### Taarifa ya Mapato

Katika kipindi cha mwaka 2020/2021 Shirika la Biashara la Taifa limefaniki wa kupata mapato ya kiasi cha Shilingi 11,217,241,926.50 kutokana na vyanzo vyake mbalimbali vya makusanyo ukilinganisha na makusanyo yashiliningi 56,795,231494.32 kwa mwaka wa Fedha 2019/2020 kukiwa na upungufu wa Shilingi 45,577,989,567.82 sawa na asilimia 80 ya upungufu.

#### Majibu ya Shirika la Biashara la Taifa

Mapato ya Shirika la Biashara la Taifa kwa kiasi kikubwa hutegemea na mauzo ya Karafuu. Kwa mwaka 2020/2021 mauzo ya Karafuu yalikuwa ni tani 213 kwa thamani ya TZS 2.9 bilioni ukilinganisha na mwaka 2019/2020 ambazo mauzo yalikuwa ni Tani 5,635 hivyo kupeleka mapato kwa mwaka 2020/2021 kupungua.

#### Uchunguzi wa Kamati

Kamati imehoji juu ya sababu za msingi zilizopelekea mapato hayo kupungua kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kwa asilimia 80 ukilinganisha makusanyo ya mapato kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Kamati imeelezewa sababu kadhaa za upungufu wa mapato hayo zikiwemo kupungua kwa uzalishaji wa zao la karafuu kwa wakulima, Shirika kununua karafuu kwa bei kubwa na Kuuza kwa bei ndogo, Kushuka kwa bei ya zao la karafuu katika soko la dunia n.k

Vile vile Kamati imehoji juu vyanzo vya mapato ya Shirika na kuarifiwa kuwa Chanzo kikubwa cha Shirika na mauzo ya karafuu ambayo kwa mwaka wa fedha 2020/2021 yameshuka kwa kuuza karafuu tani 213 zenye thamani ya TZS 2.9 ukilinganisha mauzo ya 5,635 kwa mwaka 2019/2020 jambo ambalo linatia wasiwasi kufilisika kwa shirika iwapo italitegemea zao la karafuu pekee kama ni chanzo kikuu cha mapato.

Kamati inapata hofu juu ya Shirika kufilisika ikiwa halitochukua jitihada za makusudi katika kuliimarisha shirika hilo katika kuaanda sera madhubuti ya Shirika na kuweza kujiiendesha kibiashaara aidha kuweka Mikakati maalum ya kulikuza zao la karafuu

visiwani Zanzibar.

**Mapendekezo ya Kamati**

Kamati inalishauri shirika la biashara la Taifa Kuhakikisha wanaimarisha zao la karafuu kwa vile ndio zao kuu la kibiashara ambalo hulitegemea katika kuliingizia shirika mapato, hivyo basi ni nyema kupitia upya sera na Mikakati ya Shirika katika Ugawaji wa miche ya karafuu, upandaji, utunzaji, ukodishaji wa mashamba ya Karafu na Ununuzi na Uuzaji wa Zao la Karafuu.

Vile vile Kamati inalishauri shirika kuacha kulitegemea zao la karafuu pekee badala yake wafanye tafiti mbalimbali ya mazao mengine ya kibiashara ambayo kwa upande wa Zanzibar tunaweza kunufaika iwapo tutayauza nje ya nchi kwa lengo la kuliingizia Shirika mapato na kutoa ajira kwa vijana wetu wa Zanzibar.

Aidha kamati inaishauri Serikali licha ya kuwa na umiliki wa asilimia mia 100% wa Shirika, haina budi kulipa nguvu shirika hilo Kujiendesha kibiashara ili liweze kufikia malengo yake yaliyojiwekea ikiwa ni pamoja na kuliruhusu Shirika kuweka viwango maalum vya ununuaji na uuzaji wa zao la Karafuu, utaratibu wa ugawaji wa miche ya mikarafuu, ukodishaji wa majengo ya shirika na mengineyo ili Shirika liweze kujiingizia mapato na liweze kutoa gawio kwa Serikali

**Taarifa ya Matumizi**

Katika kipindi cha mwaka wa Fedha 2020/2021 Shirika la Biashara la Taifa limefanikiwa kutumia jumla ya shilingi 19,689,792,054.86 kwa kuharamia harama za mauzo, kazi za kawaida na maendeleo ukilinganisha na matumizi ya Shilingi 84,638,754,140.61 ya mwaka wa Fedha 2019/2020 tukiwa na tofauti ya matumizi ya shilingi 64,948,962,085.75 sawa na asilimi 76.7 ya matumizi.

**Majibu ya Shirika la Biashara la Taifa**

Matumizi ya Shirika kwa mwaka 2020/2021 yamepungua kutokana na kupungua kwa manunuzi ya Karafuu pamoja na gharama zinazo ambatana nazo ambapo jumla yaTani 213 zilinunuliwa ukilinganisha na Tani 4,497.5 zilizonunuli kwa mwaka 2019/2020 hali hiyo ilipelekea gharama za matumizi kwa mwaka 2019/2020 kuwa kubwa ukilinganisha na mwaka 2020/2021.

**Uchunguzi wa Kamati**

Kamati katika kufuatilia hoja hii imebaini mambo yafuatayo:

Uwepo wa madeni makubwa ya Shirika ambayo yanatokana taasisi na watoa huduma mbalimbali kama vile ZSSF bilioni 5.0 na PBZ bilioni 8.0. Aidha Shirika

linadaiwa (takriban tani 596.4) kwa wateja waliongiza fedha kwa mwaka 2020/2021 kwa ajili ya kupata karafuu ambapo mpaka sasa hawajapatiwa karafuu zao, deni hilo linakisiwa kuwa ni Tzs bilioni 19.7 bila ya riba ambapo Kamati imearifiwa kuwa madeni hayo yameanza kulipwa ambapo ulipaji wa madeni hayo yataonekana katika hesabu ya mwisho ya mwaka (financial statement) ya mwaka 2021/2022.

Aidha Kamati imebaini Shirika kushidwa kutoa gawio kwa Serikali kutoka na kukabiliwa na uhaba wa fedha unaolikumba Shirika kwa kununua karafuu kutoka kwa wakulima kwa kutumia fedha za mikopo ambapo mikopo hiyo hulipwa kwa riba kubwa.

Kamati imebaini Shirika la biashara kupitia Tawi lake la Dubai kuendeshwa kwa hasara kwa kuwa Tawi hilo limetumia jumla ya Tzs 252.5 milioni kwa ajili ya kulipa mishahara ya wafanyakazi, kodi ya jengo, na matumizi mengineyo licha ya kwamba Tawi hilo halikupokea karafuu yoyote kutoka makao makuu Zanzibar kutokana na msimu kuwa mdogo hata hivyo Tawi hilo.

Mapendekezo ya Kamati

Kamati inaliomba Shirika la biashara la taifa katika kufikiria namna bora ya kuliimarisha zao la karafuu kwa kupitia upya sera na mikakati maalum kuanzia namna ya utoaji wa miche ya mikarafuu, upandaji wa miche ya mikarafuu na ufuatiliaji wake ili kuongeza uzalishaji wa zao la karafuu ambalo linaonekana kupungua kila uchao jambo ambalo linahatarisha Shirika kufilisika kwa kuwa zao hilo ndio tegemeo kubwa katika kuliingizia Shirika mapato.

Aidha Kamati inalishauri Shirika kwa vile Tawi la Dubai limekuwa linaendeshwa kwa hasara kwa kutopokea karafuu kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kutokana na msimu mdogo wa karafuu hivyo ni vyema Shirika kuamua kulifunga Tawi hilo au kuanza kufanya utafiti wa kina juu ya haja ya namna ya kuanzisha shughuli nyengine za kibiashara ambazo zitaleta tija kwa Shirika kwa vile Shirika hilo limeshajijengea fursa na uzoefu mkubwa wa kibiashara kupitia Ofisi yake ya Dubai.

### 5.1.5.1 Kutokufanyiwa maboresho kwa daftari za mali za kudumu za Shirika la ZSTC.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa daftari la mali za kudumu la Shirika la Biashara la Taifa halikufanyiwa maboresho ya mara kwa mara ya kuingiza taarifa za mali na thamani za mali za kudumu zilizonunuliwa katika mwaka wa Fedha unaoishia tarehe 30 June 2021 pamoja na taarifa za mali zilizouzwa kuchelewa kuondoshwa katika daftari la mali kwa wakati.

Aidha, ukaguzi umebaini kwamba Shirika la Biashara la Taifa halikuwa na fursa ya kuingia moja kwa moja katika mfumo wa uwekaji wa taarifa za mali za kudumu

unaosimamiwa na Idara ya uhakiki mali.
Kutokufanyiwa maboresho ya taarifa za mali za kudumu za Shirika mara kwa mara kunapelekea kuendelea kukwaza uandaaji wa taarifa za Kifedha ambazo zinakidhi viwango vya kimataifa vya uandaaji wa hesabu. Kukosekana kwa fursa ya kuingia moja kwa moja katika mfumo wa uwekaji wa taarifa za mali za kudumu kunadhorotesha uboreshaji wa taarifa za mali pamoja na kuchelewa kwa zoezi la ufungaji wa hesabu.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na matakwa ya kifungu cha 29(2) cha Sheria Nambari 12 ya usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Shirika la Biashara la Taifa kuboresha taarifa za mali za kudumu katika daftari la mali za kudumu kwa kusimamia pamoja na kufatilia tarifa zinazohusiana na mali zote za Shirika ili kuenda sambamba na matarajio ya Serikali katika mfumo wa ufungaji wa mahesabu na uwekaji wa kumbukumbu nzuri za mali za Serikali kwa mujibu wa Sheria, kanuni pamoja na miongozo mengine iliyopo.

### Majibu ya Shirika la Biashara la Taifa
Shirika la Biashara la Taifa kwa sasa linatumia Asset Register liloandaliwa na kusimamiwa na Wizara ya Fedha. Aidha, Shirika kwa kuzingatia ushauri wa Mkaguzi limekuwa likiwasiliana na Wizara ya Fedha kuhakikisha kunawekwa taarifa mpya kila inapohitajika kwa kila mwaka. Shirika katika kuhakikisha linaweka udhibiti mzuri wa mali zake kuanzia mwaka 2021/2022 limeanza utaratibu wakufanya uhakiki wa mali zake (Physical Verification).

### Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati
Kamati katika uchunguzi wake imebaini kuwa utaratibu wa kujaza taarifa za Mali za Kudumu katika mfumo wa unaosimamiwa na kitengo cha uhakiki mali cha Ofisi ya Rais fedha na Mipango bado unakabiliwa na changamoto kadhaa ambazo zinalalamikiwa na Taasisi mbalimbali zikiwemo kutoingizwa taarifa za mali za kudumu kwa wakati pindi taasisi za Serikali na Mashirika zinapowasilisha taarifa hizo.

Aidha Kamati inaipongeza Serikali kwa kufanya marekebisho ya Sheria ya Mitaji ya Umma kwa kuzitaka taasisi za Serikali kuwa na kitengo kinachosimamia uhakiki wa mali za kudumu za taasisi yani 'Assert Management unit' ambacho kitakuwa na wajibu wa kutunza taarifa zote za mali za kudumu za taasisi husika jambo ambalo litaleta ufanisi na kuondoa changamoto kadhaa ambazo taasisi zinakumbana nazo.

### Mapendekezo ya Kamati
Kamati inashauri taasisi za Serikali kufanya mawasiliano katika shughuli mbalimbali za kiofisi kwa kutumia njia ya Barua au maandishi maalum kama ni uthibitisho wa utekelezaji wa Shughuli fulani, Ushauri huu umetokana na Kamati kuelezwa kuwa Shirika linamtumia mtendaji wake kwenda Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kwenda

kuboresha taarifa za mali za kudumu za Shirika mara kwa mara bila ya mafanikio kutokana na changamoto ya mfumo, Kamati katika kupata ukweli wa jitihada hizo Kamati imeomba kupatiwa barua kutoka Shirika kwenda Afisi ya Rais Fedha na Mipango inayotoa uthibitisho wa kuomba kuboresha daftari la mali za kudumu za Shirika, hata hivyo Kamati haikupatiwa barua hiyo na kuelezwa kuwa mawasiliano baina yao yalikuwa yanafanyika kwa njia ya mdomo.

Vilevile, inaipongeza Wizara ya Fedha na Mipango kwa kufanya marekebisho ya Sheria ya Mitaji ya Umma ambayo inalenga kuanzisha kitengo cha utunzaji wa mali za kudumu kwa kila wizara na taasisi za Serikali kwa lengo Kurahisha Shughuli za uboreshaji wa daftari la mali za kudumu kufanywa katika taasisi husika badala ya taarifa hizo  kupelekwa Wizarani ili kuingizwa katika Mfumo, Kamati inaishauri Afisi ya Rais, Fedha na Mipango kuharakisha zoezi hilo ili liweze kuondoa kero na Changamoto ambazo kwa sasa mashirika na Taasisi zinakumbana nazo katika kuhakiki taarifa za mali za kudumu za taasisi zao

### 5.15.2. Kukosekana kwa Sera ya Usimamizi wa mali za kudumu:

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC) limeshindwa kuanzisha na kutumia sera ya usimamizi wa mali za kudumu kwa ajili ya usimamizi na kudhibiti mali za Shirika ambapo kukosekana kwa sera hiyo kunaathiri utaratibu mzima wa usimamizi wa mali za kudumu.

Aidha, kutokana na ukuaji wa uhitaji wa mali za kudumu na mitambo ya kuzalisha mafuta ya mimea kwa Shirika, uwepo wa sera ya usimamizi wa mali unahitajika kuanzishwa ili mali husika zifuatiliwe mara kwa mara kwa madhumuni ya udhibiti na kufanya maamuzi.

Kukosekana kwa sera ya usimamizi wa mali za kudumu kunaweza kupelekea kutosimamiwa kwa mali za kudumu ipasavyo pamoja na kutolewa kwa maamuzi yasiyo sahihi katika utumiaji wa mali hizo ambapo ni kwenda kinyume na Sheria, kanuni pamoja na miongozo mbalimbali iliyopo.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC) Kuhakikisha unaanda sera ya usimamizi wa mali na kufanya tathmini ya kina juu ya umuhimu wa mfumo wa kudhibiti mali ilikurahisisha ufuatiliaji wa gharama za manunuzi ya mali, nagharama za matengenezo.

### Majibu ya Shirika la Biashara la Taifa

Shirika la Biashara la Taifa limepokea ushauri wa Mkaguzi kuhusiana na uwepo wa Sera ya usimamizi wa mali za kudumu. Shirika tayari limeandaa sera hiyo ambayo imeshapita kwa upande wa uongozi na inasubiri kupelekwa kwenye Bodi ya Wakurugenzi katika Kikao kijacho kwaajili ya kuudhinishwa.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Kamati imepokea majibu hayo na kuomba kupatiwa rasimu hiyo mpya ya Sera ya usimamizi wa mali za kudumu za Shirika, na kamati imerizika baada ya kupatiwa rasimu hiyo na kuweza kuikagua, hata hivyo Kamati inatoa ushauri kwa uongozi wa Shirika kuhakikisha inaipitia vyema Sera hiyo na kuifanyia marekebisho kadri iwezekanavyo ili sera hiyo kuweza kuendanana na matumizi sahihi kwa wakati huu ya utunzaji wa mali za Shirika aidha Kamati inasisitiza juu ya uharakiswaji wa upitishwaji wa rasimu hiyo katika kikao cha Bodi ya Wakurugenzi kwa ajili ya kuanza matumizi yake.

SHIRIKA LA BIASHARA LA TAIFA (ZSTC) PEMBA

**5.15.3: Hati za malipo zenye vielelezo pungufu Shilingi 69,248,145.**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwepo kwa jumla ya Shilingi 69,248,145 ambazo zimelipwa kwa matumizi mbali mbali ya Shirika la Biashara la Taifa – Pemba lakini baadhi ya vielelezo vya matumizi husika havikuambatanishwa katika hati za malipo ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo. Kufanya hivo ni kwenda kinyume na kifungu Nambari 34(1) cha Sheria Nambari 12 ya usimamizi wa Fedha za Umma yam waka 2016. Ukaguzi unashauri uongozi wa Shirika la Biashara la Taifa –Pemba kuhakikisha malipo yote yanayofanyika yanaambatanishwa na vielelezo halisi ili kuthibitisha uhalali wa malipo hayo.
Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini;

**Jadweli Nambari 26: Hati za malipo zenye vielelezo pungufu**

| Hati Namba | Hundi Namba | Kiasi cha Fedha kilicholipwa (Tshs.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| SP00282/2020<br>21/07/2020 | 679247 | 556,800 | Chasasa Service<br>Station | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa<br>mafuta ya Diesel. |
| SP00283/2020<br>21/07/2020 | 679248 | 3,712,000 | Chasasa Service<br>Station | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa<br>mafuta ya Diesel. |
| SP00789/2020<br>10/08/2020 | 679268 | 720,000 | Chake Chake Hotel | Malipo ya fedha kwa ajili ya kukaa<br>hotelini |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| SP01101/2020<br><br>25/8/2020 | 679272 | 5,735,000 | Chasasa Services<br><br>Station | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa<br><br>mafuta ya Diesel. |
| SP01113/2020<br><br>25/8/2020 | 679474 | 3,712,000 | Zanzibar Petroleum<br><br>Ltd | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa<br><br>mafuta ya Diesel na Petrol. |
| SP01767/2020<br><br>09/10/2020 | 679362 | 313,600 | Fairsale Hardware | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa<br><br>mpira wa maji. |
| SP01991<br><br>04/11/2020 | 679404 | 6,470,200 | Chasasa Services<br><br>Station | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa<br><br>mafuta ya Diesel na Petrol. |
| SP02170<br><br>13/11/2020 | 679432 | 4,250,000 | ZSTC – Pemba | Malipo ya fedha kwa ajili ya fidia<br><br>kwa wakulima. |
| SP02225<br><br>26/11/2020 | 679437 | 950,000 | ZSTC – Pemba | Malipo ya fedha kwa ajili ya fidia<br><br>kwa wakulima. |
| SP00020/2020<br><br>13/01/2021 | 679456 | 3,640,000 | Chasasa Service<br><br>Station | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa<br><br>mafuta ya diesel. |
| SP00021/2020<br><br>13/01/2021 | 679457 | 1,484,100 | Masoud Abrahmani<br><br>Masoud | Malipo ya fedha ya kwa ajili ya ununuzi<br><br>wa vifaa vya ujenzi. |
| SP00095<br><br>04/02/2021 | 679465 | 2,770,000 | Chasasa Services<br><br>Station | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa<br><br>mafuta ya diesel. |
| SP00293/2021 | 679489 | 1,960,000 | Chasasa Service | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 09/03/2021 | | | Station | mafuta ya diesel. |
| SP00353/2021<br>010/4/2021 | 679492 | 1,063,700 | Chasasa Service<br>Station | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa<br>mafuta ya diesel. |
| SP00599/2021 | 679505 | 2,245,100 | Chasasa Service Station | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya diesel. |
| SP00600/2021<br>10/05/2021 | 679506 | 212,400 | Bakari Petrol<br>Station | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa<br>mafuta ya diesel. |
| SP00710/2021<br>27/05/2021 | 679509 | 866,000 | Chasasa Service<br>Station | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa<br>mafuta ya diesel. |
| SP00785/2021<br>04/06/2021 | 679512 | 22,900,000 | ZSTC Pemba | Malipo ya fedha kwa ajili ya kuwalipa<br>fidia wakulima. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| SP00922/2021<br>22/06/2021 | 679515 | 1,593,000 | Chasasa Service Station | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya diesel. |
| SP00932/2020<br>23/06/2021 | 679516 | 1,645,045 | Chasasa Service Station | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya diesel. |
| SP00933/2021<br>23/06/2021 | 679517 | 2,449,200 | Zanzibar Petroleum Ltd | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya diesel. |
| **Jumla** | | **69,248,145** | | |

### Majibu ya Shirika la Biashara la Taifa

Shirika linakiri kuwepo kwa hati za malipo zilizokosa vielelezo, hii ilitokana na uhaba

wa Wafanyakazi katika kitengo cha uhasibu hususan katika sehemu ya Mshika Fedha ambapo ilipelekea ufuatiliaji wa vielelezo hivyo kuchelewa na kupatikana nje ya muda sahihi.

Kwa sasa Vielelezo vyote husika vimeambatanishwa kwenye hati za malipo na tatizo la uhaba wa Wafanyakazi limesharekebishwa.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati ya LAAC**

Kamati katika uchunguzi wake imebaini kwamba kwa kiasi kikubwa hati zenye vielelezo pungufu ni katika malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya diesel na Petrol katika sheli za Chasasa Service Station na Zanzibar Petroleum ltd kwa kisingizio kuwa sheli hizo za mafuta hazikuwa na risiti pamoja ufuatiliaji mdogo wa vielelezo hivyo kutokana na uhaba wa wafanyakazi katika kitengo cha Uhasibu.

Kamati inalishauri shirika la Biashara la taifa kuhakikisha kuwa wanaponunua huduma ya mafuta katika sheli tofauti zilizopo Pemba ni lazima wapatiwe risiti ili kuthibitisha uhalali wa ununuzi wa mafuta hayo na kuachana na watoa huduma wa mafuta ambao watashidwa kutoa risiti, aidha Kamati inaendelea kulishauri Shirika kuhakikisha hati zote za malipo zinakuwa na vielelezo timilifu kwani kutokufanya hivyo kunapelekea Shirika kufanya manunuzi ya vifaa na huduma mbalimbali kinyume na sheria.

**5.1.5.4: Malipo ya mishahara kwa wafanyakazi wa wasiokuwa na mikataba ya kazi.**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 25,021,180 zimelipwa kwa wafanyakazi wa muda wa Shirika la Biashara la Taifa-Pemba lakini mikataba yao ya kazi imekosekana kwa ukaguzi.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 135(1) cha kanuni ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2014

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Shirika la Biashara la Taifa Pemba kuhakikisha kwamba kama kutakuwa na ulazima wa kutumia watumishi wa kutwa ni vyema Mkuu wa Taasisi kuomba kibali kwa tume ya Utumishi husika kwa lengo la kumjazisha mkataba mtumishi huyo.
Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:

**Jadweli Nambari 27: Malipo ya mishahara kwa wafanyakazi wasiokuwa na mikataba ya kazi**

| Hati Namba | Hundi Namba | Kiasi cha Fedha kilicholipwa (Tshs.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| SP00502/2020<br>29/07/2020 | 67925<br>3 | 2,721,650 | ZSTC Pemba | Malipo ya fedha kwa ajili ya mishahara |
| SP01233/2020<br>04/09/2020 | 67927<br>7 | 2,742,990 | ZSTC – Pemba | Malipo ya fedha kwa ajili ya mishahara. |
| SP01758/2020<br>08/10/2020 | 679359 | 2,718,240 | ZSTC – Pemba | Malipo ya fedha kwa ajili ya mishahara |
| SP01996<br>04/11/2020 | 679407 | 2,319,430 | ZSTC – Pemba | Malipo ya fedha kwa ajili ya mishahara |
| SP02310<br>10/12/2020 | 679449 | 2,664,595 | ZSTC – Pemba | Malipo ya fedha kwa ajili ya mishahara |
| SP00097<br>04/02/2021 | 679467 | 2,478,460 | ZSTC – Pemba | Malipo ya fedha kwa ajili ya mishahara |
| SP00181<br>15/02/2021 | 679478 | 2,050,815 | ZSTC – Pemba | Malipo ya fedha kwa ajili ya mishahara |
| SP00579<br>/2021<br>04/05/2021 | 67949<br>9 | 2,419,780 | ZSTC – Pemba | Malipo ya fedha kwa ajili ya mishahara |
| SP00585<br>/2021<br>06/05/2021 | 679501 | 2,534,500 | ZSTC – Pemba | Malipo ya fedha kwa ajili ya mishahara |
| SP00588<br>/2021<br>06/05/2021 | 679503 | 2,370,720 | ZSTC – Pemba | Malipo ya fedha kwa ajili ya mishahara |
| **Jumla** | | **25,021,180** | | |

Majibu ya Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC)

Shirika linakiri kuwepo kwa wafanyakazi wa mkataba ambao mikataba yao ilikuwa imeshaisha muda, Shirika kwa muda mrefu lilikuwa lina wafanyakazi ambao

walikuwa hawana mikataba, wafanyakazi hao walikuwa wanafanya kazi za uzalishaji kiwandani, na wengine wakitumikakatika kusarifu bidhaa za kilimo hai, hii ilitokana na kuchelewa kupata kibali cha uajiri au muongozo mwengine wowote kutoka kwa katibu mkuu kiongozi.
Shirika ilibidi liwalipe mishahara katika kipindi hicho cha kusubiri muongozo kutoka serikalini kwa sababu walikuwa wakitumika katika uzalishaji.

Aidha, baada ya Shirika kupata muongozo kutoka kamisheni ya kazi kwa barua nam. KK/24/06/VOL.1/39 ya tarehe 16/02/2021.liliwaondosha kazini wafakazi hao kwa kupitia zoezi la “redunducy” kwa mujibu wa Sheria ya Ajira nam. 5 ya mwaka 2011. Aidha, kwa sasa Shirika litakapotaka kufanya uajiri mpya litaandaa mahitaji ya nafasi za ajira husika, na litafuata taratibu zote za kiutumishi katika uajiri kwa kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za utumishi.

**Uchunguzi wa Kamati**
Katika kufatilia hoja hii kamati imethibitisha ni kweli wafanyakazi hao walilipwa mishahara bila ya kuwa na mikataba ya ajira hali hii imetokana na Shirika kutopatiwa kibali cha kuajiri baada ya kutoka kwa agizo Serikalini za kuwaondoa wafanyakazi wa muda, wakati huo huo shirika lilikuwa linahitaji wafanyakazi kwa ajili ya uendeshaji wa Shirika.

**Mapendekezo ya Kamati**
Kamati inashauri Serikali kuharakisha utaratibu wa kutoa vibali vya ajira kwa Tasisi zake hasa zile zenye kutoa huduma za uzalishaji wa bidhaa ambazo kwa kiasi kikubwa zinahitaji nguvu kazi katika kutekeleza shughuli zake. Aidha, Kamati inalishauri shirika linaweza kuendelea kuwatumia wafanyakazi wake kwa kuwataka kujisajli katika vikundi na kuingia nao mkataba maalum wa malipo kwa kila kipindi watakapotaka kuwatumia wafanyakazi hao katika shughuli mbalimbali za uzalishaji katika Shirika kwani kufanya hivyo itakuwa ni njia sahihi ya kuendelea kuwatumia wafanyakazi hao bila ya kwenda kinyume na kifungu nambari 135(1) cha Kanuni ya Utumishi wa Umma ya Mwaka 2014.

**5.1.5.5: Bidhaa ambazo hazikurikodiwa katika daftari la ghalani.**
Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa jumla ya shilingi 21,251,268 zimetumika kwa ajili ya ununuzi wa bidhaa mbali mbali kwa matumizi ya Shirika la Biashara la Taifa Pemba lakini bidhaa hizo hazikurikodiwa katika madaftari ya ghalani ili kuweza kuthibitisha uhalali wa mapokezi pamoja na matumizi ya bidhaa hizo. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria nambari 11 ya ununuzi na uondoshaji wa mali za umma yam waka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Shirika la biashara la Taifa Pemba kuhakikisha bidhaa zote zinazonunuliwa zinaingizwa katika daftari la kumbukumbu kabla ya kuanza kutumika kwa mujibu wa utaratibu ili kuepusha kujitokeza kwa matumizi yasioeleweka na kupelekea upotevu wa Fedha za umma.

Mchanganuo wa bidhaa hizo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:

**Jadweli Nambari 28: Bidhaa ambazo hazikurikodiwa katika daftari la ghalani**

| Hati Namba | Hundi Namba | Kiasi cha Fedha kilicholipwa (Tshs.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| SP01252/ 2020 | 679287 | 2,887,500 | Bakar Petrol Station | Ununuzi wa mafuta ya diesel lita 1500. |
| SP01253/ 2020 | 679288 | 4,211,000 | Chasasa Service Station | Ununuzi wa mafuta diesel lita 1600 na petroli lita 600. |
| SP01554/2020 25/9/2020 | 679317 | 4,815,500 | Zanzibar Petroleum Ltd | Ununuzi wa mafuta ya diesel lita 2000 na petrol lita 500. |
| SP01556/2020 25/9/2020 | 679319 | 2,703,400 | Zanzibar Petroleum Ltd | Ununuzi wa mafuta ya diesel lita 1400. |
| SP01555/2020 25/9/2020 | 679318 | 2,323,250 | ZSTC – Pemba | Ununuzi wa mafuta ya diesel lita 750. |
| SP00283/2020 01/10/2020 | 679339 | 5,791,000 | ZSTC Pemba | Ununuzi wa mafuta ya diesel lita 1000. |
| SP01767/2020 09/10/2020 | 679362 | 313,600 | Fairsale Hardware | Ununuzi wa roli 2 za mpira wa maji. |
| SP01775/2020 13/10/2020 | 679367 | 1,901,000 | Chasas Service Station | Ununuzi wa mafuta ya diesel lita 1000. |
| SP00180/2021 15/02/2021 | 679477 | 580,000 | ZSTC Pemba | Ununuzi wa paipu 4 za maji. |
| SP00184/2021 15/02/2021 | 679481 | 323,400 | Mohammed Khalfan Adeyyoum | Ununuzi wa godoro moja la 6x6. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| SP00353 /2021 01/04/2021 | 679492 | 1,063,700 | Chasasa Service Station | Ununuzi wa mafuta ya petrol lita 550. |
| SP00611 /2021<br>17/05/2021 | 679507 | 694,918 | Chasasa Service Station | Ununuzi wa mafuta ya Petrol lita 343. |
| SP00710 /2021<br>27/5/2021 | 679509 | 866,000 | Chasasa Service Station | Ununuzi wa mafuta ya Petrol lita 400. |
| Jumla | | 21,251,268 | | |

**Majibu ya Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar (ZSTC)**
Shirika linakiri juu ya hoja ya kutorikodiwa kwa bidhaa katika daftari la ghalani, hii ilitokana na Mtendaji aliekuwepo kutokuwa na uwezo wa kufanya kazi zinazohusiana na utunzaji wa Ghala baada ya aliyekuwa akifanya kazi hizo kuhamishiwa sehemu nyengine kikazi.

Baada ya Shirika kugundua tatizo hilo, liliamua kumuhamisha Mtendaji huyo na kumpeleka sehemu inayolingana na kazi zake na kuajiri Mtendaji mwenye sifa na uwezo wa kazi hizi ili kuboresha ufanisi wa kazi. Aidha, Shirika la ZSTC linaahidi kwamba tatizo kama hili halitojitokeza tena baada ya kurekebisha kasoro zote za nyuma.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**
Kamati haikuona haja ya kujadili kwa kina hoja hii kwa vile Shirika limekiri kuwepo kwa dosari hii na kamati imethibitishiwa kuwa kwa sasa Shirika limeshapata mfanyakazi ambae ana utaalamu katika shughuli za kutunza na kurikodi vifaa vya shirika ghalani jambo ambalo litasaidia dosari hii kutojitokeza tena.

Hata hivyo Kamati inalishauri shirika kuhakikisha linaajiri wafanyakazi wenye ujuzi pamoja na kuwapangia kazi watumishi kwa mujibu vigezo na sifa zinazoambatana na kazi zao ili kuepuka dosari kama hizo kutojitokeza tena

**5.15.6: kukosekana kwa mapato yatokanayo na malimbikizo ya madeni ya wakulima wa Karafuu.**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC) – Pemba linadai madeni ya muda mrefu kwa wakulima wa karafuu yenye jumla ya shilingi 7,005,000 kwa ajili ya mikopo ya wakulima wa zao la Karafuu. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na makubaliano katika mikataba ya ukopeshaji uliofanyika. Ukaguzi unashauri uongozi wa Shirika la Biashara la Taifa Pemba kuhakikisha linafanya ufuatiliaji wa haraka wa urejeshwaji wa mikopo hiyo kwa lengo la kuweza kuwapatia wakulima wengine kwa mujibu wa utaratibu uliopo.

Mchanganuo wamapato yatokanayo na malimbikizo ya madeni ya wakulima wa karafuu kwa mujibu wa kila Wilaya ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:

**Jadweli Nambari 29: Mapato yatokanayo na malimbikizo ya madeni ya wakulima wa karafuu kwa kila Wilaya.**

| Mwaka | Wilaya | Kiasi cha fedha kinachodaiwa (Tshs.) |
|---|---|---|
| 2011/2012 | Chakechake | 3,850,000 |
| 2013/2014 | Wete | 400,000 |
| | Micheweni | 210,000 |
| | Mkoani | 1,800,000 |
| 2016/2017 | Chakechake | 200,000 |
| 2017/2018 | Wete | 545,000 |
| Jumla | | 7,005,000 |

**Majibu ya Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC)**

Shirika la ZSTC linakiri juu ya hoja ya kukosekana kwa mapato yatokanayo na malimbikizo ya madeni ya Wakulima wa Karafuu.

Shirika linaitaarifu kamati kuwa deni hili sio deni la mwaka mmoja kama lilivyoainishwa bali ni malimbikizo ya madeni ya Wakulima ya miaka minne (4) – 2011/2012, 2013/2014, 2016/2017,2017/2018: katika kipindi chote hicho cha miaka minne (4) zaidi ya TZS Milioni 460 zimetolewa kwa mkopo ambapo TZS 7,005,000 ndizo ambazo hazijarejeshwa hadi sasa ambapo ni sawa na marejesho ya mikopo ya zaidi ya asilimia 98.

Shirika la ZSTC linaendelea kuhakikisha kwamba fedha hizi zinarejeshwa ingawa tatizo kubwa ni kwamba Wadaiwa wengine tayari wameshafariki.

Shirika linaendelea kufuatilia juu ya urejeshwaji wa deni hilo ili kuweza kuwapatia wakulima wengine ambapo kati ya TZS 7,005,000 ya deni lote TZS 200,000 zimerejeshwa na kubakiwa na kiasi cha TZS 6,805,000 ambazo zinaendelea kufuatiliwa.

**Uchunguzi wa Kamati ya LAAC**

Kamati imebaini kuwa mikopo iliyotolewa kwa wakulima ilikua na lengo zuri la kuwasaidia wakulima katika kuendeleza zao la karafuu ila changamoto iliyojitokeza ni kuwa mikataba ya mikopo haikuwa na vipengele madhubuti vya kumfanya

mkopeshwaji kulipa mikopo hiyo kwa wakati, kwa mfano wapo wadaiwa watatu ambao wameshafariki lakini uongozi ulipokwenda kudai fedha za mkopo kwa warithi wa marehemu walielezwa kuwa familia haitambui mkopo huo ambao marehemu hao wanadaiwa, aidha familia za marehemu hao haziko tayari kulipa deni hilo, sambamba na hayo wadaiwa ambao bado wapo hai na wameshidwa kurudisha mkopo huo Shirika bado limeshidwa kuchukua hatua za kisheria hadi sasa licha ya kuwa Shirika linawatambua wakulima hao.

### Mapendekezo ya Kamati ya LAAC

Kamati inalishauri shirika kuchukua jitihada zaidi ya kuhakikisha deni hilo linalipwa na kumalizika kwa haraka vilevile kwa wale waliofariki ni vyema Shirika likafanya utaratibu mzuri wa kukutana na warihi wa familia hizo ili kulipatia ufumbuzi deni ambalo marehemu wanadaiwa na ikishindikana basi Shirika lifate taratibu na sheria za kufuta deni hilo kuliko kuendelea kubeba mzigo wa deni ambalo halilipiki, Aidha kwa wale wadaiwa ambao wako hai basi Shirika lifanye jitihada za kuwatafuta wadaiwa hao ili waweze kulipa madeni yao.

Aidha kamati inalishauri shirika kutoa mikataba ya mikopo yenye vipengele madhubuti kwa lengo la kupatikana kwa marejesho ya mkopo kwa uhakika na kwa wakati ili Shirika liweze kujiendeleza kibiashara na lengo la utolewaji wa mikopo hiyo liweze kufanikiwa kwani urejeshaji hafifu wa mikopo utapelekea shirika kukosa fedha za kuwakopesha wakulima wengine ambao watahitaji kupatiwa mikopo hiyo.

KIWANDA CHA MAKONYO PEMBA

**5.1.6.1: Malipo ya mishahara kwa wafanyakazi wasiokuwa na mikataba ya kazi.**
Katika Ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 68,986,259 zimelipwa kwa wafanyakazi wa Kiwanda cha Makonyo na Arki za mimea Pemba lakini mikataba yao ya kazi imekosekana kwa ukaguzi. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu Nambari 135(1) cha kanununi ya Utumishi wa Umma yam waka 2014. Ukaguzi unashauri uongozi wa Kiwanda cha Makonyo na Arki za mimea –Pemba kuhakikisha kwamba kama kutakuwa na ulazima wa kutumia watumishi wa kutwa ni vyema Mkuu wa Taasisi kuomba kibali kwa Tume ya Utumishi husika kwa lengo la kumjazisha mkataba mtumishi huyo.
Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:

**Jadweli Nambari 30: Malipo ya mishahara kwa wafanyakazi wasiokuwa na mikataba ya kazi**

| Hati Namba | Hundi Namba | Kiasi cha Fedha kilicholipwa (Tshs.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| SP00511/2020 30/07/2020 | 005190 | 8,039,859 | Kiwanda cha Makonyo | Malipo ya fedha kwa ajili ya mishahara. |
| SP01719/2020 | 005265 | 11,714,400 | Kiwanda cha Makonyo | Malipo ya fedha kwa ajili ya mishahara. |
| SP01886/2020 25/10/2020 | 005278 | 12,257,000 | Kiwanda cha Makonyo | Malipo ya fedha kwa ajili ya mishahara |
| SP02337/2020 15/12/2020 | 005296 | 6,451,500 | Kiwanda cha Makonyo | Malipo ya fedha kwa ajili ya mishahara |
| SP00049/2021 25/01/2021 | 005321 | 9,086,500 | Kiwanda cha Makonyo | Malipo ya fedha kwa ajili ya mishahara |
| SP00190/2021 16/02/2021 | 005333 | 6,791,500 | Kiwanda cha Makonyo | Malipo ya fedha kwa ajili ya mishahara |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| SP00473 20/4/2021 | 005383 | 6,995,500 | Kiwanda Cha Makonyo | Malipo ya fedha kwa ajili ya mishahara |
| SP00505 22/4/2021 | 005384 | 7,650,000 | Kiwanda Cha Makonyo | Malipo ya fedha kwa ajili ya mishahara |
| Jumla | | 68,986,259 | | |

**Majibu ya Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC)**

Shirika linakiri kuwepo kwa wafanyakazi wa mkataba ambao mikataba yao ilikuwa imeshaisha muda.

Shirika kwa muda mrefu lilikuwa lina wafanyakazi ambao walikuwa hawana mikataba, wafanyakazi hao walikuwa wanafanya kazi za uzalishaji kiwandani, na wengine wakitumika katika kusarifu bidhaa za kilimo hai, hii ilitokana na kuchelewa kupata kibali cha uajiri au muongozo mwengine wowote kutoka kwa katibu mkuu kiongozi. Shirika ilibidi liwalipe mishahara katika kipindi hicho cha kusubiri muongozo kutoka serikalini kwa sababu walikuwa wakitumika katika uzalishaji.

Aidha, baada ya Shirika kupata muongozo kutoka kamisheni ya kazi kwa barua nam. KK/24/06/VOL.1/39 ya tarehe 16/02/2021. liliwaondosha kazini wafakazi hao kwa kupitia zoezi la "redunducy" kwa mujibu wa Sheria ya Ajira nam. 5 ya mwaka 2011, kwa sasa Shirika litakapotaka kufanya uajiri mpya litaandaa mahitaji ya nafasi za ajira husika, na litafuata taratibu zote za kiutumishi katika uajiri kwa kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za utumishi.

**Uchunguzi wa Kamati ya LAAC**

Katika kufatilia hoja hii kamati imethibitisha ni kweli wafanyakazi hao walilipwa mishahara bila ya kuwa na mikataba ya ajira hali hii imetokana na Shirika kutopatiwa kibali cha kuajiri baada ya kutoka agizo kwa Serikali za kuwaondoa wafanyakazi wa muda, wakati huo huo shirika lilikuwa linahitaji wafanyakazi kwa ajili ya uendeshaji wa Shirika na kwa upande wa Kiwanda cha Makonyo shirika pia lilikuwa linahitaji vibarua kwa ajili ya uzalishaji wa kiwanda hicho. Hivyo basi shirika liliamua kuendelea kuwatumia wafanyakazi hao ili kuepusha hasara ambayo shirika lingeliweza kupata ikiwa lingesimamisha shughuli zake kwa kukosa rasilimali watu.

**Mapendekezo ya Kamati**

Kamati inashauri Serikali kuharakisha utaratibu wa kutoa vibali vya ajira kwa Tasisi

zake hasa zile zenye kutoa huduma za Uzalishaji wa Bidhaa ambazo kwa kiasi kikubwa zinahitaji nguvu kazi katika kutekeleza shughuli zake Aidha kamati inalishauri shirika linaweza kuendelea kuwatumia wafanyakazi wake kwa kuwataka kujisali katika vikundi na kuingia nao mkataba maalum wa malipo kwa kila kipindi watakapotaka kuwatumia wafanyakazi hao katika shughuli mbalimbali za uzalishaji katika Shirika.

## 5.3 MAMLAKA YA VIWANJA VYA NDEGE ZANZIBAR (ZAA)

### Taarifa ya Mapato

Ukaguzi umebaini kuwa mapato ya Mamlaka ya Viwanja Vya Ndege Zanzibar yameongezeka kutokashilingi 17,363,392,528 kwa mwaka wa fedha 2019/2020, hadi kufikia shilingi 20,995,542,990 kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 20.9.

### Majibu

Mapato ya Mamlaka kwa mwaka wa fedha 2020/2021 yameongezeka kwa asilimia 20%, kutoka Tsh 17.363 bilioni mwaka wa fedha 2019/2020 hadi Tsh 20.996 bilioni mwaka wa fedha 2020/2021. Kwa upande wa mapato yatokanayo na shughuli za ndege (aeronautical revenues) yameongezeka kwa asilimia 16.91% kutoka Tsh 11.950 bilioni mwaka wa fedha 2019/2020 hadi Tsh 14.293 bilioni mwaka wa fedha 2020/2021.

Ongezeko la mapato yatokanayo na shughuli za ndege (aeronautical revenues) yametokana na kuengezeka kwa abiria wa kimataifa kutoka nchini Urusi, pamoja na kuanza kukusanywa ada ya ulinzi (security fees), hali iliyopelekea kutolewa Ankara zenye thamani ya Tsh 2,152,553,854 ambazao mapato yake yamejumuishwa kwenye hesabu hizi (recognized Revenues).

Mapato yasiyotokana na shughuli za ndege (non-aeronautical revenues), yaliongezeka kwa asilimia 31.87% kwa kiwango kikubwa engezeko hili limesababishwa na kuengezeka kwa wapangaji kama vile Unity air, Kisk Company, Peoples Bank of Zanzibar, UAS Tanzania Ltd, Aroma Flower na Furaha Mobile Services ambao wanatakiwa kulipia kodi ya pango pamoja na matumizi ya umeme.

Mapato yatokanayo na msaada wa Serikali (Government Grants and assistant), yaliongezeka kwa asilimia 19.94%, ongezeko hili, limesababibishwa na Mamlaka kupatiwa msaada wa fedha kwaajili ya kulipa mishahara ya wafanyakazi na baadhi ya gharama za uendeshaji, msaada huo ulitokana na kuathiriwa uwezo wa kifedha wa Mamlaka kutokana na athari ya maradhi ya Uviko-19.

### Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Kamati imeelezwa kuwa kupungua kwa mripuko wa maradhi ya UVIKO 19 duniani

kwa kiasi kikubwa kumechangia ongezeko la mapato kutokana kuongeza kwa uingiaji wa mara kwa mara wa watalii nchini.

Kamati imerizika na jitihada zinazochukuliwa na Mamlaka katika kukusanya mapato katika vyanzo vyake hata hivyo Kamati inaendelea kusisitiza juu ya kubuni vyanzo vipya vya mapato pamoja na udhibiti wa mapato hayo kwa kuimarisha matumizi ya mifumo ya Tehama katika ukusanyaji wake ili Mamlaka iweze kuongeza wigo wa ukusanyaji wa mapato na shughuli za Mamlaka ziweze kutekelezeka kwa ufanisi mkubwa.

**Taarifa ya Matumizi**

Ukaguzi umebaini kuwa matumizi ya Mamlaka ya Viwanja Vya Ndege Zanzibar yamepungua kutoka shilingi 63,984,120,651 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 hadi kufikia shilingi 24,427,193,977 kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ikiwa ni sawa na upungufu wa asilimia 61.8.

**Majibu**

Matumizi ya Mamlaka yamepunguwa kwa asilimia 62% kutoka Tsh 63.984 bilioni mwaka wa fedha 2019-2020 hadi Tsh 24.427 bilioni mwaka wa fedha 2020-2021. Upungaji wa gharama kwa asilimia kubwa umetokana na kutokuwepo kwa hasara ya ilioneshwa katika mwaka wa fedha 2019-2020 ambayo inajumla ya Tsh 52.519 bilioni.

Kwa upande wa mchanganauo wa matumizi, matumizi ya uendeshaji yalipunguwa kwa asilimia 18%, gharama za kifedha zilipunguwa kwa asilimia 41%, na gharama za matengenezo zilipunguwa kwa asilimia 51% upunguaji wa gharama umetokana na kufifia kazi za Mamlaka kutokana na kufifia shughuli za kiuchumi zilizotokana na athari ya maradhi ya Uviko-19. Kwa gharama za Mishahara na wafanyakazi ziliongezeka kwa asilimia 25%, ongezeko hili limesababishwa na kuengezeka kwa mishahara yaliotokana na muongozo mpya wa malipo ya mshahara kwa wafanyakazi wa Serikalikutathmini mali za Mamlaka (Revaluation loss) ambayo

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati inakubaliana na majibu yaliyotolewa na Mamlaka na imejiridhisha kuwa matumizi mbalimbali ya Mamlaka yamepungua kutoka na athari za mripuko wa maradhi ya UVIKO kwa kipindi hicho, hata hivyo Kamati inaishauri Mamlaka katika kuzipa kipao mbele baadhi ya Shughuli ambazo huleta tija katika kuongeza mapato Mamlaka kama vile Kusomesha wafanyakazi wake kwa lengo la kukusanya mapato ya ada ya ulinzi “security fees”, ambapo moja masharti ya kulipwa ada hii ni kuwa na wafanyakazi wenye weledi na mambo ya ulinzi ambao wamepatiwa mafunzo hayo Katika vyuo maalum kwa mujibu wa miongozo ya uendeshaji wa Mamlaka za Viwanja vya ndege vya Kimataifa.

**MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI**

#### 5.3.1.1 Kukosekana kwa vielelezo vinavyothibitisha marekebisho ya Mtaji wa Mamlaka shilingi 13,708,303,373

Taarifa za fedha za mwisho wa mwaka 2020/2021 zinaonyesha kuwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar imefanya marekebisho katika mtaji wake yaliyopelekea ongezeko la mtaji lenye jumla ya shilingi 13,708,303,373. Marekebisho hayo yametokana na Mamlaka kubadilisha asilimiaza kupunguza uchakavu wa mali zake kudumu.

Ukaguzi umeshindwa kupata vielelezo vinavyothibitisha marekebisho ya mtaji wa Mamlakayaliyopelekea ongezeko la mtaji kwa kiasi cha shilingi 13,708,303,373.

Kukosekana kwa vielelezo vinavyothibitisha marekebisho ya mtaji wa mamlaka ni kwenda kinyumena kifungu nambari 34(1) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya Zanzibar yamwaka 2016 na kunapelekea hesabu za Mamlaka kutotoa sura halisi na sahihi.

Ukaguzi unashauri Mamlaka wa Mamla ya Viwanja vya Ndege kuhakikisha kuwa wanaweka vielelezo vyote vinavyohusiana na taarifa za fedha zilizoripotiwa katika hesabu za mwisho wa mwaka ili ziweze kutoa sura sahihi na halisi.

**Majibu**

Mamlaka imekubaliana na hoja ya Mkaguzi, ambapo Marekebisho ya Mtaji (owner equity) yamefanyika kwa kuzingatia mahitaji ya miongozo ya kimataifa ya uwekaji kumbukumbu za kiuhasibu (IPSA -17 "Property, Plant and Equipment" and IPSAS - 19 "Provision, Contingent liabilities and contingent assets).

Marekebisho ya mtaji yalitokana na kubadilika kwa viwango vya tozo (asilimia) ya ukokotoaji wa uchakavu wa mali za Mamlaka (change in depreciation rate), viwango vya awali tangu mwaka wa fedha 2011-2012 vilikuwa vimewekwa na Mamlaka kwa kuzingatia viwango vinavyotumika katika kukotoa "depreciation allowance" kwa mujibu wa sheria ya kodi ya mapato ya mwaka 2004 (income Tax act) na kwa kuwa Mamlaka kwa kupitia Ofisi ya Raisi, Fedha na Mipango (Idara ya uhakiki mali) ilifanya tathmini ya mali zake mwaka wa fedha 2019/2020, Katika uhakiki uliofanyika, Idara ya Uhakiki Mali walitumia viwango vya uchakavu wanavyo vitumia kwa Serikali yote (standardized depreciation rate) ambazo baadhi yao zilitofautiana na viwango ambavyo vimewekwa na Mamlaka.

Katika hali hio, Mamlaka baada ya kutathminiwa mali zake ikaona ni vyema kutumia viwango vinavyotumiwa na Idara ya Uhakiki mali, kwakuwa ndio Idara ilio na majukumu ya kuweka kumbukumbu za mali zote za Serikali, na kwa kuwa taarifa ya utathmini iliopatiwa Mamlaka tayari imeshaingizwa kwenye mfumo wa Idara ya

Uhakiki (Government Assets Registar).

Kwa mujibu wa miongozo ya hesabu (IPSAS 17) inaelezea, ikiwa kutafanyika mabadiliko ya viwango vya uchakavu, gharama za uchakavu zitatakiwa kukotolewa upya kwa kutumia viwango vipya kuanzia tarehe ambayo viwango vinavyobadilishwa (old rate) vilianza kutumika (Retrospective adjustment), baada ya kupata thamani mpya ya gharama za uchakavu, 5 unalinganisha na gharama za uchakavu zilizopatikana kwa kutumia viwango vya zamani, na tofauti unatakiwa kuipeleka kwenye Mtaji (owner equity).

Mamlaka ilitafuta thamani inayotakiwa kupelekwa kwenye mtaji (transfer to owner equity) kwa kutumia njia ya makisio (best estimate) kwa kutumia njia ya "equation" (ambayo kwa mazingira ya Mamlaka, inaweza kutoa makisio bora ya gharama za uchakavu). Mamlaka imetumia njia hii, kutokana na mapungufu ya uwekaji wa taarifa za mali za Mamlaka, kwa miaka yote ya nyuma tangu ianzishwe katika kutatua, mapungufu ya uwekaji wa mali za Mamlaka, Mamlaka iliiomba Idara ya Uhakiki mali, kufanya tathmini ya mali (kwani mali nyingi zilikuwa hazijuilikani thamani yake) na baada ya kutia thamani, Mamlaka iliwataka kututengenezea buku la mali (assets register) pamoja na kuweka alama za utambulisho kwa kila mali. (Uthibitisho wa nyaraka husika zipo tayari kwa ajili ya uhakiki).

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati imebaini kuwa Mamlaka kushwidwa kutambua uchakavu wa kila mali yake kutokana na kutokuwa na daftari la kumbukumbu na kupelekea kufanya mabadiliko ya thamani ya uchakavu kutoka asilimia ya zamani kwenda asilimia mpya katika mtaji wake kwa kufanya makisio tu ya thamani ya uchakavu wa mali zake kwa jumla kinyume na taratibu na miongozo ya kimataifa ya uwekaji kumbukumbu za kiuhasibu.

Kwa vile Mamlaka tayari imeshafanya zoezi la tathmini ya mali zake basi Kamati inasisitiza kuboreshwa kwa daftari la usajili wa mali ili Mamlaka iwe na hesabu sahihi ya mtaji wake kwa ajili ya kufanyiwa tathmini kila inapohitajika kwa ukaguzi.

### 5.3.1.2 Kutokufuatwa kwa vipengele vya mikataba baina ya Mamlaka ya Viwanjavya ndege na kampuni

Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar zinazotoa huduma kwa ndege (ground handlers) imefunga mikataba baina yake na kampuni ya ZAT na kampuni ya Transworld kwa ajili ya utoaji huduma kwa ndege (ground handling services). Mkataba baina ya Mamlaka na kampuni ya ZAT umetiwa saini tarehe 3 Febuari, 2015. Mkataba huo ulikuwa ni wa muda wa miaka kumi na tano (15). Mkabata halisi baina ya Mamlaka na kampuni yaTransworld haukupatinaka kwa ukaguzi.

Kwa mujibu wa kipengele cha 5.2.1(i) cha mkataba baina ya Mamlaka na kampuni ya

ZAT ambacho kinahusiana na malipo ya kodi (concession fee), mkataba huo ulitakiwa kupitiwa kila baada ya miaka mitatu (3), ambapo ukaguzi umebaini kuwa kiwango cha kodi kilichokubaliwa awali katika mkataba ni asilimia 5% ya mapato ya kampuni.

Hata hivyo ukaguzi umebaini kuwa mikataba hiyo ya kampuni zinazotoa huduma kwa ndege haijawahi kupitiwa tokea ilipowekwa saini kinyume na makubaliano ya mikataba hiyo.

Kutokukupitiwa mikataba ya kampuni zinazotoa huduma kwa ndege ni kwenda kinyume na makubaliano ya mikataba hiyo na kunaweza kupelekea Mamlaka kupoteza mapato.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Mamlaka ya Viwanja vya ndege kufuata makubaliano ya mikataba hiyo ikiwemo kupitiwa upya vipengele vya mikata hiyo ili kuweza kulinda maslahi ya Mamlaka katika mikataba hiyo.

**Majibu**
Mamalaka ya viwanja vya ndege inakiri kuwa imefunga mikataba miwili kwa makampuni mawili tofauti, kampuni ya Transworld Aviation Limited Zanzibar na Zanzibar Aviation Services & Travel Trade Limited kwa lengo la kutoa huduma za ndege, abiria na mizigo (Ground Handling Services) Mkataba baina ya Mamlaka na Kampuni ya Zanzibar Aviation Services Travel Limited (ZAT) ni wa Miaka 15 na umeshadumu miaka 7. Mamlaka inakiri kwamba mpaka kufika mdhibiti na mkaguzi wa hesabu za Serikali haijafanya mapitio ya ibara ndogo ya 5.2.1(i) ambayo inahusika na malipo ya ada ya biashara (concession fee) ambayo imeelekeza kuwa kampuni hiyo italipa kiwango cha asilimia tano (5%) ya mapato yanayopatikana katika malipo kwa huduma ya ndege, abiria na mizigo. Ada zinazolipwa katika huduma ya usafiri wa anga pia inadhibitiwa na Mamlaka ya usafiri wa anga kwa mujibu wa sheria na miongozo ya Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA) ambapo endapo kutatakiwa kufanyika mapitio ni sharti kupata maoni kutoka kwa msimamizi wa masuala hayo pamoja na kuweza kuangalia mwenendo mzima wa sekta hiyo inavyoendelea kwa mazingatio ya sehemu nyengine duniani ikiambatana na uwekezaji ambao Kampuni imewekeza katika vifaa na rasilimali nyengine.

Hivyo, Mamlaka inakiri kutofanya mapitio na si tu kwa lengo la kupoteza mapato na kutoweza kulinda maslahi ya Serikali bali pia ni kuendeleza huduma hiyo. Hii inatokana na uwekezaji Mkubwa uliowekezwa na Serikali kwa Kupatiwa Jengo jipya la abiria la Terminal III ambalo litapelekea kuongezeka kwa huduma ikiwemo huduma ya abiria na mizigo Pamoja na uimarishaji wa huduma zinazotolewa kiwanjani hapo Kwa mujibu wa mikataba hiyo Kiwango hicho cha ada ya biashara kinaweza kufanyiwa mapitio kila baada ya miaka mitatu (3), kutokana na hali ya

kibiashara kwa sasa Mamlaka inajipanga kukaa na wadau husika kwa ajili ya kufanya mapitio ya kifungu hicho ndani ya mzunguko huu.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kwa vile Mamlaka imekiri kutofanya mapitio ya mkataba huo kinyume na ibara ndogo ya 5.2.1 (i) kamati haikuona haja kuendeleza majadiliano ya hoja hii bali imeishauri Mamlaka kufuata taratibu na masharti ya mikataba wanayoifunga na makampuni mbalimbali ya kutoa huduma ili tija iliyokusudiwa iweze kupatika na kutatua changamoto mbalimbali ambazo zinaleta usumbufu baina ya pande mbili za mkataba ziweze kupatiwa ufumbuzi.

### 5.3.1.3 Kukosekana kwa sera ya mikopo kwa Wafanyakazi wa Mamlaka

Ukaguzi umebaini kuwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar inatoa mikopo kwa wafanyakazi wake lakini hakuna sera iliyoidhinishwa inayofuatwa kwa ajili ya utoaji wa mikopo hiyo. Aidha ukaguzi umebaini kuwa ndani yam waka wa fedha 2020/2021 kulikuwa na mfanyakazi mmoja ambae alikuwa na mkopo wa shilingi 6,600,000, mfanyakazi huyo alikuwa katika likizo bila ya malipo na deni lake halikuwa likilipwa.

Kukosekana kwa sera iliyoidhinishwa ya utoaji wa mikopo kwa wafanyakazi wa Mamlaka kunaweza kupelekea kuwepo kwa udhibiti mdogo katika utoaji na ufuatiliaji wa mikopo hiyo.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Mamlaka kuhakikisha kuwa wanaandaa na kutumia sera maalum iliyoidhinishwa inayotoa muongozo wa utoaji mikopo kwa wafanyakazi wa Mamlaka ili kuongeza udhibiti katika utoaji mikopo hiyo na kuhakikisha kunakuwepo usawa katika utoaji na urudishaji wa mikopo.

**Majibu**

Mamlaka ya Viwanja vya ndege Zanzibar, ilitaarisha rasimu ya sera ya mikopo kwa wafanyakazi katika mwaka wa ukaguzi 2020-2021, Katika mwaka wa fedha 2021-2022 Sera hiyo ilipata idhini ya Bodi ya Wakurugenzi wa Mamlaka na kuanza kutumika Rasmi.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati imeelezwa kuwa wakati mkaguzi alipopita rasimu ya sera ya mikopo ilikuwa bado haijapitishwa na bodi ila kwa sasa tayari imeshapitishwa na imeshaanza kufanya kazi.

Mbali na hayo Kamati inasisitiza kufuatiliwa kwa karibu aliyekuwa mfanyakazi wa Mamlaka katika kumaliza deni lake ambapo hadi Kamati ilipomaliza ukaguzi wake tumearifiwa kuwa mfanyakazi huyo bado anadaiwa Tzs 5,600,000 baada ya

kufanyiwa uhakiki wa deni lake.

#### 5.3.1.4 Kutokuridhiwa kwa mikataba ya zabuni ya Mamlaka na Afisi ya Mwanasheria Mkuu shilingi 4,842,626,063.25 na USD 799,608

Kwa mujibu wa kifungu nambari 27(3) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016, mikataba yote inayohusiana na masuala ya zabuni baada ya kukubaliwa kwa zabuni ni lazima iridhiwe na Afisi ya Mwanasheria Mkuu kabla ya kusainiwa na pande mbili husika katika mkataba.

Ukaguzi umebaini baadhi ya mikataba ya zabuni ya Mamlaka haikupelewa katika Afisi ya Mwanasheria Mkuu kwa ajili ya kuridhiwa kabla ya kusainiwa na pande mbili kinyume na kifungu nambari 27(3)cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

Kushindwa kupata ridhaa ya Afisi ya Mwanasheria Mkuu katika mikataba ya zabuni ya Mamlaka ni kwenda kinyume na Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka

2016. Aidha Mamlaka inaweza kuingia katika mikataba ya zabuni ambayo haina manufaa kwa Mamlaka na kwa nchi kwa ujumla.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kufuata misingi ya Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016 ikiwemo kupata ridhaa ya Afisi ya Mwanasheria Mkuu kwa mikataba yote ya zabuni ya Mamlaka.

**Majibu**

Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar imekubaliana na hoja ya Mkaguzi, ili kuhakikisha changamoto hii haijitokezi tena kuanzia mwaka wa fedha 2021- 8 2022 hadi sasa mikataba yote inayoingiwa na Mamlaka inawisilishwa katika Afisi ya Mwanasheria Mkuu.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kwa vile Mamlaka imekiri kufanya dosari hii na tayari imeshaanza kuchukua juhudi ya kuhakikisha mikataba yote inapelekwa kwa mwanasheria, Kamati inalisisitizo kwani kupelekwa mikataba kwa mwanasheria mkuu kunaisadia taasisi za Serikali kufunga mikataba isiyo na tija kwa upande wao na Serikali nzima.

#### 5.3.1.5 Ununuzi wa bidhaa pasi na kufuata misingi ya ushindani, shilingi 4,842,626,063

Kwa mujibu wa kifungu nambari 37 cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016, ununuzi wa mali za umma unatakiwa kufanywa kwa kuzingatia misingi ya kutokuwa na ubaguzi; kwa uwazi, uwajibikaji na bila ya upendeleo, na kwa kuwepo kwa ushindani na kuhakikisha thamani ya fedha inapatikana.

Aidha kifungu nambari 68(1) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016 kinasisitiza kwa taasisi ya ununuzi na uondoaji wa mali za umma kutumia utaratibuwa wazi wa ndani wa zabuni.

Ukaguzi umebaini kuwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar imefanya ununuzi wa bidhaa na huduma mbalimbali pasi na kufuata utaratibu wa ushindani wa wazi.

Kufanya ununuzi wa bidhaa na huduma pasi na kuwepo kwa ushindani ni kwenda kinyume na misingi ya Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kuhakikisha kuwa ununuzi wote wa Mamlaka unafanywa kwa mujibu wa miongozo ya Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

**Majibu**

Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar imekubaliana na hoja ya Mkaguzi kwa baadhi ya watoa huduma isipokuwa huduma ziliozotolewa na Kampuni za Osaju kwa ajili ya miundombinu ya umeme utaratibu wa mzabuni mmoja (single soure) ulitumika ili kurahisisha upatikanaji wa huduma katika muda muwafaka kutokana na mazingira yaliojitokeza ikiwemo hali ya joto katika majengo ya abiria. Aidha kwa huduma zilizotolewa na kampuni ya Arinc kwa ajili ya mfumo wa kuwatambuwa abiria mfumo wa wazi wa kimataifa (open international competitive bidding) ulitumika.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati imebaini mkataba baina Zanzibar Airpot vs Sheby Enterprise Zanzibar haukuhitaji Zabuni kwasababu haukifikia kiwango cha kuitisha zabuni

Hata hivyo Mamlaka imekiri kununua baadhi ya huduma pasi na kufuata utaratibu wa misingi ya ushindani kwa kile walichosema uhitaji wa huduma hizo kwa haraka na nyengine zilikua ni za dharura hivyo ilibidi ilibidi kutekelezwa kwa haraka kwa maslahi ya uendeshaji wa shughuli za Mamlaka hiyo.

Kamati haipingani na maelezo hayo na inaishauri Mamlaka kufuata Sheria na miongozo mbalimbali ya fedha kwani upo uwezekano wa kuwasilisha matumizi ya Dharura kupitia Afisi ya Rais Fedha na Mipango na endapo taasisi ikiruhusika kufanya hivyo basi iwe na ushahidi wa maandishi ili uwe uthibitisho kwa ukaguzi.

**5.3.1.6 Kukosekana ushindani katika ununuzi wa huduma za chakula na viburudishaji, shilingi 284,157,300**

Kwa mujibu wa kifungu cha 68(1) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na

Uondoshaji wa Maliza Umma ya mwaka 2016, taasisi ya ununuzi na uondoaji wa mali za umma inatakiwa kutumia utaratibu wa wazi kwa zabuni za ndani. Aidha Jadweli la 5 la Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016 linaeleza kuwa ununuzi wa bidhaa zenye thamani ya zaidi ya shilingi 50,000,000 ni lazima yafanyike kwa kutumia njia ya Zabuni za wazi za ndani.

Ukaguzi umebaini kuwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar imenunua huduma ya chakula kutoka kwa mzabuni mmoja (Local Food Bazaar) ambapo jumla ya shilingi 284,157,300 zililipwa kwa mzabuni huyo pasi na kuwepo kwa ushindani. Aidha ukaguzi haukupata mkataba uliosainiwa baina ya Mamlaka na mzabuni huyo.

Kufanya ununuzi wa bidhaa na huduma pasi na kuwepo kwa ushindani ni kwenda kinyume na misingi ya Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016, na kunaweza kupelekea Mamlaka kununua bidhaa au huduma kwa bei ya juu ukilinganisha na bei ambayo ingepatikana kama ununuzi ungefanyika kwa njia ya ushindani.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kufanya ununuzi wa huduma za chakula na vinywaji kwa kutumia njia ya ushindani.

**Majibu**

Mamlaka kwa kipindi kirefu, inachangamoto ya kutokuwa na wafanyakazi wa kutosha, hivyo kupelekea kuwapanga wafanyakazi katika awamu tatu ambao walitakiwa kuingia masaa 12 badala ya masaa nane kwa kila siku ambayo awamu husika inatakiwa kuwepo kazini, kwa kuwa utaratibu huu, ulianza kwa haraka ilikutatua changamoto za uchache wa wawafanyakazi, kuliibuka changamoto ya kupatiwa chakula wafanyakazi kwani masaa waliokuwa wanafanya kazi yalizidi kiwango cha kawaida kwa kila mfanyakazi ambae awamu yake (shift) ipo kazini.

Katika mazingira hayo, Mamlaka ililazimika kutafuta mtoa huduma ya chakula cha mchana, maji na chai, hapo awali Mamlaka ilichukuwa huduma kutoka Kampuni ya Ocean grill, lakini kutokana na changamoto, kampuni hii, ilishindwa kuendelea na kutua huduma, Hivyo Mamlaka ilitafuta kampuni nyengine inayoitwa "Executive chef" kwaajili ya kuendelea kutoa huduma, vile vile kampuni hii, ilishindwa kuendelea na kutoa huduma hivyo kupelekea Mamlaka kutafuta Kampuni nyengine, ambayo ilikuwa ni Local food bazzar ambao iliendeleza utoaji wa huduma mpaka pale utaratibu wa kuingia kazini ulipobadilishwa na kuondokana na uhitaji wa kutoa huduma ya chakula kwa wafanyakazi. 10 Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar imekubaliana na hoja ya Mkaguzi.

Katika kutatua changamoto hiyo Mamlaka Iliomba muongozo kutoka Afisi ya Rais Utumishi wa Umma kuhusiana na chakula cha wafanyakazi wanaoingia shift ya masaa 12. Mamlaka kupitia barua ya tarehe 8 March 2022 yenye kumbukumbu

namba PCCB.167/311/01/16 ilipatiwa muongozo kutoka Afisi ya Rais Utumishi wa Umma kuwapatia posho maalum la TZS 120,000 wafanyakazi wanaoingia kazini muda wa masaa 12 ili iwasaidie kupata chakula. Utekelezaji wa muongozo huo ulianza mara tu baada ya kupatikana muongozo huo.

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Kamati haikuona haja ya kuendelea na hoja hii kwa vile Mamlaka imekiri kufanyika kwa dosari kutokana na changamoto ambazo wamezieleza katika majibu yao na kwa vile dosari hii imeshapatiwa ufumbuzi baada kuomba ushauri kutoka Afisi ya Rais Utumishi wa Ummah na Utawala bora

Hata hivyo Kamati inaishauri Mamlaka katika kufuata sheria mbalimbali za matumizi hasa kifungu cha 68(i) cha Sheria nambari 11 ya ununuzi na uondoshaji wa mali za ummah ya mwaka 2016 wakati wanapotaka kupatiwa huduma kwa wazabuni mbalimbali.

### 5.3.1.7 Ununuzi wa bidhaa pasi na kuzingatia njia za maombi ya ushindani (quotation) shilling 433,359,453.

Kwa mujibu wa kifungu nambari 68(1) na Jadweli la Tano la Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016, ununuzi wa bidhaa zenye thamani kuanzia shilingi 15,000,000 hadi shilingi 50,000,000 unatakiwa ufanyike kwa kutumia njia ya maombi ya ushindani (quotations). Aidha Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma imetoa nyaraka maalum (standard document) inayoongoza ununuzi wa bidhaa kwa njia ya ushindani.

Ukaguzi umebaini kuwa Mamlaka ya Viwanja vya ndege Zanzibar imefanya ununuzi wa bidhaa zenye thamani baina ya shilingi 15,000,000 na shilingi 50,000,000 pasi na kutumia njia ya maombi ya ushindani (quotations) na pasi na kutumia nyaraka maalum ya ununuzi wa bidhaa kwa njia ya maombi ya iliyotoliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma.

Kufanya ununuzi wa bidhaa na huduma pasi na kuwepo kwa ushindani ni kwenda kinyume na misingi ya Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016. Ukaguzi unashauri uongozi wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kuhakikisha kuwa ununuzi wote wa Mamlaka unafanywa kwa mujibu wa miongozo ya Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

Majibu

Mamlaka ya Viwanja vya ndege Zanzibar inakubaliana na hoja ya Mkaguzi, miongoni mwa sababu zilizopelekea kutokea hoja hii, nikuwa Kiwango cha fedha kilichoainishwa na sheria ya manunuzi kifungu nambari 68(1) na Jaduali la tano (5) kinahitaji ununuzi wenye thamani kuanzia Tsh 15milion kuwa ni kidogo sana, kulinganisha na uhalisia wa matumizi ya taasisi kama Mamlaka ya Viwanja vya

ndege, Hata hivyo, changamoto hii, Mamlaka iliaandikia Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshwaji wa mali za Umma, kuomba kuzidishiwa kiwango, kutoka Tsh 15 milioni angalau iwe Tsh milioni 50 kutokana na mahitaji na gharama za vitu au huduma zinazotumiwa na Mamlaka. Hata hivyo manunuzi hayo yalifanywa kwa kupitia ushindani (quotation) kwa utaratibu uliowekwa wa manunuzi kwa kiwango chini ya milioni 15.

Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar imekubaliana na hoja ya Mkaguzi. Kwa sasa Mamlaka inazingatia maombi ya ushindani katika zabuni zake kama ilivyoelekezwa na sheria.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya LAAC haikuridhika na majibu ya Mamlaka hivyo, hoja hii imebaki kama ilivyo.

Pamoja na hayo, Kamati ya LAAC inaishauri Taasisi inayohusika na Sheria ya Ununuzi kuifanyia marekebisho Sheria hiyo kwa kuwa masharti yaliyowekwa kwenye Sheria hiyo utekelezaji wake unakwaza baadhi ya Taasisi. Hivyo, ni busara ikatungwa Sheria ambayo masharti yake yataziwezasha Taasisi kuitekeleza Sheria hiyo kwa mujibu wa majukumu yao.

### 5.3.1.8 Kutokuwasilisha ripoti ya utekelezaji wa ununuzi kwa Mamlaka ya ununuzi na uondoaji wa mali za Umma.

Kwa mujibu wa Kanuni ya 64(2)(c) na (d) ya Kanuni za Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma za mwaka 2020, taasisi ya ununuzi na uondoshaji wa mali za umma inatakiwa kuwasilisha ripoti ya utekelezaji wa ununuzi kwa kila robo mwaka kwa Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma ndani ya siku saba baada ya kumalizika robo mwaka husika, na kuwasilisha ripoti ya utekelezaji wa ununuzi ya mwaka ndani ya siku 30 baada ya kumalizika kwa mwaka husika.

Hata hivyo, ukaguzi umebaini kuwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar haijawasilisha ripoti hizo katika mwaka wa fedha 2020/2021 kinyume na Kanuni za Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma za mwaka 2020.

Kutokuwasilisha ripoti za utelekelezaji wa ununuzi za robo mwaka na yam waka ni kwenda kinyume na Kanuni za Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma za mwaka 2020.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Mamlaka kufuata miongozo ya Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016 na kanuni zake katika ununuzi wa bidhaa.

**Majibu**

Mamlaka ya Viwanja vya ndege Zanzibar inakubaliana na hoja ya Mkaguzi. Kuanzia

mwaka wa fedha 2021/2022 Mamlaka imeanza kuwasilisha Ripoti ya utekelezaji wa ununuzi kwa Mamlaka ya ununuzi na uondoaji wa mali za Umma.

**Uchunguzi wa Kamati**

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC imebaini yafuatayo:

1. Watendaji wa Mamlaka hawakuwa na uelewa juu ya kanuni husika
2. Siku 7 zilizowekwa ndani ya Kanuni hiyo ni kidogo kwani inaweza kutokea kuwa ndani ya kipindi hicho watendaji wa Kitendo cha Manunuzi wanawajibika na shughuli nyengine za Taasisi na hasa ikizingatia kuwa asilimia kubwa za Taasisi za Umma zina idadi ndogo ya wafanyakazi katika Kitendo hicho.

**Mapendekezo ya Kamati**

Kutokana na kasoro hiyo, Kamati ya LAAC imependekeza yafuatayo:

1. Watendaji wa umma wahakikishe kuwa wanazijua kwa undani Sheria na Kanuni zinazowaongoza ili kutekeleza shughuli zao kwa mujibu wa Sheria na Kanuni hizo.
2. Kanuni zinazohusiana na masuala ya Ununuzi kufanyiwa marekebisho katika kanuni hiyo ili kutoa muda wa kutosha wa kutekelezwa hilo.

### 5.3.1.9 Kukosekana kwa sera ya wadaiwa sugu

Katika mwaka wa fedha 2020/2021, ukaguzi umebaini kuwa hesabu za mwisho wa mwaka za Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar zimeweka 'kiasi cha asilimia' kwa ajili ya madeni yasiyoweza kulipika yaani madeni sugu (doubtful debts) pasi na kuwepo kwa sera maalum ya kuyatambua madeni sugu iliyoidhinishwa na Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka.

Kukosekana kwa sera ya kuyatambua madeni sugu iliyoidhinishwa na Bodi ya Wakurugenzi kunaweza kupelekea kiasi cha madeni yalitambuliwa kuwa ni sugu yasiwe sahihi na hatimae kupelekea bakaa ya waidaiwa wa Mamlaka kutotoa sura sahihi na halisi.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Mamlaka kutayarisha sera maalum kwa ajili ya kuyatambua madeni sugu ili kupelekea hesabu za Mamlaka kutoa sura sahihi na halisi.

**Majibu**

Mamlaka ya Viwanja vya ndege Zanzibar inakubaliana na hoja ya Mkaguzi, kwa kipindi cha ukaguzi Mamlaka ilikua ikitumia sera ya madeni ambayo haikuridhiwa na

bodi ya wakurugenzi wa Mamlaka. Katika kurekebisha changamoto hiyo tarehe 21 Oktoba 2022, Mamlaka imefanya mapitio ya Sera hiyo ambayo inatarajiwa kuwasilishwa katika kikao cha Bodi ya Wakurugenzi kinachotarajiwa kufanyika Februari ili kupata idhini na kutumika rasmi.

#### Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Hoja hii imebaki kama ilivyo, kutokana na majibu ya Mamlaka, hata hivyo, Kamati ya LAAC imeitaka Mamlaka kuishauri na kuitumia ipasavyo Bodi ya Wakurugenzi ili Bodi hiyo iweze kutekeleza shughuli zake vyema.

### 5.3.1.10 Dosari zilizobainika katika ununuzi wa vifaa vya TEHAMA Tsh. 107,230,000

Katika ukaguzi uliofanyika kupitia hesabu za mwisho wa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni 2021 imebainikia Mamlaka ya viwanja vya Ndege Zanzibar imefanya manunuzi ya vifaa mbali mbali vya TEHAMA vyenye thamani ya shilingi 107,230,000 kwa msambazaji Hassan and Sons Limited. Dosari iliyobainika na ukaguzi katika manunuzi hayo ni kama ifuatavyo:

- Kutokuwepo kwa makubaliano ya mkataba baina ya ZAA na Msambazaji wa Vifaa.
- Kutokuainishwa kwa vifaa vya TEHAMA vilivyonunuliwa katika Mpango wa Manunuzi wa Mwaka ambapo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 42(7) cha Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.
- Kutokuidhinishwa kwa manunuzi katika Bodi ya Zabuni ya Mamlaka.
- Gharama zilizooneshwa katika ankara za malipo ni kubwa ukilinganisha na gharama halisi za vifaa hivyo katika soko.

Kukiuka taratibu na sheria za manunuzi zinazohusiana na ununuzi wa vifaa vya TEHAMA kunaweza kupelekea kufanyika kwa ununuzi wa vifaa hivyo kwa gharama kubwa ikilinganishwa na gharama halisi zilizoko sokoni jambo ambalo linapelelekea kujitokeza kwa matumizi mabaya ya fedha na hatimae kuingiza hasara Serikali.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kuhakikisha unafanya manunuzi kwa kufuata taratibu, miongozo, kanuni na sheria za Manunuzi ili kuweza kuepuka kutumia fedha za umma vibaya na kuingiza hasara Serikali.

#### Majibu

Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar imekubaliana na hoja ya Mkaguzi. Mamlaka iliomba muongozo wa suala hili katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ambapo iliamulika kuundwa timu kwa ajili ya kufanya uchambuzi na kaungalia

value for money ya vifaa hivyo na kasha kuwasilisha ripoti rasmin kwa Mwanashria Mkuu kwa muongozo. Timu imeshakaa na kufanya uchambuzi na ripoti imeshawasilishwa kwa Mwanasheia Mkuu kwa muongozo.

### Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Kamati ya LAAC haikuridhika na majibu ya Mamlaka, hivyo, hoja hiyo imebaki kama iliyo.

### MAMLAKA YA UWANJA WA NDEGE – PEMBA

#### 5.3.1.11 Kukosekana kwa mapato yatokanayo na utowaji wa huduma shilingi 12,928,375

Katika Ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Pemba inadai Taasisi za Serikali pamoja na watu binafsi jumla ya shilingi 12,928,375 zitokanazo na utoaji wa huduma mbali mbali bila ya kufanyiwa ufuatiliaji wa ukusanyaji wa mapato hayo,hali ambayo inaweza kupelekea kuikosesha Serikali mapato kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbali mbali za maendeleo ikiwa ni pamoja na utowaji wa huduma mbali mbali kwa jamii.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Pemba kuhakikisha unafuata sheria, kanuni, pamoja na miongozo mbali mbali inayohusu ukusanyaji wa mapato katika taasisi za Serikali ili kuepusha ukiukwaji wa sheria ya Usimamizi wa fedha za Umma.

### Majibu

Mamlaka inakiri kwamba mpaka kufika Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali Deni hilo lilikuwepo. Mamlaka imechukua jitihada kufuatilia madeni hayo kwa kuwaandikia barua na kuwafuata ana kwa ana na mpaka kufika Januari 2023 tayari Wizara ya Biashara na Ofisi ya Mufti Mkuu wameshalipa madeni yao na uthibitisho wa malipo hayo upo kwa ajili ya uhakiki.

Aidha, Mamlaka inapokea ushauri wa ukaguzi wa kuhakikisha Mamlaka inafuata Sheria, kanuni pamoja na miongozo mbali inayohusu ukusanyaji wa mapato katika taasisi za Serikali ili kuepusha ukiukwaji wa sheria ya usimamizi wa fedha za Umma.

### Uchunguzi wa Kamati

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC ilibaini yafuatayo:

1. Ni Afisi ya Mufti pekee iliyokamilisha deni hilo tarehe 07 Machi, 2022 kupitia hati ya malipo Namba 02176.

2. Wizara ya Biashara imepunguza deni na kulipa Tsh, 80,000,000 tarehe 17 Januari, 2023, hivyo, deni lililobakia ni Tsh. 40,000.

3. Kampuni ya Ndege ya Zan air ameomba afanye kwanza uhakiki wa deni lake ambalo ni Tsh. 8,734,600 kwa kuwa hivi sasa hatekelezi shughuli zake ipasavyo.

4. Mamlaka ya Uwanja wa Ndege Pemba haifuatilii ipasavyo ulipwaji wa madeni hayo kwani kati ya Tsh. 12,928,375 zinazodaiwa ni Tsh. 12,728,375 tu ambazo zimelipwa.

**Mapendekezo ya Kamati**

Kutokana na kasoro hizo, Kamati ya LAAC imependekeza yafuatayo:

1. Mamlaka hii ifuatilie kwa karibu ulipwaji wa madeni hayo hasa ikizingatiwa kuwa asilimia kubwa ya Wadaiwa hawajalipa.
2. Kampuni ya Ndege ya Zan air ilipe deni lake lote kwa kuwa Kampuni hiyo inajishughuli na shughuli nyengine ambazo zinawaingizia kipato.

#### 5.3.1.12 Kutokuwepo kwa kibali cha wafanyakazi wa muda.

Kanuni ya utumishi wa umma kifungu cha 135(1) kinaeleza kuwa "Hakutakuwa na utumishi wa kutwa katika utumishi wa Umma, kama kuna ulazima Katibu Mkuu au Mkuu wa Taasisi atalazimika kuomba kibali kwa Tume ya Utumishi husika na kumjazisha mkataba. Aidha kifungu nambari 135(2) kinaeleza "Utumishi wa mtumishi wa kutwa hautozidi miezi sita (6) na atalipwa pale ambapo anamaliza kazi yake kwa siku na pia kifungu nambari 135(3) kinaeleza kuwa "Mtumishi wa kutwa hatakuwa na fursa ya likizo wala hana haki ya kudai kiinua mgongo na mafao ya uzeeni".

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Pemba imeingia mkataba na watumishi wa kutwa ambao huwajazisha mikataba mipya kila mwaka na kuwalipa mishahara kila mwisho wa mwezi bila ya kuwepo kibali kutoka Tume ya Utumishi Serikalini hali ambayo inaweza kuwakosesha haki za msingi watumishi hao.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu cha Kanuni ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2014 kilichonakiliwa hapo juu.

**Majibu**

Mamlaka inakiri kwamba mpaka ukaguzi unafanyika kweli ilikua na wafanyakazi wa kutwa ambao hawakupatiwa kibali kutoka Tume ya Utumishi Serikalini na walikua wanapatiwa likizo na stahiki.

Mamlaka iliajiri wafanyakazi wa kutwa kwa lengo la kuziba uhaba wa wafanyazi

uliokuepo ili kuweza kusaidia utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka.

Kutokana na Mamlaka kuona umuhimu wa kuendelea kuwatumia watumishi hao ilichukua jitihada ya kuwasilisha mapendekezo ya maombi Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi ya kuendelea na watumishi hao kwa njia ya uajiri wa kudumu.

Wizara ilichukua jitihada ya kuliwasilisha ombi hilo Serikalini na mpaka sasa Mamlaka inasubiri kibali cha kuajiri.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Katika kufuatilia hoja Kamati ya LAAC imebaini kuwa bado wafanyakazi hao wanaendelea kutoa huduma katika Mamlaka hii kwa kuwa Mamlaka haina mbadala wa wafanyakazi kwa sasa, kwani endapo Mamlaka itawasimamisha kazi wafanyakazi hao basi shughuli za Mamlaka hazitotekelezeka ipasavyo.

Kutokana na changamoto huo, Kamati ya LAAC imeitaka Mamlaka kuchukua hatua mapema ya kuwaajiri wanaoajirika ili hoja kama hii isiendelee tena katika miaka ijayo ya fedha.

### 5.3.1.13 Malimbikizo ya madeni ya muda mrefu bila ya kulipwa shilingi 23,549,716

Katika Ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Pemba inadaiwa madeni ya muda mrefu na Taasisi za Serikali, Wafanyabiasha pamoja na Wafafanyakazi wa Wizara yenye jumla ya shilingi 23,549,716 kwa ajili ya huduma mbali mbali.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016.

**Majibu**

Mpaka kufika Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali taasisi zilokuwa zinaidai Mamlaka ni Rahisi Auto Spare, AKB Clening Enterprises na ZAWA tu. Pia kwa upande wa deni la Rahisi Auto Spares ikuwa ni Tshs 2,710,000 badala ya 3,314,960 iliyojitokeza katika hoja za Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali.

Pia deni la ZAWA lilikua ni Tshs. 26,850,782/- badala ya 16,000,000 iliojitokeza kwenye hoja za Mkaguzi. Vilevile, Mamlaka ilikua haidaiwi kiasi chochote cha Fedha na Choda General Store kama ilivyojitokeza kwenye hoja za Mkaguzi.

Hata hivyo, Mamlaka imechukua jitihada ya kulipa madeni ambayo yalikuepo na

mpaka kufikia Januari, 2023 tumeshalipa deni lote kwa Kampuni ya Rahisi na AKB Cleaning Enterprises. Na kwa deni la ZAWA tunaendelea kulilipa ambapo kiasi cha Tshs. 8,000,000/- tayari zimeshalipwa. (Vielelezo vipo tayari kwa uhakiki).

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Katika kufuatilia hoja Kamati ya LAAC imebaini yafuatayo:

1. Deni halisi linalodaiwa ni Tsh. 26,850,782.72 na sio Tsh. 23,549,716 kama ilivyoelezwa kwenye Ripoti ya Mkaguzi Mkuu.
2. Kampuni ya Choda General Store ambayo imeripotiwa na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuwa inadaiwa Tsh. 2,426,990 uthibitisho huo haukupatikana.

Kutokana na kasoro hizo, hoja hii imebaki kama ilivyo, pamoja na hilo, Kamati ya LAAC imeitaka Mamlaka hii kulipa madeni hayo haraka iwezekanavyo ili kuepusha usumbufu kwa Wadai hao.

Vile vile, Kamati ya LAAC imeishauri Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuandika taarifa sahihi ili kuepusha usumbufu kwa Watumiaji wa Ripoti yake.

### 5.3.1.14 Hati za malipo zilizokosekana kwa ukaguzi shilingi 66,933,487

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 66,933,487 zimelipwa kwa ajili ya matumizi mbali mbali ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Pemba ambapo dosari iliyobainika na ukaguzi ni kukosekana kwa hati za malipo, vielelezo vilivyotumika kwa ajili ya malipo hayo pamoja na kukosekana kwa uthibitisho unaoonesha kwamba matumizi hayo yamelipwa kwa ajili ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege.

Kukosekana kwa hati za malipo kumepelekea kushindwa kuthibitisha uhalali wa matumizi ya fedha na hivyo kuwepo kwa dosari ya kutokuzingatiwa miongozo mbali mbali inayotolewa katika matumizi ya fedha pamoja na usimamizi wa rasilimali za Umma.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

**Majibu**

Mamlaka ya Viwanja vya ndege Pemba ilifanya matumizi kwa kufuata taratibu zote za matumizi ya fedha za Serikali na kuweka kumbukumbu za hati zote za malipo kama inavyotakiwa (Vielelezo vyote vipo kwa ajili ya uhakiki). Katika kipindi cha ukaguzi Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali haikuweza kufanikiwa kuzikagua baadhi ya hati za malipo kutokana na hati hizo kuhifadhiwa kwenye files

zisizo sahihi (misplaced), na hii imetokana na matengenezo ya ofisi yaliyokua yanafanyika kipindi hicho ikiwemo ofisi ya Mhasibu wa Mamlaka Pemba.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya LAAC haikuridhika na nyaraka zilizowasilishwa na Mamlaka kwa kuwa nyaraka hizo zinaonekana kuwa ni mpya. Hivyo, hoja hii imebaki kama ilivyo.

### 5.3.1.15 Hati za malipo zenye vielelezo pungufu shilingi 3,893,165

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 3,893,165 zimelipwa kwa matumizi mbali mbali ya Viwanja vya Ndege Pemba lakini baadhi ya vielelezo vya matumizi hayo havikuambatanishwa katika hati za malipo ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu 34(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma za Zanzibar nambari 12 ya mwaka 2016.

**Majibu**

Mamlaka inakiri mpaka ukaguzi unafanyika kulikua na baadhi ya hati za malipo zenye vielelezo pungufu. Vielelezo hivyo ilikua ni pamoja na stakabadhi ya malipo na tiketi za safari, hii ilisababishwa na ucheleweshwaji wa kufanya marejesho kwa watendaji waliosafiri na watoa huduma. Mbali ya changamoto hiyo iliobainika Mamlaka ilifanya matumizi kwa kufuata taratibu zinazotakiwa. Hata hivyo, jitihada ya kuomba marejesho ya tiketi na stakabadhi yalifanyika na zipo tayari kwa uhakiki.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya LAAC haikuridhika na nyaraka zilizowasilishwa na Mamlaka kwa kuwa nyaraka hizo zinaonekana kuwa ni mpya. Hivyo, hoja hii imebaki kama ilivyo.

### 5.3.1.16 Malipo ambayo hayakukatwa kodi ya zuio shilingi 5,600,000

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 5,600,000 zimetumika kwa ajili ya matumizi mbali mbali ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Pemba kwa watoa huduma mbali mbali bila ya kukatwa kodi ya zuio.

Kutokukata kodi ya zuio ni kuikosesha Serikali mapato ambapo ni kwenda kinyume na kifungu namba 50(2) cha Sheria nambari 7 ya Usimamizi wa Kodi ya Bodi ya Mapato ya Zanzibar ya mwaka 2009 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2020.

**Majibu**

Mamlaka inakiri mpaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anafanya ukaguzi wake kuna watoa huduma mbali mbali ambao hawakukatwa kodi ya zuio.

Hoja hio iliibuka kutokana na kodi ya magari mawili ya abiria yenye nambari za usajili Z974JN na Z892DK ambayo yalikodiwa na Mamlaka kwa ajili ya kuchukua Wafanyakazi.

Mamlaka ilifanya mazungumzo na Bodi ya Mapato (ZRB) juu ya kupata ufafanuzi wa uzuiaji wa kodi kwa gari za abiria zinazokodiwa. ZRB ilitoa ufafanuzi kwa Mamlaka kwa kusema kwamba kikawaida gari ya abiria inakuwa inalipa kodi mwanzo wa mwaka kabla ya kuingia barabarani Kwa hivyo gari hizi zilikuwa tayari zimeshalipiwa kodi husika kwa Mamlaka ya Kodi (ZRB) kiasi ambacho sisi Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Pemba hatukuwajibika tena kutoza na kuzuia tena kodi hiyo kwa vile zilikuwa tayari zimeshalipa kodi iliyokusudiwa tokea mwanzo wa mwaka kabla hatujakodi magari hayo. Mamlaka na ZRB zilithibitisha kwamba gari hizo zimeshalipa kodi kupitia kwenye mifumo ya kikodi.

### Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Katika kufuatilia hoja Kamati ya LAAC imeliomba ufafanuzi Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) kufuatia barua ya tarehe 03 Februari, 2023 yenye kumbuku Namba BLW/K.10/32 VOL.II/6, hata hivyo, hadi tunawasilisha Ripoti hii tarehe 22 Februari, 2023 Mamlaka haikujibu barua hiyo, hivyo, Kamati ya LAAC imeshindwa kutoa maamuzi juu ya hoja hii.

## SEHEMU YA TATU

## 3. HITIMISHO

Kamati ya LAAC ni miongoni mwa Kamati zinazosimamia masuala ya kifedha, hufanya kazi zake za ukaguzi kwa kupitia Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kuchunguza hoja mbali mbali zilizojitokeza katika Ripoti hizo, kufanya ziara za uchunguzi pamoja na kuchunguza kwa njia yoyote inayofaa mambo yote yanayohusu hesabu za Serikali za Mitaa na Mashirika yanayojitegemea kwa mujibu wa Kanuni za Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, Toleo la 2020.

Katika kutekeleza majukumu mbalimbali kwa mujibu wa kanuni za Baraza, Kamati ya LAAC ilieleza mambo ambayo imeyabaini kupitia majibu ya Watendaji na kutoa Mapendekezo kwa Wahusika kwa lengo la kuimarisha utendaji wa Taasisi za Umma. Kwa mnasaba huo, Kamati hii inaliomba Baraza la Wawakilishi, kuipitia, kuijadili na hatimaye kuiridhia Ripoti hii kwa lengo la kufanyiwa kazi na Serikali.

Hata hivyo kwa kuwa taratibu za kihasibu hubadilika mara kwa mara na kwa kuwa asilimia kubwa ya Wajumbe wa Kamati zinazosimamia masuala ya kifedha hawana taaluma ya kutosha juu ya masuala hayo. Aidha, kufanyika kwa mabadiliko ya wajumbe wa Kamati kutokana na teuzi mbalimbali za Mh Rais, hivyo basi, Kamati ya LAAC inaiomba Serikali kuiongezea fedha za matumizi Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, kwa lengo la kuzijengea uwezo Kamati ya LAAC na Kamati ya PAC kama zinavyofanya nchi nyengine duniani.

Pamoja na sababu tulizozieleza hapo awali, Kamati ya LAAC inashauri hili pia, Kwani Kamati zilianza kuzifanyia kazi ripoti za Mkaguzi kwa mwaka wa fedha 2020/2021 bila ya kuwa na uelewa wa kutosha kwa kuwa Ofisi hiyo kwa imechelewa kuwapatia uchambuzi wa Ripoti zake za mwaka wa fedha 2020/2021 kwa Wajumbe wa Kamati hizo kutokana na uhaba wa fedha unaoukabili Ofisi hiyo.

Pamoja na maelezo hayo, Kamati ya LAAC inapenda kutoa shukurani za dhati kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi Zinazojitegemea za SMZ na wananchi wote walioshiriki kwa namna moja au nyengine kwa mashirikiano makubwa waliyoipatia Kamati hii wakati inatekeleza majukumu yake ya kikatiba. Shukurani pia ziwafikie Watendaji wote wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kwa mashirikiano

yao kwa Kamati hii.

Vile vile, tunatoa shukurani za pekee kwa Afisi ya Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kuipatia mafunzo Kamati hii ili iweze kutekeleza shughuli zake kwa wepesi na kwa weledi mkubwa.

Mwisho na sio mwisho kwa umuhimu, tunatoa shukurani zetu za dhati kwa Mheshimiwa Spika wa Baraza la Wawakilishi, Katibu wa Baraza pamoja na Watendaji wote wa Afisi ya Baraza hilo kwa mashirikiano yao ya dhati waliyoyaonesha katika muda wote ambao Kamati hii ilipokuwa ikiwajibika.